KUTOKA KATIKA KILELE CHA USTAARABU WA KIISLAMU



WAKFU, SADAKA NA HUDUMA KATIKA UISLAMU

Othman Nuri TOPBASH

ERKAM PUBLICATIONS

Istanbul / 2022

© Kimechapwa na Erkam 2022 / 1443 H

WAKFU, SADAKA NA HUDUMA KATIKA UISLAMU

Othman Nuri Topbash

Mwandishi : Vakıf İnfak Hizmet
Mshauri Taaluma : Othman Nuri Topbash
Msimamizi Mkuu : Abdi Mohamed Adam
Mfasiri : Ibrahimu H. Kabuga
Mhariri : Rajabu Saidi Mihiko
Msanifu jalada : Dkt. Abbas Gurbanov
Kupangiliwa vizuri na : Sarkhan Isgandarov
Nijat Garibov
ISBN: 978-9944-83-864-1
Mchapaji: Erkam Printhouse
Anuani: Ikitelli Organize Sanayi Bölgesi Mah.
Atatürk Bulvarı, Haseyad 1. Kısım No: 60/3-C
Başakşehir, Istanbul, Turkey
Simu: (+90-212) 671-0700 pbx
(+90-212) 671-0748
Barua pepe: info@islamicpublishing.org
Tovuti: www.islamicpublishing.org
Language : Swahili / Kiswahili

ERKAM PUBLICATIONS

KUTOKA KATIKA KILELE CHA USTAARABU WA KIISLAMU

WAKFU, SADAKA NA HUDUMA KATIKA UISLAMU

Othman Nuri TOPBASH

ERKAM PUBLICATIONS

DIBAJI

Himidi zote ni za Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu, ambaye ametujaalia baraka ya imani.

Amani na baraka ziwe juu ya Fahari ya Milele ya ulimwengu, aliyetumwa kuwa Rehema kwa walimwengu.

Kama imani, msingi wa kiroho wa Uislamu ni *tawhid* au kuamini umoja wa Mwenyezi Mungu, na katika matendo, ni tabia njema, unyoofu na huruma. Huruma ndiyo tunda la kwanza la imani. Nafsi isiyokuwa na huruma haiwezi kuhesabiwa kuwa iko hai. *Bismillah,* ambayo ni mwanzo wa matendo yote mema, na *Fatihah*, sura ya ufunguzi ya Qur'an, huanza na majina ya Mwenyezi Mungu na *"Mwingi wa rehema"* na *"Mwenye kurehemu",* ambayo ni maneno yanayoonyesha ukarimu na huruma yake. Maisha ya mitume na mawalii wa Kiislamu pia yamejaa visa vya huruma. Miongoni mwa ishara kubwa za huruma katika ulimwengu huu ni *"infaq"* au kutoa sadaka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Kujenga jamii tulivu, kwa kulea watu wenye huruma, wema na wenye kutafakari, ni mojawapo ya malengo makuu ya dini. Mchakato huu unategemea kuilea roho kwa hisia za upole na huruma na kuzionyesha sifa hizo kupitia *Zaka, infaq* na kuihudumia jamii. Baada ya yote, hizi ni fursa kwa mja kulipa deni lake kubwa la shukrani kwa Mola wake.

Ithaar (kuwatanguliza wengine juu ya nafsi yake) ndiyo alama kubwa kabisa ya upendo wa kweli. Kwa kutegemea kiwango cha upendo wake, mpendaji huona kujitolea kwake kwa ajili ya mpendwa wake kama furaha na jukumu lisiloepukika. Ndiyo maana, moyo wa muumini unatakiwa kuwazunguka na kuwakumbatia kwa huruma viumbe wote kwa kumheshimu Muumba.

Kampeni kubwa ya *infaq* na utoaji huduma inahitajika katika dunia ya sasa, ambapo hisia za undugu zimedhoofika, amani na utulivu katika jamii vimepotea, na chuki na uadui vimezidi. Mbali na matatizo haya ya jamii ya sasa, migogoro iliyopo sasa ya kijamii na

kiuchumi ambayo haijawahi kutokea na watu kujisalimisha mbele ya ulimwengu wa kimaada yamekuwa kikwazo cha sadaka za kifedha, ambalo ni miongoni mwa vipengele vinavyopuuzwa sana vya imani yetu. Katika suala hili, masomo ya kwanza kuyazungumzia ni wajibu wetu wa *Zaka na Infaq*, na taasisi za kijamii za huruma kama vile waqfu.

Miongozo ya Kiislamu ambayo inasimamia masuala yote ya maisha kuanzia utotoni mpaka tunapoingia mwanandani, inapaswa kuandikwa upya kwa kuzingatia mahitaji ya wakati. Hili lisipofanyika kwa umakini, hatutaweza kulitambua pengo kubwa na muachano wetu na mazuri ya kimaadili ya Uislamu, na wala hatutaweza kujua ni kwa kiwango gani hisia hizi zimedhoofika katika roho zetu kadri siku zinavyokwenda. Kwa mfano, miongoni mwa mambo haya tutakayoyaeleza katika hiki kitabu ni ushr au moja ya kumi.

Tumeona kuwa kuna haja ya kuandika kitabu hiki ili kujikumbusha juu ya wajibu mbalimbali wa kifedha tulionao katika dini yetu, kama vile *zaka na waqfu*, na ili tuweze kuipitia upya hali halisi ya jamii ya sasa kwa nuru ya kanuni hizi. Kwa kuwa sehemu ya ngozi ya jamii yetu imezama katika ulimwengu wa kimaada, jambo ambalo limesababisha mgogoro wa kiroho, lengo letu ni kuimarisha kampeni za *waqfu, zaka na infaq* zitakazojenga hamasa, shauku na mwamko katika jamii yetu, na hatimaye kuyatibu maradhi yanayoikabili jamii yetu kwa sasa.

Tumetumia maelezo kadhaa ya kihistoria katika kuielezea maudhui yetu kama hatua ya kudhibiti dhamira zetu. Kudumu kwa Dola ya Uthamaniyyah iliyodumu kwa karne sita na nusu na utofauti wake, ikiwa ni pamoja na jamii mbalimbali za kidini na kikabila kulitegemea juhudi yake ya dhati ya kuunga mkono na kutetea dhana ya maisha yaliyo kwenye msingi wa amani na utulivu, tofauti na maeneo mengine ya ulimwengu. Kwa hakika mafanikio ya viongozi wa kiuthmaniyyah yalitokana na taasisi za hisani na umuhimu waliouweka kwenye waqfu.

Ni muhimu kueleza kuwa historia, ambayo ni mkusanyiko wa tajruba mbalimbali ya kitaifa, inaelezea kumbukumbu za mataifa mbalimbali. Hivyo, hakuna taifa ambalo halihitaji muongozo wa yale

yanayopatikana katika historia yake ili kuendelea na safari yake. Jambo hili ni muhimu sana hasa kwa historia iliyojaa mifano isiyo kifani ya mafanikio ya kimaada na kimaanawi (kiroho), ambayo kwa ujasiri mkubwa hutengeneza njia nzuri kwa ajili ya vizazi vya baadaye.

Kutokana na mtazamo huu, namna ambavyo historia yetu imejaa adhama ya kijeshi, ustaarabu, sayansi, na maadili, miongoni mwa mambo mengine kadhaa wa kadhaa, imevipita vilele vya ustaarabu mwingine wowote ule. Lakini, katika zama zetu hizi, bado kuna baadhi ya watu wajinga ambao wamejisalimisha kwenye ulimwengu wa kimaada na kuzishambulia tunu za kihistoria na kimaanawi za watu wetu. Juhudi za kukashifu za wale wanaoishi katika ardhi hii nzuri lakini wakakosa uhusiano wowote wa kihistoria na umma wa Kiislamu, kwa hakika juhudi zao hizo zinaonyesha jinsi ulimwengu wao wa ndani ulivyo. Kwa hakika historia ya jitihada za wale waliojaribu kutuacha tukiwa masikini tusiofaidika kikamilifu na chemchem iliyochanganywa na tunu za kidini na kimaanawi zimekuwepo kwa muda mrefu sana. Wamejaribu kutumia mbinu zenye sumu kali mno ili kuzidhoofisha thamani na tunu zetu za kidini na kimaanawi, ambazo ndiyo sababu kuu na halisi zilizotufanya tuitawale dunia kwa takriban miaka elfu moja. Matokeo ya juhudi za pamoja za maadui zetu, hatua kwa hatua, kwa sababu ya baadhi yao kutojua na wengine kuwa wasaliti, tawala zao kadhaa ziliweza kujitanua na kuingia ndani ya umma wa Kiislamu.

Matokeo ya jitihada zao za pamoja ni kuwa, vilizaliwa vizazi vipya ambavyo ufahamu wao wa kihistoria umelemaa na ambao wanaukana uhusiano wao na historia yao. Leo sasa tupo kwenye hatua ya kutisha sana na mbaya mno ya janga hili. Ili kuirejesha hadhi stahili ya baba zetu, tunatakiwa kuzigeuza nyuso zetu na kuzielekeza kwa mara nyingine kwenye chanzo hicho chenye baraka. Ni kwa njia hii tu ndipo tutakapoweza kujikomboa dhidi ya hisia ya uduni na udhalili iliyotengenezwa na mafanikio ya kiteknolojia ya Magharibi, na tutaweza kupata hamasa ya kupanda juu kwa mara nyingine. Hiki ndicho chanzo pekee kitakachoupatia umma wetu nguvu na uwezo wa kutoyumba na kuinuka kimaada na kimaanawi. Kukosekana kwa chanzo hicho, kwa upande mwingine, kunaweza

kuleta na kusababisha mwisho wenye kutisha ambao ni sawa na kukosa uhai wenyewe na zaidi.

Tunaamini kuwa mateso yaliyosababishwa na kughafilika au ujinga wa kutojua matukio yaliyotokea katika mkondo wa historia yatatengeneza cheche katika umma wetu wa Kiislamu, ambayo itawafanya watafakari sababu zilizosaidia kuwabadilisha watangulizi wetu kuwa watawala wakubwa wa ulimwengu. Mojawapo katika malengo makuu ya kitabu hiki, kilichochapishwa katika msimu huo wenye baraka, ni kufungua mlango wa chanzo hiki kitukufu.

Katika kiwango cha ubinaadamu na ustaarabu, mojawapo ya kurasa zenye kung'aa sana za urithi wetu wa kihistoria ni jitihada za kukuza hali ya utoaji sadaka, wakfu na ukarimu, ambazo zilikuwa nyenzo za kuwahuisha na kuwapa watu wetu sifa za kiroho, ambayo ni njia kamilifu zaidi ya kufikia lengo la kuumbwa kwetu. Tutapenda, kwa namna maalumu, kuangazia kipengele hiki cha historia yetu.

Hakika, kama tutakavyoona baadaye katika kitabu hiki, watangulizi wetu Waislamu, baada ya kukidhi mahitaji ya masikini, walikuwa wakienda mbali zaidi kwa kuwanyooshea hata wanyama dhaifu mikono yao ya huruma, upole na kujali – kiwango cha huruma ambacho hakijafikiwa na eneo lolote la dunia ya leo, na mfano mkubwa wa somo la kujifunza katika historia yetu adhimu.

Ustaarabu wa Kiuthamaniyyah uliamiliana na mwendawazimu kwa heshima kubwa, hivyo wakapewa jina la "wanaowaheshimu masikini". Walifanya juhudi za kuwapatia tiba, lishe na kuwachangamsha kwa michezo.

Katika ustaarabu wa wakfu wa Kiuthmaniyyah, mikono ya huruma ilinyooshwa pia kwa wenye ukoma, ambao walitengwa katika jamii kutokana na maradhi yao ya kuambukiza. Taasisi zilizoitwa *"Miskinler Tekkesi"* zilianzishwa kwa ajili ya kuwapatia matibabu.

Makazi mazuri ya ndege yalijengwa chini ya pembe za paa za nyumba ili kuwalinda na kuwapa chakula korongo waliojeruhiwa ambao walishindwa kuhama.

Aidha, nukta ya huruma na upendo wa kweli ambao ni lazima usemwe ni jinsi Wauthmaniyya walivyojitahidi kwa kuangalifu mkubwa, jitihada na upole katika kuepuka kuziumiza heshima na utu wa

watu wanyonge, masikini, wajane na yatima, kwa kuweka “mawe ya sadaka” msikitini ili kuzuia mwingiliano wa uso kwa uso kati ya mtoaji na mpokeaji wa sadaka. Hata chakula kilichokuwa kikisambazwa majumbani kilikuwa kikipelekwa wakati wa usiku ili kutoivunja heshima binafsi ya masikini. Taasisi mbali mbali zilianzishwa kwa lengo la kufidia hasara iliyosababishwa kwa bahati mbaya na wafanyakazi, ili kulinda utu na heshima yao.

Zilizotajwa hapo juu ni miongoni mwa kanuni muhimu ambayo inatakiwa kutafakariwa, ambayo kwa asili iliasisiwa ili kutambua hadhi, utu na heshima ya mwanadamu.

Kupitia mifano hii, tutapata kuutambua uzuri na umuhimu wa kutoa sadaka kadri tutakavyoonyesha katika maisha yetu huruma na murua unaopatikana ndani yake – njia ya hakika ya ushauri na harakati ya uamsho, ambayo tunaihitajia sana katika wakati tulionao.

Sababu ya kutoa mifano mingi katika kitabu hiki siyo tu kuonyesha heshima na kutambua yaliyofanywa na watangulizi wetu, bali pia kujifunza kutokana na mifano yao na kuyafanyia kazi katika maisha yetu.

Utamaduni wa wakfu katika zama za Uthmaniyya ni mfano wa aina yake kwa jamii ya sasa kwa maana unaonyesha namna huruma, upendo na upole vinavyotakiwa kuenezwa katika jamii. Katika kitabu hiki, sisi, pamoja na wasomaji wetu, tutashuhudia urithi ulioletwa na utoaji sadaka na kuwajali wengine. Tunamuomba Mola wetu atujaalie baraka nyingi ili wasomaji waweze kunufaika na ufafanuzi huu.

Bila shaka, mifano mizuri na adhimu ya kuwahudumia wengine iliyotajwa hapo juu inaweza kufikiwa na watu wenye ithaar (wenye kuangalia mahitaji ya wengine kabla ya mahitaji yao) na wa mfano katika kutoa huduma. Kwa maneno mengine, kazi na huduma zote hizi za heri huzaa matunda tu kulingana na kiwango cha ukamilifu wake wa kimaanawi na wa kiroho. Majukumu ya kazi yanayowekwa mikononi mwa watu wenye uwezo, waliopata mafunzo mazuri hutoa matunda bora yenye ukamilifu, wakati ambapo kazi zilizowekwa mikononi mwa watu wasiokuwa na uwezo wala ujuzi hutoa matun-

da mabaya na yenye kusikitisha, jambo ambalo ndilo lililotufanya tuongeze sura moja inayohusu utoaji wa huduma na maadili yake. Ndani ya sura hiyo tumezungumzia kanuni na viwango vya utoaji huduma na muongozo wa shakhsia zinazotakiwa kufikia adabu na daraja husika.

Kanuni na vipimo hivi zilizopangwa katika orodha kumi na mbili zinashughulikia maeneo yote mawili ya kiroho na kimwili kama vile muonekano wa nje na tabia ya ndani, elimu na maarifa, akili na moyo, dunia na akhera, ambavyo ni shuruti za mtu mwenye kutoa huduma. Lengo letu ni kuandaa watu wenye ujuzi na uwezo ili wawe watumishi wa kumtumikia Mwenyezi Mungu, utumishi ambao uta-wapeleka kwenye wema wa milele.

Mola wetu! Tujaalie tufikie daraja hiyo.

Ningependa kuwashukuru wasomi wote walionisaidia katika mchakato wa utengenezaji wa kitabu hiki. Ninamuomba Mwenyezi Mungu azipokee kazi zao na azibadilishe juhudi zao kuwa *sadaq al-jariyah* (sadaka yenye kuendelea).

Ewe Mwenyezi Mungu Mwenye mamlaka ya kweli! Tunakuom-ba uzifanye sadaka, huduma, huruma na upendo unaotolewa katika njia Yako viwe hazina za maisha yetu ya kiroho.

Amin!

Othman Nuri TOPBASH
ÜSKÜDAR/2002

Kutoka katika kilele cha ustaarabu wa Kiislamu

Ustaarabu wa Wakfu

Sura ya kwanza

USTAARABU WETU WA WAKFU

Wakfu ni aina maalumu ya sadaka yenye kuendelea na inayodhihirisha linaloelezea huruma, upendo wa kindugu na mahabba kwa viumbe kwa ajili ya Muumba wao. Hii inahusisha kujitolea mali maalumu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Kwa maneno mengine, ina maana ya kuzuia moja kwa moja *tamlik na tamalluk*[1] ya umilikaji wake na kuitunza na kuilinda kwa faida ya jambo la heri lililokusudiwa. Lengo lake ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu kwa kuitoa kwa heri kuwapa masikini, na kuwahurumia kwa huruma na upendo wa kweli, kutoa mali - hata maisha inapohitajika – kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni amri ya Mwenyezi Mungu ambayo Waislamu wote wanalazimika kuitii kwa sababu ni sharti la ukamilifu wa imani. Imeamriwa ndani ya Qur'an Tukufu Kuwa:

"Hakika Waumini ni wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake tena wasitie shaka kabisa, na wakapiga-

1. **Tamlik** ina maana ya kutoa umiliki wa mali fulani kwenda kwa mwingine; na tamalluk inawasilisha maana ya umiliki.

"Roho zilizozama katika umaskini ni kama nyumba iliyojaa moshi. Ufungulie dirisha moshi huo uliojaa nyumba kwa kusikiliza mahitaji yao na kuwapatia tiba, hivyo moshi utaondoka, na moyo na roho yako vitalainika..."
Jalal al-Din Rumi

na Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao. Hao ndiyo wakweli." (Qur'an, 49: 15)

"Ambao huyaamini ya ghaibu na hushika Sala, na hutoa katika tuliyowapa." (Qur'an, 2: 3)

"Hakika Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao kwa kuwa wao watapata Pepo..." (Qur'an, 9: 111)

"Na katika watu yupo ambaye huiuza nafsi yake kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa waja wake." (Qur'an, 2: 207)

Uislamu, kwa kuiona dunia kama maandalizi kwa ajili ya Akhera na Akhera kuwa muendelezo wa ulimwengu huu, umeweka mizania kamili baina ya mwili na roho, maada na maanawi. Uwiano huu umeweka msingi imara wa jamii yenye amani na ustawi.

"Mwanadamu anapokufa, matendo yake yote hufikia kikomo isipokuwa mambo matatu: sadaqah al-jaariya (sadaka yenye kuendelea), au elimu yenye manufaa, au mtoto mwema anayemuombea."

(Muslim, Kitab Al-Wasiyya, 14)

Waqfu, ambazo hutumika katika maeneo mengi tofauti, ndiyo taasisi zenye kufaa zaidi za infaq. Ndani ya Waqfu kuna maadili ya kweli ya Kiislamu ya huruma na upendo. Tumeamrishwa ndani ya Qur'an Tukufu kutoa vile tunavyovipenda zaidi ili tupate radhi za Mwenyezi Mungu.

Kwa wanadamu, vitu vyenye thamani zaidi kwako katika ulimwengu huu ni nafsi (uhai) na mali zao. Kuingia peponi na kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu hufikiwa tu kwa kuisalimisha nafsi na mali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Ndiyo maana kwamba wale wanaoishi na kuwa wakarimu wa mali zao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wanaitwa **"watu waliotolewa wakfu"**. Huitwa

hivyo kwa sababu wanakuwa wamejitoa wakfu wao wenyewe na mali zao zote katika njia ya heri.

Watu hao wana mchango mkubwa mno katika kuhakikisha amani na utulivu katika jamii. Khidma na juhudi zao haziishii kwenye mipaka ya mauti yao, bali huendelea kuwepo kwa njia ya miradi wanayoianzisha na kuiasisi. Katika safu ya mbele ya "watu waliotolewa wakfu" wapo mitume, marafiki wa Mwenyezi Mungu, na wale waliofikia ukamilifu kupitia mafunzo yao. Wameieneza imani yao ulimwenguni kote kujaa katika kurasa za dhahabu za historia.

Miongoni mwa sababu za ulimwengu wa sasa kushuhudia kiwango kikubwa cha matatizo ya kijamii na kiuchumi ni kutokana na kuziharibu wakfu za kale na zenye utajiri na upungufu wa zile zilizoanzishwa. Kwa hiyo ni wajibu wa matajiri Waislamu wa zama zetu wajitahidi kuanzisha upya waqfu mbalimbali.

Mtume (s.a.w) anasema katika hadith yake moja:

"Mwanadamu anapokufa, matendo yake yote hufikia kikomo isipokuwa mambo matatu: *sadaqah al-jaariya* (sadaka yenye kuendelea), au elimu yenye manufaa, au mtoto mwema anayemuombea." (Muslim, Kitab Al-Wasiyya), 14)

Wanazuoni na wasomi wa Kiislamu wameitafsiri sadaka yenye kuendelea kuwa ni "waqfu". Sadaka yenye kuendelea ina maana ya kuacha mali inayoendelea kutoa huduma na kuwanufaisha wanadamu baada ya kifo cha mtu husika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Kuna baadhi ya mito na chemchem, ambazo zimeendelea kutiririka kwa wingi tangu ulipoumbwa ulimwengu. Na zitaendelea

Mmiliki wa mali, mmiliki wa bidhaa
Ni yupi mmiliki wake wa kwanza?
Mali ni uongo, bidhaa ni uongo,
Hapa chezacheza navyo kwa muda
Yunus Emre

kutiririka mpaka siku ya mwisho, zikikata kuwapa matumaini na furaha wenye huzuni, na kuzihuisha nafsi. Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) aliyafananisha baadhi ya matendo ya heri na chemchem hizo. Hata hivyo, chemchem hizo ni tofauti kidogo na chemchem za kawaida, kwa sababu faida zake zitaendelea kutiririka milele, hazitoishia tu mwisho wa dunia, bali milele, na zitaendelea kuongeza thawabu kwenye vitabu vya waumini. Kwa maneno mengine, hubadilika kuwa *sadaqah jariyah.*

Mwenyezi Mungu Mtukufu amekiweka kila kitu ulimwenguni kiwatumikie wanadamu na kukabidhiwa jukumu la kuviangalia. Neema zote ikiwa ni pamoja na watoto, mali, na afya ambavyo wamekabidhiwa wanadamu, ambao wanatakiwa kuvitunza kwa uangalifu. Kuvilinda kama inavyohitajika ndiyo njia pekee ya kupata baraka na rehema za Mwenyezi Mungu.

Yunus Emre anaeleza kwa uzuri kwamba:

Mmiliki wa mali, mmiliki wa bidhaa
Ni yupi mmiliki wake wa kwanza?
Mali ni uongo, bidhaa ni uongo,
Hapa chezacheza navyo kwa muda

Katika hali halisi, kila kitu ni milki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Wanadamu wamepewa haki ya muda tu ya kuvimiliki. Ndiyo maana mojawapo ya masharti ya kuwa waumini wa kweli ni kuishi tukijua kwamba vitu vyetu vyote tunavyovimiliki ni amana tu tuliyokabidhiwa. Kwa hali hii, kutumia mali zetu nje ya mipaka ya infaq ni uvunjaji wa haki ya amana. Siyo tu kwamba adhabu ya matumizi haya mabaya itakuwa kali

“Mfano wa wanao tumia mali zao katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyochipuza mashuke saba. Katika kila shuke zimo punje mia. Na Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa na Mwenye kujua.”

(Qur’an, 2: 261)

huko Akhera, lakini ni dhahiri pia kuwa itasababisha mgogoro mkubwa katika ngazi zote mbili za mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla. Kutoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu huilinda jamii dhidi ya ubepari na kuzuia hisia za kuoneana husuda na chuki miongoni mwa wanajamii.

Wanajamii wenye mali hawatakiwi kusahau hata kidogo kwamba siku moja wanaweza kupoteza kila kitu walichonacho na wakawa masikini na mafakiri wa kesho. Ndiyo maana kwamba wanatakiwa kufanya juhudi kubwa katika kujiunga na kampeni za infaq. Kitendo hiki ni hatua ya kimatendo ya shukrani zao kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kutokana na baraka na neema alizowapa.

Baraka ya kweli ya sadaka inayotolewa katika njia ya Mwenyezi Mungu hutegemea nia na Ikhlasi (usafi wa moyo). Jambo muhimu ni kutekeleza matendo yetu kwa Ikhlasi na taqwa (uchamungu). Mwenyezi Mungu Mtukufu humjaalia baraka tele yule mtu aliyetoa sadaka kwa ajili Yake hata kama kiasi alichotoa ni kidogo mno. Qur'an Tukufu inasema:

"Mfano wa wanao tumia mali zao katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyochipuza mashuke saba. Katika kila shuke zimo punje mia. Na Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa na Mwenye kujua."
(Qur'an, 2: 261)

Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu naye anasema:

Wakfu ni aina maalumu ya sadaka yenye kuendelea na inayodhihirisha linaloelezea huruma, upendo wa kindugu na mapenzi kwa viumbe kwa ajili ya Muumba wao.

"Mwenye kujenga msikiti kwa sababu ya kumpenda Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu atamjengea jengo kubwa peponi." (Muslim, Kitab al-masajid, 24)

Faida kubwa nyingine ya waqfu ni kuwa huwazuia matajiri kutotumia mali zao kwa ubadhirifu na kutozifuja kwa majivuno.

Lengo kuu la kuanzisha *waqf* ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu na kupata furaha ya Akhera. Tangu siku za mwanzo kabisa, waqfu zimekuwa zikianzishwa kwa ajili ya kufikia lengo hili. Ndiyo maana kwamba lengo hili limekuwa likijumuishwa na neno *"al-taqarrub ilallah"* (nyenzo ya kujikurubisha zaidi kwa Mwenyezi Mungu), na limekubaliwa kuwa ni mojawapo katika masharti ya usahihi na uhalali wa waqfu.

Kwa hiyo, tunatakiwa kuwa makini sana kuhusu waqfu mbalimbali na kuzitunza amana hizi za Mwenyezi Mungu. Katika historia ya Uislamu, suala hili liliangaliwa kwa dhati, na lilipovunjwa, Waislamu walikabiliwa na matokeo ya kutisha. Ngamia wa Nabii Saleh (a.s) aliyetolewa kama muujiza hakuwa mali ya mtu yeyote, bali alitolewa na Mwenyezi Mungu kama amana kwa ajili ya kuwanufaisha wanadamu. Kwa namna hiyo, ilikuwa ni sawa na wakfu. Maziwa yaliyozalishwa na ngamia huyu yaliweza kufananishwa na chemchem ya maji ya umma na mmiliki wake ni Mwenyezi Mungu Mtukufu; lakini watu wa Saleh walimuua ngamia na kwenda kinyume na amana waliyopewa. Matokeo yake wakaangamizwa.

"Mwenye kujenga msikiti kwa sababu ya kumpenda Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu atamjengea jengo kubwa peponi."

(Muslim, Kitab al-Masajid, 24)

Mfano wa Nabii Sulayman (a.s) na hudhud wawili ni wenye mazingatio.

Katika tukio moja, Nabii Sulayman (a.s) alimkemea hudhud. Ndege huyo akajibu kwa kumtisha:

"Naweza kuuangamiza ufalme wako."

Sulayman (a.s) akasema:

"Wewe ni ndege mdogo sana halafu unasema unaweza kuungamiza ufalme wangu."

Aliposikia hivyo, ndege yule mdogo akajibu:

"Ninaweza kuziloweshа mbawa zangu na kuzisugua kwenye udongo uliotolewa wakfu. Kisha ninaweza kuchukua udongo huo na kuutupa juu ya paa ya kasri lako. Hiyo itatosha kuliangamiza kasri lako!..."

Mfano huu unaonyesha jinsi tunavyotakiwa kuwa makini na waangalifu kwenye mali ya wakfu.

Kwa hakika, watangulizi wetu walituusia kuwa makini na ibada ya W (yaani kusema *wallah* [kuapakwa jina la Allah] bila msingi wowote, kuwa wana tusiotekeleza wajibu na majukumu, kuwa *wasi* [walezi]) tusiotekeleza masharti yake kikamilifu, na kutambua uzito wa majukumu ya kushughulika na mali ya waqfu pindi isipotumika kwa njia sahihi. Hata hivyo, hatutakiwi kuielewa vibaya maana ya ushauri huu. Mtu atakapokuwa na sifa sahihi na akawa na uwezo wa kuitunza kikamilifu mali ya waqfu, basi atawajibika kwa kutozitumikia waqfu. Maana hasa ya onyo lililotajwa hapo juu inasisitiza juu ya tahadhari ya la-

"Mwenye kutangua au kubadilisha masharti ya wakfu hii, basi laana ya Mwenyezi Mungu, malaika, wanadamu na viumbe wote iwe juu yake!..."
Nukuu kutoka katika hati ya wakfu ya Sultan Mehmet

zima inayotakiwa kuchukuliwa katika kulinda na kugawa mali ya waqfu. Waqfu ni mali inayohamishika au isiyohamishika ambayo mmiliki wake ni Mwenyezi Mungu Mtukufu, wakati matunda yake (faida na mazao yake) hutolewa kwa ajili ya manufaa ya wanadamu. Kwa maneno mengine, mali inapotolewa wakfu, mali hiyo inakuwa si milki ya mtoaji tena. Haiwezi kuuzwa, kutolewa kama sadaka kuwapa watu wengine au kurithiwa. Ili kusisitiza uzito wa uendeshaji wa mali ya waqfu, dua na laana hujumuishwa mwanzoni na mwishoni mwa tendo la waqfu. Dua hiyo ni kwa ajili ya kuwaombea wema wale wanaotunza kikamilifu mali hiyo ya waqfu, na laana ni kwa ajili ya wale wasiotekeleza jukumu lao vizuri, na wanaoisababishia madhara ya mali hiyo. Mfano ufuatao ni laana ya tendo la waqfu kutoka katika tendo la Waqfu ya Hagia Sophia iliyoandikwa na Mehmed II:

"Yeyote atakayetangua au kubadilisha masharti ya waqfu hii, basi laana ya Mwenyezi Mungu, malaika, wanadamu na viumbe wote iwe juu yake!..."

Aina hii ya laana katika wakfu ni kitisho cha kiroho. Waumini wa kweli wanaohofia kuhusu wokovu wao wa milele hawatopenda wakumbwe na laana kama hiyo na kwa hiyo huwa waangalifu sana.

"Wahurumieni walio ardhini, ili mpate kuhurumiwa na wale walio mbinguni"

(Tirmidhi, Birr, 16; Abu Dawud, Adab, 66).

Kuwa na uangalifu na umakini katika uendeshaji na ulinzi wa mali za waqfu tumepewa nafasi kubwa katika Uislamu kiasi kwamba maneno yasemayo «شَرْطُ الْوَاقِفِ كَنَصِّ الشَّارِعِ», "Masharti ya-

nayowekwa na mtoaji wa *waqfu* ni kama sheria iliyowekwa na Mwenyezi Mungu" yamekuwa msingi wa sheria. Kwa maneno mengine, kama ambavyo fikra ya kubadilisha sheria za Mwenyezi Mungu imeharamishwa, vivyo hivyo hairuhusiwi kubadilisha masharti yaliyowekwa na mtoaji wa waqfu. Kwa sababu ya kanuni hii, waqfu mbalimbali zilizoanzishwa karne nyingi zilizopita bado zinaendelea kufanya kazi mpaka leo.

Hapo mwanzo waqfu zilianza katika maeneo ya ibada, na kisha zikasambaa na kuenea katika nyanja nyingine za kijamii. Kwa mujibu wa riwaya, Nabii Ibrahimu (a.s) alifurahishwa mno na Malaika Jibril (a.s) katika kumsifu Mwenyezi Mungu kiasi kwamba akatoa mifugo yake yote kumpa Malaika huyo. Lakini, Jibril (a.s) hakuikubali sadaka ya Ibrahimu kwa sababu yeye ni malaika. Hapo, Nabii Ibrahimu (a.s) akauza mifugo yake, akanunua shamba na kulitoa kwa ajili ya kuwanufaisha watu. Kwa hali hiyo, waqfu ya kwanza ilianza na Nabii Ibrahimu (a.s).[2]

Mtume wetu Mtukufu (s.a.w), ambaye alitumwa kama rehema na mfano bora kwa walimwengu wote anasema:

"Wahurumieni walio ardhini, ili mpate kuhurumiwa na wale walio mbinguni" (Tirmidhi, Birr, 16; Abu Dawud, Adab, 66). Kama alivyokuwa mfano bora kwa watu wake katika vipengele vyote vya maisha, aliitekeleza wakfu kwa vitendo katika kipindi cha maisha yake, kwa kutoa mashamba yake saba

"Simjui Muhajir au Ansar yeyote mwenye mali ambaye hana waqfu"

(Ibn Qudamah, Al-Mughni, juzuu V, 58)

2. Tazama Bursawi, Ismail Haqqi, Ruh al-Bayan, juzuu 2, 293.

ya tende katika mji wa Madina na mgao wake wa mashamba ya tendo katika eneo la Khandaq na Khaybar kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Maswahaba wake (r.a) walifuata nyayo zake nao pia wakatoa mali zao zenye thamani sana. Jabir (r.a) anasema:

"Simjui Muhajir au Ansar yeyote mwenye mali ambaye hana waqfu" (Ibn Qudamah, Al-Mughni, juzuu V, 58)

Umar (r.a) alipata bustani ya tende kutoka katika ngawira za Khaybar. Kwa muda wa siku tatu mfululizo, alikuwa akiota kuwa amelitoa sadaka bustani lake. Akaja kwa Mtume (s.a.w) na kusema:

"Ewe Mtume wa Allah! Sijawahi kuwa na bustani lenye thamani kama hilo katika maisha yangu. Nitafanya chochote utakachoniamrisha."

Mtume (s.a.w) akajibu:

"Ukitaka, unaweza kulitoa sadaka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Baada ya kufanya hivyo, haliwezi kuuzwa, kutolewa sadaka au kurithiwa. Mavuno yake tu ndiyo yanayoweza kutolewa kama sadaka."

Mara moja Umar (r.a) akalitoa shamba lake hilo, ambalo liliwanufaisha masikini walioutetea Uislamu, watumwa waliotaka kukombolewa na wasafiri.[3]

"KABISA HAMTAFIKIA wema mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda. Na kitu chochote mnacho kitoa basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua."

(Qur'an, 3: 92)

3. Tazama, Bukhari, Kitab al-Wasaya, 22, 28.

Kutoa kwa moyo wa dhati kutoka katika vile unavyovipenda sana ni msingi mkuu wa sadaka. Siku moja, Maswahaba wa Mtume (s.a.w) walikuwa wamekusanyika katika msikiti wa Madina wakisikiliza khutba ya Mtukufu Mtume (s.a.w). Mtume (s.a.w) akasoma Aya ifuatayo:

"KABISA HAMTAFIKIA wema mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda. Na kitu chochote mnacho kitoa basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua." (Qur'an, 3: 92)

Baada ya Aya hii kuteremshwa Maswahaba wa Mtume (saw) walianza kutafakari namna watakavyoweza kutekeleza msingi huu katika maisha yao. Miongoni mwao alikuwepo Abu Talha (Mwenyezi Mungu awe radhi naye). Katika Ansar wa Madina, yeye ndiye aliyekuwa na mali kubwa ya shamba la tende, alikuwa akilipenda sana shamba lake, na zaidi ya hapo lilikuwa karibu sana na Msikiti wa Mtume (s.a.w). Mara kwa mara alikuwa akimualika Mtume (s.a.w) kwenye shamba lake na kumpa chakula na maji.

Abu Talha aliathiriwa mno na Aya hii kiasi kwamba akaenda kwa Mtume (s.a.w) na kusema:

"Ewe Mtume wa Allah! Mwenyezi Mungu anasema kuwa, ***KABISA HAMTAFIKIA wema mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda' Kitu ninachokipenda zaidi katika mali zangu ni hili shamba liitwalo Bairuha'.*** Ninataka kulitoa sadaka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, nikitaraji thawabu zake kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa

Mwenyezi Mungu Mtukufu amekiweka kila kitu ulimwenguni kiwatumikie wanadamu na kukabidhiwa jukumu la kuviangalia. Neema zote ikiwa ni pamoja na watoto, mali, na afya ambavyo wamekabidhiwa wanadamu, ambao wanatakiwa kuvitunza kwa uangalifu. Kuvilinda kama inavyohitajika ndio njia pekee ya kupata baraka na rehma za Mwenyezi Mungu.

hiyo, unaweza kulitumia kama Mwenyezi Mungu atakavyokuelekeza."[4]

Riwaya zinasema kuwa baada ya mazungumzo haya, Abu Talha (r.a) alikwenda shambani kutekeleza uamuzi wake. Alipofika shambani alimkuta mkewe kakaa chini ya kivuli cha mti. Abu Talha hakuingia shambani.

Mke wake akauliza: "Ewe Abu Talha! Kwa nini unasubiri nje, kwa nini hauingii?" Abu Talha akasema:

"Siwezi kuingia, nawe pia unatakiwa kuchukua vitu vyako na utoke." Kutokana na jibu hili ambalo hakulitarajia mkewe aliuliza kwa mshangao: "Kwa nini ewe Abu Talha? Je shamba hili si letu?"

Hapana, kuanzia leo shamba hili ni la masikini wa Madina," alisema. Aliendelea kumueleza mkewe habari njema inayopatikana katika Aya hiyo na kueleza kwa hamasa kuhusu sadaka aliyoitoa.

Mkewe akauliza: "Je umelitoa kwa niaba yetu sote au kwa niaba yako wewe binafsi?"

Akajibu: "Kwa niaba yetu wote." Akasikia maneno yafuatayo kutoka kwa mkewe kwa utulivu kabisa: "Mwenyezi Mungu akuridhie ewe Abu Talha! Nilikuwa na mawazo hayohayo nilipowaona masikini wanaotuzunguka, lakini sikupata ujasiri wa kukwambia. Mwenyezi Mungu aikubali sadaka yetu. Ninaondoka shambani na kuja pamoja nawe!"

"Katika zama za dola ya Uthmaniyyah, wakfu ziliibuka kuwa asasi ya hazina ambapo mali zilisambazwa katika jamii. Badala ya matajiri kujilimbikizia mali kwa maslahi yao binafsi na familia zao, matajiri hao walizitoa mali zao kwa maslahi ya jamii yao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu."

4. Tazama, Bukhari, Wasaya, 17.

Siyo vigumu kutabiri hali ya furaha ambayo ingeshamiri ulimwenguni iwapo sifa hii ya kimaadili, kama ya Abu Talha, ingekuwa imeshamiri ulimwenguni kote.

Wauthmaniyya, ambao walionyesha juhudi kubwa katika kufuata nyayo za Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) na maswahaba wake, kwa moyo imara walianzisha taasisi mbalimbali za heri na kuzifanya kuwa kipaumbele chao. Kutokana na hali hiyo, katika zama za Wauthmaniyya, wakfu zilistawi, kwa idadi na ukubwa. Katika zama za dola ya Uthmaniyyah, wakfu ziliibuka kuwa asasi ya hazina ambapo mali zilisambazwa katika jamii. Badala ya matajiri kujilimbikia mali kwa maslahi yao binafsi na familia zao, matajiri hao walizitoa mali zao kwa maslahi ya jamii yao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Katika kipindi cha Dola ya Uthmaniyyah, wakfu zilifikia kiwango ambacho siyo tu kwamba ziliyakidhi mahitaji ya wanadamu pekee, bali pia zilihusisha mahitaji ya wanyama na hata mimea. Ummah huu adhimu ulioishi kwa misingi ya Uislamu na kuwahudumia Waislamu wote, ulionyesha huruma ya Uislamu isiyokuwa na mipaka kwa ulimwengu wote. Waliasisi maelfu ya wakfu katika dola yote na hawakuacha jeraha lolote bila kutibiwa.

Wauthmaniyya waliitumia kauli ya Mtume (s.a.w) isemayo: *”Ubora wa watu ni ule unao wafaa zaidi watu”* (Suyut, Al-Jami’ a-Saghir, juzuu II, 8) kama kanuni yao na kuanzisha taasisi mbalimbali kubwa na za kudumu.

”Mbora wa watu ni yule anayewafaa zaidi watu”

(Suyut, Al-Jami’ a-Saghir, juzuu II, 8)

Huduma na juhudi mbalimbali za wakfu zilizoanzishwa katika zama za Dola ya Uthmaniyya zilijumuisha eneo kubwa sana. Mambo mbalimbali yaliyoonyeshwa na kushughulikiwa, kulingana na mabadiliko ya wakati na mahali, yanaashiria asili yenye nguvu ya wakfu.

Huduma na juhudi mbalimbali za waqfu zilizoanzishwa katika zama za Dola ya Uthmaniyya zilijumuisha eneo kubwa sana. Mambo mbalimbali yaliyoonyeshwa, kulingana na mabadiliko ya wakati na mahali, yanaashiria asili yenye nguvu ya waqfu.

Hata kama ni vigumu kuainisha na kuorodhesha maeneo yote ya huduma na shughuli za waqfu, tunaweza kuashiria maeneo kadhaa ya muhimu kama ifuatavyo:

- Ujenzi na utunzaji wa misikiti, mabweni ya wanafunzi na mafunzo ya kiroho, nyumba za kulala wageni na maeneo matukufu.
- Taasisi za kielimu, kama vile vyuo (colleges), shule za Qur'an na taasisi nyingine za kitaaluma na kielimu.
- Hoteli, nyumba za kupumzikia wasafiri, hosteli, mabafu na hospitali
- Misikiti midogo midogo, maktaba na nyumba za wageni
- Visima, mifereji, daraja na chemchem
- Migahawa ya umma, vituo vya kulelea watoto
- Kuwakomboa watumwa
- Kuwasaidia masikini kwa kuwapatia fueli
- Kuwasaidia watumishi kununua na kubadilisha vikombe na sahani walizozivunja
- Kuwasaidia mabinti yatima kwa kuwafanyia maandalizi ya ndoa zao

- Kuwasaidia wanaodaiwa kulipa madeni yao
- Kuwasaidia wajane na mafukara
- Kuwasaidia watoto wa shule kwa kuwapatia chakula na mavazi
- Kuwafurahisha watoto waliotelekezwa katika kipindi cha sikukuu za kidini
- Kushughulikia huduma za mazishi ya watu masikini
- Kuwapatia ulinzi na usalama wazee na wanawake wasiokuwa na makazi

Mbali na hayo, Wauthmaniyyah walianzisha wakfu katika kila eneo linalohitajika, na kuubadilisha ustaarabu wao kuwa wa wakfu. Kwa kweli, wakfu zinaweza kuhesabiwa kuwa ni alama inayoipambanua Dola ya Uthmaniyyah.

Tungependa kuelezea kipengele kimoja cha umuhimu wake katika kuonyesha mfano wa werevu wa kidini na watangulizi wetu. Wakfu kadhaa wa kadhaa zilianzishwa kwa ajili ya kuihudumia miji mitukufu ya Makkah na Madina, ambazo kwa ujumla zilijulikana kama “Wakfu za *Haramain* (miji miwili mitukufu ya Makkah na Madina)”. Ili kuhakikisha amani, utulivu na ustawi wa maeneo hayo matukufu, mtu angeweza kuona aina hizo za Wakfu zikiwekwa kila mahali kutoka Ulaya ya Kati mpaka Yemen na maeneo hayo matukufu yaliwekewa uongozi wake maalumu. Mbali na mapato yaliyotokana na wakfu hizi, karibu masultani wote wa Kiuthmaniyyah walikuwa wakituma zawadi kwenye maeneo hayo matukufu na mae-

Hisia ya kuwasaidia wengine katika jamii ya Kiuthmaniyya ilifikia kiwango cha hali ya juu kiasi kwamba, kama tulivyoeleza hapo awali, sio tu watu bali pia wanyama na hata mimea ilipewa ulinzi na hifadhi.

neo ya jirani wakati wa sherehe za kila mwaka za kuweka sitara mpya kwenye Ka'bah. Desturi hii iliyojulikana kama *"sürre alayı"*[5], iliendelea mpaka Dola hii ilipofikia ukomo wake. Wakati huo, zawadi hizi zilikuwa nyingi za kiwango kikubwa. Hili linaonekana pale ambapo Sharif Hussain na washirika wake walipofanya uasi dhidi ya Dola ya Uthmaniyya wakati wa Vita vya kwanza vya dunia, Fakhriddin Pasha, ambaye alikuwa akiulinda mji wa Madina dhidi ya waasi, aliziweka zawadi hizi ndani ya masanduku na kuzituma mjini Istanbul kwa lengo la kuzilinda zilinyakuliwa. Idadi ya masanduku zaidi ya mia tatu inaonyesha ukubwa na wingi wa zawadi zilizokuwa zikitumwa huko na Wauthmaniyya.

Huduma zilizotolewa katika ardhi hizo tukufu kupitia wakfu zilizoanzishwa na Masultani wa Kiuthmaniyya, viongozi wa serikali wahisani katika jamii ya Kiuthmaniyya zilitambuliwa na kushukuriwa na ulimwengu wote wa Kiislamu.

Aina nyingine yenye kukumbukwa ya wakfu ni ile iliyoanzishwa kwa ajili ya kuwahifadhi wazee na wanawake tegemezi. Badala ya kuwasaidia kwa namna ya moja kwa moja, zilianzishwa wakfu mbalimbali kwa lengo la kuwapatia sufu na pamba ya bure ili watengeneze bidhaa zinazotokana na malighafi hiyo. Kutokana na kazi yao hii waliweza

Kila mtu katika jamii ya Uthmaniyya, kuanzia Masultani mpaka watu wa kawaida, walikuwa na dhamiri, ufahamu na hisia za uhisani.

5. "sürre alayı: ni pesa, dhahabu na zawadi zilizotumwa katika mwezi wa Rajab kwa msafara maalumu kutoka kwa masultani wa Kiuthmaniyya kwa lengo la kuzigawa kwa watu wote wa Makkah na Madina, kuanzia watu maskini mpaka matajiri. (Tazama Münir Atalar, Sürre-i Hümayun ve Sürre Alayları, Diyanet işleri Başkanlığı yayınları, Ankara, 1991, uk. 2)

kupata mishahara wa kujisaidia. Kwa namna hii, wakati wakiwa ukingoni mwa uhai wao, wakfu hizi ziliwasaidia kuishi maisha ya amani na ya heshima.

Hisia ya kuwasaidia wengine katika jamii ya Kiuthmaniyya ilifikia kiwango cha hali ya juu kiasi kwamba, kama tulivyoeleza hapo awali, siyo tu watu bali pia wanyama na hata mimea ilipewa ulinzi na hifadhi. Katika zama za Uthmaniyya, hospitali za wanyama zilianzishwa kwa lengo la kuwahudumia ndege walioshindwa kuhama na kuruka kutoka na kuumwa,. Ndege hao ni kama vile korongo n.k, na gharama za kuwahudumia ziligharamiwa na wakfu. Akistaajabishwa na hisia hii, afisa wa jeshi la Kifaransa Comte de Bonneval (14 Julai 1675 – Machi 23, 1747) anazungumzia kuhusu siku alizokaa katika ardhi za Wauthmaniyya:

Kwa mujibu wa maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w) mwanamke mmoja alisamehewa dhambi zake kwa sababu tu ya kumpa maji mbwa mwenye kiu. Kwa upande mwingine, mwanamke mwingine aliadhibiwa katika moto kwa sababu ya kumuacha na njaa paka mwenye njaa na kumsababishia kifo.

"Ni kawaida kabisa kuwaona Waturuki waliovuka mipaka ya kawaida ambao walikuwa wakijitolea pesa kuwapa wafanyakazi wamwagilie maji kwenye miti kwa lengo la kuilinda isikauke."

Kwa kuwa uanzishaji wa wakfu unahitaji kiwango fulani cha ukomavu wa kiroho, muongozo wa *murshid kamil* au walimu kamili wa Kisufi ndiyo walioongoza juhudi hizo. Matunda ya mafunzo ya kiroho, ikiwa ni pamoja na ithaar, ukarimu na Ikhlasi, ni mambo yaliyofaa kwa ajili ya lengo hili.

Makazi maalumu ya wanafunzi wa kiroho (madarwesh) vilikuwa ni vituo vya mafunzo ya kiroho kwa kila mtu katika jamii ya Kiuthmaniyya. Vilikuwa vituo vya kuuteka "utamaduni simulizi" na kufikia ukomavu wa kimaadili. Ukomavu wa kiroho uliopatikana katika vituo hivi ilikuwa mojawapo

ya vichocheo vikubwa katika kuanzisha wakfu na kueneza mshikamano na umoja miongoni mwa wanajamii. Kutokana na ukweli huu, vituo hivi vyenyewe pia vilikuwa wakfu. Wanafunzi wengi kutoka katika vituo hivi walifikia sifa ya *vakf insan* yaani mtu aliyejitoa wakfu, na kuacha taasisi kadhaa za heri baada ya mauti yao.

Baadhi ya taasisi za heri zilizoanzishwa kutokana na matunda ya juhudi hizi za heri zimeendelea kuwepo mpaka sasa na zinaendelea kutoa huduma kwa jamii. Baadhi ya misikiti, visima, kambi za kijeshi, hospitali na huduma nyingine za hisani ni kumbukumbu zilizobaki zinazotukumbusha enzi za Wauthmaniyya.

Kila mtu katika jamii ya Uthmaniyya, kuanzia Masultan mpaka watu wa kawaida, walikuwa na dhamiri, ufahamu na hisia za uhisani. *Murshid Kamil* waliwahamasisha na kuwashawisha watu kuwa wakarimu. Aziz Mahmud Hudayi, kwa mfano, aliandika katika barua yake aliyomtumia Murad III:

"Kama ambavyo mtangulizi wako Sultan Suleyman alileta maji kutoka katika milima ya Strandzha na kuwaondolea watu kiu, nawe pia unatakiwa kuleta kuni kutoka katika milima ya Bolu na kuigawa kwa watu wako."

"Kama ambavyo mtangulizi wako Sultani Suleyman alileta maji kutoka katika milima ya Strandzha na kuwaondolea watu kiu, nawe pia unatakiwa kuleta kuni kutoka katika milima ya Bolu na kuigawa kwa watu wako."

Aziz Mahmud Hudayi (q.s.)

Dola ya Uthmaniyya, ambayo ilitawala eneo kubwa la dunia na kuacha athari katika historia, ilihakikisha amani na utulivu katika jamii kupitia taasisi za heri. Tajiri kwa masikini, mwenye nguvu au mnyonge, wote waliishi katika undugu wa kiroho. Kupitia taasisi za heri, jamii ya Kiuthmani-

yya ilifikia kiwango cha juu kabisa cha "uadilifu wa kijamii", kiwango ambacho bado kinatafutwa na mataifa mbalimbali katika zama hizi.

Inashangaza kuwa "Riwaya" kama literary genre haikudhihiri mpaka siku za mwisho za Dola hii. Mwandishi wa Kituruki, Cemil Meriç kwa mshangao mkubwa anaelezea sababu ya jambo hilo kama ifuatavyo:

"Katika jamii ya Kiuthmaniyyah hapakuwepo na janga la kutengenezea riwaya."

Hata kama "huruma" imekubaliwa kama moja ya misingi ya Ukristo, taasisi za heri huko Magharibi, ambazo ni alama ya sifa hii, siyo jumuishi kama ilivyo katika ulimwengu wa Kiislamu. Kutokana na maelezo ya mabalozi wa nchi za Magharibi na watendaji katika Dola ya Uthmaniyyah tunapata kuelewa kuwa hata taasisi zilizopo sasa hivi katika nchi za Magharibi zilianzishwa kutokana na ushauri na maoni yao. Maelezo ya balozi mashuhuri wa Kifaransa ni mfano halisi wa kumbukumbu hizi, zinazojumuisha aina hii ya kukiri.

Jambo lingine la kukumbukwa zaidi ni kuwa, Wauthmaniyya walikuwa waangalifu sana kuhakikisha kuwa mtoaji na mpokeaji sadaka hawajuani. Kupitia utamaduni huu, watoaji wa sadaka walilindwa dhidi ya hatari ya unafiki. Kwa kuwa sadaka ziligawiwa kupitia misikiti na vituo vya kiroho, ilisaidia pia kuimarisha hali ya kiroho na ya jamii.

Tunapata kuishuhudia hisia hii katika wakfu iliyotolewa na Sultan Mehmed II:

Sultani Mehmed aliweka kanuni kadhaa za heshima zenye maadili ya kuwasaidia maskini. Alichukua tahadhari hata katika mambo madogo kama vile "kutema mate hovyo." Wakati akiamrisha mgonjwa kulishwa katika nyama ya misitu ya hifadhi, alikataza pia kuwinda katika kipindi cha kuatamia mayai ili kulinda "mizania ya kiikolojia ya mazingira."

"Mimi, Mfunguzi wa Istanbul na mja mnyenyekevu Sultan Mehmed, nimetoa wakfu vipande 136 vya maduka yangu katika eneo la Tslik katika mji wa Istanbul, ambalo nililinunua kwa pesa zangu mwenyewe, kwa masharti yafuatayo:

Kwa mapato ya eneo lililotajwa, nimeteua watu wawili kwa kila mtaa wa Istanbul. Watu hawa watatembea katika kila mtaa na ndoo ya majivu na chokaa, na watafunika mate na makohozi ya watu kwa majivu na chokaa. Watapata akcha 20 kwa huduma yao ya kila siku.

Aidha, nimeteua madaktari 10 maalumu wa upasuaji, madaktari 10 wa kawaida na wauguzi 3 watakaoshughulikia majeraha ya watu. Watakuwa wakitoka katika siku maalumu za mwezi, na watagonga katika kila mlango bila kubagua. Wataangalia kama kuna mgonjwa yeyote, na kama yupo, watamsaidia. Kama hakuna tiba ya ugonjwa, watampeleka mgonjwa husika kwenye hospitali ya Dar –al Ajaza na kutibiwa bila malipo yoyote.

Kwa bahati mbaya kama kutakuwepo na njaa, silaha 100 zitatolewa kwa wawindaji. Watakwenda kuwinda isipokuwa kama wanyama hao watakuwa katika kipindi cha kuatamia mayai na vifaranga katika milima ya Balkan, hivyo wataendelea kumpa chakula mgonjwa.

Aidha, familia za mashahidi waliouawa katika vita na masikini wa Istanbul watapata chakula kutoka katika migahawa ya wakfu yangu. Kama hawawezi kuja mgahawani wao wenyewe, watapelekewa chakula chao wakati wa usiku wa giza pasipo kujulikana na yeyote!..."

Ni vigumu kujua kwa uhakika idadi halisi ya wakfu zilizoanzishwa katika zama za Dola ya Uthmaniyya. Hata hivyo, karibu wakfu zipatazo 26, 300 zimehesabiwa, idadi ambayo tayari ni dalili tosha inayoonyesha jinsi watangulizi wetu walivyokuwa na moyo wa ithaar, yaani uungwana.

Kama inavyoonekana katika wakfu hii, Sultan Mehmed aliweka kanuni kadhaa zenye heshima za maadili ya kuwasaidia masikini. Alichukua tahadhari hata katika mambo madogo kama vile "kutema makohozi." Wakati akiamrisha mgonjwa kulishwa katika nyama ya misitu ya hifadhi, alikataza pia kuwinda katika kipindi cha kuatamia mayai ili kulinda "mizania ya kiikolojia ya mazingira." Mbali na huruma na upendo alikuwa nao kwa watu wake, vilevile alilinda na kutunza ustawi wa wanyama.

Karne tano zilizopita, muda mrefu kabla ya mjadala unaoendelea sasa juu ya "uchafuzi" na "mabadiliko ya ikolojia," utunzaji wa mazingira ulikuwa madhubuti kwa njia rasmi kabisa – huo ukiwa ni mfano adhimu na tunaotakiwa kuuiga kutoka katika historia yetu.

Ugawaji wa chakula kwa familia za mashahidi waliouawa katika vita uliokuwa ukifanywa wakati wa usiku wa giza ni mfano mwingine mzuri unaoonyesha Ikhlasi yao katika kulinda heshima na utu wa watu. Hili pia ni mfano bora kwa vizazi vya baadae.

Vilevile tunahitaji kueleza hapa kuwa kwa kusoma yale yaliyokuwa yakihudumiwa na wakfu inatosha kutuonyesha jinsi watu walivyokuwa wameunganishwa na hisia za huruma na mshikamano katika jamii ya Kiuthmaniyya, wakiishi katika Uislamu kwa maana yake yote.

Fikiria jamii ambayo watu huweka maua mekundu mbele ya nyumba yenye mgonjwa, hivyo watu wanaopita wajue kuwa wanatakiwa kukaa

Ni rahisi kuwafikia maskini ambao wanaeleza shida zao waziwazi. Tunatakiwa kuwatafuta na kuwapata wale wenye aibu mno ya kuelezea shida zao na tuwasaidie kwa siri ili kulinda utu wao.

kimya na kutofanya ghasia, na pia kuheshimu haki za nyumba husika. Kwa kweli, ni vigumu mno kuielezea kwa ukamilifu hisia na ukomavu unaotokana na historia ya Dola ya Uthmaniyya katika kitabu kidogo kama hiki; kwa sasa tunatosheka na mifano tuliyoitaja.

Ni vigumu kujua kwa uhakika idadi halisi ya wakfu zilizoanzishwa katika zama za Dola ya Uthmaniyya. Hata hivyo, karibu wakfu zipatazo 26, 300 zimehesabiwa, idadi ambayo tayari ni dalili tosha inayoonyesha jinsi watangulizi wetu walivyokuwa na moyo wa ithaar.[6]

Kazi iliyofanywa na taasisi za heri zilikuwa na umuhimu mkubwa kihistoria katika nyakati ngumu. Baada ya kupoteza maeneo makubwa ya ardhi huko Rumelia kutokana na kushindwa katika Vita vya Urusi na Uturuki (1877 -1878) na kuwasili kwa mamia kwa maelfu ya wahamiaji katika mji wa Istanbul, wakfu zilifanya kazi kubwa mno zaidi ya Dola na serikali ya Wauthmaniyya katika kuwasaidia. Kwa muda mrefu, taasisi za heri ziliwapatia chakula na makazi. Kadhalika huduma mbalimbali zilitolewa wakati wa miaka ya tabu ya

Fikiria, jamii ambayo watu huweka maua mekundu mbele ya nyumba yenye mgonjwa, hivyo watu wanaopita wajue kuwa wanatakiwa kukaa kimya na kutofanya ghasia, na pia kuheshimu haki za nyumba husika.

6. “Katika Dola ya Uthmaniyyah, pindi mtu anapoanzisha taasisi ya kheri alitakiwa kuandikisha hati ya wakfu wake kwa jaji na kisha kuisajili kwenye ofisi inayohusika na usajili. Hati za wakfu zilizosajiliwa zimewekwa katika hazina ya Vakiflar Genel Mudurlugu mjini Ankara. Kuna hati za wakfu 26,300 katika hazina hiyo. Hata hivyo idadi ya taasisi za kheri zinazokadiriwa kuwepo katika Dola ya Uthmaniyya inaweza kujulikana tu kwa kufanya uchunguzi katika ofisi za usajili za miji.” (Tazama Ziya Kazıcı, Islami ve Sosyal Açıdan Vakıflar, uk. 43-44).

Vita vya Balkan na Vita vya kwanza vya Dunia. Mamilioni ya watu waliweza kuishi tu kwa msaada wa wakfu za kheri za Wauthmaniyya. Mfano wa hivi karibuni tetemeko la ardhi la Marmara, lililotokea Agosti 17, 1999. Kumbukumbu za huduma za kijamii zilizotolewa na wakfu mbalimbali bado ni mbichi kabisa katika akili na nyoyo za taifa letu. Lakini, taasisi za kheri, hazipo tu kwa ajili ya nyakati za majanga bali kwa ajili ya mahitaji ya kudumu ya watu wanyonge. Hii ndiyo kazi ya kwanza na ya msingi ya wakfu.

Kwa hakika, hata katika nyakati za ustawi, wamekuwepo watu ambao hawafikiwi na mikono ya serikali ambao wanahitaji msaada. Daima taasisi za kheri zilianzishwa kwa ajili ya kuwahudumia watu hao. Tunaweza kutumia wakfu mbalimbali za Sokollu Mehmed Pasha kama mfano. Sokollu Mehmed Pasha kwa asili alitokea Serbia na alikuwa Muislamu wa kweli. Alikuwa mmoja katika mawaziri wakuu wenye mafanikio katika utawala wa Wauthmaniyya, ambaye alihudumu katika kipindi cha ustawi wa Dola hiyo. Mtu huyu adhimu alijenga misikiti, mifereji ya maji, vyuo na shughuli nyinginezo, na kuzitoa kama wakfu kwa ajili ya maslahi ya umma.[7] Ni jambo lenye kujenga sana kujifunza anachosema Evliya Celebi kuhusu wakfu wake:

“Wahuzunikie watu watatu: mtu mwenye busara aliye baina ya wajinga, tajiri aliyefukarika na mheshimiwa anayepoteza heshima ya watu.”

7. Mbali na taasisi zake za kheri mjini Rumelia, yeye pia alijenga misikiti miwili mikubwa mjini Istanbul. Msikiti mmoja ni msikiti ulio katika eneo la Azarkapi, ambao una huduma kubwa sana ya maji. Mwingine ni “msikiti wa Shahid Mehmed Pasha”, ulioko katika njia itokayo kwa Sultan Ahmed kwenda Kumkapi.

"...Mgeni akija kutoka mashambani katika nyakati za katikati ya usiku, mfungulieni mlango aingie. Apewe katika chakula kilichoandaliwa. Lakini katika hali yoyote ile msimuache kukaa nje. Lazima apewe malazi wakati wa usiku.

Wakati wa asubuhi, mhudumu ataita kwa sauti kama mpigambiu wa mji:

"Enyi Ummah wa Muhammad! Je mali, uhai, vipandwa na mavazi yenu yamekamilika? Hamhitajii chochote?" wageni wakijibu wote kwa pamoja: "Kila kitu kipo sawa. Mwenyezi Mungu airehemu roho ya mhisani!" basi bawabu afungue mlango wakati wa alfajiri.

Kisha waombeeni dua na muwausieni mkiwaambia, "Kuweni makini! Tembeeni kwa uangalifu! Msisuhubiane na watu wageni! Nendeni na Allah akusaidieni!..."

Mtu mmoja alimuuliza Mtume (s.a.w), "Ni aina gani ya matendo bora katika Uislamu?" Mtume (s.a.w) akajibu, "Kuwalisha (chakula) na uwasalimie wale unaowajua na wale usiowajua" (Bukhari, Kitab al-Iman, 6)

Nukuu ifuatayo kutoka katika wakfu wa Naqb al-Ashraf[8] Esad Efendi unaonyesha huruma na upendo uliokuwa ndani ya moyo wake:

"...Mahitahi yote ya wazee, masikini na wagonjwa wasioweza kujihudumia yashughulikiwe. Vile vile maandalizi ya ndoa za mabinti masikini, walio katika umri wa kuolewa yanunuliwe kwa ajili yao."

Kwa kipindi cha karne nyingi, miradi ya kheri iliyojengwa na watangulizi wetu wenye huruma

8. **Naqib al-Ashraf:** ni jina la cheo walililopewa makarani walioteuliwa na serikali kwa ajili ya kuwahudumia watu wa ukoo wa Mtume (s.a.w).

hayakuwashangaza waandishi waadilifu wa kimangharibi peke yao, bali pia wale ambao mara zote walikuwa wakiandika makala zenye upendeleo dhidi ya Waturuki. Ismail Hami Danismend anatoa mifano kadhaa inayohusu jambo hili katika kitabu chake kiitwacho "Eski Turk Seciye ve Ahlâkı". Kwa mfano, msafiri maarufu Du Loir anaeleza katika kitabu chake cha safari kilichochapishwa mjini Paris:

"Nitaeleza kwa muhtasari desturi na ada za Waturuki kama ifuatavyo: huruma yao haikuwaenea binaadamu peke yao, bali pia wanyama. Kuna nyumba za wageni zijulikanazo kama imaret katika ardhi yote ya Wauthmaniyya. Kutokana na sharti la mtu aliyetoa wakfu, nyumba hizi zinawasaidia watu wenye shida bila kujali dini zao. Wasafiri wanaweza kukaa humo kwa siku tatu na kupata sahani ya chakula kila siku.

Mbali na hizi imaret, vilevile kuna majengo ya umma pembezoni mwa barabara zijulikanazo kama nyumba za wasafiri, ambazo milango yake iko wazi kwa kila mtu.

Baadhi ya Waturuki huweka chemchem za maji kando kando mwa barabara ili kukata kiu za wasafiri. Wengine hujenga chemchem za maji ndani ya miji kwa ajili ya wakazi wake na kuwaajiri wafanya kazi wa kuhudumia watu katika chemichemi hizo.

Matajiri hutembelea magereza, huwatafuta watu waliofungwa kwa sababu ya madeni na kuwakomboa kwa kuwalipia madeni yao. Vile vile wanawatafuta masikini ambao wanaona haya

"Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Na Yeye ni Mwenye nguvu na Mwenye msamaha."
(Qur'an 67: 2)

mno kueleza shida zao na huwasaidia kwa namna ya siri ili kulinda heshima yao."

Corneille Le Bruyn anaandika katika uchunguzi wake kama ifuatavyo:

"Ni ukweli usiokanushika kuwa Waturuki wanapenda mno kazi za kujitolea na za hisani kuliko hata Wakristo. Hii ndiyo sababu kwamba kuna ombaomba wachache mno katika jamii ya Kiuthmaniyya.

... Waturuki ambao hawana pesa za kutosha kutoa sadaka hufanya kazi ili kuwasaidia wengine. Ikibidi watafanya kazi barabarani; watajaza maji kwenye matanki yaliyo kando kando mwa barabara; yanapotokea mafuriko huwasaidia watu kuwaondoa katika maeneo yaliyojaa maji. Wanafanya kazi na huduma nyingi za kijamii, na hawahitaji kulipwa chochote kwa kazi zao hizo. Kwa hali hiyo, wakipewa malipo kwa huduma zao wanazozifanya, hukataa na kusema kuwa yote waliyoyafanya wameyafanya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu pekee."

Katika suala hili, uchunguzi wa Mouradgea d'Ohsson ni wenye kushangaza mno:

"Katika ngazi zote za jamii, wazazi na ndugu hujaribu kuwa mfano mwema kwa watoto wao na kuwazoesha kushiriki katika kazi za kheri. Matokeo ya tabia hizo njema, kama vile ukarimu na huruma, sifa hasi kama vile ubinafsi, ubahili na uroho huondoka na mahala pake huingia tamaa na hisia za kusaidia wengine. Hivyo, Waislamu hawajawahi kukabiliwa na ugumu katika kufanya

"Muislamu anapopanda mti au kulima bustani, kisha ndege, watu au wanyama wakala katika miti hiyo hiyo huhesabiwa kuwa ni sadaka kwa niaba yake."

(Muslim, Musakat, 10)

mambo ya kheri, wameyapita mataifa yote katika suala hili.”

Nukuu ifuatayo inatoka katika barua alioandikiwa baba kutoka kwa mwanawe aliyekuwa akitibiwa katika hospitali ya Waislamu, na kuonyesha jinsi taasisi za kheri zilivyofanikiwa katika kuwahudumia na kuwajali wenye shida.

“Baba yangu mpendwa! Umeniuliza kama ninahitaji pesa. Nitakaporuhusiwa kutoka hospitali, nitapewa suti na vipande vitano vya dhahabu, na hivyo sitohitaji kufanya kazi kwa muda. Kwa sasa huna haja ya kuuza mifugo yako...

Sitamani kutoka hospitali. Vitanda ni laini, shuka ni safi na nyeupe, na blanketi ni kama mahameli. Kuna bomba la maji katika kila chumba. Vyumba vyote huwekwa joto wakati wa usiku wa baridi. Watu wanaotupatia matibabu ni wema na wana huruma mno. Karibu kila siku, wagonjwa wenye siha ya kutosha wanapewa kuku na nyama ya kondoo kama chakula. Mwenzangu katika kitanda cha jirani alijifanya kuwa hajapona ili tu aweze kula kuku watamu waliokaangwa kwa wiki moja zaidi. Lakini daktari mkuu alimtilia shaka na kumruhusu kwenda nyumbani baada ya kumpa mkate na kuku, hali iliyothibitisha kuwa alikuwa na afya njema. Hivyo tafadhali njoo unione kabla hawajanipatia kipande changu cha mwisho cha kuku wa kukaangwa!”

Kwa upande mwingine, ni jambo lenye kustaajabisha kujua kwamba taasisi za kheri 1400 kati ya 26300 zilizothibitishwa zilianzishwa na wanawake. Miongoni mwao ni Nur Banu Valide Sul-

Watoto wetu wanatakiwa kulelewa wakijua kuwa mmiliki halisi wa mali zote ni Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kama tulivyo na wajibu wa kuwafundisha watoto wetu misingi ya dini yetu, ndivyo tunavyowajibika kuwawekea kasumba ya kupenda infaq na kuwazoesha wajibu wa muumini wa kuwasaidia wenye shida.

tan[9] ambaye alikuwa na miradi kadhaa iliyojengwa katika pande zote mbili za Anatolia na upande wa Ulaya wa Istanbul. Msikiti wa Uskudar Atik Valide wenye hoteli ya chakula, chuo, hospitali na bafu ni mfano wa kutajwa. Mwanamke huyu alikuwa Myahudi. Baba yake, Yasef Nassi, alikuwa mmojawapo ya mwanachama mkubwa wa jamii ya Kiyahudi, ambao walilazimika kuhama ili kukimbia mauaji baada Moor kushindwa na majeshi ya Kikristo. Kutokana na kumbukumbu za kihistoria, inaeleweka kwamba Sultan Suleiman Mkuu alimuajiri Yasef Nassi katika huduma za kiintelijensia. Katika zama za utawala wa mtoto wa Kanuni, Sari Selim, Nassi alitenda baadhi ya mambo yaliyokuwa kinyume akajikusanyia mali kwa kutumia cheo cha kuwa baba mkwe wa Sultan. Hata hivyo mfumo ulifanya kazi yake vizuri, maadili na hisia za Uislamu zikaweza kupenya ndani kabisa ya nyoyo. Binti yake Nur Banu Sultan akawa juu ka-

"Enyi mlio amini! Toeni katika tulivyo kupeni kabla haijafika Siku ambayo hapatakuwapo biashara, wala urafiki, wala uombezi. Na makafiri ndio madhaalimu."

(Qur'an, 2: 254)

9. Sifa rasmi iliyokuwa ikiongezwa kwenye majina ya wanawake wa ukoo wa familia ya kifalme ya Uthmaniyyani "Sultan Efendi". Hii ilikuwa na maana kwamba ima baba alikuwa sultan mwenyewe au mmoja wa watoto wa sultan. Iwapo mwanamke huyo akiolewa na mtu wa nje ya ukoo wa kisultan, mabinti wao walikuwa wakiitwa"Hanım Sultan" na watoto wao wa kiume walijulikana kama "Beyzade", wakiwa na mama zao "Sultanzade". Watoto hao wakiolewa au kuoa nje ya ya familia ya kisultan, watoto wao hawakuwa wakihesabiwa katika ukoo wa familia ya kisultan. Kwa upande mwingine, kama mama wa sultan hatokani na familia ya kisultan – jambo ambalo kwa kawaida halikuwepo – basi sifa yao rasmi iliyokuwa ikiongezwa katika majina yao ni "Valide Sultan". Wake wa Masultan walikuwa wakiitwa "Kadın Efendi". Wakiwa zaidi ya mmoja basi nambari ya mpangilio iliwekwa kabla ya sifa rasmi.

bisa miongoni mwa wanawake wa Kiislamu walikuwa mstari wa mbele katika kuanzisha miradi ya kheri.

Mwanamke mwingine mhisani kutoka katika familia ya kisultan ni Mâhpeyker Kösem Vâlide Sultan. Aliweka misingi ya msikiti ujulikanao kama Msikiti Mpya. Alijenga msikiti wa Üsküdar Çinili ukiwa na shule, maji, chuo cha hadith na bafu. Vilevile alijenga msikiti katika makutano ya Anadolu. Taasisi ya Wakfu aliyoianzisha kwa lengo la kuwasaidia masikini na mabinti yatima wapate kuwa na ndoa ni maarufu sana, pamoja na miradi mingine mingi.

Hata Kösem Sultan, ambaye anajulikana kwa hasira na ukali miongoni mwa wanawake wa Kisultan, alichukua nafasi yake miongoni mwa watu waliokuwa na huruma na upendo kutokana na miradi yake ya wakfu. Ingawa aliweka misingi ya Msikiti Mpya, hakuweza kuendelea kuishi ili aukamilishe. Hatice Turhan Sultan ndiye aliyepata bahati ya kuukamilisha. Alikuwa na miradi mingine ya kheri kama vile kujenga shule, vyuo, migahawa ya umma, maktaba na huduma za maji. Inastahili kutaja hapa kuwa alikuwa na sharbati za asali zikitengenezwa wakati wa mwezi wa Ramdhani na mikesha mitukufu na ikigawiwa kwa waumini baada ya Swala ya Magharibi. Hata ubora wa asali hiyo ulisajiliwa katika hati za wakfu. Katika zama hizo, asali bora kabisa ilikuwa ni ile inayotoka katika mji uitwao Atina, ambao baadae jina lake lilibadilishwa na kuwa Pazar. Iliandikwa katika hati ya wakfu kuwa aina hii ya asali inatakiwa kununuliwa bila kujali ni ghali kiasi gani. Hili pia linaonyesha jinsi hisia na uzuri wa huduma

“Muislamu anapopanda mti au kulima bustani, kisha ndege, watu au wanyama wakala katika miti hiyo hiyo huhesabiwa kuwa ni sadaka kwa niaba yake.”

(Muslim, Musakat, 10)

za wakfu zilivyokuwa. Vile vile aliacha rasilimali zenye utajiri mkubwa kwa ajili ya uendelezaji wa huduma za wakfu na kuteua wafanyakazi 116 waliokuwa wakilipwa mshahara kwa ajili ya usimamizi na uendeshaji wa wakfu hizo.

Pertevniyal Valed Sultan alitoa wakfu wa "Masjid Valide" katika mji wa Aksaray na vilevile "Masjid Ya Waduud". Mwanamke huyu pia alijenga maktaba, mradi wa maji na shule.

Mwanamke mwingine ni Mihrimah Sultan. Licha ya silika yake ya unyenyekevu mno, aliaanzisha miradi kadhaa ya kheri, miongoni mwa miradi hiyo ni "Masaajid Salatin" au "miskiti ya familia ya kifalme", ambapo mmoja upo Edirnekapi na mwingine katika mji wa Uskudar. Ufuatao ni mfano mzuri unaoonyesha wema na staha yake. Maji safi yalikuwa yameletwa kutoka Makkah na Arafat na mke wa Harun Rashid aitwaye Zubayda Hanim. Lakini katika utawala wa Sultan Suleiman, njia za maji zilikuwa zimeharibika na kujaa kutu. Mihrimah Sultan alipogundua hali hiyo, alikwenda kwa baba yake Sultan Suleiman na kuomba njia hiyo kongwe itengenezwe kwa siri na msanifu mkuu Sinan. Mihrimah akajitolea mapambo na vito vyake vyote vya madini kwa ajili ya shughuli hiyo. Fundi Sinan baada ya kuweka msingi wa Masjid Suleymaniye akatoweka kwa muda na sababu ya kutoonekana kwake ikawa haijulikani. Miongoni mwa uvumi uliojitokeza ni kuwa amekwenda kushughulikia msingi wa msikiti atakaoujenga. Lakini sababu hasa ilikuwa ni kutengeneza njia za maji zilizojulikana kama "Ayn-i Zubayda,"

"… bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na anawapa mali, kwa kupenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao, na katika ugombozi, na akawa anashika Sala, na akatoa Zaka"

(Qur'an, 2: 177)

na iliendelea kuwa siri kwa sababu mfadhili wa mradi huo ndivyo alivyotaka.

Mwanamke mwingine maarufu wa familia ya kisultani ni Bezmialem Valed Sultan, ambaye aliacha miradi kadhaa ya heri yenye kukumbukwa. Miongoni mwa misikiti aliyojenga, mkubwa kuliko yote ni Masjid Valide, ulio jirani na kasri ya Dolmabahce. Daraja maarufu la Galata nalo pia ni miongoni mwa miradi yake mingi ya wakfu.

Wakfu wake ulioasisiwa mjini Damascus nao pia ni muhimu sana. Haya hapa ni masharti mawili ya wakfu wake:

- *Kubeba maji safi kutoka Damascus kuwapelekea mahujaji*

- *Kufidia vyombo vitakavyovunjwa na wafanyakazi wa ndani ili kulitia utu na heshima yao.*

Mradi mwingine bora kutoka kwa mwanamke huyu Bezmialem Valide Sultan ni *Hospitali* ya Guhraba-i Muslimin iliyojengwa kwa ufadhili mkubwa kutoka katika mali yake mwenyewe. Mradi huu ulianza kutoa huduma zake pamoja na msikiti na chemchem ya maji mwaka 1843 na mpaka sasa umeendelea kutoa matibabu kwa watu masikini katika ummah wa Kiislamu.

Wake na mabinti wa masultani waliweka umuhimu wao mkubwa katika maji na kuanzisha miradi mbalimbali katika maeneo yote ya Makkah, Arafat na Istanbul. Walijenga mifereji- daraja ambayo imeendelea kuwepo mpaka sasa, wakakarabati njia za maji na kuupatia maji tele mji wote wa Istanbul.

Matajiri wenye kushukuru na maskini wenye subira na kujiheshimu wote kwa pamoja wanastahili heshima ya ubinadamu na radhi za Mwenyezi Mungu.



Mtu mwingine wa kheri katika historia yetu ya hivi karibuni, ni Abdulhamid Khan wa pili. Miradi yake ya maji ijulikanayo kama “Hamidiye fountains” bado ni miongoni mwa maji bora ya chemchem.

Watangulizi wetu, kwa Ikhlasi kubwa, walianzisha miradi mingi ya kheri, ambayo walikuwa wakiomba dua iendelee kutoa huduma mpaka Siku ya Kiyama. Miradi hii siyo tu kwamba ilihudumia mahitaji ya watu katika zama hizo, bali mingi miongoni mwake bado inaendelea kutoa huduma na itaendelea kukisaidia kizazi cha sasa katika kila uwanja wa huduma za ustawi na maendeleo. Miradi hiyo ni athari na alama ya imani, heshima na sadaka yenye kuendelea ya watangulizi wetu wa Kiuthmaniyya ambayo daima watakumbukwa kwayo.

Ewe Mwenyezi Mungu! Tujaalie kuwa miongoni mwa Waislamu waliojitoa kwa dhati, ambao huwahudumia viumbe kwa ajili ya mapenzi kwa Muumba wao na ambao huchunga amana Zako kihalali na moyo wa dhati.

Amin!

Mtukufu Mtume (s.a.w) alieleza kuwa utajiri na ukwasi wa kweli sio wingi wa mali bali ni utajiri wa moyo.

Kutoka katika kilele cha ustaarabu wa Kiislamu

"Sadaka na njia zake"

Sura ya pili

-Sababu za kupata Rehema na Baraka katika Dunia na katika Akhera -

ZAKA NA INFĀQ

A. *ZAKA*

Wanadamu ndiyo viumbe bora na wenye kuheshimika zaidi miongoni mwa viumbe wote. Tofauti zinazopatikana miongoni mwa wanajamii kama vile mwenye nguvu na mnyonge, mwenye afya na mgonjwa, mwenye elimu na mjinga, tajiri na masikini ni mambo yanayohakikisha amani na maelewano katika jamii.

Mali na umasikini ni ngazi mbili muhimu na sifa mbili tofauti za makundi ya kiuchumi na kijamii. Kwa kweli, hali ya kuwa tajiri au masikini ni nyenzo za majaribu na mitihani katika ulimwengu huu. Kuwa bora, na mali haina maana ya kuwa na umasikini siyo sababu ya uduni. Hali zao (za ubora) hupimwa na kuangaliwa kulingana na mwenendo na tabia ya tajiri na masikini. Mwenyezi Mungu ndiye kaweka utajiri na umasikini kwa hekima Yake ya Kimungu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

Na wapewe mafakiri walio zuilika katika njia za Mwenyezi Mungu, wasio weza kusafiri katika nchi kutafuta riziki. Asiye wajua hali zao huwadhania kuwa ni matajiri kwa sababu ya kujizuia kwao. Utawatambua kwa alama zao; hawang'ang'anii watu kwa kuwaomba. Na kheri yoyote mnayo toa, basi kwa yakini Mwenyezi Mungu anaijua."

(Qur'an, 2: 273)

“Kwani wao ndiyo wanaogawa rehema za Mola wako Mlezi? Sisi tumewagawanyia baina yao maisha yao katika uhai wa duniani, na tukawanyanyua baadhi yao juu ya wengine kwa daraja nyingi; kwa hivyo baadhi yao wanawafanya wengineo wawatumikie. Na rehema za Mwenyezi Mungu ni bora kuliko hayo wanayoyakusanya.” (Qur’an, 43: 32)

Kama ilivyoelezwa katika Aya hii, Mwenyezi Mungu amegawa tofauti kwa kila mtu. Kwa upande mwingine, kila mtu ana dhima kulingana na baraka na neema alizojaaliwa na Mwenyezi Mungu. Kwa namna hii uwiano wa kijamii na uadilifu wa Mwenyezi Mungu hupata kuonekana kwa maana yake kamili.

Waislamu wamefaradhishiwa kutoa Zaka ili kuzuia uwezekano wa matajiri kuwaonea masikini kutokana na neema ya mali na ili kuzuia masikini wasiwachukie na kuwaonea husuda matajiri. Inahakikisha amani na utulivu katika jamii na kuwafanya wanajamii wawe na mafungamano na mshikamano. Kwa kupunguza tofauti za kiuchumi baina ya tajiri na masikini, mpangilio wa kiuchumi na wa kijamii wa Uislamu unalenga kuzuia tofauti hizi zisigeuke kuwa mgogoro wa kijamii. Hivyo katika Uislamu msisitizo mkubwa umewekwa juu ya utoaji zaka na sadaka.

Matajiri wenye kushukuru na maskini wenye subira na kujiheshimu wote kwa pamoja wanastahili heshima ya ubinadamu na radhi za Mwenyezi Mungu.

Tajiri ataulizwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kuhusu namna alivyozichuma na kuzitumia mali zake. Ataulizwa iwapo alizichuma kwa njia za halali au haramu, na iwapo alitekeleza wajibu wake wa kutoa zaka na sadaka. Anatahiniwa

kwa mali zake. Ni pale tu atakapofaulu mtihani huu, pamoja na mitihani mingine, ndipo atakapopata radhi za Mwenyezi Mungu na baraka za peponi.

Na masikini naye ataulizwa juu ya ukosefu wa subira, malalamiko, kuwa mzigo kwa wenzake, kuombaomba kusikokuwa kwa lazima, ulafi, husuda, uasi na iwapo alichunga wajibu wa maadili ya mtu masikini. Kama yatastahili radhi za Mwenyezi Mungu, basi mateso ya mtu huyo hapa duniani atageuka kuwa baraka za milele huko Akhera.

Zaka imetajwa ndani ya Qur'an Tukufu mara ishirini na saba sambamba na swala, jambo ambalo linatosha kuonyesha umuhimu wake. Katika surat Mu'minuun, Aya ya 2 na ya 4, ambapo swala imetajwa peke yake, imeelezwa kuwa Waislamu wanaoswali ni wale ambao wanatoa Zaka. Hii ni kwa sababu swala ndiyo ibada ya kwanza inayotekelezwa kimwili, ambapo Zaka ndiyo ibada ya kwanza inayotekelezwa kwa kutoa mali. Ingawa muumini ataulizwa kila amali ya ibada kwa peke yake, kwa maneno mengine kutoitekeleza moja wapo hakutoiathiri nyingine, lakini Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema:

"Hakuna faida katika swala za wale wanaoswali bila kulipa Zaka zao"(Haythami, Majma' al-Zawaid, III, 62). Hakuna shaka yoyote kwamba hadith hii inawahamasisha Waislamu kutoa Zaka na kuwaonyesha umuhimu wake.

Mtukufu Mtume (s.a.w) alieleza kuwa utajiri na ukwasi wa kweli sio wingi wa mali bali ni utajiri wa moyo.

Kutokana na umuhimu wake mkubwa, kiongozi wa Waumini, Abu Bakr (r.a) aliwachukulia wale waliokataa wajibu wake kuwa ni makafiri, na

akatangaza vita dhidi yao. Kwa sababu Zaka ni deni la matajiri wanalodaiwa na masikini ambalo limeamriwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Qur'an Tukufu inasema:

وَفِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ لِّلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ

"Na katika mali yao ipo haki ya mwenye kuomba na asiyeomba" (Qur'an, 51: 19)

Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) anasema:

"Unapolipa Zaka yako unatekeleza sehemu ya wajibu wako (yaani haki ya masikini iliyo juu yako."

Kwa hali hii, Zaka ina maana ya mtu kutoa sehemu ya mali yake kuwapa watu maalum walioainishwa na Shariah, pale ambapo mali yake inapovuka kiwango maalumu. Kwa kutoa Zaka, mali iliyobaki huhalalika. Pesa au mali inayokusanywa kama Zaka hugawanywa kwa masikini katika jamii kulingana na viwango vya umasikini wao, hali inayoleta usawa, uadilifu na maelewano ya kijamii na kuitakasa mali ya tajiri.

Mali inapokuwa imechumwa kwa njia za halali, basi huwa halali kwa mmiliki wake. Lakini, Zaka, ambayo ni haki ya masikini, isipolipwa, mali hiyo haitakuwa halali kikamilifu. Kwa upande mwingine, kama mali imechumwa kwa njia haramu, basi hata kama ikitolewa Zaka haiifanyi kuwa halali. Kwa mfano, kushinda fedha kwa mchezo wa kamari au kwa njia nyingine isiyokuwa halali hakuifanyi fedha hiyo iwe halali.

Wanadamu ndio viumbe bora na wenye kuheshimika zaidi miongoni mwa viumbe wote. Tofauti zinazopatikana miongoni mwa wanajamii kama vile mwenye nguvu na mnyonge, mwenye afya na mgonjwa, mwenye elimu na mjinga, tajiri na maskini ni mambo yanayohakikisha amani na maelewano katika jamii.

Hekima ya Zaka kwa mtu mmoja na kwa Jamii

Faida na manufaa ya *Zaka* kwa wale wanaoitoa ni kubwa zaidi kuliko faida zake kwa masikini. kwa kweli Zaka, ambayo ina maana ya "usafi" na "utakaso", ina faida muhimu mno kama vile kuponya baadhi ya maradhi ya moyo na kuutakasa dhidi ya uovu na kuisafisha mali. Kuzitakasa nafsi ni miongoni mwa hekima za kuletwa Mitume na Manabii.

Tunapoyachambua maneno *"Zakat"* na *"infaq"*, tunagundua kuwa hekima ya msingi ya amali hii ya ibadani kuzitawala maada za kidunia na kuiokoa nafsi ya mwanadamu isitiwe utumwani na mali.

Vile vile inaimarisha uhusiano wa upendo na moyo wa dhati baina ya mtoaji na mpokeaji. *Zaka* ni kiwango cha chini anachopewa masikini. Aidha, Waislamu wenye imani kamili huzipamba mali zao kwa sadaka, infaq na ithaar (yaani kutanguliza mahitaji ya watu mbele ya mahitaji yako).

Pamekuwepo na mgogoro baina ya matajiri na masikini katika kipindi chote cha historia, hasa hasa masikini kuwachukia na kuwafanyia husuda matajiri, na matajiri kuwanyanyapaa masikini kwa sababu ya shida zao. Lakini hali hii haitokei pale ambapo sifa adhimu kama vile ithaar, huruma, upendo na undugu zinaonyeshwa katika maisha ya kijamii kwa njia mbalimbali za sadaka. Kwa mtazamo wa Uislamu, masikini hawahesabiwi kama tabaka linalotakiwa kudharauliwa, bali ni tabaka linalohitaji na kustahili heshima na upendo. Uisla-

"Mwenyezi Mungu anausaidia umma huu kwa sababu ya maombi, dua, na ikhlas ya wanyonge wao."

(Nasai, Jihad, 43)

mu unakwenda mbali zaidi na kuwachukulia kuwa chanzo cha baraka na ustawi. Katika Aya ifuatayo, Mwenyezi Mungu Mtukufu anamuamrisha Mtume (s.a.w) kushikamana na maswahaba masikini na kuwapa uangalizi:

"Na isubirishe nafsi yako pamoja na wanaomuomba Mola wao Mlezi asubuhi na jioni, hali ya kuwa wanataka radhi yake. Wala macho yako yasiwaruke kwa kutaka pambo la maisha ya dunia. Wala usimtii tuliyemghafilisha moyo wake asitukumbuke, na akafuata matamanio yake yakawa yamepita mpaka." (Qur'an, 18: 28)

Vile vile katika hadith ifuatayo ya Mtume (s.a.w) imeelezwa kuwa masikini ni sababu ya baraka na ustawi:

Abu al-Darda (r.a) anasimulia kuwa Mtume (s.a.w) anasema: *"Niitieni watu wanyonge! Kwa maana mtaruzukiwa na kusaidiwa kwa (maombi na baraka za) wanyonge wetu."* (Bukhari, Jihad, 76)

Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema:

"Mwenyezi Mungu anausaidia umma huu kwa sababu ya maombi, dua, na Ikhlas ya wanyonge wao." (Nasai, Jihad, 43)

Kwa mujibu wa riwayah ya Umayya bin Khalid (r.a), Mtume (s.a.w) alikuwa akimuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu awape ushindi Waislamu kwa ajili ya watu masikini. (Tazama Tabarani, Mujam al-Kabir,I, 292)

Iwapo watu wote wangetoa Zaka zao kikamilifu, ni dhahiri kuwa idadi ya masikini na mafakiri

"Na toeni katika tulicho kupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, tena hapo akasema: Mola wangu Mlezi! Huniakhirishi muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema?"

(Qur'an, 63: 10)

katika jamii ingepungua sana. Katika zama za utawala wa Omar bin Abd al-Aziz magavana walimpa taarifa Khalifa kuwa "hawakupata mtu wa kumpa Zaka", na wakataka ushauri wake wafanye nini. Sababu ni kuwa matajiri walikuwa wakitoa Zaka zao kikamilifu. Hali hii ya jamii ni ishara ya kutoa mali na nafsi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Wakati mwingine Omar bin Abd al-Aziz alimuajiri mtu atangaze:

"Wako wapi wadeni? Wako wapi wenye shida, yatima, masikini wanaotaka kuoa, wako wapi mafakiri? Wenye haki na masikini! njooni mchukue haki zenu." Nguvu ya kimaanawi iliyosababisha mafanikio ya Omar bin Abd al-Aziz haiwezi kusahaulika. Baada ya kufanya tathmini kuhusu ulimwengu wake wa kiroho, kwa namna moja, kunaonyesha sababu za mafanikio makubwa yaliyopatikana wakati wa utawala wake.

Mkewe, Fatimah, anasimulia:

"Siku moja nilikwenda mbele ya Omar bin Abd al-Aziz. Alikuwa amekaa msikitini, akilia na machozi yakitiririka kwenye mashavu yake. Nikamuuliza tatizo la kilio chake, akasema:

"Ewe Fatimah! Nimebeba mzigo wa umma huu mabegani mwangu. Watu wenye njaa, masikini, wagonjwa wasioweza kupata dawa, wenye shida wasiokuwa na mavazi ya kuvaa, mayatima, wajane walioachwa pekee yao, mafakiri wasioweza kupata haki zao, mateka na Waislamu waliolazimishwa kuishi katika ardhi za makafiri, vikongwe na wazee wasiokuwa na nguvu za ku-

"Ukitaka kuulainisha moyo wako, wape chakula maskini, vipapase vichwa vya mayatima..."

(Ahmad bin Hanbal, Musnad, II, 263)

fanya kazi ili kukidhi mahitaji yao, masikini wenye familia ambao wanawajibika kuzihudumia familia zao zenye watu wengi... ninahisi kuelemewa pale ninapofikiria ndugu hawa walio karibu na wale walio mbali. Kesho nitamjibu nini Mola wangu atakaponiuliza? Mtume wa Mwenyezi Mungu akinihoji nitamjibu nini?" (Ibn Kathir, Tafsir, IX, 201)

Maneno yaliyosimuliwa na mke wa Omar bin Abd al- Aziz yanapaswa kuwa katika akili na moyo wa kila Muumini. Njia ya kuupamba moyo wa muumini kwa huruma, upendo, upole na kujali inapatikana kwa kuitoa nafsi na mali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mtukufu Mtume (s.a.w) alimuusia swahaba mmoja aliyelalamika kuhusu ugumu wa moyo wake:

"Ukitaka kuulainisha moyo wako, wape chakula masikini, vipapase vichwa vya mayatima..." (Ahmad bin Hanbal, Musnad, II, 263)

Mawlana (q.s) anasema kuhusu faida za kiroho na kimaanawi zinazopatikana kwa kuwajali masikini na wenye shida:

"Roho zilizozama katika umasikini na shida ni kama nyumba iliyojaa moshi. Ufungulie dirisha moshi huo uliojaa nyumba kwa kusikiliza mahitaji yao na kuwapatia tiba, hivyo moshi wake utaondoka, na moyo na roho yako vitalainika..."

"Bila kuangalia kiasi cha mali ambacho mtu anamiliki, ni katika asili binadamu kutaka zaidi, kuwa na uchoyo na tamaa. Lakini Waislamu ambao wana mazoea ya kutoa Zaka wana nyoyo zenye ukarimu."

Wakati Uislamu umeonyesha njia ya kupatanisha masuala mbalimbali kuhusu masikini na matajiri kwa njia iliyo nzuri, mifumo isiyokuwa ya Kiislamu imeshindwa kufikia lengo hili, na zimeyatia chumvi na kuyapigia chuku kwa namna moja

au nyingine. Baadhi ya mifumo imepiga marufuku kabisa kuwaomba watu, na mifumo mingine imeruhusu moja kwa moja. Uislamu, kwa upande mwingine, umelishughulikia suala hili la kijamii kwa njia ya hekima na kutoa tiba mujarrabu kupitia *Zaka na infaq.*

Zaka ni katika tunu muhimu mno ambazo Uislamu umempatia binaadamu. Kwa msaada wa Zaka, shida za masikini, msafiri, yatima na wajane hupata kushughulikiwa. Uislamu ndiyo dini iliyoondosha minyororo ya utumwa katika shingo ya mwanadamu. Hakuna shaka yoyote kuwa, suluhisho jingine lililotolewa na Uislamu ili kuwakomboa na kuwatunza watumwa ni wale wenye watumwa kuwapa watumwa wao kiwango cha maisha wanayoishi wao wenyewe. Kutokana na amri hizo, matokeo yake ikawa kwamba badala ya utumwa kuwa faida ukawa mzigo mkubwa kwa wale wanaowamiliki. Uislamu uliwahamasisha wale wenye watumwa kuwaacha huru kwa sababu mbalimbali. Wakati mwingine katika hatua ya awali Uislamu ukaeleza kuwa fidia ya dhambi ni kumuacha huru mtumwa.

Uislamu unawasaidia watu wenye shida bila kutarajia malipo yoyote na kuyaponya majeraha yao. Uislamu pia umeharamisha riba ambayo ikiangaliwa kwa nje inaonekana kuwa jambo jepesi, lakini katika hali halisi ni kuwafanyia dhuluma watu walio katika shida kubwa. Kwa sababu mla riba anataka wengine wawe katika taabu na kufaidika na matatizo yao. Ruhusa ya kuwapa Zaka wale wanaodaiwa ni moja ya tahadhari za kuwalinda watu wenye madeni wasiangukie katika

“Zaka ni katika tunu muhimu mno ambazo Uislamu umempatia binadamu. Kwa msaada wa Zaka, shida za maskini, msafiri, yatima na wajane hupata kushughulikiwa.”

bwawa chafu la riba. Watu wanaotoa Zaka hushirikiana na masikini katika matatizo yao. Nia yake ya pekee ni kuwasaidia wenye shida kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Bila kuangalia kiasi cha mali ambacho mtu anamiliki, ni katika asili ya binadamu kutaka zaidi, kuwa na uchoyo na tamaa. Lakini Waislamu ambao wana mazoea ya kutoa Zaka wana nyoyo zenye ukarimu. Huridhika na kile kidogo wanachokimiliki, wakati ambapo mla riba hutaka kuongeza mali yake kwa kuwahatarisha na kuwanyonya wengine. Ni rahisi kuona hali kama hiyo katika karibu kila kituo cha biashara ulimwenguni. Aya Tukufu inasema:

يَمْحَقُ اللهُ الرِّبٰوا وَيُرْبِي الصَّدَقَاتِ

"Mwenyezi Mungu huiondolea baraka riba, na huzibariki sadaka..." (2: 276)

Kwa maneno mengine, Mwenyezi Mungu huondoa baraka katika mali ya mla riba. Hali hii ya mla riba isiyokuwa na baraka ina maana ya kuwa muflisi katika Akhera. Wakati mwingine hali hii ya kuwa muflisi yaweza kutokea hapa hapa duniani, na kiasi kikubwa cha mali kinaweza kupotea baada ya maradhi au janga; au inaweza kuangukia mikononi mwa mrithi mbadhirifu.

"Waja wa Mwenyezi Mungu wenye busara kamwe hawasahau kwamba "kutakuwa na kuulizwa kwa kile cha halali, na kutakuwa na kuadhibiwa kwa kile cha haramu."

Siri nyingine inayopatikana ndani ya Zaka na infaq ni kuzuia mkusanyiko wa mali katika mikono ya wachache, na kuzuia masikini kunyonywa, hivyo kuepusha chuki dhidi ya wale wenye ukwasi. Mali ikiwa nyenzo ya ufahari na kiburi, hatima ya tajiri huwa mbaya mno na yenye kusikitisha.

Ikumbukwe kuwa wanajamii wote, tajiri kwa masikini, wanahitajiana kiroho na kimaada. Mpangilio na nidhamu hii ya Mwenyezi Mungu ina mafunzo mengi na hekima ndani yake.

Katika Uislamu, mali zote ni milki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kumiliki mali katika dunia hii ni kama kubadilishana muda. Ikifika muda fulani, kila mwanadamu anatakiwa kuzikabidhi mali zake kwa wengine kabla hajaondoka katika huu ulimwengu.

Ukweli huu umeelezwa katika aya ifuatayo:

يَا أَيُّهَا النَّاسُ أَنْتُمُ الْفُقَرَاءُ إِلَى اللهِ
وَاللهُ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ

"Enyi watu! nyinyi ndiyo wenye haja kwa Mwenyeezi Mungu na Mwenyeezi Mungu ndiye Mkwasi, Mwenye kusifiwa." (Qur'an, 35: 15)

وَلِلَّهِ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالأَرْضِ
وَاللهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

"Na Ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu." (3: 189)

kama Aya hizo zinavyoaonyesha, mali siyo milki ya mtu mmoja wala jamii. Kwa hakika mali ni milki ya Mwenyezi Mungu. Kwa maana binadamu wanaishi ndani ya mamlaka ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na wanaishi kwa riziki Yake. Kitu pekee walichopewa wanadamu ni haki ya kutumia mali kwa muda.

"Kwa hakika mali ni milki ya Mwenyezi Mungu. Kwa maana binadamu wanaishi ndani ya mamlaka ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na wanaishi kwa riziki Yake."

Mshairi mmoja analielezea hili kama ifuatavyo:

Binadamu wote ni wasafiri; dunia ni nyumba ya wageni
Hakuna wakazi; jumba hilo la ajabu
Mali ya mwisho itakuwa sanda kwa shah na kwa masikini
Sasa ni wapi hao wanaojivuna na hilo, kama siyo wendawazimu

Mali, utajiri na vyeo ni miongoni mwa mitihani migumu mno kwa binadamu. Muda ulifika ambapo utawala mkubwa wa Sulaiman (a.s) uliondolewa mikononi mwake, ulirudishwa baada ya kuwa ametubu. Rafiki mmoja wa Mwenyezi Mungu, ambaye alijifunza kutokana na tukio hili na mfano wake, anasema:

"Usiikimbilie riziki, bali mkimbilie Mwenye kuruzuku!"

Mwisho wenye kutisha kwa wale wanaopuuza kutoa Zaka

Kama tulivyoeleza hapo kabla, mali ni amana ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu amewakabidhi waja wake. Inapotumika kinyume na maamrisho ya Mwenyezi Mungu, inabadilika kiurahisi na kuwateka nyara wanadamu na kuwatumbukiza kwenye kiburi, uonevu na dhulma. Mapenzi ya kupenda mali huweka makazi ndani ya nyoyo za wale wanaokumbwa na janga hili. Sababu ya Mwenyezi Mungu kusema kuwa mali na watoto ni "fitnah (mtihani)" inatokana na hatari kwamba vitu hivyo vinaweza kupenya moyoni na kubadilika

"Usiikimbilie riziki, bali mkimbilie Mwenye kuruzuku!"

kuwa masanamu. Mwenyezi Mungu anawaonya wale wanaojitumbukiza katika msiba huu:

"Enyi mlioamini! Hakika wengi katika makuhani na wamonaki wanakula mali za watu kwa ubatili na wanazuilia Njia ya Mwenyezi Mungu. Na wanaokusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wabashirie habari ya adhabu iliyo chungu. Siku zitapotiwa moto katika Moto wa Jahannamu, na kwanza vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao, wakaambiwa: Haya ndiyo mliojilimbikia nafsi zenu, basi onjeni mliyo kuwa mkilimbika." (Qur'an, 9: 34-35)

Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema:

"Hakuna siku inayompitia mwanadamu ila hutembelewa na malaika wawili. Malaika mmoja husema: Ewe Allah, mzidishie yule anayetoa (kwa ajili ya Mwenyezi Mungu), na mwingine husema: Ewe Allah, mletee maangamizi yule anayejizuilia kutoa."

Katika hadith nyingine, Mtume (s.a.w) anawapa ishara njema wale wanaolipa zaka, moja ya kumi, na kutoa sadaka, na anatoa onyo kali kuhusu wale wanaoendelea kuwa viziwi kwa kufanya ubakhili:

"Ukarimu ni mti kutoka mbinguni, mizizi yake ipo peponi na matawi yake yapo duniani. Wale wenye ukarimu miongoni mwenu watakaoshikamana na tawi moja katika matawi hayo litampeleka peponi. Ubakhili ni mti ambao mizizi yake ipo motoni

Mali zote ni milki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kumiliki mali katika dunia hii ni kama kubadilishana muda. Ikifika muda fulani, kila mwanadamu anatakiwa kuzikabidhi mali zake kwa wengine kabla hajaondoka katika huu ulimwengu.

na matawi yake yapo duniani. Yule atakayeshika tawi moja katika matawi yake kwa kuwa mbakhili, litampeleka Motoni." (Bayhaki, Shuab al-Iman, VII, 435)

Kwa maneno mengine, katika Aya hizo za Qur'an na hadith za Mtume (s.a.w), inaelezwa kuwa pindi mapenzi ya kupenda mali yanapouvamia moyo na pindi haki za masikini zinapodhulumiwa, basi utatokea mwisho wenye kusikitisha. Waumini wanatakiwa kutafakari kuhusu maonyo ya Mwenyezi Mungu na kufanya jitihada za kutoa sadaka sambamba na asilimia 2.5 ya wajibu inayotakiwa kutolewa kama zaka kutoka katika pato la mtu husika. Kuhusu suala hili, Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaongoza waja wake kama ifuatavyo:

"...Na wanakuuliza watoe nini? Sema: Kilicho chepesi..." (Qur'an, 2: 219)

Maswahaba (r.a) walikuwa wakishindana kutoa sadaka. Omar (r.a) alitoa nusu ya mali yake kwa ajili ya vita vya Tabuk wakati Abu Bakr (r.a) akitoa mali yake yote. Mtume (s.a.w) alipomuuliza:

"Umewaachia nini familia na watoto wako?"

Akajibu:

"Mwenyezi Mungu na Mtume Wake" (Abu Dawud, Zakat, 40)

"Tena bila ya shaka mtaulizwa siku hiyo juu ya neema."

(Qur'an, 102: 8)

Tukio lifuatalo baina ya Sheikh Shibli na mwanafiqhi mmoja ni lenye mafunzo sana.

Mwanafiqhi (mwanasheria) alimuuliza Sheikh Shibli (q.s) kiasi cha mali kinachotakiwa kutolewa sadaka, ili kumjaribu. Sheikh Shibli akasema:

“Ungependa nikujibu kwa mujibu wa wanafiqi au marafiki wa Mwenyezi Mungu?”

Mwanafiqhi akasema:

“Kwa mujibu wa wote”

Shibli akajibu:

“Kwa mujibu wa wanafiqhi, mtu anatakiwa kutoa dirham 5 katika dirham 200 baada ya kupitiwa mwaka. Kwa mujibu wa utaratibu wa marafiki wa Mwenyezi Mungu, mtu anatakiwa kutoa dirham zote 200 na kisha atamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumuokoa.”

Mwanafiqhi akasema:

“Tumejifunza kanuni za zuo letu (kutoa asilimia 2.5 ya mali) kutoka kwa wanazuoni wetu.”

Shibli akajibu:

“Tumejifunza utaratibu wetu kutoka kwa Abu Bakr as-Sidiq. Alitoa kila alichokuwa nacho na kumpa Mtume wa Allah.

Mtume wa Allah, ambaye aliwapandikizia maswahaba wake mapenzi ya kupenda kutoa sadaka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, walitoa mfano bora wa kujitolea.

Siku moja familia ya Mtume (s.a.w) ilichinja kondoo na kuigawa nyama yake kwa watu. Mtume (s.a.w) akauliza: “Je kuna nyama iliyobaki?”

Aisha (r.a) akasema:

“Ni mfupa wa bega tu ndio tuliobaki nao”

“Ukarimu ni mti kutoka mbinguni, mizizi yake ipo peponi na matawi yake yapo duniani. Wale wenye ukarimu miongoni mwenu watakaoshikamana na tawi moja katika matawi hayo litampeleka peponi. Ubakhili ni mti ambao mizizi yake ipo motoni na matawi yake yapo duniani. Yule atakaye shika tawi moja katika matawi yake kwa kuwa mbakhili, litampeleka Motoni.”

(Bayhaki, Shuab al-Iman, VII, 435)

"Kama ni hivyo nyama yote tumebaki nayo isipokuwa mfupa wa bega!" (Tirmidhi, Sifat al-Qiyama, 35)

Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa haoni raha kukaa na vipande vya dhahabu nyumbani mwake na angezitoa sadaka haraka sana. Lakini, hakuwa akitarajia kila mtu kufanya hivyo; alikuwa akiwashauri na kuwaelekeza maswahaba wake kufanya kadri ya uwezo wao. Kwa mfano, wakati akiikubali mali yote ya Abu Bakr kama sadaka, alimwambia swahaba mwingine:

"Bakisha baadhi ya mali yako kwa ajili yako, hiyo ni bora kwako"

"Kwa hakika khofu yangu ni kuwa mtapewa mali za kidunia kwa wingi kama walivyopewa wale waliokuwa kabla yenu, na mtaanza kushindana kwa ajili ya mali hiyo kama walivyofanya, na kisha itawazuieni (kufanya wema) kama ilivyowazuia."

(Tazama, Muslim, Zakat, 121; Bukhari, Riqaq, 7)

Kwa maneno mengine, Uislamu umekiacha kiwango cha sadaka ya hiyari tofauti na kiwango cha wajibu cha Zaka katika uamuzi wa mtu husika. Katika kufanyia kazi msingi huu, Abu Dhar (r.a) asingekubali kuacha kiasi kilichozidi katika mali yake mpaka siku ya pili, wakati Abdurrahman bin Awf (r.a) aliona kuwa inafaa kuweka akiba kiasi cha mali kwa ajili ya mahitaji ya baadae. Kwa upande mwingine alikuwa akifanya kazi sana ili kuzidisha kipato na kwa upande mwingine alifanya kila awezalo kupunguza matatizo ya Waislamu wenzake. Angewalisha wengine ilhali yeye amekabwa na njaa. Kwa sababu, yeye na maswahaba wengine kama yeye ni watu waliokuwa wamezipamba nyoyo zao kwa kujua kuwa wao ni mawakala tu wa mali waliyopewa kama amana na Mwenyezi Mungu.

Matajiri wote wanataka wokovu wa milele wanatakiwa kuishi katika ulimwengu huu wakijua kwamba wao ni mawakala tu na wataulizwa na

mmiliki halisi wa mali walizonazo, yaani Mwenyezi Mungu Mtukufu. Aya tukufu inasema:

ثُمَّ لَتُسْأَلُنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيمِ

"Tena bila ya shaka mtaulizwa siku hiyo juu ya neema." (Qur'an, 102: 8)

Kwa sababu ya ukweli huu, waja wa Mwenyezi Mungu wenye busara kamwe hawasahau kwamba "kutakuwa na kuulizwa kwa kile cha halali, na kutakuwa na kuadhibiwa kwa kile cha haramu."

Ndiyo maana kwamba matajiri ambao wamekuwa watumwa wa tamaa zao zisizokuwa na kikomo na wasiotoa sadaka ni wabebaji wa kuni za tanuru lao wenyewe.

Kufanya kazi na kupata mali kwa njia za halali ni jambo ambalo Uislamu unalihamasisha na kulishajiisha, maadamu mali hizo hazitogeuka kuwa sanamu katika nyoyo na zikatumiwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Vinginevyo, mali hugeuka kuwa mzigo katika dunia hii na sababu ya kupata adhabu kali huko Akhera.

Lengo sahihi la mali ni kuifikia maana ya hadith isemayo "mtu bora miongoni mwenu ni yule anayewafaa watu." (Suyuti, al-Jami' al-Saghir,II,8). Pesa zinatakiwa kukaa mfukoni, siyo moyoni. Tungo zifuatazo za mshauri mmoja mwenye busara zinaelezea kwa uzuru ukiziwi na hali ya kughafilika kwa watu:

Dunia ni nyumba ya wageni
Ndani yake, makasri na magofu

Siku moja familia ya Mtume (s.a.w) ilichinja kondoo na kuigawa nyama yake kwa watu. Mtume (s.a.w) akauliza: "Je kuna nyama iliyobaki?" Aisha (r.a) akasema: "Ni mfupa wa bega tu ndio tuliobaki nao" "Kama ni hivyo nyama yote tumebaki nayo isipokuwa mfupa wa bega!"

(Tirmidhi, Sifat al-Qiyama, 35)

yanafanana
Nimezama katika upendo mkubwa wa kuipenda hii dunia
Nimejenga nyumba katika nyumba ya wageni

Ieleweke kuwa maombi na dua za wanyonge na masikini ni chanzo cha amani ya wale wenye nguvu na kwa wakwasi. Maombi yao pia ni msaada wa kiroho kwa matajiri. Ieleweke kuwa umasikini na ufukara siyo fedheha na uduni, vitu hivyo vinaweza kuwa ishara ya baraka na hekima huko Akhera.

Matajiri wenye kushukuru na masikini wenye subira na kujiheshimu wote kwa pamoja wanastahili heshima ya ubinadamu na radhi za MwenyeziMungu. Uislamu hauwapendi matajiri wenye kiburi na masikini wenye majivuno. Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa akiomba dua akisema:

"Mola wangu! Ninajilinda kwako na shari ya mtihani wa ukwasi na shari ya mtihani wa umasikini" (Muslim, Dhikr, 49)

Hivyo yule mwenye sifa njema kama vile kutosheka, kumtegemea na kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu huyo ndiye mkwasi wa kweli.

Ndiyo maana kwamba kila mja anayependa kupata fadhila na neema za Mwenyezi Mungu na mwenendo mwema anatakiwa kushirikiana na masikini na wenye shida katika baraka alizojaaliwa na Mwenyezi Mungu. Lengo ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu kwa kuwa Muislamu ambaye watu wote watanufaika naye na kuwa salama dhidi ya ulimi na mkono wake. Zaka ni ishara ya

"Toeni (sadaka), kwa maana nitawafidia (maradufu)."

(Bukhari, Tawhid, 35)

kimatendo ya kuonyesha shukrani kwa mali na utajiri unaopewa na Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu anaahidi kuwa kutoa shukrani huzidisha baraka mara dufu:

"...Mkishukuru nitakuzidishieni; na mkikufuru, basi adhabu yangu ni kali." (14: 7)

Mtume wetu Mtukufu (s.a.w) alikuwa akipenda kutoa sadaka na aliwahamasisha maswahaba wake kuwa watu wenye kujitolea. Katika Hadith Qudsi (hadith tukufu ambapo Mtume s.a.w ananukuu moja kwa moja maneno ya Mwenyezi Mungu), imeelezwa kuwa:

"Toeni (sadaka), kwa maana nitawafidia (mara dufu)." (Bukhari, Tawhid, 35)

Badala ya kujuta na kutubu kwa kile walichofanya, wale wanaoipuuza Zaka na sadaka wakisema "Nimeipata kwa jasho na uwezo wangu" na wakawanyanyapaa masikini, kwa hakika watakabiliwa na mwisho wenye kusikitisha kama ule uliompata Qarun.

Qarun, ambaye hapo kabla alikuwa mtu masikini na mnyoofu, alipata utajiri mkubwa kwa elimu ya alkemia aliyofundishwa na Nabii Musa (a.s). Lakini, kwa kuwa alishindwa kuulinda moyo wake dhidi ya matamanio na mielekeo mibaya, alipoteza sifa zake nzuri za unyoofu na uchaji. Akawa na kiburi kwa sababu ya mali yake. Qur'an Tukufu inatueleza kuwa aligeuka kuwa miongoni mwa mafedhuli, na onyo la Mwenyezi Mungu juu yake likawa kama ifuatavyo:

"…mkishukuru nitakuzidishieni…"

(Qur'an 14: 7)

Rumi anasema: "Kitu gani kinachowatokea wanadamu wanapokuwa watumwa wa dhahabu na mali? Mali ina manufaa gani kama haitumiki katika njia ya Mwenyezi Mungu? Inawakilisha nini? Ni upi utumwa wa kuwa mtumwa wa dunia na kutambaa kama nyoka mbele ya mlango wake kama hautokuwa sababu ya taabu inayompeleka mwanadamu mbinguni akiwa mikono mitupu?"

"Hakika Qaruni alikuwa katika watu wa Musa, lakini aliwafanyia dhuluma. Na tulimpa hazina ambazo funguo zake zinawatopeza watu wenye nguvu kuzichukua. Walipomwambia watu wake: Usijigambe! Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wanao jigamba." (Qur'an, 28: 76)

Lakini, Qarun aliyaziba masikio yake yote dhidi ya onyo hili na maonyo mengine ya Musa (a.s). Nabii Musa (a.s) alipomwambia atoe zaka, ingawa mali yake ilitokana na Musa, alijibu: "Unazitamani mali zangu? Nimezichuma kwa nguvu na uwezo wangu!"

Tukio hili limesimuliwa ndani ya Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

"Na utafute, kwa aliyokupa Mwenyezi Mungu, makazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyokufanyia wema wewe. Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi mafisadi. Akasema: Kwa hakika nimepewa haya kwa sababu ya ilimu niliyo nayo. Je! Hakujua kwamba Mwenyezi Mungu keshawaangamiza, katika vizazi vya walio kabla yake, watu waliokuwa wenye nguvu zaidi kuliko yeye, na wenye makundi makubwa zaidi kuliko yake. Na wakosefu hawataulizwa habari ya dhambi zao. Basi akawatokea watu wake katika pambo lake. Wakasema wale waliokuwa wanataka maisha ya duniani: Laiti tungelikuwa tunayo kama aliyopewa Qaruni! Hakika yeye ni mwenye bahati kubwa. Na wakasema wale waliopewa elimu: Ole

wenu! Malipo ya Mwenyezi Mungu ni bora kwa mwenye kuamini na akatenda mema. Wala hawatapewa hayo isipokuwa wenye subira. Basi tukamdidimiza yeye na nyumba yake katika ardhi; wala halikuwepo kundi lolote la kumnusuru kwa Mwenyezi Mungu, wala hakuwa miongoni mwa wanaojitetea. Na wale waliotamani kuwa pahala pake jana, wakawa wanasema: Kumbe Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye katika waja wake, na humdhikisha amtakaye. Ingeli kuwa Mwenyezi Mungu hakutufanyia hisani angelitudidimiza. Kumbe makafiri hawafanikiwi!" (Qur'an, 28: 77-82)

Kisa hiki ni mfano mkubwa unaoonyesha hatima ya wale ambao nyoyo zao zimevutwa na mali na kuisahau Akhera. Kwa maana Qarun, ambaye alipoteza utajiri na baraka za Mwenyezi Mungu, sasa ni ombaomba huko Akhera. Kwa sababu makazi ya Akhera ni ya wachamungu ambao huishi maisha ya wema na Ikhlasi. Aya tukufu inasema:

"Hayo ndiyo makazi ya Akhera, tumewafanyia wale wasiotaka kujitukuza duniani wala ufisadi. Na mwisho mwema ni wa wachamngu." (Qur'an, 28: 83)

Akishangazwa na hali yao, Mawlana Jalaladdin Rumi (q.s) anazungumza kuhusu wale wanaotaka manufaa ya kidunia na kuwa muflisi huko Akhera:

"Kitu gani kinachowatokea wanadamu wanapokuwa watumwa wa dhahabu na mali? Mali ina manufaa gani kama haitumiki katika njia ya Mwenyezi Mungu? Inawakilisha nini? Ni upi utumwa

Mali inapaswa kukaa mfukoni sio moyoni"

wa kuwa mtumwa wa dunia na kutambaa kama nyoka mbele ya mlango wake kama hautokuwa sababu ya tabu inayompeleka mwanadamu mbinguni akiwa mikono mitupu?"

Kama ilivyokuwa kwa Qarun, ambaye alikuwa mtumwa wa mali, kisa cha Tha'labah ni chenye kuamsha tafakari na ni cha mfano. Tha'labah, Muislamu kutoka Madina, alikuwa na raghba kubwa ya kupata mali. Alitaka kuwa tajiri, akamuomba Mtume (s.a.w) amuombee ili awe tajiri. Mtukufu Mtume (s.a.w) akamjibu: "Mali ndogo inayokufanya umshukuru Mwenyezi Mungu ni bora kuliko mali nyingi inayokufanya usishukuru..."

Aliposikia maneno haya ya Mtume (s.a.w) akaachana na nia yake kwa muda lakini baadae tamaa yake ikamrudia tena na hivyo akarudi kwa Mtukufu Mtume (s.a.w) na ombi lile lile:

"Ewe Mtume wa Allah! Niombee niwe tajiri."

Mara hii Mtume (s.a.w) akamwambia:

"Je mimi sitoshi kuwa mfano kwako? Naapa kwa Mwenyezi Mungu, lau ningeomba milima ile ingebadilika kuwa dhahabu na fedha na kunifuata, lakini sikuomba."

Tha'alabah akabadilisha tena mawazo yake. Lakini tamaa yake haikutulia. Alikuwa akijisemea: "Nikipata mali, nitawasaidia masikini na kupata thawabu nyingi kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu." Kisha akaenda kwa Mtukufu Mtume (s.a.w) kwa mara ya tatu na kusema:

"Na utafute, kwa aliyokupa Mwenyezi Mungu, makazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyo kufanyia wema wewe. Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi mafisadi."

(Qur'an 28: 77)

"Ninaapa kwa jina la yule aliyekutuma kama Mtume Wake, nikipata mali nitawalinda masikini na wenye shida, na nitampa kila mtu haki yake."

Katika kujibu ombi la mara kwa mara la Tha'labah, Mtume (s.a.w) akamuombea akisema:

"Mola wangu! Mjaalie Tha'labah mali ya kidunia anayoomba."

Haikupita muda mrefu baada ya dua hii ya Mtume (s.a.w), Mwenyezi Mungu Mtukufu akamjaalia Tha'labah mali nyingi. Mifugo yake ilijaa katika maeneo ya malisho ya mji wa Madina. Lakini Tha'labah ambaye hapo mwanzo alikuwa akiitwa "njiwa wa msikitini" akaanza kuzembea swala za jamaa. Akaanza kuswali Ijumaa tu, na hatimaye akaacha kabisa kuswali swala za jamaa.

Siku moja Mtume (s.a.w) alipopata taarifa kuhusu Tha'labah akasema:

"Jambo gani limempata Tha'labah!"

Kughafilika na ujinga wa Tha'labah haukuishia hapo. Alifikia mpaka kuwaambia maafisa wa Mtume (s.a.w) waliokwenda kukusanya zaka:

"Mnachokifanya ni wizi wa wazi."

Achilia mbali kutoa sadaka aliyoahidi, alikataa hata kutoa haki za wajibu za masIkini na hivyo akawa mnafiki. Tabia hii ya wanafiki imeelezwa katika Aya kama ifuatavyo:

"Na miongoni mwao wapo waliomuahidi Mwenyezi Mungu kwa kusema: Akitupa katika fadhila yake hapana shaka tutatoa sadaka, na tutakuwa katika watendao mema. Alipowapa

Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema: "Mali ndogo inayokufanya umshukuru Mwenyezi Mungu ni bora kuliko mali nyingi inayokufanya usishukuru..."

(Tabari, Jami' al- Bayan, XIV, 370,372)

katika fadhila yake wakaifanyia ubakhili na wakageuka, na huku wakipuuza." (Qur'an, 9: 75-76)

Kwa sababu ya upumbavu wake, hakusikiliza maonyo ya Mtume (s.a.w) na akastahiki kukumbwa na hatima yenye kusikitisha. Kwa sababu ya kudanganyika na furaha za muda mfupi za dunia hii, Tha'labah alipoteza baraka za milele za Akhera. Alipokuwa akifariki dunia, maneno ya Mtume (s.a.w) aliyomwambia:

"Mali ndogo inayokufanya umshukuru Mwenyezi Mungu ni bora kuliko mali nyingi inayokufanya usishukuru..." yalikuwa yakijirudiarudia masikioni mwake.

Kama tulivyoona, binadam, kimaumbile wana silika ya kupenda ulimwengu wa kimaada. Wale wanaolaghaiwa na mng'ao wake hawawezi kutosheka. Mtukufu Mtume (s.a.w) anauelezea ukweli huu:

"Lau mwana wa Adam (mwanadamu) angepewa mabonde mawili ya dhahabu, angetamani la tatu, kwa maana hakuna kinachoweza kulijaza tumbo la mwana wa Adam isipokuwa udongo. Na Mwenyezi Mungu huwasamehe wenye kutubu." (Bukhari, Riqaq, 10)

Binadamu ndiyo viumbe pekee waliopewa utashi, tofauti na viumbe wengine ambao maumbile yao ni kujisalimisha kwenye utashi wa Mwenyezi Mungu. Binadamu wanaweza kuchagua kati ya zuri na baya, wanaweza kufanya maamuzi na wanaweza hata kumkataa Mungu au kumuabudu.

"Lau mwana wa Adam (mwanadamu) angepewa mabonde mawili ya dhahabu, angetamani la tatu, kwa maana hakuna kinachoweza kulijaza tumbo la mwana wa Adam isipokuwa udongo. Na Mwenyezi Mungu huwasamehe wenye kutubu."

(Bukhari, Riqaq, 10)

Ni muhimu kuifahamu asili na tabia ya mwanadamu katika maumbile yake ya kawaida – hamu ya kihayawani, nafsi. Uislamu hukielezea kila kitu kwa namna ya uwastani, kwa sababu kitu chochote kinapopindukia huweza kuwa balaa. Kwa hiyo, mtu anapokusanya mali, kuna muelekeo wa kuwa mchoyo. Watu wenye uchoyo kwa kawaida hupoteza hali ya kuwa na huruma na upendo kwa wengine. Wanaweza hata kujidanganya kwa ahadi tupu kwamba watakapokuwa na mali watawasaidia masikini. lakini, huwa wagonjwa na kusumbuliwa na nyoyo zenye maradhi. Wataingizwa katika watu wenye hasara waliotajiwa katika msemo usemao *"wale wenye kusema 'nitalifanya kesho' wameangamia."*

Kisa hicho cha Tha'labah ni mfano bora kwetu tuelewe mwisho wenye kuhuzunisha wa wale wanaodanganywa na mali za dunia hii, lakini pia wale wanaolazimisha hatma na hawazingatii maadili ya kuomba. Wajibu wetu ni kumuomba Mwenyezi Mungu ayakubali maombi yetu kama yana faida kwetu, badala ya kung'ang'ania na kuziamini sana akili zetu na kuomba vitu ambavyo hatujui kama ni vizuri au ni vibaya kwetu. Vinginevyo tunaweza kujisababishia matatizo yatakayotuzuia kuziona baraka zilizofichwa ndani ya sadaka zetu. Hata hivyo, haiwezekani kwa akili zetu dhaifu kufikiri jinsi dua zetu zinavyofanya kazi. Dua ni idhini, baraka na amri ya Mwenyezi Mungu kwetu. Ni ukweli wa kidini kwamba dua huondosha matatizo, lakini hatuwezi kujua kipi ni kizuri na kipi ni kibaya kwetu; kwa hali hiyo badala ya kusisitiza tupewe

"Kitu chenye kupendeza ni mali ya halali na yenye manufaa katika mikono ya waja wema."

(Ahmad b. Hanbal, Musnad, 202)

kitu fulani tunachokihitaji wakati tunapoomba tuongeze kusema:

"Mola wangu! Tujaalie iwapo ni la kheri kwetu."

Kama tulivyosema ili kuzibadilisha mali zetu kuwa zenye manufaa na faida tunatakiwa kuzitumia kulingana na maamrisho ya Mwenyezi Mungu. Jambo hili ni muhimu kwa ajili ya ustawi na wokovu wa mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla hapa duniani na kesho Akhera.

Mali kama mali siyo kitu kibaya katika Uislamu. Kinyume chake, kama miongozo iliyowekwa ikifuatwa, mali huwa kitu chenye kusifiwa. Mtukufu Mtume wetu (s.a.w) anashajiisha kuwa na mali katika maneno yake yafuatayo:

"Kitu chenye kupendeza ni mali ya halali na yenye manufaa katika mikono ya waja wema." (Ahmad b. Hanbal, Musnad, 202)

Kuomba msaada kutoka kwa watu wengine hali ya kuwa una nguvu za kufanya kazi ni miongoni mwa tabia zinazolaaniwa na Uislamu.

Kwa mujibu wa hadith iliyosimuliwa na Anas bin Malik (r.a), mtu mmoja alikuja kwa Mtume (s.a.w) na kumuomba.

Mtukufu Mtume (s.a.w) akamuuliza: Huna chochote nyumbani mwako? Akajibu: naam, nina kipande cha nguo ambacho sehemu moja ukivaa na sehemu nyingine ukitandika (sakafuni), na bakuli ya mbao ambayo huitumia kunywea maji.

Akasema: vilete. Alipokwishavileta mtukufu Mtume (s.a.w) akavishika mkononi mwake na ku-

"Mola wangu! Ninajilinda kwako na shari ya mtihani wa ukwasi na shari ya mtihani wa umaskini"

(Muslim, Dhikr, 49)

uliza: Nani atakayevinunua? Mtu mmoja akasema: nitavinunua kwa dirham mmoja. Akasema kwa mara ya pili au ya tatu: Nani atakayetoa zaidi ya dirham mmoja? Mtu mmoja akasema: Nitavinunua kwa dirham mbili.

Alichukua dirham hizo mbili na kumpa na kisha akamwambia: Kanunue chakula kwa dirham mmoja kwa ajili ya familia yako na ununue shoka na ulilete kwangu. Akafanya hivyo na kulileta. Mtukufu Mtume (s.a.w) akaliwekea mpini kwa mkono wake na kisha akamwambia: Nenda kakusanye kuni uziuze, na uje hapa baada ya wiki mbili.

Mtu huyo akaenda, akakusanya kuni na kuziuza. Alipopata dirham kumi, alikuja na akanunua nguo na pesa nyingine akanunulia chakula.

Mtume (s.a.w) akamwambia:

"Hii ni bora kwako kuliko kuomba kutakakokufanya uje siku ya kiyama ukiwa na alama usoni mwako. Watu watatu pekee ndiyo wanaoruhusiwa kuomba: yule aliye katika umasikini thakili, aliye katika deni zito, au yule anayewajibika kutoa fidia na ikiwa ni vigumu kwake kulilipa."[10]

Ingawa Uislamu haujakataza moja kwa moja kuomba, unaliona suala hilo kuwa lisilofaa kimaadili. Mtume (s.a.w) alimwambia mtu mmoja aliyekuwa na tabia ya kuombaomba:

"Mwenyezi Mungu Mtukufu hakuliacha suala la kugawa zaka (kwa makundi yanayostahiki)

"Ni tabia nzuri kutomfukuza muombaji mikono tupu, bali mpe hata kama unachoweza kutoa ni tende moja. Ewe Aisha! Usimuondoshe maskini mikono tupu, mpe hata kama unachoweza kumpa ni kipande cha tende."

(Tirmidhi, Kitab al-Zuhd, 37)

10. Tazama Abu Dawud, Kitab al-Zakat, 26.

mikononi mwa yeyote, hata utashi wa Mtume Wake haukupewa nafasi hiyo. Aliyataja makundi nane yanayotakiwa kupewa. Kama umo katika haya makundi nane, basi tunaweza kukupa fungu lako." (Bayhaki, Sunan al-Kubra, VII, 6)

Huu ni mchanganuo mzuri sana kuhusu ugawaji wa Zaka kuwapa wale wanaostahiki. Makundi haya yaliyotajwa katika Aya ndiyo pekee wanaotakiwa kupewa Zaka. Makundi haya yametajwa katika Aya hii:

"Wa kupewa sadaka ni mafakiri, na masikini, na wanaozitumikia, na wa kutiwa nguvu nyoyo zao, na katika kukomboa watumwa, na wenye madeni, na katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na wasafiri. Huu ni wajibu uliofaridhiwa na Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hekima." (Qur'an, 9: 60)

Watu wengine wasiokuwa katika makundi haya nane wanaweza kupewa msaada kwa sadaka nyingine zisizokuwa Zaka ambazo huitwa khayraat. Mtume Mtukufu (s.a.w) hakupata kutoa pesa za Zaka kuwapa watu wasiokuwa katika makundi hayo nane yaliyotajwa, na aliyakataa maombi yao. Kanuni hii aliitumia tu kwenye Zaka pekee na siyo katika sadaka nyingine zisizokuwa zaka. Kuhusu sadaka nyingine Mtume (s.a.w) alikuwa akifanya kwa mujibu wa Aya isemayo "Na anayeomba au kuuliza usimkaripie," (Qur'an, 93: 10) na alikuwa akisema:

"Ni tabia nzuri kutomfukuza muombaji mikono mitupu, bali mpe hata kama unachoweza kutoa ni tende moja. Ewe Aisha! Usimuon-

Musa Topbas (q.s) alikuwa akitoa sadaka kwa waliokuwa wakiomba na akisema:
"Ili tusizoee kuwakataa maskini, tunapaswa kutoa hata kama ni kidogo"

doshe masikini mikono tupu, mpe hata kama unachoweza kumpa ni kipande cha tende." (Tirmidhi, Kitab al-Zuhd, 37)

Katika kutekeleza maana ya hadith hii, Musa Topbas (q.s) alikuwa akitoa sadaka kwa waliokuwa wakiomba na akisema:

"Ili tusizoee kuwakataa masikini, tunapaswa kutoa hata kama ni kidogo"

Pia ieleweke kuwa Uislamu haukubali kuomba isipokuwa katika hali ngumu mno; kwa sababu, kuomba ni kitendo chenye kuaibisha na kudhalilisha. Ndiyo maana kwamba Mtume (s.a.w) aliwataka wale waliokula kiapo cha utii kwake wasiwaombe watu.[11]

Kwa njia hii tunatakiwa kuwatofautisha wale wanaomuomba pesa kila mtu wanayekutana naye na wale masikini ambao wanaona haya kuwaeleza watu shida zao. Kuhusu suala hili Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema:

"Masikini siyo yule anayepita akiwaomba watu na kufukuzwa kwa tonge moja au mawili, na tende moja au mbili. Wakasema (Maswahaba): Ewe Mtume wa Allah! Maskini ni yupi basi? Akasema: yule asiyekuwa na chochote cha kukidhi haja yake, na hadhaniwi kuwa hivyo (ili kutowavuta watu wakarimu) wampe sadaka, na hawaombi watu chochote." (Muslim, Kitab al-Zakat, 102)

Kwa hadith hii, Mtukufu Mtume (s.a.w) alitaka kusema kwamba wale wanaomuomba yey-

"Shet'ani anakutieni hofu ya ufakiri na anakuamrisheni mambo machafu."

(Qur'an 2: 268)

11. Tazama Muslim, Kitab al-Zakat, 108.

ote wanayekutana naye wanapata kile wanachohitaji. Masikini wa kweli ni wale wanaoficha hali yao, wakastahimili na kuvumilia shida na tabu za umasikini. Umuhimu wa kuwasaidia watu wa aina hii umeelezwa ndani ya Qur'an Tukufu:

"Na wapewe mafakiri waliozuilika katika njia za Mwenyezi Mungu, wasioweza kusafiri katika nchi kutafuta riziki. Asiyewajua hali zao huwadhania kuwa ni matajiri kwa sababu ya kujizuia kwao. Utawatambua kwa alama zao; hawang'ang'anaii watu kwa kuwaomba. Na heri yoyote mnayotoa, basi kwa yakini Mwenyezi Mungu anaijua." (Qur'an, 2: 273)

Abu Huraira (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa mwenyezi Mungu alisema: Kwa vyovyote vile sadaka haipunguzi mali na mja anayesamehe Mwenyezi Mungu humuongezea heshimayake, na yule anayeonyesha unyenyekevu Mwenyezi Mungu humuinua mbele ya macho ya watu.

(Muslim, Kitab al-Birr, 69)

Zaka ya Mazao ya Kilimo: 'Ushr (moja ya kumi)

'Ushr ambayo ni miongoni mwa amali za ibada zinazohusu pesa inaelekea kusahaulika. Ni aina ya Zaka ambayo hutolewa kwa mazao. Wale wasiolipa 'ushr yao ni wenye hatia sawa na mnyang'anyi. Wananyang'anya haki ya masikini, mafakiri na wale wanaopigana katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kwa mujibu wa simulizi moja, mtu mmoja mkarimu kutoka Yemen alikuwa na mabustani ya mizabibu, tende na mashamba ya nafaka karibu na mji wa Sana'a. Mtu huyu alikuwa akiweka akiba ya sadaka kwa ajili ya masikini na mafukara wakati wa kipindi cha mavuno. Alipofariki dunia, watoto wake wakashikwa na uchoyo na kuambiana:

"Tuna familia kubwa na mali yetu ni kidogo. Tusitoe chochote kuwapa masikini, na tuyavune mazao yetu kabla hawajaja kutuomba."

Jawabu na radiamali ya dhamira na nia zao mbaya, Mwenyezi Mungu Mtukufu akayateketeza kwa moto mabustani yao na kuyageuza kuwa mabaki. Shamba hili kubwa likawa halitambuliki. Watu hao mabakhili walipoliona walipatwa na mshituko wakadhani kuwa wameingia katika shamba lisilokuwa lao.

Lakini, hawakuwa wakijua kuwa dua za masikini kwa baba yao ndizo zilizokuwa zikilifanya shamba hilo kupata baraka nyingi. Masikini na mafukara wote walikuwa wakinufaika na shamba hilo. Lakini baada ya baba yao kufariki dunia zaka ya 'ushr iliyokuwa ikitolewa na baba yao kuwapa masikini ikaonekana kuwa ni kubwa mno machoni mwao, na hivyo wakaacha kuitoa. Walikuwa hawajui neema za shamba hilo zilikuwa zikitoka wapi, kwa sababu hali ya ukiziwi na kughafilika ilikuwa imeyaziba macho yao.

Ndiyo maana kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: **"...Wala usiwe miongoni wa walioghafilika."** (Qur'an, 7: 205). Tukio hili lijulikanalo kama kisa cha Watu wa Kondeni limetajwa ndani ya Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

"Hakika tumewajaribu hawa kama tulivyo wajaribu wale wenye shamba, walipo apa kwamba watayavuna mazao yake itakapo kuwa asubuhi. Wala hawakusema: Mungu akipenda! Basi lilitokea tukio juu yake kutoka kwa Mola wako Mlezi, nao wamelala! Likawa kama

Maulana Jalaladdin Rumi (q.s) anasema: "Maisha katika hii dunia ni ndoto tu. Kuwa tajiri katika hii dunia ni kama kupata mali ndotoni. Mali za duniani huhama kutoka katika kizazi kimoja kwenda kingine na kuendelea kubaki hapa hapa duniani."

usiku wa giza. Asubuhi wakaitana. Ya kwamba nendeni kondeni mwenu ikiwa mnataka kuvuna. Basi walikwenda na huku wakinong'onezana, Ya kuwa leo hata masikini mmoja asikuingilieni. Na walikwenda asubuhi, nao wameshikilia azimio hilo. Basi walipoliona, wakasema: Hakika tumepotea! Bali tumenyimwa!" (Qur'an, 68: 17 – 27)

Hii ni ishara ya ajabu ya hali yenye kusikitisha ya wale wanaomsahau Mwenyezi Mungu Mtukufu na wanaosahau kutoa haki za masikini katika neema walizojaaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ikumbukwe kuwa nia zote zilizo moyoni zinajulikana kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ukuu Wake umekizunguka kila kitu.

Maulana Jalaladdin Rumi (q.s) anasema:

"Maisha katika hii dunia ni ndoto tu. Kuwa tajiri katika hii dunia ni kama kupata mali ndotoni. Mali za duniani huhama kutoka katika kizazi kimoja kwenda kingine na kuendelea kubaki hapa hapa duniani."

"Malaika wa mauti humuamsha yule aliyeghafilika kutoka usingizini mwake. Mtu huyo huanza kuugulia shida alizozipitia kwa ajili ya kitu ambacho hasa hakukimiliki. Hujuta sana, lakini amechelewa na kila kitu kimefikia tamati ..."

Uzuri ulioje wa maneno ya Ali (r.a):

"Watu wamelala; huamka wanapokufa."

Mwenyezi Mungu Mtukufu pia anaelezea hali ya kujuta ya mtu anayeamka wakati wa mauti yake:

Abu Huraira (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa mwenyezi Mungu alisema: Kwa vyovyote vile sadaka haipunguzi mali na mja anayesamehe Mwenyezi Mungu humuongezea heshimayake, na yule anayeonyesha unyenyekevu Mwenyezi Mungu humuinua mbele ya macho ya watu.

(Muslim, Kitab al-Birr, 69)

رَبِّ لَوْلَا أَخَّرْتَنِيٓ إِلَىٰٓ أَجَلٍ قَرِيبٍ
فَأَصَّدَّقَ وَأَكُنْ مِنَ الصَّالِحِينَ

"...tena hapo akasema: Mola wangu Mlezi! Huniahirishi muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema?" (63: 10)

Lakini wapi, atakuwa amechelewa na ombi lake halitokubaliwa. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu anawaamrisha waje wake watoe sadaka katika vile alivyowaruzuku kabla hawajafikwa na mwisho huo wenye kuhuzunisha.

Kwa muhtasari, kila muumini anapaswa kuwa muangalifu asipuuze mali za ibada zinazohusu pesa. Vinginevyo anatakiwa kujua kuwa atakuwa miongoni mwa walioghafilika ambao hawajui kuwa hizo mali wanazozizuia ni za nani.

Mola wetu! Tupe baraka ya kuwa miongoni mwa waumini ambao hutekeleza kwa hamasa wajibu wao wa kifedha na kutoa haki za masikini ambao wanaodhihirisha au wasiodhihirisha shida zao kwa sababu ya staha walionayo, na utupe baraka ya radhi zako.

Amin!

Maulana Jalaladdin Rumi (q.s) anasema: "Maisha katika hii dunia ni ndoto tu. Kuwa tajiri katika hii dunia ni kama kupata mali ndotoni. Mali za duniani huhama kutoka katika kizazi kimoja kwenda kingine na kuendelea kubaki hapa hapa duniani."

“Mwana wa Adam hudai: Mali yangu, mali yangu. Naye (Mtukufu Mtume) akasema: Ewe Mwanadamu! Huna chochote chako isipokuwa kile ulichokula, ulichokitumia au ulichokivaa kikaisha au ulichokitoa sadaka na kukitanguliza?”

(Muslim, Zuhd, 3-4)

B. INFAQ

a. Asili yake

Maneno kama vile infaq ambayo yanaonyesha ya kujitolea mali na nafsi katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu yametajwa katika zaidi ya maeneo mia mbili ndani ya Qur’an Tukufu. Idadi hii pekee inatosheleza kuelewa daraja na umuhimu wa infaq.

Katika makubaliano ya Aqabah ya pili (Bay’ah Aqabah), Abdullah bin Rawaha (r.a) alisema:

“Ewe Mtume wa Allah! Unaweza kuweka masharti uyapendayo kwa ajili ya Mola wako na kwa ajili yako.” Na Mtume (s.a.w) akasema:

“Sharti langu kwa ajili ya Mola wangu ni kuwa mtamuabudu na hamtomshirikisha na chochote. Na sharti langu kwa ajili yangu mwenyewe na kuwa mtanilinda kama mnavyozilinda nafsi zenu na mali zetu.”

Maswahaba wakauliza:

“Tuna malipo gani iwapo tutafanya hivyo utakavyo?”

Mtukufu Mtume (s.a.w) aliposema:

“Mtapata pepo,” wakasema:

“Faida iliyoje ya biashara hii! Hatutovunja ahadi yetu na wala hatutaki ivunjike.” (Ibn Kathir, Tafsir, II, 406)

Baada ya majadiliano haya Aya ifuatayo ikateremka:

إِنَّ اللهَ اشْتَرَى مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنْفُسَهُمْ
وَأَمْوَالَهُم بِأَنَّ لَهُمُ الْجَنَّة

"Hakika Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao kwa kuwa wao watapata Pepo." (Qur'an, 9: 111)

Ishara kubwa na ya msingi na ya mtu kuuza nafsi yake ni kifo cha kishahidi na kuwa askari. Kisa cha mtu wa kwanza kufa kishahidi katika Uislamu, Bibi Sumayyah, ni cha mfano. Aliitoa nafsi yake katika njia ya Mwenyezi Mungu. Alinunua pepo kwa nafsi yake na anasubiri pindi malipo ya milele yatakapotolewa. Tunapaswa kufuata njia hiyo hiyo na kuwa tayari kutoa mali zetu na nafsi zetu kwa ajili ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu.

Mfano mwingine ni katika vita vya Dardanelles. Japokuwa jeshi la Kituruki halikuwa limebaki na baruti yoyote, walishinda vita kwa sababu walionyesha mojawapo ya mifano mikubwa mno ya kutoa mali na nafsi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Kuna mifano mingi ya aina hii. Kumuuzia mali Mwenyezi Mungu ni istiari yenye maana ya kutumia mali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anaeleza yafuatayo wakati akitaja sifa za wachamungu:

"Ambao huyaamini ya ghaibu na hushika Sala, na hutoa katika tuliyowapa." (Qur'an, 2: 3)

Sadaka na infa, ambazo ni istilahi mbili zinazohusu sadaka katika Uislamu, zina aina nyingi. Sadaqa na infaq zinaanza na kutoa chochote. Kwa hali hiyo, hata kutoa kipande cha tende ki-

"Malaika wa mauti humuamsha yule aliyeghafilika kutoka usingizini mwake. Mtu huyo huanza kuugulia shida alizozipitia kwa ajili ya kitua ambacho hasa hakukimiliki. Hujuta sana, lakini amechelewa na kila kitu kimefikia tamati ..."

Jalal al-din Rumi



***Ithaar* (uungwana) ndiyo alama ya upendo. Mtu hujitolea kwa ajili ya mpenzi wake kwa kadiri ya upendo alionao kwake. Huona kujitolea kuwa ni raha. Anaweza kwenda mbali zaidi katika kujitolea mpaka akayatoa dhabihu maisha yake kwa ajili ya mpendwa wake. Kuwapa sadaka viumbe wa Mwenyezi Mungu Mtukufu ndio ishara kuu kabisa ya upendo.**

nakubaliwa kama infaq na kinamkinga mtoaji dhidi ya moto wa Jahannam. Mtume (s.a.w) alimuona kila Muislamu kuwa ni tajiri. Kwa sababu alifundisha kupitia maneno yake kuwa matendo mbalimbali ya Waislamu kama vile kuamrisha mema na kukataza mabaya, kuwasaidia wanyonge, kumfariji muumini, kuzifurahisha nyoyo zenye huzuni, kuondosha vitu barabarani ambavyo vinaweza kuwasababishia matatizo wapita njia, kuwatembelea wagonjwa n.k yote hayo yanahesabiwa kuwa ni infaq. Na haya hayategemei uwezo wa kifedha tu. Hii ina maana kwamba hata yule mtu ambaye ni masikini kabisa ana namna ambayo anaweza kutekeleza infaq na kutoa sadaka.

Sadaka siyo fedha tu. Matendo kadhaa ambayo kila mtu anaweza kuyafanya kama vile kuwaelekeza watu, kuwafariji, kutoa ushauri na kutabasamu ni miongoni mwa mambo ambayo hutengeneza jamii yenye amani na utulivu, na kusaidia hisia za undugu na mshikamano kushika mizizi katika jamii.

Kwa kuwa inaimarisha nidhamu na uwiano wa jamii, kwa namna moja, kuwapa sadaka masikini na wenye shida katika jamii huwa ni chanzo cha kupata baraka hapa duniani na kesho Akhera. Kisa kifuatacho ni mfano mzuri wa ukweli huu:

Siku moja masikini mmoja alisimama mbele ya Ali (r.a) na kumuomba kitu. Ali (r.a) akawambia watoto wake, Hassan na Hussein (r.a) waende nyumbani wakalete dirham sita walizokuwa nazo nyumbani. Hassan na Hussein wakaenda nyumbani na kuzileta hizo pesa, na Ali (r.a) akampatia

masikini hali ya kuwa wao wenyewe wanazihitajia. Fatimah (r.a) alitaka kwenda kununua ngano kwa pesa hizo. Baadae Ali (r.a) alipokuwa njiani kuelekea nyumbani, alikutana na mtu mmoja aliyetaka kumuuza ngamia wake. Mtu huyo akamuuzia Ali (r.a) ngamia wake kwa dirham 140 kwa makubaliano kuwa atamlipa baadae. Kabla Ali (r.a) hajafika nyumbani, akakutana na mtu mwingine aliyetaka kumnunua ngamia uyo kwa dirham 200.

Ali (r.a) akapata pesa, akalipa deni la dirham 140 na dirham 60 zilizobaki akampatia Fatimah. Kisha akasema:

"Hii ni ahadi ya Mwenyezi Mungua kwetu aliposema **"Afanyae wema atalipwa mfano wake mara kumi."** (Qur'an, 6: 160). Tulitoa dirham 6 na Mwenyezi Mungu akatulipa mara kumi."

Mbali na baraka hizo za Mwenyezi Mungu zilizotajwa hapo juu, kwa mujibu wa Aya isemayo **"Ati yaweza kuwa malipo ya ihsani ila ihsani?"** (Qur'an, 55: 60) Zaka na infaq hufungua milango ya rehema na kufunga milango ya shari.

Tukio lifuatalo lililotokea wakati wa kilele cha mashambulizi ya kigaidi ya miaka ya 1970 ni tukio la mfano.

Majambazi watano au sita waliingia dukani na kumtaka mmiliki wa duka awape pesa zote zilizokuwa katika kasha la fedha. Wakati mzee huyo masikini akichukua funguo kwa unyonge na kutaka kufungua kasha hilo, jambazi aliyekuwa akilinda nje ya mlango alimkimbilia na kusimama

"Hakika Waumini ni wale walio muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake tena wasitie shaka kabisa, na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao. Hao ndio wakweli."

(Qur'an, 49: 15)

mbele yake. Akawaonyesha bunduki rafiki zake na kufoka:

"Hapa hatuibi hata sarafu moja ya fedha."

Marafiki zake walishituka na kushangazwa na tabia ya rafiki yao, wakamuuliza:

"Kuna tatizo gani? Mpaka sasa tumeshaiba maduka mengi na hukusema kitu, sasa hivi kimetokea kitu gani? Tupishe tufanye kazi yetu."

Lakini mtu huyo ambaye alikuwa ameamua kumlinda mwenye duka akasema:

"Hapana. Hatutochukua chochote katika hili duka. Msilazimishe. Labda mtembee juu ya maiti yangu, vinginevyo hamchukui kitu katika hili duka. Mnamjua mtu huyu ni nani? Kwa miaka mingi nilipokuwa nimejiingiza katika kunywa vileo na kucheza kamari, mzee huyu alikuwa akiisaidia familia na watoto wangu. Ni mtu wa pekee ambaye aliwasaidia watoto wangu wapate elimu inayotakiwa."

Baada ya marafiki zake kusikia hivyo walimuomba radhi mwenye duka na kuondoka. Huu ni mfano mzuri sana unaosadikisha hadith isemayo "sadaka kidogo huondosha matatizo mengi."

"Kutabasamu mbele ya wajihi (uso) wa ndugu yako katika Uislamu ni sadaka".

(Tirmidhi, Kitab al-Birr, 36)

Mfano mzuri wa kuwasaidia masikini na kutibu majeraha yao unaonekana katika maisha ya Mtume wetu mpendwa (s.a.w). Kwa upande mmoja aliwataka Waislamu kugeuza ukarimu kuwa tabia ya kawaida. Alihamasisha infaq kwa kusema:

"Mkono wa juu ni bora kuliko mkono wa chini (yaani yule anayetoa sadaka ni bora kuliko yule anayeipokea)." (Bukhari, Zakat, 18)

"Usitamani kuwa kama yeyote isipokuwa katika hali mbili. (Ya kwanza) mtu ambaye Mwenyezi Mungu amempa mali na anaitumia kwa njia iliyo sahihi; (ya pili ni) mtu ambaye Mwenyezi Mungu amempa hekima (Qur'an) na anaifanyia kazi na kuifundisha kwa wengine." (Bukhari, ilm, 15)

Kwa upande mwingine alikuwa akiomba dua akisema:

"Mola wangu! Nipe maisha kama ya masikini, nifishe kama masikini na siku ya kiyama unifufue katika kundi la masikini." (Tirmidhi, Kitab al-Zuhd, 15) na alitenga eneo fulani la msikiti wake kuwa makazi ya maswahaba wasiokuwa na makazi, masikini na mafukara. Aliyaangalia kwa ukaribu sana mahitaji ya Maswahaba hawa waliokuwa wakijulikana kama "Maswahaba wa Suffah" na akawa faraja kwao kwa mtindo wa maisha yake ya staha.

Pia alisema:

"Masikini (ambaye hatokuwa na wasiwasi wa kuulizwa kuhusu mali siku ya kiyama) ataingia Peponi kwa nusu siku (ambayo ni sawa na miaka 500 ya duniani) kabla ya tajiri." (Tirmidhi, Kitab al-Zuhd, 37)

Katika hadith nyingine, aliashiria kwamba utu wa kweli haupimwi kwa mali bali kwa unyoofu na uchamungu *"Wale wanaoongeza mali zao (kwa*

"Hata kama giza litakuwa na nguvu kiasi gani, kijiti kimoja kinatosha kulipatia mwanga."

Jalal al-Din Rumi

kutotoa sadaka) ndiyo wanaopunguza malipo yao akhera" (Bukhari, Riqaq, 13)

Vile vile aliwashauri watu masikini katika umma wake kwa kusema: *"Jilindeni na moto wa jahannam hata kama ni kwa kipande cha tende na yule ambaye hana hata hicho, basi (afanye hivyo) kwa (kusema) neno zuri lenye kufurahisha."* (Bukhari, Adab, 34) na akaonyesha kuwa infaq ni jambo linalowezekana katika hali yoyote ile. Kwa hiyo, watu wasiokuwa na mali ya kutosha kutoa sadaka wakiwatendea wenzao wema na kuzungumza nao kwa maneno mazuri, hiyo itahesabiwa kama ni sadaka. Katika Aya moja imeelezwa kuwa sadaka ya aina hiyo ni bora kuliko hata sadaka ya pesa inayofuatishwa na matusi:

"Kauli njema na usamehevu ni bora kuliko sadaka inayofuatiliwa na maudhi. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujitosha na Mpole." (Qur'an, 2: 263)

Maneno ya Mtume (s.a.w) yaliyotajwa hapo juu hayahamasishi umaskini wala ukwasi. Kinyume chake, yanaonyesha kwamba pande zote mbili kila moja ina upande wake mzuri na ni mhumu kwa mtu kuridhika na kuishi kulingana na hali yake ya kifedha. Jambo la muhimu ni kwamba mja, tajiri au masikini, anatakiwa kuishi kulingana na radhi za Mwenyezi Mungu.

"Ziokoeni nafsi zenu dhidi ya moto hata kwa kutoa kipande cha tende, na yule asiyekuwa hata na kiasi hicho, basi (afanye hivyo) kwa kusema maneno mazuri."

(Bukhari, Adab, 34)

Mtukufu Mtume (s.a.w) alikubali kwamba waumini wote wana ukarimu katika nyoyo zao. Japokuwa Abu Dhar (r.a) hakuwa akimiliki chochote katika hii dunia, Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa akimwambia:

"Ewe Abu Dhar! Unapoandaa mchuzi wako, ongeza maji na kumpa (kama zawadi) jirani yako." (Muslim, Kitab al-Birr, 142) kwa sababu Abu Dhar hakuwa hata na kitu cha kuongeza katika mchuzi wake.

Kuwa masikini katika mfuko hakuna madhara kwa wale walio na utajiri nyoyoni mwao. Iwapo mtu atakuwa tajiri wa moyo sambamba na kuwa na utajiri wa mfuko (mali), jambo hilo litaongeza ukarimu wake. Kwa maana wale walio masikini katika nyoyo zao, kwa upande mwingine, utajiri wa mali hauwezi kuwanufaisha chochote. Kinyume chake, huongeza umasikini wake wa moyo. Na wale walio masikini katika mifuko na katika moyo watakuwa wamekasirika hapa duniani na Akhera, Mtukufu Mtume (s.a.w) anaeleza kuwa ukwasi na utajiri wa kweli siyo kuwa na mali nyingi, bali kuwa na ukwasi na utajiri moyoni.[12]

Kwa hali hiyo utajiri wa kila mtu hutegemea kiasi cha utajiri wa moyo alicho nacho. Kwa upande mwingine, kutosheka ni hazina isiyo na kikomo kama ilivyoelezwa katika hadith ya Mtukufu Mtume (s.a.w),[13] na waumini wa kweli ni wale wenye hazina hii na wakatoa sadaka. Infaq ni ishara na mfano mkuu wa werevu na uwajibikaji wa waumini.

Omar (r.a) alipokuwa safari kuelekea Damascus alikuwa akifanya zamu na mtumishi wake ya kupanda ngamia. Walipofika katika lango la mji ili-

Amesimulia Jabir bin Abdillah kuwa: Mtume alisema, "kila jambo zuri ni sadaka."

(Bukhari, Adab, 33)

12. Ahmad bin Hanbal, Musnad,II, 389.
13. Bayhaki, Kitab al-Zuhd,II, 88.

kuwa zamu ya mtumishi wake. Kutokana na uvumilivu wa Umar, alikuwa akitembea kwa miguu na mtumishi wake akiwa amepanda farasi huku wakiingia katika mji huo. Hili ni dhihirisho lingine kubwa la infaq na ithar kutoka katika historia ya Kiislamu.

Ithar ina maana ya kuchukua kitu chetu kuwapa wengine pamoja na kwamba tuna shida nacho, kuwatanguliza wengine juu ya nafsi zetu na kuchukua haki zetu na kuwapa wao, jambo ambalo ni nadra kupatikana katika jamii ya sasa. Tunatakiwa kuhamasisha kwenda mbali zaidi ya kutoa zaka ya lazima. Ukusanyaji na ugawaji wa sadaka vinatakiwa kuandaliwa na taasisi. Vilevile tunatakiwa kuwapa mafunzo idadi ya kutosha kwa ajili ya taasisi hizi. Ni jukumu muhimu pia la jamii ya leo kuanzisha hospitali mbalimbali na makazi ya uuguzi kwa ajili ya watu masikini katika jamii.

Infaq inapaswa kuwa tabia ya kawaida ya Muislamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

اَلَّذِينَ يُنْفِقُونَ فِي السَّرَّاءِ وَالضَّرَّاءِ وَالْكَاظِمِينَ
الْغَيْظَ وَالْعَافِينَ عَنِ النَّاسِ وَاللهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ

“Ambao hutoa wanapokuwa na wasaa na wanapokuwa na dhiki, na wanajizuia ghadhabu, na wasamehevu kwa watu; na Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema.” (Qur’an, 3: 134)

“Ambao hutoa wanapo kuwa na wasaa na wanapo kuwa na dhiki, na wanajizuia ghadhabu, na wasamehevu kwa watu; na Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema”

(Qur’an 3: 134)

Kwa mujibu wa riwaya moja, Ja’far al-Sadiq (r.a) alikuwa na mtumishi aliyekuwa akimsadia katika huduma binafsi. Siku moja mtumishi huyo alimdondoshea Ja’far (r.a) bakuli la mchuzi kwa

bahati mbaya. Ja'far (r.a) akapatwa na ghadhabu. Mtumishi alipoona hivyo akasema:

"Ewe Bwana wangu! "Wale wanaojizuia na ghadhabu" wamesifiwa ndani ya Qur'an Tukufu na kisha akaisoma hiyo aya."

Ja'far al-Sadiq (r.a) akamwambia kuwa ameizuia ghadhabu yake.

Mtumishi akasema tena:

"Wale walio wasamehevu kwa watu nao pia wamesifiwa katika Aya hiyo na akasoma kipande cha Aya kinachohusika." Ja'far (r.a) akasema:

"Sawa, nimekusamehe"

Kisha mtumishi akamwambia:

"Katika sehemu ifuatayo ya Aya, imeelezwa kwamba "Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema" akasoma sehemu iliyobaki ya Aya hiyo."

Ja'far (r.a) akasema:

"Waweza kwenda. Uko huru. Nimekuacha huru kwa ajili ya Mwenyezi Mungu."

Kwa mujibu wa maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w) mwanamke mmoja alisamehewa dhambi zake kwa sababu tu ya kumpa maji mbwa mwenye kiu. Kwa upande mwingine, mwanamke mwingine aliadhibiwa katika moto kwa sababu ya kumuacha na njaa paka mwenye njaa na kumsababishia kifo. Mifano hii inaonyesha hali ya kweli ya moyo wa muumini; kwa hiyo, Muislamu anapaswa kuwa mwenye hisia, mwenye ithaar, ukarimu na huruma.

Waislamu wanatakiwa kuufanya ukarimu kuwa tabia yao ya mazoea.

Ukarimu unaokubaliwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kutoa kilicho bora katika mali. Iwapo ubora huu utazingatiwa katika utoaji wa sadaka, basi itakuwa ni sababu ya mtoaji kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

As-hab al-Suffa, ambao walijitolea nafsi zao katika njia ya Uislamu na kutofikiria kitu kingine zaidi ya kumuabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu, hawakuweza kupata muda wa kutafuta kipato. Ndiyo maana Waislamu wengine walikuwa wakiwaleta tende za kula. Siku moja baadhi ya watu waliwaletea tende zilizoharibika na kwa sababu as-hab al-Suffa walikuwa na njaa sana, hawakuwa na jinsi bali kula tende hizo. Kutokana na tukio hili Mwenyezi Mungu akatoa onyo lifuatalo:

“Enyi mlio amini! Toeni katika vile vizuri mlivyo vichuma, na katika vile tulivyo kutoleeni katika ardhi. Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya, hali nyinyi wenyewe msinge vipokea ila ingekuwa mmefumba macho. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha na Msifiwa.” (Qur’an, 2: 267)

“Enyi mlio amini! Toeni katika vile vizuri mlivyo vichuma, na katika vile tulivyo kutoleeni katika ardhi. Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya, hali nyinyi wenyewe msinge vipokea ila ingekuwa mmefumba macho. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha na Msifiwa.”

(Qur’an 2: 267)

Katika Aya nyingine, Mwenyezi Mungu Mtukufu anatueleza tutoe vile tunavyovipenda ili kuwa karibu Naye:

“KABISA HAMTAFIKIA wema mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda. Na kitu chochote mnacho kitoa basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua” (Qur’an, 3: 92)

Neno “birr” limetafsiriwa kama lilivyo katika maana kamili kuwa ni wema, rehema za Mwe-

nyezi Mungu, radhi Zake na Pepo. Katika Aya nyingine, Mwenyezi Mungu Mtukufu analielezea neno birr kama ifuatavyo:

"Siyo wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anayemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na anawapa mali, kwa kupenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao, na katika ugombozi, na akawa anashika Sala, na akatoa Zaka, na wanaotimiza ahadi yao wanapoahidi, na wanaovumilia katika shida na dhara na wakati wa vita; hao ndiyo waliosadikisha, na hao ndiyo wajilindao." (Qur'an, 2: 177)

Aya hii pia ina sifa nyingine nzuri ambazo Muislamu anatakiwa kuwa nazo, zaidi ya birr.

Tunahitaji kampeni ya dhati ya infaq katika jamii yetu ambayo hisia za undugu na mshikamano zinadhoofika; amani na utulivu wa kijamii vinatoweka; huku hisia za chuki na uadui zinaimarika. Kampeni hii ni muhimu sana kwa watoto wetu na sisi wenyewe binafsi. Watoto wetu wanatakiwa kulelewa wakijua kuwa mmiliki halisi wa mali zote ni Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kama tulivyo na wajibu wa kuwafundisha watoto wetu misingi ya dini yetu, ndivyo tunavyowajibika kuwawekea kasumba ya kupenda infaq na kuwazoesha wajibu wa muumini wa kuwasaidia wenye shida. Tukishindwa kuwazoesha hivyo tangu wanapokuwa wadogo, basi hiyo itakuwa ni hasara kwa mustakabali wao.

"Kabisa hamtafikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyo vipenda. Na kitu chochote mnacho kitoa basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua."

(Qur'an 3: 92)

Ukarimu unaokubaliwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kutoa kilicho bora katika mali. Iwapo ubora huu utazingatiwa katika utoaji wa sadaka, basi itakuwa ni sababu ya mtoaji kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Wale wanaotaka kuwa waumini kamili wanatakiwa kuwasaidia, kuwaunga mkono na kuwaombea masikini kadri wawezavyo. Kushirikiana na masikini katika shida zao nayo ni sehemu ya infaq. Twaweza kuona kutokana na dua hii ya Nabii Musa (a.s) kwamba kuwafurahisha waliovunjika nyoyo humfanya mtu awe karibu zaidi na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa mujibu wa riwaya siku moja Nabii Musa (a.s) aliomba akisema:

"Mola wangu! Nikutafute wapi?" Mwenyezi Mungu Mtukufu akamjibu:

"Nitafute miongoni mwa wale waliovunjika moyo" (Abu Nuaym, Hilya, II, 364).

Moja ya huduma muhimu katika zama za sasa ni kutumia rasilimali zetu kuimarisha taasisi zitakazowapa mafunzo watu watakaoshika hatima hii. Kama ilivyoelezwa kwa ufasaha na mwanafikra mmoja kwamba "Tofauti kubwa baina ya mataifa yaliyoendelea na yale masikini ni uwepo wa watu wengi waliofunzwa vizuri." Wanachohitaji watu ni watu hao waliofunzwa vyema.

Kama leo hii ulimwengu wa Kiislamu umepata hasara ya kijamii, ni kwa sababu wamekabiliwa na ukandamizaji ambao hawawezi kujikwamua. Ikumbukwe kuwa ili kubadilisha hali mbaya ya ulimwengu wa Kiislamu, Waislamu wanapaswa kufanya juhudi kuwa kuliko kipindi walichokuwa na nguvu. Waislamu wanapaswa kutumia maneno ya Mwenyezi Mungu yasemayo: "Hakika pamoja na uzito upo wepesi" kama msingi wa maisha na kuwa na azma ya kutafuta njia ya kujikomboa. Hili ni jukumu kubwa ambalo baadhi ya hatua ambazo

kwa kawaida ni halali hubadilika kuwa yanayowajibishwa na kisheria. Ni sawa na hali ya mama, ambaye wakati akimnyonyesha mtoto wake, hujikuta akiwa katikati ya moto. Akiendelea kumnyonyesha na kuyaweka maisha yake na ya mwanaye hatarini, ataulizwa kwa hatua hiyo. Hili ni suala muhimu katika sayansi za Kiislamu lijulikanalo kama *"maslahah"* au maslahi ya umma. Kwa hiyo, Waislamu wanatakiwa kuyapima maslahi ya jamii ya Kiislamu kwa sasa na kisha wafanye jinsi maslahi yanavyotaka lakini pasipokwenda mbali ya mahitaji hayo. Huwenda hapo Waislamu wakapata njia ya kujikwamua na matatizo yao.

Kama tulivyoeleza hapo kabla, taasisi za kidini ambazo zimekuwa alama adhimu za ustaarabu wa Kiislamu, ni mifano ya hakika inayoonyesha namna walivyochukua maamuzi na kushughulikia kikamilifu mahitaji na matatizo ya wakati huo.

Mali na watoto vina uwezo mkubwa sana wa kuutoa moyo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumvutia upande wake. Kwa sababu hiyo Mwenyezi Mungu anasema katika Qur'an Tukufu:

"Hakika mali yenu na watoto wenu ni jaribio. Na kwa Mwenyezi Mungu upo ujira mkubwa." (Qur'an, 64: 15)

"Enyi mlioamini! Yasikusahaulisheni mali yenu, wala watoto wenu, kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Na wenye kufanya hayo ndio walio khasiri." (Qur'an, 63: 9)

Infaq inaweza kufanywa kwa njia bora kupitia taasisi za kidini. Taasisi hizo ni njia salama zaidi

Wale wanaotaka kuwa waumini kamili wanatakiwa kuwasaidia, kuwaunga mkono na kuwaombea maskini kadiri wawezavyo. Kushirikiana na maskini katika shida zao nayo ni sehemu ya infaq.

kwa matajiri kuwafikia masikini. Kwa namna moja ni daraja baina ya masikini na matajiri. Wale wanaotoa sadaka zao kwenye taasisi za kidini wana uwezekano wa kuwafikia masikini hata baada ya umauti wao.

b. Adabu za infaq

Adabu ni muhimu mno katika mali za hisani kama vile zaka na sadaka. Adabu kubwa kushinda zote ni mtoaji kutotarajia shukrani kutoka kwa mpokeaji, kwa sababu mpokeaji anakuwa amemuokoa mtoaji kutokana na deni la wajibu na kumhakikishia kupata thawabu za Mwenyezi Mungu. Sadaka pia humkinga mtoaji dhidi ya kila aina ya matatizo na majanga. Masikini, fukara na wenye shida kiukweli ni baraka kwa tajiri, kwa sababu milango ya pepo hupata kufunguliwa na dua zao.

Yafuatayo yameelezwa ndani ya Qur'an Tukufu kuhusu adabu za infaq:

"Enyi mlioamini! Msiharibu sadaka zenu kwa masimulizi na maudhi, kama anayetoa mali yake kwa kuwaonyesha watu, wala hamuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho. Basi mfano wake ni kama mfano wa jabali ambalo juu yake pana udongo, kisha likapigwa na mvua kubwa, ikaliacha tupu. Basi hawatakuwa na uweza wowote kwa walivyo chuma. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu makafiri." (Qur'an, 2: 264)

Sadaka inayofuatiwa na kuvunja nyoyo, kumdhalilisha maskini, kukumbushia ukarimu uliomfanyia na matusi haina thamani yoyote mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Ingawa utoaji zaka na sadaka umehamasisha na kushajiishwa ndani ya Aya hii, adabu inayotakiwa kuchungwa katika infaq nayo pia imetajwa kwa

uwazi kabisa. Sadaka inayofuatiwa na kuvunja nyoyo, kumdhalilisha masIkini, kukumbushia ukarimu uliomfanyia na matusi haina thamani yoyote mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Mtume (s.a.w) anasema:

"Watu watatu siku ya kiyama Mwenyezi Mungu hatozungumza nao, hatowatazama, hatowasamehe na watapata adhabu kali."

Baada ya kusikia Mtume (s.a.w) akirudia maneno hayo mara tatu, Abu Dharr akasema:

"Wameshindwa na wamekasirika; ni watu gani hao ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?"

Mtukufu Mtume (s.a.w) akajibu:

"Hao ni: mvutaji wa nguo ya chini,yule anayekumbushia ukarimu wake na anayeuza bidhaa zake kwa kiapo cha urongo." (Muslim, Kitab al-Iman, 171)

Maneno haya yanathibitisha kwamba sadaka zinazofuatiwa na matusi na masimulizi ni dhambi kubwa itakayomsababishia adhabu mja, kwa sababu nyoyo ni mahali anapopatazama Mwenyezi Mungu. Rumi anasema:

"Toa kwa uzuri mali yako, utajiri wako na ufanye moyo uwe na furaha ili kwamba dua ya moyo huo iwe nuru katika kaburi lako, na nuru katika njia yako wakati wa usiku wa giza."

Rumi anasema: "Toa vizuri mali yako na ufanye moyo uwe na furaha ili dua ya moyo huo iwe nuru katika kaburi lako, na iwe nuru yako katika usiku wa giza."

Katika tungo zake nzuri, Rumi (q.s) anaashiria kuwa masikini na mafukara kwa namna moja ni baraka kwa matajiri kwa sababu kupitia masikini, matajiri hupata kutoa shukrani zao kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Vile vile anaeleza katika kifungu

kijacho kuwa fadhila inaweza tu kuonekana kupitia watu wenye shida na hivyo matajiri wanatakiwa kuwa waangalifu wasiziumize hisia za masikini:

"Masikini ni kioo cha fadhila,Jihadhari! Usipumue kwenye kioo kwa kusema mambo yenye kuumiza kwenye wajihi wa kioo.

Ishara moja ya fadhila za Mwenyezi Mungu ni watu masikini. Mwenyezi Mungu Mtukufu amemfanya masikini aombe,kwa hali hiyo njia zielekeazo kwenye furaha zikaandaliwa kwa ajili ya wakarimu. Ishara nyingine ya fadhila za Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kuweka hisia za upendo na huruma ndani ya moyo wa wenye mali ili kuwasaidia masikini.

Kadhalika kama ambavyo masikini huhitajia ukarimu na wema, ukarimu na wema nao pia humhitajia masikini. Kama ambavyo mtu mzuri huhitajia kioo kisafi, kisichokuwa na vumbi na kinachong'aa ili auone uzuri wake, mtu karimu naye humhitajia maiskini na mwenye shida.

Kwa hiyo, masikini ni vioo vya fadhila za Mwenyezi Mungu. Hapo wakasi hupata kuzitazama fadhila zao. Matajiri wanyoofu ambao wameungana na Mfadhili Mkuu hutambua kuwa mali waliyonayo ni amana tu waliyokabidhiwa na wanaujua udhaifu wao mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na kuwa kioo cha fadhila za Mwenyezi Mungu. Kwa kupata fungu katika fadhila za Mwenyezi Mungu, huzama katika ukarimu.

Wale wabebao mali yao nyingi au kidogo nyoyoni mwao ndiyo wenye kukhasirika katika Akhera. Aina hii ya watu haitokuwa mlangoni mwa

"Maskini ni kioo cha fadhila, jihadhari! Usipumue kwenye kioo kwa kusema mambo yenye kuumiza kwenye wajihi (uso) wa kioo."

Jalal al-Din Rumi

Mwenyezi Mungu. Uwepo wao ni kama umbile la nje na taraza ya mlango.

Hao ndiyo wanyonge wa kweli na masikini wa kiroho, wale ambao wametupwa mbali na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Uwepo wao wa kweli ni kama taraza isiyokuwa na uhai na picha iliyochujuka ya mateso yao. Hao ni wale wasiokuwa na moyo na hawaujui ukweli. Jiepushe nao! Usitupe mfupa mbele ya picha ya mbwa!

Tahadhari na usiweke sahani ya chakula mbele ya picha hizi zisizokuwa na uhai! Usiamiliane nao kwa wema na usifanye nao urafiki! Aina hii ya matajiri watakuwa masikini wa siku ya Kiyama.

Madervish hao ni madervish wa mkate siyo wa roho. Wanadhani kuwa mateso yao ni furaha kwao. Katika mawazo yao wanakula chakula kizuri na kunywa sharubati tabu, lakini kiuhalisia hawana hata chembe katika neema za Mwenyezi Mungu.

Ewe usiyetaka kukutana na maumivu kama hayo! Wazunguke viumbe kwa fadhila ulizopewa ili upate kuwa miongoni mwa wenye busara."

Adabu nyingine muhimu inayotakiwa kuchungwa wakati wa kutoa zaka au sadaka, ni kuwa makini kuhusu usiri. Kutoa sadaka wazi wazi inaweza kuondosha aibu ya masikini, akazoea kuomba na kuacha kabisa kufanya kazi. Vilevile inaweza kusababisha matajiri kuwa na kiburi.

Hata hivyo, wakati mwingine, kutoa sadaka hadharani kuna baadhi ya faida. Kwa kufanya hivyo, jamii hupata kuhamasika kuwasaidia masi-

"Wanao toa mali zao kwa Njia ya Mwenyezi Mungu, kisha hawafuatishii masimbulizi wala udhia kwa walicho toa, wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi, wala haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika."

(Qur'an, 2: 262)

kini. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an Tukufu:

"Mkizidhihirisha sadaka ni vizuri; na mkizificha mkawapa mafakiri kwa siri basi hivyo ni heri kwenu, na yatakuondoleeni baadhi ya maovu yenu. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda." (Qur'an, 2: 271)

Wachambuzi wameitafsiri Aya hii kwamba Zaka inatakiwa kutolewa waziwazi na aina nyingine zote za sadaka zinatakiwa kufanywa kwa siri.

Adabu bora katika sadaka ni kutoa sadaka kwa siri sana kiasi kwamba "mkono wa kushoto usijue kilichotolewa na mkono wa kulia." Watu wanaochunga adabu hii wamepewa habari njema ya kwamba watakuwa chini ya kivuli cha Mwenyezi Mungu katika ile siku ambayo hapatakuwepo na kivuli isipokuwa kivuli Chake. Watangulizi wetu walionyesha mifano bora ya adabu na tabia hii.

"Wale wanao toa mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhahiri, wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi; wala haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika."

(Qur'an, 2: 274)

Kwa mfano, Mehmed II, aliweka masharti kadhaa katika hati yake ya wakfu kuhusu adabu za kuwasaidia masIkini. Raia wa Sultan huyo makini walikuwa wakiweka sadaka zao katika makasha na kuziacha chini ya mawe ya sadaka na masikini walikuwa wakienda hapo na kuchukua kiasi wanachohitaji bila kukutana na mtoaji.

Japokuwa usiri una umuhimu mkubwa katika kutoa sadaka, wakati mwingine uwazi nao umehamasisha ili kuulinda moyo dhidi ya unafiki. Aidha, hakuna kikomo cha muda wa kutoa sadaka. Muumini anaweza kutoa sadaka usiku na mcha-

na pindi inapohitajika. Hili limetajwa katika Aya ifuatayo:

"Wale wanaotoa mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhaahiri, wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi; wala haitakuwa na hofu juu yao, wala hawatahuzunika." (Qur'an, 2: 274)

Abu Bakr (r.a) alitoa wakati wa mchana sadaka ya dinar elfu kumi katika dinar elfu arobaini alizokuwa nazo, dinar elfu kumi usiku, dinar elfu kumi akazitoa kwa siri na elfu kumi zilizobaki akazitoa kwa wazi. Inasemekana kuwa ukarimu huu ulioonyeshwa na Abu Bakr (r.a) ndiyo sababu ya kuteremshwa kwa Aya iliyotajwa hapo juu.

Kwa upande mwingine, Ali (r.a) alitoa wakati wa mchana sadaka ya dirham moja katika dirham nne alizokuwa nazo, dirham nyingine wakati wa usiku, dirham moja kwa siri na dirham moja kwa wazi, japokuwa hakubaki na pesa yoyote. Mtukufu Mtume (s.a.w) alipomuuliza "kwa nini amefanya hivyo", akasema:

"Ili nistahiki kupata kile ambacho Mola wangu ameniahidi." Hapo Mtume (s.a.w) akamwambia:

"Umepata ulichokitaka." (Wahidi, Asbab al-Nuzul al-Qur'an, 95)

Ithaar ni alama ya upendo. Mtu hujitolea kwa ajili ya mpenzi wake kwa kadri ya upendo alionao kwake. Huona kujitolea kuwa ni raha. Anaweza kwenda mbali zaidi katika kujitolea mpaka akayatoa dhabihu maisha yake kwa ajili ya mpendwa wake. Kuwapa sadaka viumbe wa Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiyo ishara kuu zaidi ya upendo.

"Enyi mlio amini! Msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na maudhi, kama anaye toa mali yake kwa kuwaonyesha watu, wala hamuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho. Basi mfano wake ni kama mfano wa jabali ambalo juu yake pana udongo, kisha likapigwa na mvua kubwa, ikaliacha tupu. Basi hawatakuwa na uweza wowote kwa walivyo chuma. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu makafiri."

(Qur'an 2: 264)

Kwa sababu zaka na sadaka hutolewa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Imeelezwa katika Qur'an Tukufu kwamba **"Mwenyezi Mungu huzikubali sadaka".** Aya ifuatayo inasema:

"Je! Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu anapokea toba ya waja wake, na anazikubali sadaka, na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kupokea toba na Mwenye kurehemu?" (Qur'an, 9: 104)

Katika kusisitiza na kuifafanua nukta hiyo hiyo, Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema:

"Mwenyezi Mungu huzikubali sadaka zote zitokanazo na kipato halali, Mwenyezi Mungu huzikubali na kuzipokea kwa Mkono wa Kuume." [14]

Hivyo basi, sharti muhimu zaidi katika kutoa sadaka ni uaminifu, Ikhlas na kuifanya kwa ajili tu ya Mwenyezi Mungu. Kuhisi ufahari na kusubiri kushukuriwa baada ya kutoa sadaka ni jambo lisilokubaliwa kabisa. Aina hii ya fikra hubatilisha thawabu zote za sadaka. Kinyume chake, mtoaji anatakiwa kumshukuru masikini na asitarajie chochote zaidi ya radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hii ndiyo adabu ya utoaji wa sadaka inayokubaliwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Katika Aya ifuatayo, Mwenyezi Mungu Mtukufu anaisifu sadaka ya Ali na Fatimah (r.a) na kuwausia waumini kuwa na hisia kama hizo:

Sharti muhimu zaidi katika kutoa sadaka ni uaminifu, ikhlas na kuifanya kwa ajili tu ya Mwenyezi Mungu.

"Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa. Haki-

14. Muslim, Kitab al-Zakat, 63.

ka sisi tunakulisheni kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani. Hakika sisi tunaiogopa kwa Mola wetu Mlezi hiyo siku yenye shida na tabu. Basi Mwenyezi Mungu atawalinda na shari ya siku hiyo, na atawakutanisha na raha na furaha." (Qur'an, 76: 8-11)

Katika Aya hii kuna nukta muhimu za kuzingatia kuhusu utoaji wa sadaka:

1. Imeashiriwa kuwa ithaar na kuwatanguliza Waislamu wenzetu juu ya nafsi zetu ni sifa yenye kusifiwa

2. Sadaka itolewe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na siyo kwa ajili ya manufaa ya kidunia

3. Msisitizo umewekwa juu ya umuhimu wa kutoa sadaka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ili mtoaji apate kuokolewa na adhabu zenye kutisha za siku ya Kiyama

4. Sadaka zitolewazo kwa siri hukubaliwa na Mwenyezi Mungu na zitaufanya uso wa mtoaji uwe na nuru Siku ya Kiyama

5. Vile vile imeashiriwa kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anawataka waja wake watekeleze matendo ya heri kama hayo.

mtoaji akifuata miongozo iliyotolewa katika Aya hii, unyoofu na Ikhlasi katika moyo wake pia vitaonekana kwa yule mpokeaji. Na hata kama hakustahiki kupata hiyo sadaka, atapata mazingatio kutokana na kitendo hicho. Sadaka ikitolewa kwa nia ya dhati, basi mtoaji atapata thawabu

Kampeni kabambe ya infaq na utoaji huduma inahitajika katika jamii yetu, ambapo hisia za undugu zimedhoofika, amani na utulivu katika jamii vimepotea, na chuki na uadui vimezidi.

hata kama ilipokelewa na mtu asiyetahili. Hili limeelezwa katika hadith ifuatayo:

"Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alisema, "Mtu mmoja alionyesha nia yake ya kutoa sadaka, hivyo akatoka na sadaka yake na bila kujua akampa mwizi. Asubuhi watu wakasema kuwa sadaka yake alimpa mwizi. (Alivyosikia hivyo) akasema: :Ewe Mwenyezi Mungu, himidi zote ni zako. Nitatoa sadaka kwa mara nyingine." Na hivyo kwa mara nyingine akatoka na sadaka yake na (bila kujua) akampa mwanamke mzinifu. Asubuhi watu wakasema kuwa sadaka yake aliitoa kumpa mwanamke mzinifu. Mtu huyo akasema, "Mola wangu! Himidi zote ni zako. (Sadaka yangu nilimpa) mzinifu. Nitatoa sadaka tena." Hivyo akatoka tena na sadaka yake na (bila kujua) akampa tajiri. Asubuhi watu wakawa wanazungumza na kusema kuwa: tajiri kapewa sadaka. Akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu, himidi zote ni zako. Hakika sadaka yangu zimekwenda mikononi mwa mtu mwizi, mzinifu na tajiri." Kisha mtu mmoja akaja na kumwambia, "Sadaka uliyompa mwizi yaweza kumfanya akaacha wizi, na ile uliyompa mzinifu yaweza kumfanya akaacha uzinifu, na ile uliyompa tajiri yaweza kumfanya achukue mazingatio kutokana na sadaka hiyo na kuzitumia mali alizopewa na Allah katika njia ya Mwenyezi Mungu."
(Bukhari, Kitab al-Zakat, 14)

Zaka ndio tiba na suluhisho bora la matatizo yanayosababishwa na hatua ya kugeuza mali kuwa mgogoro wa kijamii.

Tukio kama hilo lilimtokea Mahmud Sami Ramazanoğlu (q.s). Siku moja alipokuwa ziarani katika mji wa Anatolia, mtu mmoja alisimamisha gari lake na kuomba fedha ya sigara.

Hata kama rafiki zake hawakubaliani naye, anasema:

"Kwa kuwa ameomba, tunatakiwa kumpa fedha" na bila wasiwasi akatoa pesa huku marafiki zake wakitazama kwa mshangao. Masikini huyo alifurahishwa na kile alichokiona akasema:

"Sasa nitakwenda kununua chakula kwa pesa hii" akaondoka akiwa ni mwenye furaha.

Huu ni mfano mzuri unaoonyesha jinsi sadaka iliyotolewa kwa moyo safi inavyoweza kuwa na athari chanya kwa masikini. Itakuwa furaha kubwa kwetu kama tukianza kabisa kufikiria hisia za masikini badala ya hisia zetu.

Ewe Mola! Zifanye ishara za huruma kuwa hazina za milele katika nyoyo zetu.

Amin!

Zaka ndio tiba na suluhisho bora la matatizo yanayosababishwa na hatua ya kugeuza mali kuwa mgogoro wa kijamii.

ZAKA KUTOKANA NA MTAZAMO WA KISHERIA[15]

"Hakika wale walio amini na wakatenda mema na wakashika Sala na wakatoa Zaka, wao watapata ujira wao kwa Mola wao Mlezi, wala haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika."

(Qur'an, 2: 277)

Shuruti za wajibu wa Zaka

1. *Zaka* ni wajibu kwa mtu mzima aliye huru na anayestahili kisheria mwenye akili timamu.

2. Awe anamiliki zaidi ya kiwango kilichobainishwa kiitwacho *nisab*, cha mali inayokuwa baada ya kutoa mahitaji yake ya msingi na madeni. Mahitaji ya msingi ni vile vitu ambavyo mtu huviihitajia ili kudhamini (kutunza) uhai na uhuru wake. Miongoni mwa vitu hivyo ni nyumba, vitu vyote vya nyumbani isipokuwa dhahabu na fedha, mavazi, gharama za maisha za watu wa kaya yake kwa mwezi – kwa mujibu wa mtazamo mwingine kwa kipindi cha mwaka – vitabu vyake vya kujisomea, na vifaa vya kazi zake za mikono.

"Nisab" ni kiwango cha chini kilichowekwa kama sharti la kutoa *zaka.* Kiwango cha nisab hutofautiana kutegemeana na vitu husika.

---

15. Katika sura hii upande wa kisheria wa zaka umeelezewa tu kwa mukhtasari. Kwa maelezo ya kina tazama Döndüren, Hamdi, Delilleri ile İslâm İlmihali; Bilmen, Ömer Nasuhi, Büyük İslâm İlmihali; Zühayli, Vehbe, İslâm Fıkhı Ansiklopedisi; vilivyoandikwa na kamati ya (İSAV), İbâdet ve Müessese Olarak Zekât. Iwapo vitabu hivi haviwezi kupatikana, basi mawali yanaweza kutumwa kwa wataalamu wenye elimu kutoka katika ofisi ya Rais wa mambo ya dini.

3. Sharti lingine linalofanya mali ilipiwe zaka ni kuwa mali inayolipiwa zaka lazima iwe na sifa ya namaa yaani mali lazima ima iwe inakuwa na kuongezeka yenyewe au iwe na uwezekano wa kukua na kuongezeka. Kulingana na istilahi ya sheria ya kodi, hili linaelezwa kama ifuatavyo: “mali lazima ima ikuwe yenyewe au itoe faida na manufaa kwa mmiliki.” “Kukua yenyewe” hutokea kutokana na kuzaa, kuzaliana, biashara n.k. “Mali yenye kuwezekana kukua /kuongezeka” kwa upande mwingine ni kwamba aina husika ya mali inayomilikiwa ina uwezekano wa kuongezeka.

4. Ipite miezi kumi na mbili kamili ya kalenda ya mwezi mwandamo tangu mali husika ilipoanza kumilikiwa. Zaka inatakiwa kutolewa kwa mujibu wa kalenda ya mwezi mwandamo, kwa maneno mengine kwa kila siku 354 asilimia 2.5 ya mali inatakiwa kutolewa kama zaka. Hata hivyo, katika zama hizi baadhi ya makampuni uhesabu zaka yao kulingana na mwaka wa kalenda ya jua au siku 365, ikiwa na maana kwamba wanatakiwa kufanya mahesabu na kuongeza siku 11 zaidi za zaka kwenye malipo yao. Ieleweke kuwa “sharti hili linahusu mifugo, pesa, mali za biashara. Halihusu mazao, matunda, asali, madini yaliyoziduliwa (extracted minerals), hazina iliyookotwa, n.k, ambapo katika vitu hivi hakuna sharti la mwaka mmoja kwa misingi kwamba zaka kwenye vitu hivyo ni aina ya *zaka* ya mapato.”[16]

Zaka ndio tiba na suluhisho bora la matatizo yanayosababishwa na hatua ya kugeuza mali kuwa mgogoro wa kijamii.

16. Qaradawi, Yusuf, Fiqh al-Zakah: A Comparative Study of Zakah,Regulations and Philosophy in the Light of Qur’an and Sunnah,kimetafsiriwa na Monzer Kahf, Scientific Publishing Center King Abdulaziz University, Jeddah, kwenye mtandao

5. Mmiliki wa mali hizo lazima awe na haki ya umiliki isiyogawika na ya moja kwa moja.

Wale wanaotoa zaka wanatakiwa kuwa waangalifu sana kuhusu **tamlik na taharri**, kwa sababu uhalali wa Zaka unategemea vitu hivi. Kama ilivyoelezwa hapo awali, tamlik ina maana ya kutoa au kuhamisha umiliki wa Zaka, kwa maneno mengine yule anayepewa Zaka lazima apewe umiliki kamili wa zaka husika. Taharri, kwa upande mwingine ina maana ya kufanya utafiti kabla ya kutoa zaka. Yaani kufanya utafiti ili kujua iwapo mpokeaji wa zaka ni mtu anayestahili kupewa au la. Kama mtu asiyekuwa na sifa akipewa Zaka, na baadae ikadhihirika kuwa mpokeaji hayupo katika orodha ya makundi manane yanayostahiki kupewa zaka ambayo yametajwa katika Qur'an Tukufu, zaka husika huwa imebatilika na itatakiwa kutolewa upya. Lakini iwapo mhusika alifanya utafiti kabla ya kutoa zaka yake, lakini baadae ikadhihiri kuwa aliyepewa hakustahili, basi hakutokuwa na haja ya kutoa upya.

Kampeni kabambe ya infaq na utoaji huduma inahitajika katika jamii yetu, ambapo hisia za undugu zimedhoofika, amani na utulivu katika jamii vimepotea, na chuki na uadui vimezidi.

Kanuni nyingine inayohusu Zaka ni kutowasahau wanafamilia na jamaa. Wanadamu awali ya yote wana haki kwa nafsi zao wenyewe, kisha huja haki za wanafamilia na kisha haki za ndugu na jamaa. Mpangilio huo huo wa haki pia unazingatiwa katika sheria ya mirathi. Kipaumbele katika mpangilio wa haki hizo hutegemea vitu viwili: kwanza, nguvu na ukaribu wa uhusiano, na pili, ni kiwango cha umasikini na haja.

---

wa internet juzuu 1, uk. 71 < http://islamiccenter.kaau.edu.sa/arabic/Index.htm>

Kuwatanguliza ndugu juu ya watu wengine haina maana kumpa zaka ndugu yako hali ya kuwa kuna mtu mwenye shida kubwa. Kipaumbele hutolewa kwa ndugu iwapo kiwango cha uhitaji ni kilekile. Kiwango cha uhitaji daima kinatakiwa kuzingatiwa. Kama mtu asiyekuwa ndugu ana haja zaidi, basi ndugu hawezi kupendelewa.

Hatua na kanuni hizi zote ni ishara inayoonyesha jinsi Uislamu, kwa upande mmoja, unavyohamasisha huruma na, kwa upande mwingine, unavyozingatia uwiano. Kwa sababu tunda la kwanza la imani ni huruma. Wale wasiokuwa na huruma katika nyoyo zao hawawezi kuhesabiwa kuwa ni waumini wa kweli. Bismillah, ambayo imewekwa kama mwanzo wa kila jambo jema, na Fatiha, ambayo ni sura ya kwanza ya Qur'an Tukufu, zinaanza na sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu za Rahman (Mwingi wa Rehema) na Rahim (Mwenye kurehemu). Maisha ya mitume na maisha ya marafiki wa Mwenyezi Mungu Mtukufu yamejaa mifano tele ya huruma. Maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w) yasemayo: "Wahurumieni walio ardhini ili mpate kuhurumiwa na walio mbinguni" yanaashiria kwamba huruma ya Muislamu inatakiwa kuwajumuisha na kuwaenea viumbe wote. Ibada za kijamii zinazohusisha mali, kama vile Zaka, infaq na ushr, zote zinadhihirisha huruma hii.

Aina na viwango vya mali zinazotolewa Zaka

Kiwango cha chini cha mali inayotakiwa kulipiwa zaka kwa upande wa kondoo na mbuzi ni pale watakapofikia idadi ya kondoo/mbuzi 40, kwa ng'ombe ni pale itakapofikia idadi ya ng'ombe 30 na kwa ngamia ni pale idadi yake itakapofikia ngamia 5. Kiwango cha chini cha dhahabu inayotakiwa kulipiwa zaka ni pale itakafikia gra-

Huruma ya Muislamu inatakiwa kuwajumuisha na kuwaenea viumbe wote. Ibada zinazohusisha umoja na kutoa mali, kama vile zaka, infaq na ushr, zote hizo ni dhihirisho la huruma.

mu 81,[17] na fedha italipiwa Zaka pale itakapofikia gramu 561. Wakati kuna kiwango maalumu kilichowekwa kinachotakiwa kulipwa ambacho ni 1/40 kwa dhahabu na fedha inayovuka kiwango cha kulipiwa zaka, kiwango kinachotakiwa kulipwa kwa mali nyingine kinatofautiana. Idadi ya mifugo inapobadilika, kiwango kinachotakiwa kulipwa hubadilika. Maelezo ya kina yanapatikana katika vitabu vya sheria za Kiislamu. Vilevile kiwango kinachotakiwa kwa madini na vyakula vya baharini kinaweza kupatikana katika vitabu hivyo.

Mali zote zinazohamishika na zisizohamishika zinazozalisha faida zinatakiwa kuwa na masharti ya Zaka. Mapato yanayotokana na mali zilizokodishwa yanatakiwa kuhesabiwa (kwa ajili ya kulipiwa zaka) baada ya kutoa madeni, gharama binafsi na za familia na gharama nyingine kama vile mishahara, matengenezo, kodi, na mengineyo. Ardhi zilizonunuliwa kwa madhumuni ya biashara yanahusika na Zaka kwa msingi wa bei yake ya awali (kama ipo, tofauti ya mfumuko wa bei inatakiwa kuongezwa kwenye mahesabu). Majengo yaliyojengwa kwa ajili ya kuuzwa, kwa upande mmoja, yanahusika na zaka kwa msingi wa thamani zake baada ya kuondoa gharama mbalimbali.

Mahesabu ya Zaka kwa hesabu ya biashara hufanywa kama ifuatavyo, iwapo italipwa na kampuni badala ya wenye hisa. Mapato na matumizi

"Watu ambao biashara wala kuuza hakuwashughulishi na kumdhukuru Mwenyezi Mungu, na kushika Sala, na kutoa Zaka. Wanaihofu Siku ambayo nyoyo na macho yatageuka."

(Qur'an, 24: 37)

17. Kuna mahesabu tofauti kwa upande wa dhahabu. Kiwango cha chini kinachoifanya ilazimikiwe kutolewa zaka huhesabiwa kwa gram 96, 90, 85 na 81. Hapa sisi tumechukua gram d 81 kwa maslahi ya maskini.

ya kwanza yanatakiwa kuhesabiwa ima mwanzoni mwa mwaka au mwishoni. Baada ya kuongeza madeni na amana zilizopokelewa, ima asilimia 2.5, ikihesabiwa kwa kufuata mwaka wa mwezi muandamo, au asilimia 2.6 ya pato kamili, ikihesabiwa kwa kufuata mwaka wa kalenda ya jua, itatakiwa kulipwa kama zaka. Ieleweke kuwa zaka kwa ajili ya mapato ya biashara haipimwi kwa kiwango cha faida tu bali pia kwa mtaji wa kampuni.

Makampuni ya uzalishaji (viwanda) kama vile viwanda, karakana, vinu, nk. Mahesabu ya zaka zake ni kama ifuatavyo:

1. Hakuna Zaka kwa vyombo vya mashine na mitambo. Hata hivyo, kama vimetengenezwa kwa dhahabu au fedha, basi thamani zake zinatakiwa kufanyiwa mahesabu kwa ajili ya Zaka.

2. Rasilimali (mitaji) ya biashara inahusika na zaka. Baada ya kutoa matumizi na gharama, zaka itahesabiwa kwa rasilimali iliyobaki.

3. Kama mishahara inalipwa kwa mwezi, basi kupanda na kushuka wakati wa mwaka hakutozingatiwa. Akiba (balance) tu ya mwisho wa mwaka ndiyo muhimu kwa mahesabu ya Zaka.

Zaka ikilipwa kwa pesa taslimu, basi ni muhimu sana kuzingatia athari za mfumuko wa bei katika mahesabu. Ili kulinda haki za masikini na kuweza kufanya mahesabu yenye usahihi zaidi, ni muhimu kuanzisha njia maalumu ya kuhesabu zaka. Vinginevyo, thamani halisi ya kiwango kilichotolewa inaweza kuwa chini ya asilimia 2.5.

"Na tukawafanya maimamu wakiongoa watu kwa amri yetu. Na tukawafunulia watende kheri, na washike Sala, na watoe Zaka; na walikuwa wanatuabudu Sisi tu."

(Qur'an 21: 73)

Masikini wataathirika, na wajibu wa Zaka hautotekelezwa kikamilifu.

Uislamu, kimsingi, uliagiza zaka ilipwe kwa vitu (siyo pesa). Kwa maneno mengine, inashauriwa zaka ilipwe kwa dhahabu kwa wale wenye dhahabu, fedha kwa wale wenye fedha, kondoo kwa wale wenye kondoo, ngano kwa wale wenye ngano na nguo kwa wale wanaomiliki nguo. Hata hivyo katika zama za Mtume (s.a.w) zaka ilikusanywa ima katika vitu (siyo pesa) na kwa pesa, na katika zama za Abu Bakr na Umar (r.a) hali iliendelea kuwa hivyo hivyo. Ndiyo maana hakuna tatizo katika zama zetu kulipa zaka kwa pesa taslimu.

"Angalieni! Nyinyi mnaitwa mtumie katika njia ya Mwenyezi Mungu, na wapo katika nyinyi wanao fanya ubakhili. Na anaye fanya ubakhili basi anajifanyia ubakhili mwenyewe. Na Mwenyezi Mungu si mhitaji, na nyinyi ndio wahitaji. Na mkigeuka atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi."

(Qura'n 47: 38)

Watu wanaostahili kupokea Zaka

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Wa kupewa sadaka ni mafakiri, na masikini, na wanaozitumikia, na wa kutiwa nguvu nyoyo zao, na katika kukomboa watumwa, na wenye madeni, na katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na wasafiri. Huu ni waajibu uliofaridhiwa na Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hekima." (Qur'an, 9: 60)

Aya hii kwa uwazi kabisa inaonyesha watu wanaostahili kupewa Zaka, ambao ni:

1. **Mafakiri:** wale ambao mali yao haifikii kiwango cha chini kabisa cha kutoa zaka au nisab. Watu walio katika kundi hili wanaweza kupewa zaka, hata kama wana kazi maalum ya kufanya.

2. **Masikini:** wale ambao ni mafakiri wa hali ya chini kabisa na ambao hawana hata chakula cha kila siku.

3. **Wale wanaozitumikia Zaka (wanaozikusanya)**

4. **Wale ambao wanatakiwa kutiwa nguvu nyoyo zao**

5. **Watumwa:** Watumwa ambao wameingia makubaliano na wamiliki wao ili wapate kujikomboa.

6. **Wale wenye madeni:** Wale wenye madeni makubwa yanayozidi mali zao na ambao wameshindwa kabisa kuyalipa wanaweza kupewa zaka.

7. **Katika njia ya Mwenyezi Mungu:** wale wanaopambana katika njia ya Mwenyezi Mungu, wale waliokwenda katika Hijja na wakaishiwa njiani, wale wanaosoma na kufundisha ili wawe na manufaa kwa jamii na umma wa Kiislamu.

8. **Wasafiri:** wasafiri ambao wameishiwa njiani na kubaki bila chochote, hata kama huko kwao ni matajiri wanaweza kupewa zaka.

Zaka hupewa mtu mmoja mmoja kwa mahitaji yao ya msingi. Mashirika hayawezi kupewa zaka. Ndiyo maana misikiti, shule na hospitali haziwezi kujengwa kwa mapato ya zaka.

Orodha ya wale wasiopewa Zaka

Mama, baba, bibi, babu, wajukuu wa kiume na wa kike, matajiri na wasiokuwa Waislamu hawawezi kupewa zaka. Aidha, mke na mume hawawezi kupeana *zaka*.

Zaka hupewa mtu mmoja mmoja kwa mahitaji yao ya msingi. Mashirika hayawezi kupewa zaka.

Ndiyo maana misikiti, shule na hospitali haziwezi kujengwa kwa mapato ya zaka. Karamu wanazoandaliwa masikini haziwezi kuhesabiwa kuwa ni zaka, kwa sababu hakuna uhamishaji wa umiliki.

Adabu bora katika sadaka ni kutoa sadaka kwa siri sana kiasi kwamba "mkono wa kushoto usijue kilichotolewa na mkono wa kulia." Watu wanaochunga adabu hii wamepewa habari njema ya kwamba watakuwa chini ya kivuli cha Mwenyezi Mungu katika ile siku ambayo hapatakuwepo na kivuli isipokuwa kivuli Chake.

'Ushr (moja ya kumi): Zaka ya mazao ya kilimo

1. Kwa mujibu wa Abu Hanifa (q.s) hakuna kikomo cha nisab kwa mazao ya kilimo. Kwa maneno mengine, katika mazao ya kilimo hakuna sharti la kiwango kinachotakiwa kufikiwa na mali husika ili istahili kulipiwa zaka wala sharti la kupitiwa na mwaka. Kwa mujibu wa Abu Yusuf na Muhammad Shaybani kiwango cha chini kinachotakiwa kufikiwa na mazao ya kilimo ili yastahili kulipiwa zaka ni kilo 653.

2. Iwapo mazao yatavunwa kwa zaidi ya mara moja kwa mwaka, basi 'ushr italipwa kwa kila uvunaji kutokana na aina ya mazao.

3. Tofauti na zaka, mazao ya ardhi za watoto na wendawazimu yanatakiwa kulipiwa'ushr . vilevile inaweza kulipwa kutoka katika mirathi ya marehemu.

4. Mazao ya kilimo yawe yanaweza kuhifadhika kwa kipindi cha mwaka. Ndiyo maana hakuna 'ushr kwa matunda na mbogamboga, kwa kuwa ni mazao yanayoharibika.

5. Mazao ya kilimo yaliyopata maji bila kutumia gharama, kwa mfano maji ya mvua, mto au ziwa, basi 'ushr itakayolipwa ni moja ya kumi. Kama mazao yanahitaji gharama za ziada kwa

zaidi ya nusu mwaka, basi kiwango kinachotakiwa kutolewa kitashuka mpaka kwenye moja ya ishirini. Hata hivyo kiwango hicho kinapopungua mpaka kwenye moja ya ishirini, gharama nyingine kama vile mbegu, wafanyakazi, udhibiti wa wadudu/wanyama waharibifu, n.k hazitaondolewa.

6. ‘Ushr inapolipwa kwa mazao husika, kama vile zeituni, ufuta na mbegu za alizeti, basi hakuna haja ya mafuta yake kuyalipia ‘ushr. Lakini mtu anayenunua mafuta hayo kwa malengo ya biashara atatakiwa kulipa zaka ya mapato ya biashara.

7. Hairuhusiwi kulipa ‘ushr kwa kutumia makadirio ya kabla ya mavuno.

8. Mmiliki akitaka kutumia mazao yake ya kilimo kabla ya kulipa ‘ushr, anatakiwa kufidia ‘ushr ya kile kilichotumiwa. Kwa mfano kama akitumia kilo 10 za mazao husika atatakiwa kulipa kilo moja ya ziada kama ‘ushr.

9. Ardhi zinazokamatwa na majeshi ya Kiislamu katika vita lakini zikawa hazijagawiwa kwa Waislamu huitwa ardhi za miri. Waislamu ndiyo wanaomiliki ardhi hizo, lakini haki ya kuzitumia hupewa wakulima. Wakulima wanakuwa kama wapangaji na kodi tozo wanazolipa ni sawa na kodi za pango. Katika aina hii ya ardhi hakuna ‘ushr au aina nyingine yoyote ya zaka. Katika zama za Dola ya Uthmaniyya, ardhi zilikuwa chini ya mfumo huu.

“Hao ndio wanao sema: Msitoe mali kwa ajili ya walioko kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, ili waondokelee mbali! Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye hazina za mbingu na ardhi, lakini wanafiki hawafahamu.”

(Qur’an 63: 7)

Badaye maeneo makubwa ya ardhi za miri mjini Anatolia na Rumelia yaliuzwa kwa watu binafsi katika kubadilisha umiliki wa ardhi. Kwa namna hii aina mpya ya umiliki ardhi iliibuka ambayo ilijulikana kama ardhi za mulki. Aina hii ya ardhi lazima ilipiwe ‘ushr, kwa sababu zinaweza kununuliwa na kuuzwa. Iwapo serikali haukusanyi ‘ushr, basi Waislamu wenyewe wanatakiwa kuihesabu na kuigawa kwa wahusika.

“Mfanyabishara mwenye kuaminika, mwaminifu na muumini atakuwa pamoja na mashahidi siku ya Kiyama.”

(Ibn Majah, Tijarah, 1)

Mahojiano Kuhusu Wakfu, Zaka Na Infaq[18]

MALI NI AMANA

Umiliki una maana gani kwa mujibu wa Uislamu?

Kulingana na mtazamo wa Kiislamu, umiliki wa kweli siyo wa mtu mmoja au jamii, bali moja kwa moja ni wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Waja wamepewa haki ya kutumia mali hizo kwa kipindi cha muda tu na chini ya masharti yaliyowekwa. Kwa hiyo, waja hawawezi kutumia mali kama wapendavyo. Mali hiyo inatakiwa itumike kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa na mmiliki halisi, yaani Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hii ina maana kwamba matajiri wanalazimika kushirikiana mali na masikini na wale wenye shida kutokana na taratibu zilizowekwa na Uislamu. Lengo hapa ni kuwa muumini ambaye watu watakuwa salama na kufaidika na mikono, ulimi na mali yake.

Tabia na sifa hii ni matokeo ya kutambua kwamba mali ni amana ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu amewakabadhi waja Wake. Kuitumia mali kinyume na ukweli huu itakuwa ni kuifuja amana na hili litasababisha matatizo mengi ya kijamii kama ilivyo katika jamii ya sasa.

"Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kila nafsi iangalie inayo yatanguliza kwa ajili ya Kesho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo habari ya mnayo yatenda."

(Qur'an, 59: 18)

18. Sehemu hii imechukuliwa kutoka katika mahojiano baina ya jarida la Altinoluk na mwandishi wa kitabu hiki.

Ni ipi nafasi ya utajiri kutokana na mtazamo wa Kiislamu?

Uislamu unawahamasisha wafuasi wake kupata utajiri kwa njia za halali. Nguzo mbili katika nguzo tano za Uislamu hutakiwa kufanywa na Waislamu wenye mali. Nguzo hizo ni Hijja na Zaka.

Kwa namna moja Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaambia waja Wake kwamba "Tafuteni mali kwa njia halali kisha toeni Zaka na mtembelee nyumba Yangu."

Kwa upande mwingine Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema: *"Mkono wa juu ni bora kuliko mkono wa chini (yaani yule atoaye sadaka ni bora kuliko yule anayeipokea)."* (Bukhari, Zakat, 18). Hivyo anawahamasisha watu kuwa watoaji, na kuwahamasisha kupendelea kuwa watoaji kuliko kuwa wachukuaji.

Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema: "Mkono wa juu ni bora kuliko mkono wa chini (yaani yule atoaye sadaka ni bora kuliko yule nayeipokea)."

(Bukhari, Zakat, 18).

Mambo gani yanayotakiwa kuzingatiwa katika utafutaji wa mali uliohamasishwa na Uislamu?

Biashara imehamasishwa katika Uislamu. Hata hivyo uhamasishaji huu hauna maana ya kuiacha huru bila hatua zozote, kama ilivyo katika chumi za kiliberali, na haujaiwekea kikomo kabisa kama ilivyo katika mtazamo wa kisoshalisti. Kwa kuzingatia faida binafsi na za kijamii, biashara imewekewa mipaka kama ifuatavyo na baadhi ya kanuni zinazohusu eneo la utendaji wake na namna inavyotakiwa kufanywa.

Hairuhusiwi kabisa kufanya biashara ya bidhaa haramu zilizoharamishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hii ina maana kwamba sharti la

kwanza la biashara kuwa halali ni kuwa eneo la shughuli yake lazima liwe halali.

Masharti mengine ni namna inavyotakiwa kufanywa.

Ni haramu kulimbikiza bidhaa na kuzifanya ziadimike sokoni kwa lengo la kuongeza bei, na jambo hili hujulikana kama ulanguzi. Katika istilahi ya Kiislamu hujulikana kama ihtikaar na imeharamishwa vikali.

Uharamisho mwingine katika sheria ya biashara ya Kiislamu ni udanganyifu na kutoza bei kubwa zaidi katika miamala. Hii ina maana ya kutumia nafasi ya mteja kutoelewa, kutojua, kutokuwa na uzoefu au matatizo ya kiakili na kumtoza bei kubwa zaidi, kwa mfano kununua bidhaa ya wizi kwa bei ya chini sana, au bidhaa yenye thamani kuilipia kwa bei iliyo chini mno ya thamani yake.

Kwa upande mmoja, muuzaji anatakiwa kueleza mapungufu ya bidhaa yake kumwambia mnunuzi. Kwa upande mwingine, ni haramu mnunuzi kuzungumza mabaya kuhusu bidhaa husika kwa lengo la kupunguza bei yake.

Kwa kuwa lengo letu siyo kuzungumzia masharti yote ya sheria ya kibishara ya Kiislamu, itatosha kuzungumzia sharti moja la mwisho kuhusu suala hili.

Chini ya mazingira maalumu, kiwango cha faida (bei) kinaweza kupangwa. Suala hili ni muhimu zaidi katika kipindi cha majanga ya vita, magonjwa ya milipuko, na mengineyo. Uislamu unawaruhusu viongozi wa dola kuchukua hatua muhimu na

“Hao ndio wanao sema: Msitoe mali kwa ajili ya walioko kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, ili waondokelee mbali! Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye khazina za mbingu na ardhi, lakini wanaafiki hawafahamu.”

(Qur’an 63: 7)

kutoa taratibu za kisheria kwa msingi wa maslahi ya umma. Kuna mifano mingi ya msingi huu katika sheria ya biashara. Ni lazima Waislamu kutii kanuni za watawala wao, hususan zile zinazohusu kiwango cha faida (bei), kwa ajili ya maslahi ya umma. Hata hivyo, kuna baadhi ya vipengele vya sheria ya biashara, ambapo upangaji wa faida (bei) hauwezi kuhusika kwa sababu ya gharama kubwa.

Kuna hadith mbalimbali za Mtukufu Mtume (s.a.w) zinazohamasisha biashara. Baadhi yake ni kama ifuatavyo:

"Mfanyabishara mwenye kuaminika, mwaminifu na muumini atakuwa pamoja na mashahidi siku ya Kiyama." (Ibn Majah, Tijarah, 1)

"Mfanyabishara jasiri asiyelimbikiza bidhaa zake ni mwenye kubarikiwa; na mlanguzi ni mwenye kulaaniwa." (Ibn Majah, Tijarah,6)

"Mfanyabishara mwoga ni mwenye kunyimwa; mfanyabishara jasiri ni mwenye kubarikiwa." (Daylami, Musnad, II, 79)

"Chakula bora na cha halali anachokula mtu ni kile anachokichuma yeye mwenyewe." (Ibn Majah, Tijaraha, 1)

"Mfanyabishara mwenye kuaminika, mwaminifu na muumini atakuwa pamoja na mashahidi siku ya Kiyama."

(Ibn Majah, Tijarah, 1)

Muislamu akipata utajiri kwa misingi ya Uislamu, je anaweza kutumia mali yake kwa uhuru?

Kuna vitu vingi vinavyochukuliwa kama vitu vyenye thamani, kwa mfano, wanyama, mali, vito vya mapambo, na vingine vingi. Uislamu umewe-

ka baadhi ya masharti na sheria kwa mataumizi ya vitu hivi. Kwa mfano katika Uislamu ni haramu kuwapa punda chakula kidogo na kuwabebesha mizigo kupita kiasi. Kutumia mali kwa ajili ya kumdhuru mtu nalo pia ni haramu. Huwezi kujenga ukuta mrefu mno kuzunguka bustani yako ili kumzuia mtoto wa jirani yako. Huruhusiwi kuharibu bidhaa za biashara, hasa chakula, zinazohitajika na jamii kutokana na matumizi yasiyokuwa sahihi. Kwa mfano, huwezi kutupa jalalani mboga mboga kutoka bustanini mwako kwa lengo la kupinga kitu, kwa sababu zinatakiwa kutumiwa na umma.

Huwezi kushusha uzalishaji wa kiwanda chako ili tu kuongeza faida yako. Utengenezaji wa ulaghai wa bei unaofanywa siku hizi na makundi ya kibishara yajulikanayo kama muungano wa wakiritimba wanaooungana ili kudhibiti biashara nao pia ni miongoni mwa mambo yaliyoharamishwa na Uislamu.

Ni yapi majukumu na wajibu wa kifedha kwa Muislamu mwenye mali?

Zaka ndiyo wajibu muhimu zaidi katika mali ya Waislamu wenye mali. Neno zaka linatokana na msamiati wa lugha ya Kiarabu wa tazkiyah, wenye maana ya utakaso. Kwa maneno mengine, zaka huitakasa mali. Kwa kuwa imeamrishwa na Mwenyezi Mungu, zaka ni haki ya masikini iliyo katika mali za matajiri. Kuizuia zaka na kutoitoa ni sawa na kupora na kunyang'anya mali ya mtu. Mwenyezi Mungu aliweka kiwango cha chini kinachotakiwa kutolewa zaka (nisab au kiwango cha utajiri) kwa baadhi ya mali. Mali iliyozidi kiwango hiki inatakiwa kutolewa Zaka.

Chakula bora na cha halali anachokula mtu ni kile achokichuma yeye mwenyewe."

(Ibn Majah, Tijaraha, 1)

Utajiri kwa mujibu wa viwango vya Kiislamu ni tofauti sana na viwango vya matajiri wakubwa wa leo. Gramu 81 za dhahabu au mali sawa na hiyo ndiyo kiwango cha kisheria cha utajiri kwa mujibu wa Uislamu. Kama Muislamu anamiliki mali iliyo sawa na kiwango cha nisab au zaidi, anatakiwa kutoa zaka yake baada ya kupitiwa na mwaka mmoja wa kalenda inayofuata muandamo wa mwezi.

Katika Uislamu asilimia mbili na nusu ya mali ni ya masikini. Wanatakiwa kupewa haki yao kwa uzuri kadri iwezekanavyo. Kwa maneno mengine zaka ni kuwafanya masikini wawe washirika katika mali kwa asilimia mbili na nusu. Zaka ni kiwango cha chini anachotakiwa kulipwa masikini. Hata hivyo zaka hupanda juu mpaka asilimia kumi kwa mazao ya kilimo, na kwa wanyama kiwango huwa tofauti tofauti kulingana na aina ya mnyama.

Mali vile vile inatakiwa kupambwa kwa shughuli za ziada za sadaka, infaq, n.k. Abu Bakr (r.a) alitangaza vita kwa wale waliokataa kulipa zaka, jambo linaloonyesha umuhimu wa suala hili.

Mshirika mwenye nguvu anapokataa kutoa haki za mshirika mnyonge, anakuwa dhalimu na mnyang'anyi. Mali zake zinaendelea kutokuwa safi.

Wale wanaostahili kupewa zaka wametajwa kwa uwazi kabisa ndani ya Qur'an Tukufu. Wanaotakiwa kupewa zaka ni masikini, wenye madeni, wanafunzi wale wanaofanya kazi katika njia ya Mwenyezi Mungu na wasafiri walioishiwa mahitaji. Leo Waislamu wenye mali wanapaswa kutoa zaidi ya kile wanachotakiwa kutoa, kwa sababu ya matatizo magumu ya kifedha ya ulimwengu wa sasa.

Mali vile vile inatakiwa kupambwa kwa shughuli za ziada za sadaka, infaq, nakadhalika.

Pia tunapaswa kuzungumzia umuhimu wa suala la ‘ushr, ambalo limepuuzwa katika ulimwengu wa Kiislamu kwa kitambo cha muda. Usimamizi wa ardhi katika Dola ya Uthmaniyya ulikuwa ni utaratibu unaoitwa miri. Lakini leo mfumo umebadilika na kuwa usimamizi wa ardhi wa mulki. Tofauti na ardhi za miri, ardhi za mulk zinaweza kutumika kwa miamala mbalimbali. Mwenye kumiliki ardhi kwa utaratibu wa milk anaweza kuitumia vyovyote atakavyo. Kwa namna hii anatakiwa kulipa asilimia tano ya mavuno kama alitumia gharama za umwagiliaji; kama hakutumia, basi kiwango kinapanda mpaka asilimia kumi, ambacho katika istilahi ya kidini hujulikana kama ‘ushr. Wale wasitoa ‘ushr zao ni mnyang’anyi sawa na wale wasiotoa zaka. Wanaiba haki za masikini na za wale wanaofanya juhudi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Suala hili linatakiwa kuchukuliwa kwa umakini na Waislamu wanatakiwa kujifunza masuala husika kutoka katika vitabu au kuwauliza wasomi wa kidini.

Mahitaji ya maskini wakati mwingine huvuka kiwango cha kawaida. Wakati huo Waislamu wenye mali katika jamii yetu huwa na umuhimu zaidi ili kuhakikisha amani na utulivu.

Umeeleza kwamba kuna njia nyingine za kuwasaidia masikini mbali na Zaka. Unaweza kuliweka wazi jambo hili?

Hakika, hizi siyo tozo za wajibu kama Zaka, bali ni zenye kuhamasishwa na za hiari. Hizi zinaitwa infaq, ithaar (kutoa zaidi) na kuitoa mali wakfu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Zaka ni malipo ya wajibu na ya lazima yanayofanywa ili kuwasaidia masikini. Pia mali inatakiwa kupambwa kwa sadaka za hiari, infaq na ithaar.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur’an Tukufu:

"...na wanaokusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wabashirie habari ya adhabu iliyo chungu." (9: 34)

Kama tunavyoona katika Aya hii, mafikio ya wale wanaonyang'anya haki za masikini yatakuwa motoni. Tunatakiwa kutafakari kuhusu onyo hili la Mwenyezi Mungu Mtukufu na kujaribu kutoa zaidi ya kiwango cha wajibu cha asilimia mbili na nusu. Kwa maana imeelezwa katika Aya nyingine kuwa:

"...Na wanakuuliza watoe nini? Sema: Kilicho chepesi..." (Qur'an, 2: 219)

Nchi yetu imo katika kipindi kigumu kiuchumi. Je sasa hivi zaka na sadaka zetu huenda zikawa na umuhimu mkubwa zaidi?

kama ulivyosema, leo hii nchi yetu imo katika mgogoro wa kidunia na kiroho, kijamii na kiuchumi. Ndiyo maana kampeni kubwa ya utoaji sadaka inahitajika. Tunapaswa kuhisi huzuni kwa wagonjwa, wenye shida, wanyonge na vijana wapweke, kwa sababu huruma ni habari njema kwa mafikio yetu ya milele na amani ya akili katika ulimwengu huu. Mbali na kutoa Zaka, ndugu zetu wenye mali wanatakiwa kwenda mbali zaidi kwa kuongeza juhudi za heri. Kwa maana Zaka hukidhi kiwango cha kawaida cha mahitaji ya lazima ya masikini. Lakini mahitaji ya masikini wakati mwingine huvuka kiwango cha kawaida. Wakati huo Waislamu wenye mali katika jamii yetu huwa na umuhimu zaidi ili kuhakikisha amani na utulivu. Hatupaswi kujifunga kwa kutoa Zaka pekee yake ilhali msaada wetu unahitajika zaidi. Daima tunatakiwa kukum-

Abu Huraira amesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alisema: Kiyama hakitosimama mpaka mali iwe nyingi mno kiasi kwamba mtu atapeleka Zaka yake na hatopata mtu wa kuipokea na mpaka ardhi ya Arabia itakuwa na malisho na mito mingi.

(Muslim, Kitab al-Zakat, 74)

buka kuwa tungekuwa masikini kama wao na wao wangekuwa matajiri kama sisi. Hivyo kutoa sadaka pia ni njia ya kumshukuru Mola wetu.

Kama ambavyo tuna jukumu na wajibu wa kuwafundisha watoto wetu misingi ya dini yetu, pia tuna wajibu wa kuwapandikiza hamasa ya kuwa na infaq na kuwazoesha wajibu wa muumini wa kuwasaidia wenye shida. Tukishindwa kuwazoesha wakiwa bado wadogo, basi itakuwa ni kuangamiza mustakabali wao. Watoto wetu wanapaswa kulelewa hali ya kuwa wakijua kwamba mmiliki halisi wa mali ni Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa namna ambayo watajiona kuwa wao ni sawa na mhasibu wa benki au mtu aliyepewa amana ya watu kuitunza. Vizazi ambavyo vimelelewa katika njia hii vinaweza kufufua na kuhusisha kampeni za utoaji sadaka za historia yetu, na historia yetu imejaa mifano mingi ya shughuli za infaq.

Ngoja nikupe mfano: mwaka 1913 pale majeshi ya Kiuthmaniyyah yalipokuwa yakishindwa vita huko Balkan, kundi la Jawhari Brothers na wakuu wa jumuia za Kiislamu nchini India walikuwa wakifanya maandamano, wakiwatolea wito Waislamu wote kuwasaidia Wauthmaniyyah na kuwahamasisha kutoa Zaka na sadaka kuwapa Wauthamaniyyah. Palitokea matukio mengi yenye kusisimua sana. Kwa mfano, kijana mmoja alitoa kanzu yake na mzee mmoja akatoa sanda yake.

Huruma huzipa utulivu nyoyo katika dunia hii na kuwa wokovu wa milele huko Akhera.

Matukio haya na mengine mengi yaliimarisha ustaarabu mkubwa wa kujitolea. Kuonyesha ithaar na kuwatanguliza wengine, hali ya kuwa wewe mwenyewe unakihitaji, ni jambo linaloonye-

sha upana wa moyo. Ndiyo maana, kwa maoni yangu, kuwapa zaka wale wanaofanya juhudi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni muhimu zaidi kuliko makundi mengine yanayostahili kupewa Zaka.

Tunashuhudia kwamba taasisi za kidini zimefanya kazi kubwa sana katika shughuli za heri. Unaweza kutueleza mtazamo wako kuhusu wakfu?

Urahisishaji wa infaq hupelekea kuanzisha waqfu mbalimbali. Waqfu ina maana ya kufanya mali ya Mwenyezi Mungu idumu milele. Ni kutenga na kutoa mali kwa madhumuni ya heri mpaka milele. Lengo la kuanzisha waqfu ni kuwahurumia-viumbe kwa huruma na upendo kwa ajili ya Muumba wao. Ni juhudi za kujitolea nafsi, mali na kila kitu kwa lengo la kununua Pepo. Kama tulivyoeleza hapo awali, katika Dola ya Uthmaniyyah kulikuwa na taasisi za kidini elfu 26. Taasisi hizi ziliendeleza shughuli zake za heri kupitia watu wenye ithaar. Pia palikuwepo na vituo vya ugawaji wa misaada. Kwa hakika katika zama hizi tuna haja kubwa mno ya aina hizi za taasisi. Katika wakati wetu huu tunapaswa kuzifufua, kuzihuisha taasisi hizi na kuzifanya ziwahudumie wenye shida.

Ninashangaa ni kwa kiwango gani matajiri Waislamu wanahisi uchungu na maumivu ya ndugu zao masikini. Je wanajua jinsi ndugu zao masikini wanavyoishi? Je wanajua kwamba watu hao wapo?

Uhai na mali tulizonazo ni amana tuliyopewa. Siyo hivyo tu, bali kila kitu katika dunia hii ni amana. Kuzilinda amana hizi kutatufanya tupate

"Sema: Kwa hakika Mola wangu Mlezi humkunjulia riziki na humdhikisha amtakaye katika waja wake. Na chochote mtakacho kitoa Yeye atakilipa. Naye ni Mbora wa wanao ruzuku."

(Qur'an 34: 39)

baraka. Infaq inaweza kutekelezwa siyo tu kwa mali pekee. Inaweza kufanywa kwa kila kitu tulichojaaliwa.

Njia bora ya kufanya infaq ni kuishi kulingana na taratibu na kanuni za Uislamu na kuwa Muislamu wa mfano. Maswahaba walijitolea nafsi zao kuupeleka Uislamu kwenye pembe za mbali za dunia. Katika zama hizi kuishi katika Uislamu kama walivyoishi na kwa namna na kwa hamasa ile ile ndiyo njia bora ya kufanya infaq. Sababu hasa ya matatizo makubwa ya kiuchumi katika nchi yetu leo hii, kama vile mgogoro wa mfumuko wa bei, siyo sababu ya kimaada bali ni ya kimaanawi na kiroho. Mwenyezi Mungu Mtukufu ameondosha baraka kwa waja Wake kwa sababu ya waja hao kufanya usaliti katika amana aliyowapa. Matatizo na shida yameanza kuandamana moja baadala jingine. Historia yetu ni shahidi tosha na bora anayetuonyesha jinsi Zaka na infaq vinavyoleta amani na utulivu katika jamii.

Tumeona katika historia yetu kwamba watangulizi wetu waliwafikiria majirani na wenye shida sana kama walivyojifikiria wao wenyewe au zaidi. Leo, kwa upande mwingine, watu wengi wamebadilika kuwa wabinafsi kutokana na athari za ubepari. Unadhani ni zipi sababu na athari za mabadiliko haya?

Kama Waislamu wote wangetoa zaka zao kikamilifu, baada ya muda asingebaki Muislamu yeyote anayehitaji Zaka. Kwa upande mwingine, kama wale wote wanaomiliki ardhi za kilimo wakitoa ‘ushr zao kwa mazao ya kilimo na zaka za mifugo yao,

“Sadaka unayoitoa hali ya kuwa una siha, kwa shingo upande na hofu ya kufukarika na tamaa ya kuwa na mwenye mali. Usiichelewesheshe mpaka wakati kifo kinapokaribia na ukaanza kusema ‘Mpeni kiasi kikubwa fulani na fulani, na kiasi kadhaa kwa fulani na fulani.’ Lakini utasema hivyo hali ya kuwa mali hiyo imeshakuwa ya fulani na fulani (umeshachelewa).”

(Bukhari, Kitab al-Zakat, 11)

ninaamini hatobaki masikini yeyote katika jamii yetu. Kuna mifano mingi ya jambo hili katika historia yetu. Wakati wa Ukhalifa wa Omar bin Abd al-Aziz hakubaki masikini yeyote, kwa sababu matajiri walikuwa wakitoa Zaka zao kikamilifu.

Watangulizi wetu walikuwa wakishindana kutoa sadaka. Walifikia kiwango cha juu mno cha infaq au ithaar. Ithaar ina maana ya "kutoa sana kile ulicho nacho" au "kumsaidia nduguyo japokuwa wewe mwenye wakihitajia kitu hicho" jambo ambalo kwa bahati mbaya ni nadra sana kuapatikana katika jamii yetu ya sasa. Kufikia daraja ya ithaar siyo jambo linalotarajiwa kufanywa na kila mtu. Lakini, kiwango cha ithaar kilikuwa juu mno katika jamii zilizolelewa na Mitume na marafiki wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Leo tuna haja ya kujikita kwenye infaq na kuwahamasisha watu kutoa. Ni katika wajibu mkubwa wa jamii yetu kuanzisha taasisi za kutoa mafunzo kwa vizazi vipya, na kujenga hospitali za kuwahudumia masikini na nyumba za matunzo kwa ajili ya wazee.

Zaka inatakiwa kutolewa namna gani? Kitu gani tunachotakiwa kukizingatia?

Muislamu kamili anapaswa kutoa zaka bila kuumiza hisia za masikini. Watangulizi wetu waliliangalia kwa ungalifu na umakini mkubwa sana jambo hili. Hapo zamani palikuwa na "mawe ya sadaka" msikitini. Waislamu wenye mali walikuwa wakiweka sadaka zao chini ya mawe haya na wale wenye shida walikuwa wakienda mahali hapo na kuchukua kiasi wanachohitajia. Watu wenye shida hawakuwa wakitumia vibaya njia hii na walikuwa

Sadaka iliyo bora kabisa ni kuufikisha ujumbe wa Uislamu kwa watu.

wakichukua kile kiasi tu wanachohitajia. Bado kuna mawe ya sadaka katika baadhi ya misikiti yetu. Kwa bahati mbaya vizazi vipya vinayaona mawe hayo lakini hawajui ni kitu gani. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika Aya ifuatayo:

"HAKIKA wamefanikiwa Waumini, ambao ni wanyenyekevu katika Sala zao," (Qur'an, 23: 1-2). Siyo katika Swala pekee bali pia katika Zaka zetu tunapaswa kuwa wanyenyekevu. Adabu za sadaka zimeelezewa katika Aya ifuatayo:

"Enyi mlioamini! Msiharibu sadaka zenu kwa masumbulizi na maudhi, kama anaye toa mali yake kwa kuwaonyesha watu, wala hamuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho. Basi mfano wake ni kama mfano wa jabali ambalo juu yake pana udongo, kisha likapigwa na mvua kubwa, ikaliacha tupu. Basi hawatakuwa na uweza wowote kwa walivyo-chuma. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu makafiri." (Qur'an, 2: 264)

Kwa hakika tunatakiwa kutoa sadaka zetu zikiandamana na upendo na huruma kana kwamba tunajipa wenyewe. Tunapaswa kuwaza kuwa tungeweza kuwa masikini. Tunapaswa kujua kuwa hisia zetu huathiri hisia za mpokeaji wa Zaka. Ikhlasi ya mpokeaji itaonekana kulingana na Ikhlasi za nyoyo zetu. Kwa upande mwingine tukitaka kutoa Zaka yetu haraka haraka na kuondoka basi baraka zetu za kiroho zitakuwa katika kiwango cha hisia zetu.

Adabu yetu katika kutoa Zaka nayo pia ni msingi mkuu. Tukitoa Zaka zetu, kana kwamba tunaiwasilisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kama alama ya

"Toa sadaka kwa sababu utafika muda ambao watu watakwenda na sadaka zao kutafuta watu wa kuwapa lakini hatopata yeyote wa kuipokea."

(Bukhari, Fitan, 24)

shukrani yetu kwa baraka Zake, tutapata manufaa makubwa sana ya kiroho kutokana na Zaka hiyo. Tunatakiwa kuwaheshimu na kuwashukuru masikini kwa kutuwezesha kutekeleza mojawapo ya nguzo za Uislamu. Ndiyo maana tunatakiwa sisi wenyewe kwenda kwa masikini na kuwapa Zaka zetu. Hadith isemayo kwamba sadaka iliyopatikana kwa halali hupokelewa kwanza na Mwenyezi Mungu Mtukufu kabla ya kwenda kwa masikini[19] ni hadith muhimu sana. Hii ina maana kwamba tunatakiwa kutoa Zaka kana kwamba tunampa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tukitoa Zawadi, tuhudhurishe moyo katika kila kitu. Kama tunavyokuwa makini sana kwenye samani tunazonunua, tunatakiwa kuwa makini kwenye Zaka tunayompelekea mhusika. Tusijizuie hata tabasamu dogo au maneno mazuri hata kama ni machache. Ramazanoglu Mahmud Sami (q.s) alipokuwa akimuona masikini, kama akiwa katika gari, angesimamisha gari, akashuka, akatabasamu na kutoa sadaka yake. Ithaar, upole na upendo ni sifa zinazotakiwa kumpambanua Muislamu.

Tena Qur'an Tukufu inaeleza kuhusu adabu za *sadaqa na infaq:* **"Enyi mlioamini! Toeni katika vile vizuri mlivyovichuma, na katika vile tulivyo kutoleeni katika ardhi. Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya, hali nyinyi wenyewe msingevipokea ila ingekuwa mmefumba macho. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha na Msifiwa."** (Qur'an Tukufu, 2: 267)

Imani ni amali ya moyo na huruma ni tunda la roho. Tunatakiwa kuwahurumia wale walio ardhini, ili tuhurumiwe na aliye mbinguni.

Jukumu la mja ni kutekeleza ibada hii ya kijamii kwa upendo, hamasa na msisimko. Rumi

19. Muslim, Kitab al-Zakat, 63.

(q.s) anasema: *"Mahali panapotazamwa na Mwenyezi Mungu ni moyoni."* Imani ni amali ya moyo na huruma ni tunda la roho. Tunatakiwa kuwaonyesha huruma wale walio ardhini ili wale walio mbinguni watuonee huruma. Tukifanya hivyo, Mola Wetu Mtukufu, Mwenye nguvu na uwezo, atatuhurumia na kutusamehe.

Upande wa kiroho wa Zaka na infaq nao pia ni wenye kuvutia. Taasisi yetu ya Hudayi[20] hupokea msaada mbalimbali. Huwa tukijihisi amani kwa baadhi ya misaada. Hii hutokana na kiwango cha uhalali wa msaada husika. Kama mali yako ni ya halali, unajihisi amani ya akili na masikini humuombea mtoaji mara elfu, na huu ni upande wa kiroho wa amali hii.

Suala jingine muhimu ni kwamba masikini anayeeleza shida zake na yule asiyeweza kueleza shida zake, wote wana haki katika mali ya tajiri. Jambo hili limeelezwa ndani ya Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

"Na katika mali yao ipo haki ya mwenye kuomba na asiye omba." (Qur'an, 51: 19)

Katika Aya hii wale ambao heshima zao zinawazuia kuomba ndiyo wenye malezi bora na wenye adabu adhimu. Tusidanganyike na muonekano wao tukadhani kuwa siyo wenye kuhitaji.

Adabu yetu katika kutoa Zaka nayo pia ni msingi mkuu. Tukitoa Zaka yetu, kana kwamba tunaiwasilisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kama alama ya shukrani yetu kwa baraka Zake, tutapata manufaa makubwa sana ya kiroho kutokana na Zaka hiyo.

20. Hii ni taasisi ya kheri iliyoanzishwa na Aziz Mahmud Hudayi yapata miaka mia nne iliyopita na kuhusishwa na kundi la Waislamu wema wa Kituruki mwaka 1985. Miongoni mwa huduma zitolewazo na taasisi hii ya kidini ni pamoja na kukusanya Zaka na sadaka na kisha kuzigawa katika ngazi ya kitaifa na kimataifa.

Tunatakiwa kuwaheshimu na kuwashukuru maskini kwa kutuwezesha kutekeleza mojawapo ya nguzo za Uislamu. Ndiyo maana tunatakiwa sisi wenyewe kwenda kwa maskini na kuwapa Zaka zetu.

Kwa maneno mengine unamaanisha kuwa tunatakiwa kuwa waangalifu katika kumtafuta mpokeaji wa Zaka?

Kweli kabisa. Taharri au umakini katika kutafuta ni sharti la Zaka. Zaka ikitolewa tu bila utafutaji makini, na baadae ikabainika wamepewa watu wasiostahili, basi Zaka hiyo inatakiwa kutolewa tena. Kama aliyepokea ni mtu anayestahili kupokea, basi haitohitajika kutoa tena. Kuna masharti mawili ya Zaka, la kwanza ni taharri na la pili ni tamlik au kuhamisha umiliki wa mali hiyo kwenda kwa masikini.

Kama Zaka ikipelekwa kwenye wakfu kwa ajili ya kugawiwa, je hili haliondoi sharti la Zaka la kutafuta watu? Kwa maneno mengine, je sharti litahamia kwenye wakfu husika?

Ndiyo, iwapo ugawaji wa Zaka utafanywa na taasisi za kati, basi jukumu hilo litakuwa la taasisi hizi. Wakfu zinatakiwa kuwa na wafanyakazi wenye jukumu la kuwatafuta wastahiki wa Zaka. Wanapaswa kwenda kwenye wilaya za watu hao na kuwaulizia kwa wale wanaowajua. Ikiwezekana, waende kuwatembelea majumbani mwao, kwa sababu baadhi ya watu wanaweza kuzifanyia udanganyifu taasisi za kidini. Baada ya kufanya utafiti wa kina, ninaamini jukumu litakuwa limekwisha, lakini Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi.

Watu husika tu ndiyo wanaopewa *Zaka*. Mashirika hayawezi kupewa Zaka. Mapato ya Zaka hayawezi kutumika kujengea misikiti, hospitali, shule, n.k. bali kazi hizo zinaweza kuifanywa kwa kutumia vyanzo vya sadaka nyingine tofauti na

Zaka. Kutokana na suala hili, sadaka za hiari zina nafasi kubwa sana katika Uislamu. Kwa mfano, zaidi ya taasisi elfu 26 za Waqfu zilizoanzishwa katika zama za Dola ya Uthmaniyyah zilikuwa zikitegemea moja kwa moja sadaka za hiari. Aina kadhaa za huduma zilitekelezwa kupitia taasisi hizi. Kulikuwa na wakfu zenye jukumu la huduma ya maji katika mji, hospitali, kuwaozesha mabinti masikini wasiokuwa na uwezo wa kufanya maandalizi ya ndoa zao. Kulikuwa hata na wakfu zinazohudumia wapagazi, ndege, n.k. Leo hii hatuwezi hata kufikiria kuhusu aina hizi za huduma, yalikuwa matunda ya akili na roho safi. Katika Dola ya Uthmaniyyah unapojengwa msikiti, hospitali, huduma ya maji na shule navyo vilikuwa vikijengwa mahali hapo. Huduma zote hizi za kijamii ziliwekwa pamoja katika eneo la msikiti. Kwa namna hii jamii ilihisi kuwa ndiyo mmiliki wa kweli wa mali hiyo na hili lilitengeneza uwiano katika jamii. Tajiri na masikini waliishi kwa amani katika wilaya moja na nyumba za matajiri zikawa hifadhi ya masikini. Masikini waliweza kuwaambia matajiri shida zao. Kimakazi, hapakuwepo na tofauti kubwa baina ya nyumba za matajiri na zile za masikini. Masikini na tajiri walipendana. Matajiri katika jamii waliwaheshimu na kuwashukuru masikini kwa kuwawezesha kutekeleza mojawapo ya nguzo za Uislamu. Na masikini waliwashukuru matajiri kwa kuwa mawakala wa baraka za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Katika historia yetu kuna matukio kadhaa ya mfano. Hata kama siyo mengi, unaweza kutupatia baadhi ya mifano iliyoacha athari kwako kutoka katika historia yetu ya hivi karibuni?

Mtukufu Mtume (s.a.w) amesema kuwa, maskini sio yule anayeomba tonge moja au mawili (ya chakula) kutoka kwa watu, bali maskini wa kweli ni yule ambaye hana chochote na anaona aibu kuwaomba watu."

(Bukhari, Zakat, 53)

Awali ya yote ninamkumbuka baba yangu na mjomba wangu. Walipokuwa wakitaka kutoa kitu kumpa masikini, walikuwa wakikifunga vizuri na kukiwasilisha kwa masikini kwa adabu na heshima bila kuumiza hisia zake. Mpokeaji alikuwa akifurahi na mtoaji akahisi amani. Mmoja wao alikuwa akipokea zawadi zao akijua kwamba kweli zimetoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na mwingine alikuwa akitekeleza amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Vile vile kuna mifano kadhaa kutoka katika taasisi ya Hudayi. Ningependa kutoa baadhi yake. Tulikuwa tukimsaidia mama mmoja na mwanae. Mtoto huyu alikuwa amepooza na alikuwa na digrii ya BA. Siku moja mwanamke huyo alikuja na kuishukuru taasisi ya Hudayi. Alisema kwamba alikuwa hahitajii msaada wetu tena na kutuambia tuelekeze misaada yetu kwa masikini wengine. Alisema muda si mrefu mtoto wake alikuwa amefariki dunia na tukatumia sadaka yetu ya mwisho kugharamia mazishi ya mwanae. Kisha akasema kuwa kwa kuwa yuko pekee yake, kwa kiasi fulani angeweza kujihudumia.

Katika tukio lingine, tulikuwa tukimhudumia mwanamke mmoja kutoka Uholanzi ambaye alikuwa amefiwa na mumewe na alikuwa akiwatunza watoto yeye peke yake. Siku moja alituma barua akitushukuru na kusema: “Nililipa madeni ya mume wangu na kumuokoa dhidi ya haki za watu. Sasa ninaweza kujitegemea.” Kuna matukio mengi kama hayo yanayoonyesha ithaar, ambapo masikini wanaopokea Zaka walihawilisha haki zao kwenda kwa masikini wengine.

Ahsante sana kwa mahojiano hayo mazuri.

“Tumepaa katika njia hii sio kwa kusoma vitabu bali kwa kuyaingiza yale tunayoyasoma katika maisha yetu na kuhudumia umma. Kila mtu hupelekwa katika njia fulani nasi tumepelekwa katika njia ya kutoa huduma.”

Ubaydullah Ahrar (q.s)

Kutoka katika kilele cha ustaarabu wa Kiislamu

Huduma na Adabu Zake

Sura ya kwanza

HATUA KUU KUELEKEA KWENYE KILELE CHA KIROHO

KUTOA HUDUMA KWA AJILI YA MWENYEZI MUNGU

Tunaona kuwa upendo na Ikhlasi ndiyo msingi wa maadili ya Kiislamu katika kuwa karibu na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na pia tunaona kuwa alama ya dhahiri na ya muhimu kuliko zote katika ukaribu huu ni "kuwahudumia watu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu." Kwa sababu, kutokana msingi wa "wale wanaowahudumia watu uhudumiwa na watu," kuwahudumia watu ni hatua ya kipekee na tukufu inayozipeleka roho kwenye vilele vya Kimungu.

Hii ni hatua ambayo kwa sababu yake mitume na marafiki wote wa Mwenyezi Mungu walipata kutukuzwa. Kwa maneno mengine walikuwa dhihirisho la msingi ya hadith ifuatayo ya Mtume (s.a.w):

"Mabwana wa umma ni wale wanaouhudumia umma wao..." (Daylami, Musnad, II, 324)

Kwa hiyo njia inayompeleka mja kwenye vilele vya Kimungu inapitia kwenye kuwahudumia wanadamu kwa moyo wa dhati na Ikhlasi. Wakati mwingine, hudu-



Wale wanaowahudumia watu huhudumiwa na watu

ma ndogo inayopata radhi za Mwenyezi Mungu yaweza kuwa bora na kupata thawabu nyingi kuliko ibada nyingi za hiari (za sunna).

Siku moja Mtukufu Mtume (s.a.w) na maswahaba wake waliweka kambi wakati wa safafri yao. Ilikuwa siku yenye joto kali. Baadhi ya maswahaba walikuwa wamefunga, na baadhi hawakufunga. Maswahaba waliofunga walisinzia kutokana na uchovu. Wale ambao hawakufunga waliwabebea maji wale wenzao waliofunga na kuwatengenezea mahema. Muda wa kufuturu ulipofika, Mtukufu Mtume (s.a.w) akasema:

"Leo wale ambao hawakufunga wamepata malipo mengi zaidi." (Muslim, Kitab al-Sawm, 100-101)

Mtume (s.a.w) ambaye aliwafundisha wafuasi wake kanuni nyingi zenye muongozo kama hiyo iliyotangulia hapo juu, alibeba matofali begani mwake kwa ajili ya ujenzi wa msikiti wa Quba na msikiti wa Mtume (s.a.w) mjini Madina licha ya maswahaba kujaribu kumzuia asifanye kazi. Staha yake na upendo aliokuwa nao wa kuwahudumia wanadamu ni mifano isiyo kifani kwa umma wake wa Kiislamu. Kwa hakika alitumia uhai wake wote akiwahudumia wanadamu na viumbe wote.

Hiyo ndiyo sababu kwamba kuwahudumia binadamu ni miongoni mwa sifa na tabia za wazi za wale wanaofuata nyayo zake. Kwa maneno mengine, wale wanaompenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanapaswa kuwa katika watu wa kutoa huduma. Kwa upande mmoja, kutoa huduma kwa ajili ya Mwenyezi Mungu huwa ni vyanzo vya kuwasaidia watu; kwa upande mwingine

"Tumepaa katika njia hii sio kwa kusoma vitabu bali kwa kuyaingiza yale tunayoyasoma katika maisha yetu na kuuhudumia umma. Kila mtu hupelekwa katika njia fulani nasi tumepelekwa katika njia ya kutoa huduma."

Ubaydullah Ahrar (q.s)

huwapa mi'raji ya kiroho wale wanaotoa huduma kwa juhudi na Ikhlasi ya hali ya juu. Kwa hali hiyo, huenda yule anayetoa huduma akapata manufaa zaidi kuliko yule anayepewa huduma.

Mtoaji huduma ni kama mto ambao hutoa uhai kwa maelfu ya viumbe vinavyouzunguka. Kituo cha mwisho cha mto huo ni bahari ya kuungana na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Wale wanaoutambua ukweli huu hujiona kuwa ni watumishi wa umma hata kama wao ni Masultani. Pindi Sultan wa Kiuthmaniyyah, Sultan Yavuz Salim, alipomsikia imam mmoja akimsifu katika khutba yake kwa kumuita: "Hakim al-Haramain al-Sharifayn, yaani mtawala wa miji miwili mitukufu (Makka na Madina)" alipinga huku akilia na kusema: "Kinyume chake, Mimi ni mtumishi wa miji hii miwili (Khadim al-Haramain al-Sharifayn)."

Ubaydullah Ahrar (q.s) anasema kuhusu hali aliyoifikia kutokana na kuwahudumia watu:

"Tumepaa katika njia hii siyo kwa kusoma vitabu bali kwa kuyaingiza yale tunayoyasoma katika maisha yetu na kuuhudumia umma. Kila mtu hupelekwa katika njia fulani nasi tumepelekwa katika njia ya kutoa huduma." Maneno haya yanaonyesha kuwa elimu kama elimu haitoshi mpaka iwekwe katika matendo na huduma.

Wale wanaowahudumia wengine hutimiza wajibu wao na kuitunza staha yao huku wakipaa kwenye safu za kiroho na kufikia ukomavu unaotakiwa.

Hata hivyo ili huduma ikubaliwe mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu inatakiwa kutimiza baadhi ya masharti. Huduma yenye kukubaliwa inatakiwa ifanywe kwa moyo wenye Ikhlasi, huruma na ithaar na iwe ni kwa ajili ya kutaka radhi za Mwenyezi Mungu. Kwa maneno mengine hu-

duma inatakiwa kufanywa pasipo kulenga manufaa yoyote binafsi bali kupata malipo ya milele. Huduma iliyopambwa kwa sifa hii huwa ni sababu ya kupata wokovu wa milele, hata kama huduma hiyo itakuwa ni kutoa kipande cha tende kama ilivyoelezwa katika hadith.

Ubaydullah Ahrar (q.s) anasimulia:

"Siku moja nilikwenda sokoni. Mtu mmoja akanijia na kuniambia: "Nina njaa. Je waweza kunipa chakula kwa ajili ya Mwenyezi Mungu?" Sikuwa na chochote cha kutoa zaidi ya kilemba changu kikuukuu. Tukaenda kwenye mgahawa mmoja na kumwambia mpishi: "Chukua kilemba hiki. Ni kikuukuu lakini ni kisafi. Unaweza kukitumia kukaushia vyombo vyako. Na mpe chakula mtu huyu kwa malipo ya kilemba hiki?" Mpishi akampa chakula na akakataa kuchukua kilemba changu. Lakini nilikataa. Nikasubiri mpaka masikini yule alipomaliza kula, japokuwa mimi mwenyewe nilikuwa mwenye njaa."

Mtoaji huduma ni kama mto ambao hutoa uhai kwa maelfu ya viumbe vinavyouzunguka. Kituo cha mwisho cha mto huu ni bahari ya kuungana na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Baadae Ubaydullah Ahrar alipata utajiri mkubwa sana kiasi cha kuajiri maelfu ya wafanyakazi kwenye mali yake. Lakini hakuacha kuwahudumia watu. Huduma yake kwa kila mtu, kuanzia mwanzo mpaka mwisho wa njia hii ya kiroho, ilikuwa ya kiwango cha juu mno. Anasimulia moja ya huduma zake kama ifuatavyo:

"Nilikuwa nikiwahudumia wagonjwa wanne katika Madrasah ya Maulana Qutbuddin mjini Samarkand. Kwa sababu ugonjwa wao wa kuharisha ulishtadi, wakaanza kulowanisha vitanda vyao. Nilikuwa nikiwasaidia kuwaogesha na kufua nguo

zao. Kwa sababu ya kuendelea kuwahudumia niliathirika nikaumwa. Pamoja na hayo niliendelea kutoa huduma zangu na kusafisha nguo na vitanda vyao."

Tabia za mfano za watangulizi wetu, sadaka na huduma walizozitoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni mifano bora mno kwetu. Bila kuangalia utajiri alionao, Muislamu hutekeleza shuruti za mali yake kulingana na ukomavu wa moyo na hali yake ya kiroho. Wale wanaotekeleza majukumu na wajibu wao na kuendeleza staha yao huku wakipanda katika daraja na safu za hali ya kiroho hufikia hali ya kuigwa iliyotajwa katika simulizi ya Ubaydullah Ahrar.

Daraja nyingine ambayo ni vigumu sana kufikia ni kuwahudumia watu katika kiwango kinachoshuhudiwa katika kisa kifuatacho cha Ma'ruf al-Karkhi: Mtu mmoja mgonjwa na mzee alimtembelea Ma'ruf al-Karkhi. Alikuwa fakiri, alikuwa na upara na alionekana kuchoka mno kana kwamba alikuwa katika dakika za mwisho za uhai wake. Ma'ruf al-Karkhi alimuandalia kitanda na kumhudumia vizuri. Mgonjwa huyo alikuwa akipiga mayowe na kulia kutokana na maumivu. Usiku mzima yeye mwenyewe hakupata kulala na aliwaonya watu wengine waliokuwa nyumbani wasilale. Licha ya hivyo alianza kumuudhi kila mtu kwa malalamiko yake. Hatimaye kila mtu aliikimbia nyumba isipokuwa Ma'ruf al-Karkhi na mkewe.

"Ubora katika kuwahudumia watu ni kuubeba mzigo wa mtu maskini pale unapohisi kuwa una nguvu na mwenye afya."

Sheikh Sadi

Ma'ruf al-Karkhi alikuwa akijitahidi kufanya kila kitu alichoweza ili kumhudumia. Lakini, usiku mmoja hakuweza kustahmili hali ya kukosa us-

"Moyo uliojaa upendo ni moyo wenye kusamehewa. Kama unafanya ili uonekane tu, basi utakapokufa, jina lako litakufa pamoja na mwili wako. Ukiishi kama mtu mkarimu na ukawa mtu wa kuhudumia, uhai wako utaendela baada ya mauti yako kulingana na kiwango chako cha kujitolea na kuingia ndani ya nyoyo za watu. Je huoni kuwa kuna makaburi mengi katika mji wa Karkh, lakini hakuna kaburi maarufu na linalotembelewa sana kama kaburi la Ma'ruf al-Karkhi."

Sheikh Sa'di

ingizi akasinzia. Mgonjwa huyo mwenye mghafala alipomuona amelala, badala ya kumshukuru akaendeleza lawama zake na kusema:

"Darwesh gani huyu? Watu kama hawa wanaonekana kuwa ni wazuri, lakini kwa uhakika ni wanafiki. Nje ni wasafi lakini ndani wamejaa uchafu. Wanawashauri wengine kuwa wema lakini wao wenyewe hawafuati ushauri wao wenyewe. Angalia mtu huyu alivyolala bila kufikiria hali yangu mbaya. Mtu aliyeshiba na kulala atajua nini kuhusu hali ya mgonjwa asiyekuwa na msaada?"

Ma'ruf al-Karkhi, kwa upande mmoja, alivumilia malalamiko haya na akajifanya kama hayasikii. Lakini mkewe hakuweza kuvumilia hata kidogo na akamwambia taratibu mumewe:

"Umesikia alichosema mtu huyu aliyehamaki. Hatuwezi kuwa naye tena katika hii nyumba. Tusimuache akuumize tena. Mwambie ajitafutie mwenyewe sehemu nyingine ya kuishi. Wema unafanywa kwa wale wanaoutambua. Kumfanyia hisani mtu asiyeshukuru ni kutozitendea haki hisani hizo. Mto hautakiwi kuwekwa chini ya kichwa cha mtu mwenye chawa. Kichwa chake kinastahiki kuwa kwenye jiwe."

Baada ya kusikiliza kwa makini maneno ya mkewe, Ma'ruf al-Karkhi akasema huku akitabasamu:

"Mpenzi wangu, kwanini maneno yake yanakuumiza? Kama amesema kitu basi alinisema mimi; kama amefanya kitu kibaya, amenifanyia mimi; humuoni kuwa yu katika maumivu makali?

Hawezi hata kulala. Unatakiwa kujua kuwa wema na huruma ya kweli ni kuweza kuwavumilia watu kama hawa..."

Sheikh Sadi ambaye amesimulia kisa hicho anatoa ushauri ufuatao:

"Ubora katika kuwahudumia watu ni kuubeba mzigo wa mtu masikini pale unapohisi kuwa una nguvu na mwenye afya."

"Moyo uliojaa upendo ni moyo wenye kusamehewa. Kama unafanya ili uonekane tu, basi utakapokufa, jina lako litakufa pamoja na mwili wako. Ukiishi kama mtu mkarimu na ukawa mtu wa kuhudumia, uhai wako utaendela baada ya mauti yako kulingana na kiwango chako cha kujitolea na kuingia ndani ya nyoyo za watu. Je huoni kuwa kuna makaburi mengi katika mji wa Karkh, lakini hakuna kaburi maarufu na linalotembelewa sana kama kaburi la Ma'ruf al-Karkhi."

Uzuri ulioje wa maneno ya marafiki wa Mwenyezi Mungu pale waliposema:

"Tasawwuf au Usufi maana yake ni kuwa yaar (rafiki) siyo kuwa baar (mzigo)". Kwa maneno mengine ni kubeba mzigo wa kila mtu badala ya kuwa mzigo kwa kila mtu.

Kwa huruma na huduma za dhati, umma wa Kiislamu utafunguliwa milango ya rehema. Thamani ya huduma hutegemea ukubwa wa kujitolea na kuifanya kwa hisia za ibada. Vilevile, huduma yenye kukubaliwa ni ile inayofanywa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na bila kuumiza hisia

Thamani ya huduma hutegemea ukubwa wa kujitolea na kuifanya kwa hisia za ibada. Vilevile, huduma yenye kukubaliwa ni ile inayofanywa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na bila kuumiza hisia za yule anayepewa huduma.

za yule anayepewa huduma. Kama asemavyo Abdullah bin Munazil (q.s):

"Tabia na adabu njema katika kutoa huduma ni kitu chenye thamani zaidi kuliko huduma yenyewe."

Mawlana Jalal al-Din Rumi anasema kuhusu jambo hili:

"Fanya kazi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, toa huduma kwa ajili ya Mwenyezi Mungu; kuna tofauti gani iwapo watu wataikataa au kuikubali? Je Mwenyezi Mungu hatoshi kuwa mteja wako mwenye kukupa faida? Kitu gani watu wanachoweza kukupa ikilinganishwa na kile unachoweza kupata kutoka kwa Mwenyezi Mungu? Kwa hiyo yageuze macho na moyo wako kutoka kwenye shukrani za watu ukielekee kile utakachopata kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu."[21]

Hiki ndicho kiwango cha ukuu na uzuri ambacho Usufi unataka kuupeleka moyo wa mwanadamu. Kuhusu suala hili, Amir Kulaal anamuusia mwanafunzi wake Bahauddin Naqshiband:

"Zipe faraja nyoyo, wahudumie wanyonge. Walinde wanyonge na masikini. Hao ni watu ambao hawana matarajio kutoka kwa watu. Lakini, wengi wao wanaishi na amani kamili ya akili na staha katika kumshukuru Mwenyezi Mungu. Watafute na uwapate watu wa aina hii."

Katika miaka ya mwanzo ya kuuitumia twariqa ya Sufi, Bahauddin Naqshiband (q.s) aliwa-

"Tabia na adabu njema katika kutoa huduma ni kitu chenye thamani zaidi kuliko huduma yenyewe."

Abdullah bin Munazil (q.s)

21. Juzuu VI, utenzi 839.

hudumia wagonjwa, wanyama waliojeruhiwa na kusafisha barabara kwa kipindi cha miaka saba ili kufikia hali ya kutokuwa chochote au kuondosha kiburi na fahari. Anasimulia:

"Nilifanya kazi kwa namna alivyoniamrisha mwalimu wangu. Nilifanya huduma zote. Nafsi yangu ilifikia daraja ambalo nilipokuwa nikimuona kiumbe yeyote wa Mwenyezi Mungu akipita njiani nilikuwa nikisimama na kusubiri mpaka apite. Huduma yangu iliendelea kwa muda wa miaka saba. Mwishoni mwa miaka hii saba daraja hilo ilionekana kwangu kiasi kwamba nilianza kusikia sauti zao za kuomba kimbilio kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu."

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an Tukufu kuhusu Waislamu wema:

"...wanakimbilia katika mambo ya kheri. Na hao ndio miongoni mwa watenda mema." (Qur'an, 3: 114). Na matunda makubwa ya waumini hawa wema ni taasisi za kidini. Watu waliojitoa wakfu ni Mtume, marafiki wa Mwenyezi Mungu na wale waliofundishwa na watu hawa. Walibeba hamasa na msisimko wa imani katika nyoyo zao kuupeleka wenye kona zote za dunia na kuandika kurasa za dhahabu za historia.

Inavutia sana kujua kuwa katika Hijja ya kuaga (hijja ya Mwisho ya Mtume s.a.w) walikuwepo maswahaba wapatao laki moja na elfu ishirini. Miongoni mwao, zaidi ya maswahaba laki moja walitawanyika ulimwenguni na kujitoa wakfu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Walifariki dunia wakiwa mbali na nyumbani kwao. Makaburi ya watoto wa

"…wanakimbilia katika mambo ya kheri…"

(Qur'an, 3: 114)

Uthman na Abbas (r.a) yapo Samarkand na makaburi ya maswahaba kadhaa yapo Istanbul. Wale waliobaki Makka na Madina waliyalinda makao ya Dola ya Kiislamu na kuihudumia miji hii mitukufu.

Khalid bin Zaid Abu Ayyub al-Ansari alikuja Istanbul mara mbili japokuwa wakati huo alikuwa na miaka 80 na alifariki dunia akiwa huko. Huu ni mojawapo ya juhudi za mifano ya maswahaba kuwaita watu kwenye Uislamu na kuwaokoa hapa duniani na Akhera. Mapenzi na hamasa yao ya kuwahudumia watu na juhudi zao za kutaka kupata maisha ya milele hutoa hamasa ya kueneza huduma zao ulimwenguni kote.

Wahb bin Kabsha (r.a) ni mfano mwingine mkubwa katika kuwahudumia watu. Kaburi lake liko China.[22] Mtukufu Mtume (s.a.w) alimtuma kwenda China kufikisha ujumbe wa Uislamu; wakati huo ilimchukua mtu mwaka mmoja kutoka Arabia kwenda China. Baada ya kazi yake nchini China kwa muda mrefu, swahaba huyo alielekea Madina ili kutuliza shauku yake ya kumuona Mtume (s.a.w). Alifika Madina baada ya mwaka mmoja baada ya safari yenye tabu nyingi mno, lakini kwa bahati mbaya hakuweza kumuona Mtume (s.a.w), kwani wakati huo Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa amekwishafariki dunia.

Kwa kweli kile ambacho sisi wote tunajaribu kukifikia ni wokovu wa nafsi zetu, au kupata amani na utulivu, ikiwa tunajua au la. Na hii ni hazina ya ndani ambayo hupatikana kwa kuwahudumia watu kwa furaha ile ile tunayokuwa nayo wakati wa kumuabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu.

22. Kuna kaburi linalohusishwa na Sa'd b. Abi Waqqas (r.a) huko Guangzhou, nchini China. Ni ukweli unaojulikana kihistoria kuwa makaburi ya maswahaba yametunza na kulinda hisia za kidini za umma husika. Kuna mifano mingi inayothibitisha ukweli huu katika miji ya eneo la Katikati mwa Asia kama vile Samarkand, Bukhara, Turkistan na Tashkent.

Alipofikiria jukumu lake akarudi China na alifariki dunia akiuhudumia Uislamu.

Imani thabiti na upendo ndivyo vitu vinavyoweza kustahimili huduma hizi zenye ithaar ndani yake. Upendo na moyo wao wa kuwasaidia watu umekuwa nyota zinazoangaza njia zao.

Naam, maswahaba watukufu walifikia daraja hii kwa kufuata mafunzo ya Mtukufu Mtume (s.a.w), hususan misingi minane ifuatayo:

1. Kumtumikia Mwenyezi Mungu Mtukufu; kufuata amri na makatazo yake kwa moyo wa dhati na kutumia juhudi zote katika kuinua neno la Mwenyezi Mungu.
2. Kumhudumia Mtukufu Mtume (s.a.w); kumpenda na kuwasaidia watu waishi kulingana na sunnah zake.
3. Kuwahudumia wazee wa Kiislamu; kuwaheshimu, kuwatii na kuwasikiliza.
4. Kuwahudumia wazazi; kupata radhi zao kwa kutowavunjia heshima.
5. Kuwahudumia watoto; kuwalea vyema ili wawe Waislamu wema
6. Kuwahudumia jamaa; kuwatembelea na kuwasaidia.
7. Kuwahudumia Waumini; kushiriki katika furaha na huzuni zao.
8. Kuwahudumia wanadamu wote; kufanya kila liwezekanalo kuwanufaisha watu kwa mikono na ndimi zao.
9. Kuwahudumia viumbe; kuvihurumia viumbe vyote.

"Kuna watu wengi wanaowasaidia watu lakini wakawakumbushia wema wao. Lakini ni watu wachache mno wanaoona hali ya kuwatumikia na kuwahudumia wengine kuwa ni baraka. Ichukulie fursa ya kuwasaidia kuwa ni baraka kwako na uwashukuru wale unaowasaidia; kila mtu atakuwa radhi nawe na malalamiko yao yatapungua."

Ali Ramiteni (q.s)

Kuhusu suala hili, Musa Topbas (q.s) daima alikuwa akisimulia maneno yafuatayo ya Ali Ramiteni:

"Kuna watu wengi wanaowasaidia wengine lakini mara kwa mara huwakumbushia wema wanaowafanyia. Lakini kuna wale wachache sana ambao huchukulia suala la kuwahudumia wengine kama baraka. Ione fursa ya kuwahudumia wengine kuwa ni baraka kwako na washukuru wale unaowasaidia, kila mtu atafurahishwa na wewe na malalamiko yao yatapungua."

Kwa kweli kile ambacho sisi wote tunajaribu kukifikia ni wokovu wa nafsi zetu, au kupata amani na utulivu, ikiwa tunajua au la. Na hii ni hazina ya ndani ambayo hupatikana kwa kuwahudumia watu kwa furaha ile ile tunayokuwa nayo wakati wa kumuabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hii ndiyo sababu kwamba waumini, ambao huvihudumia viumbe kwa utambuzi, hujua kutafuta fursa na njia za kutoa huduma katika mazingira yoyote yale. Wanakuwa na azma na bidii kubwa ya kuwasaidia watu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu zaidi ya wale wanaowasaidia watu kwa lengo la kupata manufaa ya kidunia.

"Utoaji huduma ni sharti na matokeo ya imani ya kumuamini Mwenyezi Mungu.

Bidii ya kuwahudumia watu inapopata makazi ndani ya moyo, humbadilisha mja kuwa msafiri wa milele. Moyo hujikomboa kutoka kwenye ukali wa Hajjaj muonevu[23] na kujifunga ndani ya sufu ya huruma. Elimu, maarifa, sanaa na maadili ya-

23. Al-Hajjāj ibn Yūsuf (661-714) alikuwa mtawala wa kijeshi wa utawala wa Bani Umayya.

nayopatikana kwa hali hii ya kiroho hupata umilele wenye kuvutia. Kwa hiyo, huduma za kweli na za Ikhlasi ni matunda ya ukomavu wenye kuchangamsha. Nyoyo za aina hiyo ni mahali panapotazamwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Aidha, hasara iliyoje kuishi mbali na neema hizo zenye kuchangamsha! Baraka iliyoje kwa wale waliozijaza nyoyo zao kwa upendo wa kweli wa kupenda kuwahudumia watu!

Mola wetu! Zijazo nyoyo zetu kwa upendo, shauku na hamasa ya kupata radhi zako. Tupe baraka ya hamasa kama ile ya maswahaba ya kuwahudumia viumbe!

Amin!

Shauku ya kuwahudumia watu inapokuwa ndani ya moyo, humbadilisha mja kuwa msafiri wa milele.

Uislamu huupa uhai ubinadamu

Lengo na madai makuu ya kila mfumo wa fikra ni kuinua hali ya wanadamu na kuyapelekea mahusiano ya binadamu kwenye ngazi ya juu zaidi. Hata hivyo hakuna mfumo wowote uliotengenezwa na mwanadamu ambao uliweza kufikia kiwango ambacho Uislamu umefanikiwa kufikia. Sababu kubwa ya jambo hili ni kuwa, mifumo iliyotengenezwa na mwanadamu inategemea uwezo wenye kikomo wa akili ya mwanadamu. Kwa upande mweingine, kwa kuwa Uislamu umetoka kwa Mola wetu, uliweka mfumo wenye uwiano baina ya ubinadamu na hali halisi ya ulimwengu. Binadamu kujitambua na kuwatambua viumbe wengine, na mifumo yao waliyoianzisha ili kuyatawala mambo yao si chochote ikilinganishwa na uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu usiokuwa na kikomo, ambao, kinyume na madai yao, ndiyo maana kwamba mifumo mingi ya kifalsafa na dini zilizotengenezwa na wanadamu zimeshindwa kumuonyesha mwanadamu njia iliyonyooka. Zimemuacha mwanadamu akiwa fakiri badala ya kumtosheleza.

Matokeo ya mifumo mingi kuanzia kwa Freud alimkokota mwanadamu kumpeleka kwenye muonguko wa kimaadili, mpaka Marx aliyedai kumpeleka mwanadamu kwenye ustawi wa kiuchumi wamekuwa kinyume na madai yao. Mwishowe wakasababisha mvurugiko na shida za kijamii.

Ni ukweli wa kihistoria kuwa Mtume (s.a.w) aliukumbatia ubinadamu kwa upendo na huruma.

Yule anayekuja kukuua anatakiwa kupata uhai kwako.

Ubinadamu ambao ulikuwa ukizama ndani ya tope la uonevu na dhulma. Vile vile alikuwa mfano bora kwa binadamu kwa tabia yake ya huruma na upendo. Kabla ya kupewa utume, binadamu walikuwa watu wanaopigana, kunyanyasana na kushambuliana kuanzia utotoni mwao. Lakini kwa mikono yake mitukufu kila mmoja akaokolewa dhidi ya tabia mbovu na kuwa watu wenye nuru na wa kipekee kama "nyota zilizo mawinguni." Mfano ufuatao umechukuliwa katika maisha ya Mus'ab bin Umair.

Mus'ab bin Umair (r.a) pamoja na As'ad bin Zurarah (r.a) walikwenda katika eneo la Abd-i Ashal na Bani Zafar mjini Madina. Katika kipindi hicho Sa'd bin Mu'az na Usayd bin Hudayr ndiyo waliokuwa viongozi wa bani Abd –i Ashal. Walikuwa washirikina. Sa'd aliposikia ujio wa Mus'ab akamwambia Usayd:

"Unasubiri nini? Nenda ukawafukuze watu hawa. Wapo hapa kuwaghadhibu watu wetu wanyonge na dhaifu."

Usayd akaja kwa Mus'ab bin Umayr na As'ad bin Zuraraha na kuanza kuwatuhumu. Aliwaelekezea mkuki wake na kusema:

"Kama mnataka kuishi, ondokeni hapa!"

Mus'ab (r.a) akamjibu huku akitabasamu:

"Ungekaa na kusikiliza, tuna kitu tunataka kukwambia. Wewe ni mtu mwerevu na mwenye utambuzi. Ukikipenda tunachosema, unaweza kukikubali; kama hutoyapenda, basi unaweza kujitenga nasi."

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu! Hofu yangu sio kwamba mtawaabudu wengine pamoja na Mwenyezi Mungu baada yangu, bali hofu yangu ni kuwa mtapigana na kupambana kwa ajili ya mambo ya kidunia."

(Bukhari, Janaiz, 71)

Usaid alitafakari kwa muda kisha akasema:

"Uko sahihi" akauacha mkuki wake na kuanza kusikiliza.

Baada ya kusikiliza, alipendezwa na kilichozungumzwa na kusilimu. Kisha akaondoka kwa amani na kwenda kwa Sa'd:

"Nimewasikiliza na sikuona lolote baya katika mazungumzo yao."

Sa'd akaghadhibika sana akaenda kwa Mus'ab. Mus'ab (r.a) akamsalimia na kumtuliza. Alimueleza Sa'd kwa upole mambo kadhaa kuhusu Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mara hii Sa'd akapata baraka ya kusilimu.

Hakika tukio hili linaonyesha kiwango kilichofikiwa na Maswahaba chini ya mafunzo ya Mtukufu Mtume (s.a.w). Watu hao wenye fanaka waliandika katika kurasa za historia kanuni ya "yule anayekuja kukuua anatakiwa kupata uhai kwako".

Kwa muktadha huu Mtukufu Mtume wa Allah (s.a.w) aliwasamehe wahalifu wengi, hata Wahshi aliyemuua ami yake, akaamuliana nao kwa huruma. Katika maisha ya Mtukufu Mtume (s.a.w) daima huruma na msamaha vilikuwa vya mwanzo kabla ya hasira. Moto mkubwa wa mghafala na uovu ulizimwa na mto wa ukweli alioleta. Watu wa zama zake, ambao mshairi maarufu wa Kituruki Mehmed Akif Ersoy anaelezea tabia yao kwamba "kama mtu hana meno ndugu zake wangemtafuna", waliokolewa kutoka katika unyama huo. Wakawa watu ambao walifikia hatua

Njoo tuwe marafiki,
Tuyafanye mambo yetu kuwa rahisi
Tupende na tupendwe,
Ulimwengu hautoachwa mikononi mwa yeyote.

kwamba wanapokuwa katika uwanja wa vita wangesema: “mpelekee maji haya ndugu yangu” hali ya kuwa anayesema hivyo yeye mwenyewe anateseka na kiu kali.

Mtukufu Mtume (s.a.w), ambaye aliwapeleka watu wake kwenye vilele vya hali ya kiroho, daima aliongoza msafara wake wa kiroho. Mwanzoni mwa karne iliyopita, kundi la wanazuoni walikusanyika mjini The Hague, Uholanzi na kuwachagua watu mia moja walioacha athari kubwa katika historia ya binadamu. Japokuwa kamati husika ya uteuzi ilikuwa ikiundwa na wasomi wa Kikristo, walimchagua Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) kuwa mtu aliyekuwa na athari kubwa kuliko watu wote katika historia ya binadamu kutokana na kigezo cha maadili, ambacho walikuwa wakikitafuta ndani ya mshindani husika.

Vilevile ni muhimu kueleza kuwa takriban asilimia tisini ya Maswahaba waliingia katika Uislamu kwa sababu tu ya shakhsia kamili ya Mtume (s.a.w), tabia njema na mwenendo mzuri aliokuwanao kama mfano bora wa kuigwa (al-Uswa al-hasanah). Hata wale waliokuwa maadui wakubwa wa Mtukufu Mtume (s.a.w) kamwe hawakumuita “muongo” au “muonevu” pindi walipojaribu kumshusha hadhi, badala yake walikuwa wakizisifu tabia na mwenendo wake mzuri.

Wale wanaoukubali Uislamu kwa moyo wa dhati na Ikhlasi na wakataka kuutumikia Uislamu wanapaswa kujua kwamba njia hii tukufu kwanza inalenga kuhusisha ubinadamu. Kila mwanadamu anatakiwa kuchukuliwa kama kiumbe bora zaidi

“Shikamana na kusamehe, na amrisha mema, na jitenge na majaahili.”

(Qur’an, 7: 199)

ya viumbe wote. Kwa maana lengo la Uislamu ni kuzifanya tabia bora zitawale sifa za wanadamu. Hii ina maana ya kusafisha sifa hasi za ziada za wanadamu na kuwahusisha katika tabia yao ya asili. Njia pekee ya kulifikia hili ni kuhuisha na kuamsha uzuri mbalimbali wa kiroho.

Ndiyo maana kwamba Uislamu unaweka kipaumbele kwenye tabia na ukomavu wa kimaadili wa mwanadamu tangu anapozaliwa. Na umefanikiwa kuwabadilisha wafuasi wake kuwa watu wanaostaajabiwa na kila mtu. Uislamu umewapa ukamilifu kwa sifa za kimalaika watu wengi ambao mwanzo walikuwa wameghafilika, ambao walikuwa wakiishi kama wanyama. Kwa mfano, Umar bin al-Khattab (r.a), ambaye hapo kabla alimzika binti yake mwenyewe hali ya kuwa yu hai, alibadilika na kuwa Muislamu mwenye moyo laini kiasi kwamba alikuwa akiogopa hata kuwaumiza sisimizi.

Katika jambo hili Uislamu unawakilisha roho inayoamiliana na mwanadamu kwa upendo na huruma. Hisia ya uwajibikaji itokanayo na mbegu ya huruma humpeleka mwanadamu kwenye ukamilifu wa tabia na furaha katika ulimwengu huu na ule wa kesho. Kwa maana Uislamu ni mhuishaji wa ubinadamu. Tabia zote zitokanazo na mfumo huu mtukufu wa Uislamu ndiyo za kibinadamu. Yunus Emre anasema kuhusu jambo hili:

Njoo tuwe marafiki,
Tuyafanye mambo yetu kuwa rahisi
Tupende na tupendwe,
Ulimwengu hautoachwa mikononi
mwa yeyote.

Njoo tuwe marafiki,
Tuyafanye mambo yetu kuwa rahisi
Tupende na tupendwe,
Ulimwengu hautoachwa mikononi mwa yeyote.

Hisia hii ya huruma ilikuwa kubwa mno katika historia yetu kiasi kwamba ilimfanya kamanda wa jeshi aseme “Ewe huruma! Hakika wewe ni katili, umenifanya mpaka nampenda adui yangu.”

Leo hii kuna watu waovu na wenye kughafilika wanaolitaja jina la Uislamu kwa kuliweka pamoja na dhana ya “vitisho”. Kwa namna moja wanajaribu kulisiliba jua kwa tope. Kwa kawaida huwachagua watu wasiokuwa na hatia kwa lengo la kueneza hofu na vitisho na kuwashawishi watu kwa hatari ya kubuni na isiyokuwepo. Kwa upande mwingine Uislamu unaamrisha kuamiliana hata na mkosaji na mwenye dhambi kwa namna ya huruma na msamaha. Kwa hiyo kama Uislamu una huruma kiasi hicho je inaingia akilini kuwaza kuwa Uislamu utakubali kuwahofisha na kuwatisha watu wasiokuwa na hatia?

Tangu kudhihiri kwake, Uislamu uliamiliana na kila mtu, muumini au asiyekuwa muumini, kwa uadilifu na upendo. Ulikataza vikali aina yoyote ya vitendo vya maangamizi dhidi ya mali, nafsi na mazingira. Unaiamrisha dola kulinda maisha, mali, heshima na familia na kuweka ustawi wa kisaikolojia, nidhamu na uwiano wa kijamii. Hakuna mahusiano hata kidogo kati ya fikra halisi ya Uislamu na vitisho. Ijulikane pia kwamba Uislamu haukatazi tu vitisho bali pia unakataza aina zote za vitendo vinavyosababisha hali hiyo.

“Shikamana na kusamehe, na amrisha mema, na jitenge na majaahili.”

(Qur’an, 7: 199)

Muslim bin Harith (r.a.) anasimulia:

Siku moja Mtukufu Mtume (s.a.w) alitutuma vitani. Tulipokaribia eneo husika niliendesha kwa kasi farasi wangu na kuwapita wenzangu. Nili-

zungumza na watu wa kijiji kile wakaingia katika Uislamu. Kwa hali hiyo hapakuwa na haja tena ya vita. Lakini baadhi ya wenzangu ambao hawakuwa wakifahamu umuhimu wa jambo hili walinijia na kusema:

"Tumekosa ngawira kwa sababu yako." Tuliporudi kwa Mtume (s.a.w) walimueleza nilichofanya. Mtukufu Mtume (s.a.w) akaniita na kunisifu kwa kitendo changu:

"Fahamu kwamba Mwenyezi Mungu amekulipa mema kwa kila mtu uliyemuokoa leo." Kisha akaendelea: *"Nitaandika barua kukupendekeza kuwa kiongozi wa baadae wa Kiislamu."* Kisha aliandika, akaiwekea muhuri na kunipatia.[24]

Tukio lingine la mfano ni hili lifuatalo:

Baada ya mauaji yaliyofanywa dhidi ya walimu sabini katika mkasa wa Bir Ma'unah na mashambulizi mengine, Mtukufu Mtume (s.a.w) alianza kutuma askari kulisindikiza kila kundi la walimu aliowatuma. Askari hao hawakuruhusiwa kutumia silaha zao isipokuwa pale itakapolazimika. Siku moja Khalin bin Walid alitumia upanga wake kinyume na maagizo yaliyotolewa na Mtume (s.a.w). Mtukufu Mtume (s.a.w) aliposikia yaliyotokea, alisikitika sana na kusema: *"Ewe Mwenyezi Mungu! Ninajitenga na yale yaliyofanywa na Khalid bin Al-Walid,"* na akarudia kusema hivyo mara tatu. Kisha akamtuma Ali bin Abi Talib (r.a) kwenda eneo la tukio na akamuagiza kutoa fidia, siyo tu

"Ewe Ali! Naapa kwa Allah! Kama mtu mmoja ataingia katika Uislamu kwa mikono yako (yaani kwa sababu yako), ni bora kwako kuliko ngamia wekundu."

(Bukhari, Kitab al-Jihad,143)

24. Tazama, Ibn Sa'd Tabaqat,VII, 419 – 20.

kwa ajili ya watu waliouawa bali pia kwa ajili ya wanyama na hata mbwa.[25]

Wauthmaniyyah, ambao waliukubali mwenendo huu kama kauli mbiu yao, hawakuwalazimisha wasiokuwa Waislamu kusilimu na kamwe hawakuwatesa watu kwa mauaji au ubeberu wa kiutamaduni. Walikubali wale wasiokuwa Waislamu waishi katika ardhi yao kama amana kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kuamiliana nao ipasavyo. Hii ndiyo sababu kwamba msemo usemao "Nchi hii haitopata uhuru wake mpaka farasi wa kiuthmaniyyah wanywe maji ya Mto Vistula" ukawa methali maarufu miongoni mwa watu wa Lechia.

Kutokana na hali hii Dola ya Kiuthmaniyya ikawa nchi ambayo watu wengine walitamani kuishi ndani yake. Kwa mfano, wakati majeshi ya Kiuthmaniyya yakisonga mbele kuzivunja kuta za mji wa Istanbul, mtawala mkuu mkristo aitwaye Notaras aliwajibu wale waliomtaka kuomba msaada kutoka kwa Papa:

"Ni bora kuona vilemba vya Kituruki hapa kuliko kuona kofia za kikadinali."

Sisi, kama Waislamu, lazima tuishi kwa kuonyesha huruma na upendo kwa viumbe wote hususan katika zama zetu hizi. Hii ndiyo njia bora ya kuwa karibu na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kisa kifuatacho ni mfano mzuri sana kuonyesha hali ya fikra ya muumini:

Wale wanaowahudumia watu wanatakiwa kuwa na hisia mno na kuwa makini katika muamala wao.

25. Tazama: Bukhari, Ahkam, 35; Ibn Kathir, al-Bidayah wa al-Nihayah, IV, 304-05.

Tangu kudhihiri kwake, Uislamu uliamiliana na kila mtu, muumini au asiyekuwa muumini, kwa uadilifu na upendo. Ulikataza vikali aina yoyote ya vitendo vya maangamizi dhidi ya mali, nafsi na mazingira. Unaiamrisha dola kulinda maisha, mali, heshima na familia na kuweka ustawi wa kisaikolojia, nidhamu na uwiano wa kijamii.

Bayazid al-Bistami alipumzika chini ya mti, akala chakula chake na kisha akaendelea na safari yake. Muda ya muda akaona mchwa kwenye begi lake akawaza kwa masikitiko:

"Nimemtenganisha mdudu huyu na makazi yake."

Akarudi haraka mpaka kwenye eneo alililokuwa amepumzika na kumuacha mdudu yule, kwa sababu Bayazid alijua umuhimu wa kuonyesha huruma kwa viumbe wote kwa ajili ya Muumba wao.

Uislamu, ambao huwafanya watu wafikie kiwango hicho cha juu cha huruma kwa wanyama, unawachukulia wanadamu kuwa viumbe watukufu zaidi na kuwataka waelekee kwenye anga tukufu. Kwa maneno mengine, pindi asili ya mwanadamu ya *"kiumbe bora (ahsan-i taqwim)"* utakapozingatiwa; umuhimu unaotakiwa kutolewa kwenye dhana ya ubinadamu utapata kueleweka vizuri sana. Hali hii ya fikra inaonekana katika misingi yote ya Uislamu kuhusu wanadamu. Mojawapo ya malengo ya Uislamu ni kuwapeleka wanadamu kwenye daraja hizo za juu zinazohusudiwa hata na malaika.

Leo hii sababu ya kushuhudiwa kwa uonevu na dhulma kubwa ulimwenguni ni watu kuziacha sifa na tabia tukufu kama vile upendo na huruma, na badala yake wakaanza kufuata matamanio ya kihayawani ya nafsi zao. Haya ndiyo matokeo ya moja kwa moja yanayopatikana pale mazuri ya Uislamu yanapowekwa kando. Kwa hali hiyo, kuuelewa vizuri Uislamu, kusikiliza unavyosema,

moyo na nafsi kutambua kuwa dunia hii ni ya mpito, yote hayo yatatoa fursa ya wokovu wa mwanadamu. Kwa maneno mengine, hitajio halisi la mwanadamu ni kujifunza misingi ya Uislamu na kuyapangilia maisha yetu kulingana na misingi hii. Je maneno yafuatayo ya Yunus Emre: *"Wapende viumbe; kwa sababu ya Muumba wao"* hayatoi ulinzi wa nafsi kwa yule anayekwenda kinyume na ukweli, na kumuokoa katika ulimwengu huu na kesho Akhera? Na, kama Waislamu, kuwasaidia ni jukumu letu. Nyenzo za kisasa za usafiri na mawasiliano zimeongeza jukumu letu. Matumizi ya maendeleo ya kiteknolojia katika kufikisha ujumbe wa Uislamu kwa wanadamu na kuondosha ukungu wa sifa mbaya inayotangazwa dhidi ya Uislamu yamejitokeza sana katika zama hizi kuliko hapo zamani. Jambo hili linafanya majukumu yetu ya mtu mmoja mmoja na jamii kwa kiujumla kuwa majukumu ya kiulimwengu. Kuelewa vizuri hali hii, tutazame kisa kifuatacho:

Daktari mmoja wa Kimarekani alisilimu na akaandaa shughuli ya kusilimu kwake katika msikiti. Katika shughuli yake hiyo iliyohudhuriwa na Waislamu kadhaa kutoka mbali na pia maeneo ya karibu, daktari huyo angetoa hotuba na kueleza kwa nini amechagua kuingia katika Uislamu. Kabla ya kuanza hotuba yake, akasema:

"Nina swali nataka kuwauliza. Nataka mnijibu kabla sijaanza hotuba yangu." Kisha akauliza:

"Wazazi wangu wote wawili walikufa wakiwa Wakristo. Ningependa kukuulizeni kuhusu hali yao huko Akhera."

Watu waliohudhuria wakaanza kuwa na wasiwasi. Je jibu lao litamghadhibisha mgeni huyo wa Uislamu? Kwa hali hiyo wakajibu:

"Wapende viumbe kwa sababu ya Muumba wao"

Yunus Emre

"Kama hawakufikiwa na ujumbe wa Uislamu katika maisha yao, basi wana udhuru. Wanasubiri kwenye ulimwengu ulio baina ya huu na ule wa Akhera. Hali yao itakuja bainika Siku ya Hukumu.

Baada ya jibu hili, daktari akaendelea kusema:

"Enyi Waislamu! Wazazi wangu walikuwa na elimu, maadili na uadilifu kuliko mimi. Lakini, kwa sababu ya shinikizo la jamii waliishi kama Wakristo na kufariki kama Wakrsito. Walidhani kuwa Nabii Isa (a.s) ni mungu. Hawakujua chochote kuhusu Uislamu. Labda walisikia jina lake tu.

Mwenyezi Mungu awe radhi nanyi nyote. Mliokuja Marekani na kujenga msikiti huu. Mliniambia kuhusu Uislamu na ikawa sababu ya kusilimu kwangu. Ahsanteni sana kwa hilo. Lakini baba na mama yangu ni watu waliostaafu. Kwanini hakuna yeyote miongoni mwenu aliyewaendea na kuwaambia kile mlichoniambia? Kama mngefanya hivyo, ninaamini wangeukubali Uislamu kwa hamasa zaidi yangu mimi.

Sisi, kama Waislamu, lazima tuishi kwa kuonyesha huruma na upendo kwa viumbe wote hususan katika zama zetu hizi. Hii ndio njia bora ya kuwa karibu na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Ninajua imani ni majaaliwa. Lakini, ulimwengu huu ni ulimwengu wa sababu. Kwa nini mliacha kutekeleza jukumu lenu? Ninaamini kwamba kupuuza kwenu na kughafilika kwenu ndiyo sababu ya wao kufariki bila kupata baraka ya Uislamu. Watawawajabisha kwa hilo nami pia nitawalaumu kwa hilo." Kisha akalia na kuanza kuzungumzia sababu za kusilimu.

Tukio hili la mfano linatakiwa kutuhofisha na kutufanya tutafakari. Kwa sababu kufikisha

ujumbe wa Uisalmu ni jukumu letu tulililopewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu tunalotakiwa kulitekeleza. Na jukumu hili sasa limekuwa zito zaidi kutokana na nyenzo za kisasa za mawasiliano. Siyo tu watu walio mbali nasi bali pia watu walio karibu nasi watatufanya tuwajibishwe kwa kupuuza kwetu na kutotilia maanani katika kufikisha ujumbe wa Uislamu.

Tunaeleza wazi kuwa dini haiwezi kutumika kama chombo cha mambo ya kisiasa. Kwa hali hiyo mambo ya kidini na masuala ya kisiasa yanapaswa kutenganishwa. Kwa mfano, "Makhawariji" walikuwa wakidai kuwa chochote walichofanya walikifanya kwa jina la Uislamu, lakini kinyume chake walichokuwa wanakitaka katika kufanya hivyo ni mawazo ya kisiasa na fujo, mambo ambayo yapo nje kabisa na fikra za Kiislamu. Katika historia, watu, makundi na wakati mwingine hata madola ambayo yanataka kuvuruga amani ya jamii kwa maslahi yao binafsi na kunufaika na migogoro wametumia aina hii ya ujanja na hila za kisiasa. Watu hawa walitumia mambo yanayokubaliwa na jamii, hasa dini, ili kufanya mambo yao maovu yaonekane kuwa ni mema. Kisha wakaanza kampeni na harakati za kuwachafua watu wa dini. Tunaweza kutaja kile ambacho Abdullah bin Saba, ambaye aliandaa mazingira ya Vita vya Jamal, alichokisema kuwaambia wafuasi wake:

"Enyi watu! Maisha na heshima yenu inategemea machafuko na mapigano katika jamii. Hivyo basi wafanyeni wapigane. Kesho watu hao watakapoanza kupigana, hamasisheni mapigano.

Pindi asili ya mwanadamu ya "kiumbe bora (ahsani taqwim)" utakapozingatiwa; umuhimu wa unaotakiwa kutolewa kwenye dhana ya ubinadamu utapata kueleweka vizuri sana. Hali hii ya fikra inaonekana katika misingi yote ya uislamu kuhusu wanadamu.

Msiwaache wajishughulishe na kitu kingine chochote. Kwa hiyo, watu mlio pamoja nao wanatakiwa kudhani kuwa kuna dharura ya kuendelea kwa mapigano baina ya Ali, Zubair, Talha na wale wenye fikra kama zao, na hilo litawalazimisha waachane na kile msichokitaka, yaani amani..." (I. Canan, HadisAnsiklopedisi, XIII, 334)

Haya maneno yanaweza kuwa muongozo wa kuelewa sababu ya hali ya kughafilika kwa Waislamu na migogoro hapo zamani na hata sasa. Katika karne iliyopita tunaona kuwa ulimwengu wa Kiislamu uliachwa bila kiongozi na umekuwa ukikabiliana na aina mbalimbali za migogoro na mapigano. Ili kujua sababu hasa iliyo nyuma ya uhasama huu, tunatakiwa kuichunguza kwa makini maana ya maneno yaliyotajwa hapo juu.

Leo hii sababu ya kushuhudiwa kwa uonevu na dhulma kubwa ulimwenguni ni watu kuziacha sifa na tabia tukufu kama vile upendo na huruma, na badala yake wakaanza kufuata matamanio ya kihayawani ya nafsi zao.

Jalal al-Din Rumi (q.s) anaeleza kwa uzuri yafuatayo:

"Ewe unayepandikiza mbegu ya mabaruti ulimwenguni! Zinduka na uache kutafuta mwiba ulioupanda katika bustani la mawaridi ambapo kurumbizi huimba; usiyalaumu mawaridi kwa makosa yako mwenyewe." [26]

"Ni kwa hali gani ya akili unatafuta makosa na kasoro katika uso wa mwezi; jaribu kuokota miiba katika pepo. Ewe mwenye kutafuta miiba badala ya mawaridi! Ukienda peponi, huwezi kukuta miiba zaidi yako wewe mwenyewe"

26. Juzuu II, utenzi 153.

Rumi anawaonya Waislamu dhidi ya waharibifu:

"Kuna wale wanaowala wanadamu kama wanyama. Salamu zao na maneno yao ya "la hawla" yote ni upuuzi. Kwa maana nyoyo zao ni vitanda vya mashetani, na wao wenyewe, ni mashetani wa kibinadamu."

"Wengine huonekana kama wauza nyama ambao wangependa kuzichuna ngozi za wenzao. Kwa upande mmoja husema "rafiki yangu, mpendwa wangu", kwa upande mwingine anakiandaa kisu chake. Kwa ufupi hukulaghai kwa maneno matamu yenye kufurahisha ili kuichuna ngozi yako. Na lakini ubaya ulioje wa hali ya wale wanaomeza afyuni wanayopewa na maadui zao."

Kila mtu katika hali hii hutumia ubinadamu kama kichaka kwa sababu haijui heshima ya kweli ya binadamu; hajaonja upendo wa Mwenyezi Mungu na hajawahi kupata fungu la huruma. Kama haya yangekuwa mawazo, wangeuuwa ukweli; kama wangekuwa washairi, wangezifisidi nyoyo; kama wangekuwa watetezi wa maadili, wangeyaharibu. Rumi anawazungumzia akisema:

"Akishika ua mkononi mwake, hubadilika kuwa mwiba kwa wengine; na akienda kwa rafiki, hung'ata kama nyoka."

Mwenyezi Mungu Mtukufu anaelezea mazingira ya hali hii ya kughafilika:

"Na wanapoambiwa: Msifanye uharibifu ulimwenguni. Husema: Bali sisi ni watengen-

"Ewe unayepandikiza mbegu ya mbaruti ulimwenguni! Zinduka na uache kutafuta mwiba ulioupanda katika bustani la mawaridi ambapo kurumbizi huimba; usiyalaumu mawaridi kwa makosa yako mwenyewe."

Jalal al-Din Rumi (q.s)

ezaji. Hakika wao ndio waharibifu, lakini hawatambui." (Qur'an, 2: 11-12)

Basi jambo muhimu siyo maamuzi, matakwa na raghba binafsi za mtu bali matakwa na maagizo ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Wale wanaotumia sura na misingi ya dini kama maficho ya malengo yao ya kiovu na kijanja ndiyo wenye kuhasirika na kukosa radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwenyezi Mungu anasema yafuatayo kuhusu wale wanalioifisidi ardhi na kuwaua mitume wao:

"Kwa sababu ya hayo tuliwaandikia Wana wa Israili ya kwamba aliyemuuwa mtu bila ya yeye kuuwa, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama amewauwa watu wote. Na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote. Na hakika waliwajia Mitume wetu na hoja zilizowazi. Kisha wengi katika wao baada ya haya wakawa waharibifu katika nchi." (Qur'an, 5: 32)

Kwa sababu mtu anayeua nafsi bila hatia, kwa kuushambulia utakatifu wa nafsi hiyo anakuwa hakutambua haki ya nafsi hiyo kuishi na huwahamasisha wengine kutenda uhalifu kama huo. Hivyo, kwa mujibu wa maneno ya Mwenyezi Mungu, yeyote anayeua nafsi anastahiki ghadhabu na adhabu ya Mwenyezi Mungu na huchukuliwa kama amewaua wanadamu wote. Na kuokoa uhai ni sawa na kuwaokoa wanadamu wote.

Katika jambo hili Mawlana Jalal al-Din Rumi (r.a) anaufananisha Uislamu na kiovu:

"Ewe unayepandikiza mbegu ya mbaruti ulimwenguni! Zinduka na uache kutafuta mwiba ulioupanda katika bustani la mawaridi ambapo kurumbizi huimba; usiyalaumu mawaridi kwa makosa yako mwenyewe."

Jalal al-Din Rumi (q.s)

"Hakuna anayekufa kwenye ufukwe wa maji ya uhai". Hivi ndivyo anavyoakisi na kuonyesha wema wa dini hii.

Tunaweza kusema kuwa misingi ya Uislamu inazunguka kwenye aina hii ya hisia. Katika muktadha huu Uislamu huanza kuwatengeneza watu imani sahihi na kisha kwa tabia njema, huruma, kuwahudumia watu, elimu na maarifa, fadhila, kutii sheria na viwango vya juu vya kimaadili. Kwa njia hii humhuisha mwandamu kwenye hisia na maana ya kweli ya ubinadamu.

Katika zama zetu hizi sifa pekee inayoweza kuiokoa, kuingia ndani na kuipamba nafsi ni huruma. Na matunda ya huruma ni ukarimu, staha, kuwahudumia watu, kusamehe na kutokuwa na husuda.

Huduma zote zenye Ikhlasi zinazowafikia watu bila kuangalia manufaa ya kidunia huinyenyekeza nafsi na kumleta mja karibu zaidi na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ni kwa kuwahudumia viumbe tu ndipo milango ya matumaini katika nyoyo zetu hupata kufunguliwa, na hivyo kuongeza nafasi na fursa za kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Vinginevyo, mielekeo na tabia za ubinafsi zinazoonekana katika matendo yetu ni vigumu sana kuzifuta kwa sababu zinakuwa zimeweka kivuli na kuliziba lengo kuu la kuzaliwa kwetu.

Kwa muhtasari, imani na tabia njema ni msingi wa amani na furaha ya Kiislamu. Hii ndiyo sababu kwamba waja wema huzigeuza akili na nafsi zao kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kujitolea viungo vyao katika kufanya mambo mema na yenye

"Na wanapo ambiwa: Msifanye uharibifu ulimwenguni. Husema: Bali sisi ni watengenezaji. Hakika wao ndio waharibifu, lakini hawatambui."

(Qur'an, 2: 11-12)

faida. Kama asemavyo Jalal al-Din Rumi: *"Oh, mwenye furaha ni mbaya kwa yule ambaye mtu mwema amesuhubiana naye; huzuni kwa yule mwenye wajihi wa uwaridi ambalo kipupwe kime-andamana naye!"*

Ewe Mwenyezi Mungu! Tupe baraka ya ma-zuri ya Uislamu katika ulimwengu huu na ke-sho akhera. Tulinde sisi, dola yetu, umma wa Kiisalmu na wanadamu wote dhidi ya kila aina ya masaibu na majanga.

Huduma zote zenye ikhlasi zinazowafikia watu bila kuangalia manufaa ya kidunia hu-inyenyekeza nafsi na kumleta mja karibu zaidi na Mwenyezi Mungu Mtuku-fu. Ni kwa kuwahudumia viumbe tu ndipo milango ya matumaini katika nyoyo zetu hupata kufunguliwa, na hivyo kuongeza nafasi na fursa za kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu Mtuku-fu.

Njia na Mbinu ya Muongozo wa Kiroho na Huruma Katika Kuwahudumia Watu

Kwa amali inayofanywa katika kuwahudumia viumbe lazima pawe na sifa fulani ili amali hiyo ipate kukubaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Sifa muhimu zaidi kuliko zote ni nia. Nia ya kitendo chochote lazima iwe ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu, siyo kwa ajili ya kujulikana kuwa "mkarimu" au kusifiwa na watu. Nia safi haitakiwi kuzibwa na hisia za umimi na misukumo ya siri yenye lengo la kuiridhisha nafsi. Huduma inayotolewa inatakiwa kutolewa kwa huruma na wema pamoja na tahadhari kubwa ya kutoziumiza hisia za wale wanaopewa huduma husika.

Kuhusu suala hili, kisa kifuatacho cha Erzurumlu Hakki ni cha mfano wa hali ya juu. "Siku moja Ibrahim Hakki alialikwa kwenye kijiji kimoja kwa ajili ya kutoa Khutba. Kijana mmoja asiyekuwa Muislamu akakodishwa kwa ajili ya kwenda kumchukua. Wakaanza safari. Walikuwa na farasi mmoja tu na Ibrahim Hakki na mtumishi huyo wakafanya zamu ya kumpanda farasi kama alivyofanya Umar (r.a) na mtumishi wake walipokuwa safarini kuelekea Jerusalem. Pamoja na hivyo kijana huyo alikataa akisema: "Wanakijiji wakisikia jambo hili watanifokea na hawatonilipa pesa yangu". Ibrahim Hakki akamwambia:

"Ewe mwanangu! Hatujui kitakachotokea katika nyakati zetu za mwisho. Unawahofia wanakijiji, hali yakuwa mimi naihofia hukumu kubwa tutakayokutana nayo mbele ya Mola wetu." Wakaanza kufanya zamu ya kumpanda farasi.

Jambo muhimu sio maamuzi, matakwa na raghba binafsi za mtu bali matakwa na maagizo ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Wakati wanaingia kijijini ilikuwa zamu ya kijana. Kijana huyo akakataa kupanda farasi, lakini Ibrahim Hakki akasisitiza afanye hivyo na wakaingia kijijini hali ya kuwa Ibrahim Hakki anatembea na kumkokota farasi.

Kama ilivyotarajiwa na yule kijana, wanakijiji waliwazunguka na kuanza kumsema yule kijana. Ibrahim Hakki akawaelezea mazingira husika wakaacha kumsema. Kisha wanakijiji wakamwambia yule kijana:

"Leo umeona na kushuhudia mema hayo ya ajabu. Kwa nini huukubali ujumbe wa Uislamu?" Yule kijana akawajibu:

"Kama mnaniita kwenye dini yenu, hilo sitalikubali. Lakini kama mnaniita kwenye dini ya mtu huyu mtukufu, nimeshaikubali tulipokuwa safarini kuja hapa."

Mawlana Jalal al-Din Rumi (r.a) anaufananisha Uislamu na kioevu: "Hakuna anayekufa kwenye ufukwe wa maji ya uhai". Hivi ndivyo anavyoakisi na kuonyesha wema wa dini hii.

Kitendo hiki cha mfano kilichofanywa na mtu wa Mungu kinatuonyesha athari ya huruma na muongozo wa kiroho katika kuwahudumia watu. Kwa namna moja kuweza kuamiliana na wengine kama binadamu wanavyostahili ni kuwa na uwezo wa kuwaangalia viumbe kwa daraja ya Muumba ambapo ndiyo sababu ya watu wema kuwaangalia wanadamu kama makhalifa wa Mwenyezi Mungu Mtukufu ardhini. Na wanaishi wakiutambua ukweli kwamba kuna siri ya Mungu iliyopulizwa ndani mwao.[27] Hawa waumini wema hawaigeuzi migongo yao dhidi ya wakosaji hata kama wakosaji hao watakuwa wametenda madhambi mengi

27. Tazama Qur'an, 15: 29.

kiasi gani, kwa sababu ya ukamilifu unaopatikana katika asili ya binadamu. Hawapotezi matumaini kutokana na wakosaji na wala hawawafanyi wakosaji wakose matumaini. Kiukweli majina ya Mwenyezi Mungu yanayorudiwarudiwa sana ndani ya Qur'an Tukufu ni "al Rahman – Mwingi wa Rehma" na "al Rahim – Mwenye kurehemu" na vilevile kuna sura ndani ya Qur'an iitwayo Rahman, ambayo pia inaanza na jina hilo hilo la Mwenyezi Mungu.

Kwa hiyo kuwatazama wanadamu katika mtazamo huu, yaani kuamiliana nao kwa huruma na uongofu, ndiko kunakoendana zaidi na radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu na njia yenye baraka zaidi ya kuamiliana nao. Vilevile njia hiyo ina sifa za hali ya juu ambazo zinaweza kuzitoa sifa fichu za binadamu na kuzileta kwenye nuru na mwanga, kwa sababu, hii ni tabia adhimu ambayo huwapatia watoaji na wapokeaji uzuri, ukomavu, upendo na ukuruba wa kuwa karibu na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Vilevile ni nyenzo inayowafanya watu watukufu kuwa watukufu, kama vile Masufi mashuhuri Yunus Emre na Mawlana Jalal al-Din Rumi. Ni kama kielevu kinachoweza kuzipa uhai roho zilizokufa.

Hiyo ndiyo sababu kwamba yale yaliyomo ndani ya Usufi na mbinu zake za kufikisha ujumbe wa Uislamu zina umuhimu mkubwa. Ni ukweli wa kihistoria kuwa pindi mpangilio wa kijamii mjini Anatolia ulipotikiswa na uvamizi wa Wamongol, Masufi kama vile Yunus Emre na Mawlana Jalal al-Dini Rumi walihakikisha amani na utulivu kwa ajili ya jamii hiyo iliyosongwa. Masufi hawa waliwachukulia watu walioghafilika kama wagonjwa wanaohitaji ponyo. Walihakikisha wanaendelea kuwa mbali na "chuki na uadui." Tungo zifuatazo za Yunus Emre inatoa mfano wa mwenendo huu:

"Sikuja kupigana
Nimekuja kwa ajili ya upendo
Nyoyo ni makazi ya Rafiki (Mwenyezi Mungu)
Nimekuja kuzifariji nyoyo"

Yunus Emre

Sikuja kupigana
Nimekuja kwa ajili ya upendo
Nyoyo ni makazi ya Rafiki (Mwenyezi Mungu)
Nimekuja kuzifariji nyoyo

Kwa kuwa watu hawa muhimu walikuja kuzifariji nyoyo, daima waliwatazama watu kupitia nyoyo zao wenyewe; kwa kuwa waliamiliana na kila mtu kwa huruma na upendo, wakawa sababu ya watu wengi kuuchagua Uislamu. Kama wangefanya kinyume, wangepoteza mawasiliano na watu hawa kwenye ncha ya mteremko mkali na wangeshindwa kuwaelezea kuhusu Uislamu. Na hilo lingekuwa kinyume na Mwenyezi Mungu anavyotaka. Kwa maana Mwenyezi Mungu Mtukufu anataka waja Wake waokolewe kutoka katika vinamasi walivyozama ndani yake, na akawatuma maelfu ya mitume katika historia ya mwanadamu na akawaagiza kuzitakasa nafsi za watu kwa muamala laini. Kwa lengo hilo hilo, watu wa Mungu waliendeleza muamala huohuo katika mafunzo yao ya kiroho kwa wanadamu.

Mawlana Jalal al-Din Rumi (r.a) anaufananisha Uislamu na kioevu: "Hakuna anayekufa kwenye ufukwe wa maji ya uhai". Hivi ndivyo anavyoakisi na kuonyesha wema wa dini hii.

Mola wetu, ambaye ndiyo chanzo pekee cha huruma na rehema, anaelezea njia ya kuwaita watu kwenye ujumbe wa Uislamu kama ifuatavyo:

"Waite waelekee kwenye Njia ya Mola wako Mlezi kwa hekima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola wako Mlezi ndiye anayemjua zaidi aliyeipotea Njia yake, na Yeye ndiye anaye wajua zaidi walioongoka." (Qur'an, 16: 125)

"Na ni nani mbora wa kusema kuliko aitaye kwa Mwenyezi Mungu na akatenda mema, na

akasema: Hakika mimi ni katika Waislamu? Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu." (Qur'an, 41: 33-34)

Kwa kufuata njia hii kutoka kwa Mwenyezi Mungu, nyoyo kadhaa zilizokuwa kama miba zilibadilishwa kuwa mawaridi na nafsi zenye giza zikafunikwa na nuru ya Uislamu.

Kutokana na ukweli huu, Jalal al-Din Rumi anaelezea umuhimu wa kuwaongoza wale wasiokuwa Waislamu na wale wakosaji pamoja na lugha inayotakiwa kutumiwa katika mafunzo na muongozo wa kiroho:

"Japokuwa chuma kilikuwa na giza na hakikuwa na nuru, ung'arishaji ukaondoa giza lake. Chuma kiliona ung'arishaji na kuufanya uso wake kuwa mzuri, ili kwamba picha zake ziweze kuonekana ndani yake."

"Umeyafanya maji kuwa yenye tope: usizidi kuyafanya kuwa hivyo. Usiyatingishe (kuyachafua): acha maji yawe safi, na (kisha) tazama mwezi na nyota zinazozunguka ndani yake. Kwa maana mtu ni kama maji ya mto: yanapokuwa na tope, huwezi kuona kilicho ndani yake."

Kama inavyoelezwa na Mawlana Jalal al-Din Rumi (q.s), nafsi ya mwanadamu ni kama maji masafi; lakini inapokuwa na tope kutokana na dhambi na matendo machafu, hakuna anayeweza kuona kilicho ndani yake. Hivyo ili kuona lulu za hali ya kiroho na nuru ya ukweli, tunahitaji maji

"Basi nitakapo mkamilisha na nikampulizia roho yangu, basi mumwangukie kumsujudia."

(Qur'an 15: 29)

safi. Kwa hiyo, lengo la Usufi ni kuzitakasa nafsi na kuwapa watu na jamii kwa ujumla amani. Kwa maana Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwapamba wanadamu kwa uzuri, ukarimu na sifa za hali ya juu. Thamani ya mtu huongezeka kwa kadri anavyoboresha sifa hizi. Nyoyo zenye kujazwa hali ya kiroho ni mahali panapoonekana matendo mema, unyoofu na hali za kiroho. Kwa namna hii mja hupata kufikia daraja la "kuwa mfano uliokamilika."

Kwa hali hiyo, mwanadamu hawezi kuacha muongozo wa kiroho hata kama atakuwa amezama kiasi gani katika kutenda maovu na maasi. Ifuatayo ni mifano kadhaa wa kadhaa.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alimtuma swahaba mmoja kwenda kwa Wahshi, aliyemuua Hamza, kwa lengo la kumlingania kwenye Uislamu. Wahshi akajibu:

"Ewe Muhammad! Mwenyezi Mungu amekwishaeleza kuwa "Na wale wasio mwomba mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu, wala hawaui nafsi aliyo iharimisha Mwenyezi Mungu isipo kuwa kwa haki, wala hawazini - na atakaye fanya hayo atapata madhara, atazidishiwa adhabu Siku ya Kiyama, na atadumu humo kwa kufedheheka;" (25: 68-69), unawezaje sasa kuniita kwenye Uislamu? Nimefanya matendo yote haya ya kutisha. Ninawezaje kupata njia ya wokovu?"

Hapo Mwenyezi Mungu Mtukufu akateremsha ufunuo kuwa:

Kuweza kuamiliana na wengine kama binadamu wanavyostahili ni kuwa na uwezo wa kuwaangalia viumbe kwa daraja la Muumba aambapo ndiyo sababu ya watu wema kuwaangalia wanadamu kama makhalifa wa Mwenyezi Mungu Mtukufu ardhini.



قُلْ يَا عِبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَى أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ جَمِيعًا إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ

"Sema: Enyi waja wangu waliojidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu." (Qur'an, 39: 53)

Hatimaye, Wahshi akafarijiwa na habari hii njema, akatubu na kuingia katika Uislamu, akasema:

"Mola wangu! Upana ulioje wa msamaha Wako."

Maswahaba waliposikia hili wakamuuliza Mtukufu Mtume wa Allah:

"Ewe Mtume wa Allah! Je huruma na msamaha huu ni kwa Wahshi pekee au kwa Waislamu wote?" Mtukufu Mtume (s.a.w) akasema: *"Ni kwa Waislamu wote."*[28]

Wahshi ambaye alimuua Hamza (r.a) akawa Swahaba wa Mtume (s.a.w). Kutokana na msisimko wa kiroho aliokuwa nao kutokana na kusamehewa na Mwenyezi Mungu na muongozo wa kiroho, aliyahatarisha maisha yake katika vita akamuua Musaylimah al-Kadhdhaab aliyekuwa amedai utume wa uwongo na kumaliza msukosuko huo wa kijamii. Kwa njia moja hii ilikuwa kama

"Waite waelekee kwenye Njia ya Mola wako Mlezi kwa hikma na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hekima Mola wako Mlezi ndiye anaye mjua zaidi aliye ipotea Njia yake, na Yeye ndiye anaye wajua zaidi walio ongoka."

(Qur'an, 16: 125)

28. Tazama: Haythami, Majma' al-Zawaid, X, 214-15.

fidia yake kwa mauaji aliyoyafanya dhidi ya amri ya Mtume (s.a.w), Hamza.

Kama tunavyoona katika kisa kilichotajwa, habari njema ya kiwango cha juu kabisa cha huruma na msamaha zilitolewa na mwenyewe Mtume (s.a.w) kwa wale waliotubia kwa dhati na kwa Ikhlasi. Kwa muhtasari, mwanadamu amesikia habari za faraja, zenye ponyo na zenye kufurahisha kutoka katika kinywa cha Mtukufu Mtume (s.a.w). Na hata kama ni wakosaji kiasi, wanadamu wamebarikiwa kwa kuitwa na Mwenyezi Mungu kwa wito wa upole na huruma **"Enyi waja Wangu"**, kwa ajili ya Mtume Wake.

Kwa hiyo kuwatazama wanadamu katika mtazamo huu, yaani kuamiliana nao kwa huruma na uongofu, ndiko kunakoendana zaidi na radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu na njia yenye baraka zaidi ya kuamiliana nao.

Kwa hiyo ni jambo la msingi kutumia muamala huohuo wa upole, huruma na wenye ahadi ili kuiokoa jamii yetu kutoka katika hatari na mbinyo wa umaada wa kisasa. Ni jambo lifaalo zaidi kuzivuta nyoyo badala ya kuzisukumia kwenye matatizo ya kiakili; kwa sababu, baadhi yao wanaweza kuwa na hali fulani ya kiakili ambayo yaweza kuwa vigumu na hata kutowezekana kabisa kuzivuta (nyoyo hizo) kwa njia ya "mapambano na migogoro", kwa sababu akili zenye maradhi hasi hufungwa zisiukubali ushahidi wa kiakili. Ili kuzizoesha nyoyo ukweli, kwanza zinahitaji kuonyeshwa uvumilivu na sifa zake nzuri zisididimizwe. Hii ni njia yenye kufaa mno.

Kabla ya kumkosoa, kumshutumu mtu ambaye amezama katika kina kirefu cha maovu na madhambi, na kumtaka kufuata sheria za Uislamu, tunatakiwa kutoa kipaumbele kwenye kuuvuta moyo wake. Ili kufanya hivyo, tunatakiwa tujita-

hidi kuanzisha uhusiano wenye upendo na urafiki, ambao utaweka misingi na mazingira mazuri ya kuuvuta moyo wake. Baada ya kuziandaa nyoyo, makosa yanaweza kurekebishwa kidogo kidogo. Vile vile muamala wa kimaada na kimwili pamoja na maneno mazuri vinatakiwa kuzingatiwa kutokana na mchango wake katika kuongeza ufanisi wa matokeo. Kuhusu hili, maneno yafuatayo ya Mtukufu Mtume (s.a.w) yanatakiwa kukumbukwa:

"Uombezi wangu ni kwa wale watu wa ummah wangu waliotenda madhambi makubwa." (Abu Dawud, Sunnah, 20)

Jalal al-Din Rumi anauelezea muamala wa Mtukufu Mtume (s.a.w) kwa wakosaji katika misitari ifuatayo:

"Dawa huwatafuta wagonjwa na watu waliojeruhiwa ili kuwapa ponyo. Mahali maumivu yalipo, dawa huenda huko: Mahali palipo na tundu au uwanda wa chini, maji hukimbilia huko."

"Ukitaka maji ya huruma, nenda, usiwe na makuu kisha kunywa kinywaji cha huruma."

Hata hivyo, ili dawa au ponyo iwe na athari, jeraha linatakiwa lisafishwe kwanza dhidi ya vijidudu. Vivyo hivyo nafsi zenye maradhi zinatakiwa kusafishwa kwanza dhidi ya vijidudu vya dhambi; kwa maneno mengine zinatakiwa kuoshwa kwanza na maji ya toba. Dawa, au uombezi, utafuata baada ya usafishaji huo.

Maneno mengine ya Mtukufu Mtume (s.a.w) yasemayo:

"Japokuwa chuma kilikuwa na kiza na hakikuwa na nuru, ung'arishaji ukaondoa giza lake. Chuma kiliona ung'arishaji na kuufanya uso wake kuwa mzuri, ili kwamba picha zake ziweze kuonekana ndani yake."

Jalal al-Din Rumi

Umeya-" fanya maji kuwa yenye tope: usizidi kuyafanya kuwa hivyo. Usiyatingishe (kuyachafua): acha maji yawe safi, na (kisha) tazama mwezi na nyota zi-nazozunguka ndani yake. Kwa maana mtu ni kama maji ya mto: yanapokuwa na tope, huwezi kuona kilicho ndani ".yake

Jalal al-Din Rumi

"Mwenye kutubia kwa dhati ni mfano wa mtu ambaye hajatenda dhambi kabisa." (Ibn Majah, zuhd, 30) kwa upande mmoja yanatoa habari njema kwa wale waliotenda dhambi, na kwa upande mwing-ine yanaelezea sharti la awali la habari hii njema.

Mitume na watu wa Mungu wamefuata kwa umakini mbinu hii tukufu. Huruma inahesabiwa kuwa ni tunda la kwanza la imani na utiifu kwa Mwenyezi Mungu umeelezewa katika vifungu hivi viwili vya maneno:

a. *"Ta'dhim li Amrillah"*, yaani kutekeleza maagizo ya Mwenyezi Mungu kwa heshima kub-wa.

b. *"Shafaqat li khalqillah",* yaani kuwahuru-mia viumbe wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili ya Muumba wao.

Rafiki mmoja wa Mwenyezi Mungu, Fudayl bin 'Iyad, ni miongoni mwa mifano bora ya nyoyo hizi zenye imani zinazofuata kanuni hizi. Watu walimuona akilia, wakamuuliza:

"Kwa nini walia?"

Akajibu:

"Ninamlilia Muislamu ambaye alinidhulumu; kwa sababu ninahofia juu ya hali yenye kusikitisha atakayokutana nayo huko Akhera."

Rumi anaelezea kitu kinachowaongoza watu hawa watukufu kwenye kiwango hicho cha juu cha huruma:

"Bahari ya Huruma inapoanza kupiga kwa nguvu, hata mawe hupata kunywa Maji ya Uhai. Yule aliyekufa miaka mia moja huinuka kutoka ka-

burini; shetani mwenye kulaaniwa hupata kuhusudiwa hata na mahurul ayn kutokana na uzuri wake." [29]

Imesimuliwa kuwa Ibrahim bin Adham alikisafisha kinywa kichafu cha mtu aliyelewa. Watu walipomuuliza kwa nini kafanya hivyo akawajibu:

"Ingekuwa ni utovu wa heshima kukiacha kinywa kichafu kilichoumbwa kwa ajili ya kutaja majina ya Mwenyezi Mungu."

Mlevi yule alipozinduka watu wakamwambia:

"Ibrahim Adham, mtu wa Mungu kutoka Khorasan, alikisafisha kinywa chako."

Mtu huyo akaona aibu na kutubu. Ibrahim Adham akaambiwa ndotoni ya kwamba:

"Ulikisafisha kinywa chake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu; na Mwenyezi Mungu akausafisha moyo wake kwa ajili yako."

Mwenyezi Mungu Mtukufu anamwambia Mtume (s.a.w) na Waislamu wote:

خُذِ الْعَفْوَ وَأْمُرْ بِالْعُرْفِ

"Shikamana na kusamehe, na amrisha mema..." (Qur'an, 7: 199)

Naam, Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa mfano bora wa kulitekeleza agizo hili. Hata malaika waliyahusudu ukamilifu wa maadili, huruma na msamaha wake. Ufuatao ni mfano:

Siku ya ufunguzi wa Makka, Mtukufu Mtume (s.a.w) alitangaza msamaha kwa watu wote. Mji

Lengo la Usufi ni kuzitakasa nafsi na kuwapa watu na jamii kwa ujumla amani. Kwa maana Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwapamba wanadamu kwa uzuri, ukarimu na sifa za hali ya juu. Thamani ya mtu huongezeka kwa kadiri anavyoboresha sifa hizi.

29. Juzuu V, 2281-83.

wa Makka ambao hapo kabla ulikuwa ukishuhudia uonevu na uadui, ukapata kushuhudia ishara ya ajabu ya huruma, upole na upendo. Lakini, mkazi mmoja wa Makka aitwaye Fudalah alisogea karibu na Mtukufu Mtume (s.a.w) akijaribu kumuua. Mtukufu Mtume (s.a.w) akafunuliwa na Mwenyezi Mungu kuhusu nia ya Fudalah, ambapo, bila kuonyesha dalili yoyote ya kuhamaki wala kukasirika, alimuuliza Fudalah:

"Wewe ndiwe Fudalah?"

Akajibu:

"Ndiyo"

Hapo Mtukufu Mtume (s.a.w) ambaye ni Rehema kwa walimwengu akasema:

"Ewe Fudala! Tubia juu ya nia yako", na kisha akauweka mkono wake mtukufu juu ya kifua cha Fudalah.

Bila kuchelewa, Fudalah akatubu na kuukubali ujumbe wa Uislamu. Akawa miongoni mwa maswahaba wanaopendwa sana na Mtukufu Mtume (s.a.w).[30]

Mwanadamu hawezi kuachwa bila muongozo wa kiroho hata kama atakuwa amezama kiasi gani katika kutenda maovu na maasi.

Naam, hali hii ni ishara kamili ya kanuni ya "wale wanaokuja kwa lengo la kuua wanatakiwa kuhuishwa ndani mwako". Kuna mifano mingi ya kanuni hii katika historia ya Kiislamu. Kwa hakika Umar (r.a) na wengine wengi ni matunda yaliyotokana na uelewa huu. Rumi anasema:

"(Kwa sababu) Yeye (Mwenyezi Mungu), kutokana na ukamilifu wa huruma Yake na mawimbi

30. Ibn Hisham, al-Sirah, IV, 46; Ibn Kathir, al-Sirah, III, 583.

ya ukarimu Wake, hujaalia mvua na unyevunyevu kwenye kila ardhi kame." [31]

"Ewe unayewaita watu kwenye njia iliyonyooka! Dawa ya jicho ovu ni jicho jema. Hulifanya jicho baya kuwa hafifu kwa pigo lake. Rehema (ya Mwenyezi Mungu) imeitangulia (ghadhabu ya Mwenyezi Mungu): (jicho jema) linatokana na huruma na rehema (ya Mwenyezi Mungu), (ilhali) jicho baya limetokana na ghadhabu na hasira (ya Mwenyezi Mungu). Kwa hiyo, jicho jema hulishinda jicho baya kwa sababu limetokana na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hali hii ni dhihirisho la Hadith Tukufu: "Rehema Yangu imekitangulia kisasi changu" (Bukhari, Tawhid, 55). Ujue kuwa daima rehema ya Mwenyezi Mungu imekitangulia kisasi chake: ni kwa sababu hiyo mitume waliwashinda wapinzani wao."[32]

"Kwa hiyo fujo na malalamishi siyo njia ya kuzuia na kukinga majanga. Dawa yake ni huruma, msamaha na wema. Onyo la Mtume lisemalo "Sadaka ni njia ya kuzuia mabalaa"[33] linatakiwa kukuzindua. Sasa ni vyema ukaielewa njia na mbinu ya kuponya maradhi na mabalaa."[34]

"Lakini, usisahau kwamba kuwahurumia madhalimu ni kuwakandamiza wanyonge. Kuwahurumia wezi na mtu yeyote mwenye madhara ni kuongeza kipigo na kutomuonea huruma mnyonge."[35]

Nyoyo zilizojazwa hali ya kiroho ni mahali pa matendo mema, unyoofu na hali za kiroho. Kwa namna hii mja huweza kufikia hali ya "kuwa mfano kamili."

---

31. Juzuu IV, 1489.
32. Juzuu V, 513 -515.
33. Tazama: Tirmidhi, Zakat, 28; Suyuti, al-Jami' al-Saghir, I, 108.
34. Juzuu VI, 2590 -91.
35. Juzuu VI, 4261.

Hali ya uwiano inatakiwa kuangaliwa vizuri. Kwa sababu, japokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Ghafur al-Rahim, yaani, Msamehevu na Mrehemevu, lakini pia ni Azizun dhuntiqam, yaani, Mwenye nguvu na mkali wa kuadhibu na Mwenye kulipa kisasi dhidi ya dhulma na uonevu. Ndiyo maana kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w) katika moja ya hadith zake alisema:

"Mnusuru nduguyo akiwa ni dhalimu au aliyedhulumiwa."

Mtu mmoja akauliza: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Nitamsaidia kama atakuwa ameonewa, lakini kama atakuwa ndiye ameonea nitamnusuruje?"

Mtukufu Mtume (s.a.w) akasema: "Kwa kumzuia asidhulumu (kuwaonea wengine), kwani huko ndiko kumnusuru." (Bukhari, Ikrah, 7; Muslim, Birr, 62)

Kwa muhtasari, tungependa kusema kuwa leo hii watu katika nchi yetu kwa namna maalumu na watu wa dunia nzima kwa ujumla ni kama ndege waliojeruhiwa kuhusiana na suala zima la imani na Uislamu. Ni muhimu kuwa na huruma ili kuweza kuyatibu majeraha yao. Hili linaweza kufikiwa tu kwa kufuata misingi na njia zilizotajwa.

Mola wetu! Tujaalie kuwa miongoni mwa waja Wako wema wanaoielewa maana ya "Huruma Yangu huishinda hasira yangu" na tuwe ni wenye kuamiliana na wengine kwa huruma na msamaha.

Amin!

"Sema: Enyi waja wangu waliojidhulumu nafsi zenu! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu."

(Qur'an, 39: 53)

Ulaini na upole katika kuwahudumia watu

Kuwatazama wanadamu kwa mipaka ya misingi ya Uislamu kunahitaji kuwatazama na kuiheshimu asili yao safi badala ya kuangalia hali zao zilizochafuliwa na madhambi. Muumini wa kweli humchukulia mkosefu kama ndege aliyevunjika bawa, ambaye anahitaji kuangaliwa na kuhurumiwa. Huhisi uzito wa mzigo wa kumfariji na kuiponya roho ya mkosefu iliyo ndani ya mahangaiko. Kwa maana kuwahurumia viumbe wote kwa ajili ya Muumba wao ni njia yenye athari sana ambayo humpeleka muumini kwenye ukamilifu na baraka.

Uislamu umeukubali wastani kama kanuni yake kuu katika kuwafunza na kuwaongoza wanadamu. Hili linaweza kufikiwa kwa ulaini wa mwenendo na tabia. Kuanzia katika maisha ya Mtukufu Mtume (s.a.w), maswahaba na maisha ya watu wema yamejaa mifano ya ulaini wa hali ya juu katika kuamuliana na wakosaji.

Abu al-Darda, moja katika swahaba wa Mtume (s.a.w), alikuwa hakimu mjini Damascus. Katika tukio moja aliwasikia watu wakimshutumu mkosaji. Akawauliza:

"Mtafanya nini iwapo mtamuona mtu akitumbukia katika kisima?"

Wakajibu: "Tutateremsha kamba na kujaribu kumuokoa." Hapo Abu al-Darda akasema: "Kwa nini hamfikirii kumsaidia mtu huyu aliyetumbukia katika kisima cha madhambi?" Watu wakashangazwa na maneno yake wakasema: "Je huchukii

Kabla ya kumkosoa, kumshutumu mtu ambaye amezama katika kina kirefu cha maovu na madhambi, na kumtaka kufuata sheria za Uislamu, tunatakiwa kutoa kipaumbele kwenye kuuvuta moyo wake.

dhambi?" Abu al-Darda akawapa jibu lifuatalo: "Ninachukia dhambi zake lakini simchukii yeye."

Katika mfano huu, kuna mafunzo mengi makubwa, ambayo Abu al-Darda anakusudia kuyaweka katika nyoyo za waumini. Mafunzo haya ni ming'ao adhimu inayoakisi kutoka katika maagizo na radhi za Mwenyezi Mungu na maadili adhimu ya Mtume Wake. Katika historia ya Kiislamu, mafunzo haya yamekuwa ishara ya ukomavu na kuwa muamala madhubuti wa muongozo.

Muamala huu haumnyongi mkosaji katika makosa yake; kinyume chake muamala huu unalenga kumuokoa katika bahari ya toba kwa njia ya huruma, upole, msamaha na upendo. Mtukufu Mtume (s.a.w) aliwatendea upole hata washirikina wakubwa, kama vile Abu Jahl, na hakujishughulisha hata kidogo na madhambi yao. Aliwalingania wajitakase katika bahari ya imani ya wokovu. Imeelezwa katika Aya ifutayo kwamba baada ya mtu kusilimu madhambi yake ya nyuma hufutika na kubadilishwa kuwa mema.

إِلَّا مَنْ تَابَ وَ اٰ مَنَ وَعَمِلَ عَمَلاً صَالِحاً فَأُولٰئِكَ
يُبَدِّلُ اللهُ سَيِّئَاتِهِمْ حَسَنَاتٍ
وَكَانَ اللهُ غَفُوراً رَحِيماً

"Isipokuwa atakayetubu, na akaamini, na akatenda vitendo vyema. Basi hao Mwenyezi Mungu atayabadilisha maovu yao yawe mema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu." (Qur'an, 25: 70)

"Dawa huwatafuta wagonjwa na watu waliojeruhiwa ili kuwapa ponyo. Mahali maumivu yalipo, dawa huenda huko: Mahali palipo na tundu au uwanda wa chini, maji hukimbilia huko."

Jalal al-Din Rumi

Wale wasiokuwa na sehemu au fungu katika huruma hii tukufu ni maadui wa nafsi zao na ni maadui wa watu wote. Watu hao walioghafilika hawajui chochote kuhusu huruma na upendo. Kwa upande mmoja, marafiki wa Mwenyezi Mungu kama Jalal al-Din Rumi na Yunus Emre, ambao walifikia chimbuko hilo la huruma, walipendwa siyo tu na wanadamu bali hata viumbe wengine na wanyama. Wao ni kama mawaridi ya Peponi kwa nyuso zao zenye tabasamu na muonekano wenye ukarimu. Hata wakiwa katika mazingira magumu mno, waliendelea kueneza uzuri na wema duniani na kuwaponya wale wenye majeraha. Kudumisha wajihi wenye tabasamu na tabia ya ukarimu ni jambo muhimu katika dunia hii; kwa maneno mengine, kueneza uzuri katika mazingira ya aina yoyote ile. Rumi analielezea jambo hili kwa uzuri kabisa:

Kwa sababu mwezi haukuogopeshwa na haukulikimbia giza, ulipata kuangazwa na waridi likapata harufu yake tamu kwa sababu ya kuishi vizuri na miba."

"Usikilize ukweli huu kutoka kwenye mawaridi. Sikia yanachosema: Kwa nini nijisikie huzuni, kwanini nijisikie udhalili kwa kuwa pamoja na mwiba; nilipata uwezo wangu wa kutabasamu kwa kuvumilia kuwa pamoja na mwiba, na kwa sababu ya kuuvumilia, nikapata uwezo wa kutawanya uzuri na kueneza harufu nzuri ulimwenguni."

Eşrefoğlu Rûmî anaelezea kwa muhtasari muamala unaotakiwa ili kufikia hali hii katika utenzi wake ufuatao:

"Mwenye kutubia kwa dhati ni mfano wa mtu ambaye hajatenda dhambi kabisa."

(Ibn Majah, zuhd, 30)

Kwa ajili ya marafiki
Sumu inatakiwa kunywewa kama sharubati

Swahaba mmoja alimlaani mtu mmoja aliyekuwa mlevi sana ambaye alikuwa ameadhibiwa mara kadhaa. Mtukufu Mtume (s.a.w) aliposikia hivyo akasema:

"Usimlaani, kwani naapa kwa Mwenyezi Mungu, najua kwamba mtu huyo anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake." (Bukhari, Kitab al-Hudud, 5)

Mwanafunzi mmoja wa Ramazanoğlu Mahmûd Sâmî (q.s.) baada ya kukumbwa na msongo mzito alikwenda kulewa na kuja mlangoni kwa mwalimu wake. Mtu mmoja akamfungulia mlango na kuanza kumshutumu:

"Una tatizo gani? Unajua hapa uko wapi?"

Mwanafunzi akasema:

"Je kuna mlango mwingine unaoweza kunikumbatia kwa huruma?"

Mahmud Sami aliposikia majadiliano hayo, alikwenda mlangoni na kumkaribisha ndani mwanafunzi wake, akaufariji moyo wake uliovunjika. Kutokana na muamala mzuri wa mwalimu, mwanafunzi huyo alitubia na kuungana na safu za waumini wema.

"Kuwa na uwezo wa kuwatazama viumbe kwa macho ya Muumba" kumeelezewa katika hadith ifuatayo ya Mtukufu Mtume (s.a.w):

"Naapa kwa Allah, hamuwezi kuingia Peponi mpaka mhurumiane."

"Bahari ya Huruma inapoanza kupiga kwa nguvu, hata mawe hupata kunywa Maji ya Uhai. Yule aliyekufa miaka mia moja huinuka kutoka kaburini; shetani mwenye kulaaniwa hupata kuhusudiwa hata na mahurul ayn kutokana na uzuri wake."

Jalal al-Din Rumi



Maswahaba wakasema:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Sisi wote ni wenye kuhurumiana."

Mtukufu Mtume (s.a.w) akajibu:

"(Simaanishi) huruma ya kuhurumiana nyinyi kwa nyinyi tu, bali huruma kwa viumbe wote, (naam) huruma kwa viumbe wote." (Hakim, Mustadrak, IV, 185)

Hata kama mtu atajiweka mbali kiasi gani na lengo la kuumbwa kwake, bado ana hadhi ya juu ya kuwa "mwanadamu". Kuzama kwake katika madhambi kwa sababu ya kutojua utukufu unaopatikana katika asili yake ni sawa na Jiwe Jeusi kuanguka kutoka kwenye ukuta wa Ka'bah na kuchafuka. Hata likiwa katika hali hiyo, Waislamu hawawezi kuacha kuliheshimu. Wataliinua na kushindana kuliweka mahali pake patukufu. Watakachowaza ni asili yake ya Mbinguni na thamani ya asili yake. Wanadamu ni kama Jiwe Jeusi lililoteremka kutoka mbinguni, na bila kuangalia amezama kiasi gani katika madhambi, thamani yake ya msingi inaendelea kuwepo.

Hali ya uwiano inatakiwa kuangaliwa vizuri. Kwa sababu, japokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Ghafur al-, Rahim yaani, Msamehevu na Mrehemevu, lakini pia ni Azizun dhuntiqam, yaani, Mwenye nguvu na mkali wa kuadhibu na Mwenye kulipa kisasi dhidi ya dhulma na uonevu.

Kwa upande mwingine hakuna daktari mwenye ufanisi anayekasirishwa na mgonjwa wake kwa kuwa ameugua. Hata kama ameugua kutokana na makosa yake mwenyewe, daktari atalichukulia hilo kuwa linatokana na udhaifu wa mgonjwa wake. Na badala ya kumhoji kwa makosa yake, mara moja daktari ataanza kumpa matibabu ili kupunguza maumivu ya mgonjwa wake. Atajichukulia kuwa mtu mwenye kuwajibika kum-

tibu mgonjwa wake. Sufi huwa na hisia hizo hizo za daktari, na hisia hizi ni kama mwokozi (buoy) wa maisha kwa wale waliopotea.

Kumpelekea mkosaji boya la uokozi na kumuokoa asiendelee kuzama zaidi kwenye madhambi yake ni sababu hasa ya kupata furaha ya milele. Wosia wa Mtukufu Mtume (s.a.w) kwa Ali (r.a) wakati wa vita vya Kharbar ni wenye kututanabahisha:

"Ewe Ali! Naapa kwa Allah! Kama mtu mmoja ataingia katika Uislamu kwa mikono yako (yaani kwa sababu yako), ni bora kwako kuliko ngamia wekundu." (Bukhari, Kitab al-Jihad,143)

Ukweli huo huo umeelezwa ndani ya Aya ifuatayo:

وَمَنْ أَحْيَاهَا فَكَأَنَّمَا أَحْيَا النَّاسَ جَمِيعاً

"...na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote..." (Qur'an, 5: 32)

Hii ni imani. Lakini ukafiri ni dosari kubwa mno la hisia na fikra za binadamu. Kwa sababu nafasi ya kuokolewa na dhambi hii kubwa huwa kubwa zaidi pale yanapotumika maneno laini. Mwenyezi Mungu Mtukufu alipomtuma Nabii Musa (a.s) kwenda kwa Fir'aun kufikisha ujumbe wake alimuamrisha kutumia "qawlan layyin au maneno laini." Kwa sababu mafanikio katika kuwalingania watu kwenye ujumbe wa Uisalmu ni amali njema ya muhimu sana ambayo ni daraja la kuelekea kwenye furaha ya milele, kama ilivyoelezwa hapo juu. Kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu aliujua ukali wa ukafiri wa Fir'aun. Kwa hiyo tunatakiwa kufuata muamala wa ulaini hata kwa makafiri wakali sana badala ya kutumia shutuma, vitisho,

Muumini wa kweli humchukulia mkosefu kama ndege aliyevunjika bawa, ambaye anahitaji kuangaliwa na kuhurumiwa. Huhisi wajibu wa kumfariji na kuiponya roho ya mkosefu iliyo ndani ya mahangaiko.

hasira na vurugu. Rumi anatolea mfano wa jambo hili katika namna nzuri:

"Yaelewe vizuri maneno ya Mwenyezi Mungu: "Ewe Musa zungumza mbele ya Fir'aun kwa maneno laini."

"Ukiweka maji ndani ya mafuta yanayochemka, utayaharibu mafiga na birika..."[36]

Mwenyezi Mungu Mtukufu anauelezea ukweli huu katika Aya ifuatayo:

فَبِمَا رَحْمَةٍ مِنَ اللهِ لِنْتَ لَهُمْ وَلَوْ كُنْتَ فَظّاً
غَلِيظَ الْقَلْبِ لاَ نْفَضُّوا مِنْ حَوْلِكَ
فَاعْفُ عَنْهُمْ وَاسْتَغْفِرْ لَهُمْ

"Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungeli kuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia. Basi wasamehe, na waombee maghfira, na shauriana nao katika mambo. Na ukishakata shauri basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaomtegemea." (Qur'an, 3: 159)

Muamala huu unatakiwa siyo tu kutendewa makafiri au wakosaji bali pia ni muhimu katika kuamiliana na wale Waislamu wanaoishi kwa mujibu wa Uislamu lakini wakati mwingine wakawa wanafanya makosa. Mazungumzo makali na yenye kuvunja moyo yanaweza kuleta matokeo

"Isipokuwa atakayetubu, na akaamini, na akatenda vitendo vyema. Basi hao Mwenyezi Mungu atayabadilisha maovu yao yawe mema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu."

(Qur'an, 25: 70)

36. Juzuu IV, utenzi 3815 -16.

yaliyo kinyume na matarajio, kwa sababu watu wanaweza hata kushindwa kuwastahimilia wazazi wao wenyewe. Katika hali kama hiyo hata kusema ukweli kunaweza kuleta athari mbaya na kukosa thamani na mvuto wake. Rumi anasema:

"Baba yako anapokukaripia kwa makosa yako, hata yeye huonekana mbele yako kama mnyama mkali na mwenye kutisha..."

"Hii ni athari ya ukatili na vitisho vya baba yako. Kwa maneno mengine, japokuwa onyo la baba yako ni kwa ajili ya manufaa yako, ukali na ukaripiaji wake huifanya huruma na upendo wa baba yako uonekane kama unyama kwako."

Tunapaswa kuukumbuka upande huu wa saikolojia ya mwanadamu na hata kama amezama kiasi gani katika madhambi, tunapaswa kuamiliana naye huku tukijua akilini mwetu thamani inayopatikana ndani ya asili yake. Hii ndiyo sababu Mtukufu Mtume (s.a.w) akasema:

"Ni dhambi tosha kwa Muislamu kumdharau ndugu yake." (Muslim, Kitab al-Birr, 32)

Wakfu wa Bezmiâlem Vâlide Sultan mjini Damascus kwa ajili ya kufidia hasara inayosababishwa na wafanyakazi ni dhihirisho zuri la maneno haya ya Mtume (s.a.w) ndani ya historia ya Uislamu. Muumini anayeifahamu adabu hii yenye kupendeza anatakiwa "kujielekezea maswali yeye mwenyewe na kuwavumilia wengine." Kwa maana Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Enyi mlioamini! Jiepusheni na dhana nyingi, kwani baadhi ya dhana ni dhambi. Wala

Kwa sababu mwezi haukuogopeshwa na haukulikimbia giza, ulipata kuangazwa na waridi likapata harufu yake tamu kwa sababu ya kuishi vizuri na miba."

Jalal al-Din Rumi

msipelelezane, wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi. Je! Yupo katika nyinyi anayependa kuila nyama ya nduguye aliyekufa? Mnalichukia hilo! Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba, Mwenye kurehemu." (Qur'an, 49: 12)

Katika hadith ya Mtukufu Mtume (s.a.w) imeelezwa kwamba:

"Muumini hawezi kuwa mtu anayesingizia, kulaani na kuwaonyesha watu tabia za kukirihisha." (Tirmidhi, Kitab al-Birr, 48)

Waislamu wa mfano wanaofuata misingi hii katika maisha yao huwa mashujaa wa maadili na tabia bora za Kiislamu. Hata kama Mtume (s.a.w) angejua kwamba mtu fulani kafanya kosa, alikuwa halisemi jina lake wazi wazi katika kuwaonya wengine. Badala yake alikuwa akisema:

"Kwa nini ninawaona mkifanya hivi na hivi..."[37] kwa namna hii alikuwa akijielezea kuwa yeye ndiye alikuwa ameona ovu fulani.

Adabu hii ya kutoumiza hisia za wakosaji na kutowadharau ni sifa ya kawaida ya wale wanaouelewa vizuri Usufi; kwa sababu njia ielekeayo kwa Mwenyezi Mungu haipitii katika kuzivunja nyoyo, bali katika kuzifariji. Yunus Emre analielezea hili kwa uwazi katika tungo zifuatazo:

Moyo ni kiti cha enzi cha Mwenyezi Mungu
Mwenyezi Mungu hutazama moyoni
Amekasirika katika dunia mbili
Yule anayeuvunja moyo

"Usisahau mambo mawili: Mwenyezi Mungu na mauti. Sahau mambo mawili: mema yako unayowafanyia wengine na yale mabayo wanayokufanyia."

Luqman Hakim

37. Tazama Bukhari, Manaqib, 25; Muslim, Kitab al-salat, 119.

Ukweli wa jambo hili ni kuwa nyoyo kadhaa ambazo zilikuwa zimepotea kwa sababu ya muamala wa kukirihisha na wa ukali zimeokolewa kwa baraka ya njia hii ya kutafakari.

Kwa mujibu wa simulizi moja, Junayd al-Baghdadi alikuwa na mwanafunzi. Siku moja mwanafunzi huyu alikutwa akitenda kosa. Alijisikia aibu mno kiasi kwamba aliyaacha makazi ya wanafunzi wa kiroho na akawa hakurudi tena. Baada ya muda kupita, Junayd al-Baghdadi alipokuwa akitembea sokoni alimuona na kumkimbilia. Lakini mwanafunzi alipomuona mwalimu wake, alijisikia aibu na akatembea haraka kumkimbia. Junayd (q.s) aliwageukia watu waliokuwa pamoja naye na kuwaambia:

"Mnaweza kwenda, nina ndege ametoroka nyumbani" kisha akamfuata mwanafunzi wake. Mwanafunzi alipogundua kuwa mwalimu wake anamfuata, akaanza kutembea haraka haraka. Lakini alikwenda sehemu mbaya na kwa bahati mbaya akajigonga kichwani. Alipomuona mwalimu mbele yake, aliinamisha kichwa chake kwa aibu. Junayd (q.s) akasema:

"Ewe mwanangu! Unakwenda wapi? Unamkimbia nani? Mwalimu anapaswa kumsaidia mwanafunzi wake hususan katika nyakati ngumu kama hizi." Kisha akamchukua mwanafunzi wake na kumpeleka kwenye makazi ya wanafunzi wa kiroho. Mwanafunzi akamuomba msamaha mwalimu wake na kutubu. Hali hii ni mojawapo ya matokeo matukufu ya ukomavu wa kiroho katika kuwaongoza watu kwenye njia ya kweli ya Uislamu.

Kwa upande mwingine kuweza kwenda mbali zaidi ya kusamehe makosa na kulipa ubaya kwa wema na hata kuweza kumuombea

"Usikilize ukweli huu kutoka kwenye mawaridi. Sikia yanachosema: Kwa nini nijisikie huzuni, kwa nini nijisikie udhalili kwa kuwa pamoja na mwiba; nilipata uwezo wangu wa kutabasamu kwa kuvumilia kuwa pamoja na mwiba, na kwa sababu ya kuuvumilia, nikapata uwezo wa kutawanya uzuri na kueneza harufu nzuri ulimwenguni."

Jalal al-Din Rumi

uongofu na mafanikio mtu ambaye amekutendea mabaya inapaswa kuwa tabia na sifa kuu ya Muislamu. Badala ya kuomba laana, dua ya Mtume (s.a.w) kuwaombea uongofu watu wa Taifa waliompiga mawe ni mfano tosha wa tabia hii ya hali ya juu. Vilevile dua ya Mtume (s.a.w) kuwaombea wema watu wa Makkah ilisababisha makafiri kadhaa kuiona njia ya haki.

Katika hadith moja ya Mtukufu Mtume (s.a.w), imeelezwa kwamba:

"Wema siyo kumlipa wema yule aliyekufanyia wema na kumlipa ubaya yule aliyekutendea ubaya. Wema wa kweli ni kumlipa wema yule aliyekutenda ubaya." (Tirmidhi, Kitab al-Birr, 63)

Kwa sababu iwapo mtu aliyetendewa wema ni adui huwa rafiki; iwapo yupo katikati husongea karibu zaidi na upendo wake hukuwa na kuimarika. Hii ndiyo sababu kwamba watu wa zama hizi, ambao wapo katika janga la kiroho chini ya mbinyo usiokuwa na huruma wa umaada, huelekea kwenye mienendo ya kimaanawi na hivyo utumiaji wa mbinu na njia za Kisufi katika kufikisha ujumbe wa Uislamu huonekana kuwa wenye mafanikio. Leo hii Wamagharibi wengi waliouchagua Uislamu huvutiwa na vitabu vya Masufi wakubwa kama vile Mawlana Jalal al-Din Rumi na Ibn Arabi. Kwa maneno mengine, vitabu vinavyohusiana na Usufi ndiyo vitabu vya Kiislamu vinavyosomwa zaidi katika nchi za Magharibi. Tunahitaji mno moyo unaoeneza huruma kwa watu wote kama inavyoelezwa katika tungo zifuatazo za Rumi:

"Njoo, njoo vyovyote ulivyo,

"Isipo kuwa atakaye tubu, na akaamini, na akatenda vitendo vyema. Basi hao Mwenyezi Mungu atayabadilisha maovu yao yawe mema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu."

(Qur'an, 25: 70)

Haijalishi kama wewe ni kafiri, muabudu sanamu au muabudu moto,

Njoo, makao yetu siyo sehemu ya kukatisha tamaa.

Njoo, hata kama ulivunja kiapo chako mara mia moja,

Njoo tena."

Katika wito huo wenye stahamala, lengo la Rumi ni kuwatambulisha wanadamu asili yao kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kuwatukuza kwa Uislamu kwa kuwaokoa kutoka kwenye makosa yao. Vinginevyo wito wake hauna maana ya watu kuukubali Uislamu bila kubadilisha mtindo wa maisha yao ya awali. Lengo ni kuurekebisha ulimwengu wa kiroho wa mtu husika. Kitu kikivunjika, basi kinahitaji kupelekwa kwa fundi. Nyoyo za walimu wa Kisufi ni sawa na karakana, ambapo huwasaidia watu kurekebisha makosa yao ya zamani. Kwa hivyo ni jambo la kawaida kwa Rumi kuelekeza wito wake kwa watu waliotenda makosa.

Ni jambo la muhimu sana kuwakabili watu kwa ithaar (yaani kutoa kitu kumpa mtu mwenye shida hali ya kuwa wewe mwenyewe wakihitajia), huruma na uvumilivu hususan katika zama ambazo hisia za kidini zimedhoofika na watu wanatenda dhambi kulia na kushoto bila kuhisi wasiwasi wowote. Muamala huu utaongeza uwezekano wa kuwaokoa.

Lakini, lazima tueleze kuwa uvumilivu wa kuwavumilia wakosaji unakomea kwenye mambo binafsi tu. Vinginevyo, makosa na udhalimu wa kuvunja haki za wengine na kuvuruga amani na utulivu wa jamii haviwezi kusamehewa na kuvumiliwa. Aidha, inaeleweka kwamba wale wanaoishi katika Uislamu kwa juu juu hufadhaika pale

"Muumini anatakiwa kufanya juhudi katika kufanya mambo mema kwa ikhlasi bila kujali udogo wake; kwa sababu watendaji wengi wa mambo mema huyapuuza yale madogo. Kwa maana haijulikani ni jambo gani linalovuta baraka na radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu."
Musa Topbash (q.s)

wanapomuona mtu akitenda dhambi. Kwao wao, ni muhimu kujitenga na dhambi na kuwatenga watenda dhambi ili kujilinda dhidi ya athari zake zenye madhara; kwa sababu dhambi ni kama kipande kizuri cha muziki, kinaweza kuwavutia wale wanaoishi katika mghafala. Ndiyo maana kuyadharau makosa ni hatari mno kwa jamii, kwa sababu yanaweza kusababisha watu kuzitweza sheria za Mwenyezi Mungu na pia yanaweza kuziambukiza na kuziathiri nyoyo. Kwa maneno mengine, anayetakiwa kustahimiliwa ni mkosaji na siyo kosa; na uadui unatakiwa kuwa dhidi ya madhambi na siyo watendaji wa madhambi husika.

Kwa ujumla, tunaweza kuhitimisha sehemu hii kwa maneno ya Mtume wetu mpendwa (s.a.w):

"Warahisishieni watu mambo (yanayohusu dini), na msiyafanye kuwa magumu kwao na wapeni habari njema na msiwafanye wakimbie (kuukimbia Uislamu)." (Bukhari, Kitab al-'Ilm,11)

Mola wetu! Tupe baraka kwa kuzijaza siku zetu kwa hekima na kutufanya kuwa wenye upendo wa kweli! Tuangazie kwa siri za dunia mbili! Zifanye nyoyo zetu kuwa chimbuko la huruma kwa viumbe wote kwa ajili ya Muumba wao! Yabadilishe makosa na madhambi yetu kwa thawabu na wema!

Amin!

"Ni dhambi tosha kwa Muislamu kumdharau ndugu yake."

(Muslim, Kitab al-Birr, 32)

Adabu na kanuni za maadili katika kutoa huduma

"Huduma ya wenye upendo na malipo ya huduma zao ni Mwenyezi Mungu Mtukufu, au radhi, baraka na fadhila zake"

Mawlana Jalal al-Din Rumi

Kuwahudumia viumbe ni wajibu wa kijamii, ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu amewataka waja Wake kuutekeleza. Maisha ya muumini hubarikiwa na hupata maana na hadhi kwa kuwahudumia viumbe. Huduma, ambayo ni kipengele kikubwa cha maadili ya Kiislamu, ina maana ya kumtafuta Mwenyezi Mungu Mtukufu na radhi Zake kwa kuiweka huru nafsi dhidi ya mawazo ya ubinafsi na kuwaelekea viumbe kwa moyo wenye ithaar. Matendo yote ya huduma, yaliyo mbali na mawazo ya ubinafsi ya kupata manufaa ya kidunia na yakatendwa tu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, hudhihirisha kwa matendo kiu na shauku ya kutaka kuwa pamoja na Mola Mtukufu.

Kwa hiyo, huduma zote zinatakiwa kutekelezwa katika namna na kiwango kamili, na hili linaweza kufikiwa kwa kufuata kanuni kadhaa za kimwenendo. Kwa maneno mengine, juhudi katika kutekeleza huduma za kimaada na kimaanawi ni muhimu; na pia ni muhimu kama itakuwa imetekelezwa kwa kiwango na hali gani ya kiroho,

"...na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote..."

(Qur'an, 5: 32)

kwa sababu baraka ya huduma fulani na kukubaliwa na Mwenyezi Mungu hutegemea mambo hayo. Ndiyo maana Masufi wameelezea umuhimu wa kufuata adabu na njia maalumu katika kutoa huduma wakasema:

"Kuwahudumia viumbe ni muhimu lakini adabu katika kutoa huduma ni muhimu zaidi."

Kwa sababu, Mwenyezi Mungu hatazami tu jinsi tunavyofanya jambo kwa Ikhlasi bali pia hutazama ni kiwango gani cha hatua za unyoofu tulizozichunga na kuzizingatia. Ndiyo maana kwamba muumini ambaye ni masikini kwa mali lakini akawa mkarimu anaweza kupata baraka za Pepo kwa kutoa tu kipande cha tende, ilhali muumini mwenye utajiri wa mali lakini akawa masikini wa kiroho, yaani mwenye kughafilika na mwenye maradhi katika moyo anaweza kuwa mwenye hasara siku ya kiyama hata kama alitoa sadaka mali zake zote.

Kwa hali hiyo, kukubaliwa kwa ibada zetu mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kunategemea kiwango cha upendo na Ikhlasi ya nyoyo zetu. Matendo mengi ya kidini makubwa kwa nje hutupa kwenda kwenye kiwango cha kazi bure ndani ya moyo mdogo, ilhali matendo mengi madogo na ya kawaida kwa nje yanaweza kuwa sababu ya kupata malipo makubwa na manufaa ya milele ndani ya moyo wenye Ikhlasi.

Hivyo basi, suala muhimu ni hali ya hisia ya nyoyo zetu au mwenendo na misingi inayofuatwa na nyoyo zetu katika ibada zetu. Msingi huu hupata umuhimu zaidi katika suala la kuwahudumia viumbe. Mtukufu Mtume (s.a.w) aliamrishwa

"Wema sio kumlipa wema yule aliyekufanyia wema na kumlipa ubaya yule aliyekutenda ubaya. Wema wa kweli ni kumlipa wema yule aliyekutenda ubaya."

(Tirmidhi, Kitab al-Birr, 63)

kuswali katika Msikiti wa Quba, ambao ulikuwa umejengwa kwa Ikhlasi na taqwa, na akaamrishwa kuuvunja msikiti wa Dhiraar uliojengwa na wanafiki kwa misingi ya uchochezi na maasi. Tunapoitazama misikiti hii, tunaona kwamba yote miwili kwa nje ni misikiti, lakini tukiitazama kwa ndani, kuna tofauti kubwa mno kati yake kama tofauti ya Mashariki na Magharibi au Pepo na Moto. Hii ndiyo tofauti iliyopo baina ya huduma zinazotolewa na kutekelezwa kulingana na adabu za Kiislamu na zile huduma zinazotekelezwa bila kuchunga adabu hizo. Hivyo basi ni muhimu kuwa na maarifa, kufaa, utu, tabia na shakhsia madhubuti. Haina faida kutarajia kupata baraka na manufaa kutoka katika huduma zisizokuwa na Ikhlasi na zenye mghafala ndani yake.

Mtoaji huduma hatakiwi kuwa mtu mwenye kiburi. Badala yake, ili kuziokoa nyoyo, anatakiwa kuwa Muislamu aliyejitoa kwa dhati, ambaye yuko tayari kutumia siyo tu mali, muda, jina na umashuhuri wake, bali pia kila anachokimiliki. Mtoaji huduma wa kweli huingia katika ada ya kuwa katika ukaribu wa kila aina ya mateso, huzuni, karibu na hali ya kukosa matumaini. Hutekeleza majukumu yake kwa upendo; ni mtu wa moyo, chimbuko la matumaini na imani.

"Muumini hawezi kuwa mtu anayesingizia, kulaani na kuwaonyesha watu tabia za kukirihisha."

(Tirmidhi, Kitab al-Birr, 48)

Zifuatazo ni baadhi ya tabia na kanuni za maadili:

1. Kutambua umuhimu wa kutoa huduma:

Awali ya yote, mtoaji huduma anatakiwa kutambua na kuukubali msingi wa kwanza wa utoaji

huduma, kwamba huduma ni baraka na pia ni hazina. Vilevile anatakiwa kujua kuwa kuendelea kwa baraka kunategemea na yeye kuwa mwenye shukrani kwa Mola wake Mtukufu.



Huduma bora kuliko zote ni huduma ya i'la Kalimatillah au kuliinua neno la Mwenyezi Mungu.[38] Hii ni kazi kubwa na jukumu tukufu walilokabidhiwa waumini. Qur'an Tukufu na sunnah za Mtume (s.a.w) ni amana za Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume Wake kwetu sisi. Hata hivyo maswahaba wa Mtume (s.a.w) na watangulizi wetu wema waliibeba amana hii kwa zaidi ya miaka 1400; tuna wajibu wa kufanya vivyo hivyo kwa ajili ya vizazi vijavyo. Huduma hizi sasa zikawa mtaji wetu huko Akhera na viza zetu za kuingilia Peponi.

Baba yangu Musa Topbas (q.s), ambaye alijitolea kwa dhati kuwahudumia viumbe, alielezea umuhimu na thamani ya huduma kama ifuatavyo:

"Muumini anatakiwa kufanya juhudi katika kufanya mambo mema kwa Ikhlasi bila kujali udogo wake; kwa sababu watendaji wengi wa mambo mema huyapuuza yale madogo. Kwa maana haijulikani ni jambo gani linalovuta baraka na radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Yapaswa kueleweka kuwa fursa ya kuwahudumia watu huwa haimuangukii kila mtu. Kuna watu wengi wenye uwezo wa kufanya mambo

"Wema sio kumlipa wema yule aliyekufanyia wema na kumlipa ubaya yule aliyekutenda ubaya. Wema wa kweli ni kumlipa wema yule aliyekutenda ubaya."

(Tirmidhi, Kitab al-Birr, 63)

38. **I'la Kalimatillah:** ina maana ya kulipandisha jina la Mwenyezi Mungu na kuufikisha ujumbe wa Uislamu unaopatikana kwa ujumla wake ndani ya Kalimat al-Tawhid, yaani tamko la umoja na upekee wa Mwenyezi Mungu.

mema lakini kwa sababu ya ufinyu wa muda na nafasi wanashindwa kutoa huduma zao kwa watu. Wale wanaotoa huduma wanapaswa kuukubali utoaji wa huduma kama baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu; waongeze staha yao na waende mbali zaidi kwa kuwashukuru wale wanaohudumiwa kwa wao ndiyo sababu yao kupata baraka hii."

Imam Rabbani anaelezea umuhimu na ulazima wa kuwashukuru wale wanaohudumiwa:

"Namna ambavyo mtu mmoja anaweza kuwa sababu ya ukamilifu wa watu wengine, watu wengi pia wanaweza kuwa sababu ya ukamilifu wa mtu mmoja. Ingawa mwalimu wa kiroho huwaongoza wanafunzi wake kwenye ukamilifu, kwa hakika wao huwa sababu ya ukamilifu wa mwalimu wao kwa kila mmoja kumuakisi mwenzake."

Tunapaswa kutambua baraka za Mwenyezi Mungu Mtukufu juu yetu na kufanya juhudi ya kuzitumia katika njia Yake. Hii ni ishara ya ukweli wa imani zetu. Hili limeelezwa ndani ya Aya ifuatayo:

"Hakika Waumini ni wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake tena wasitie shaka kabisa, na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao. Hao ndio wakweli." (Qur'an, 49: 15)

Kwa upande mwingine, viwango vya wajibu vinavyotakiwa kutolewa kama Zaka katika mali vimeelezwa katika vyanzo mbalimbali vya Uislamu. Kwa hali hiyo, mtu anayetoa zaka yake anakuwa ametekeleza wajibu anaotakiwa kuutekeleza kulingana na mali yake. Lakini, kwa kuwa haiweze-

"Warahisishieni watu mambo (yanayohusu dini), na msiyafanye kuwa magumu kwao na wapeni habari njema na msiwafanye wakimbie (kuukimbia Uislamu)."

(Bukhari, Kitab al-'Ilm,11)

kani kupambanua viwango vya chini vya vipawa vingine tulivyopewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, tunatakiwa kujitolea kwa dhati kufanya kazi katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa kadri tuwezavyo mpaka mwisho wa pumzi yetu; ingawa hili halijulikani kwetu, linajulikana kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kitu ambacho ndiyo maana tunalazimika kufanya juhudi kubwa katika kuwasaidia na kuwahudumia wengine.

Mola wetu Mtukufu anasema: **"Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya iwezavyo..."** (Qur'an, 2: 286). Ndiyo maana muumini anatakiwa kutoridhika na huduma azitoazo na ajitahidi kuendelea kutafuta njia mpya za kutenda mema. Mojawapo ya mifano bora ya maisha ya namna hii ni maisha ya Swahaba Abdullah bin Maktum (r.a). Kwa kuwa alikuwa kipofu, alisamehewa kushiriki vita mbalimbali. Lakini, alijiunga na jeshi katika vita vya Qadisiyah akidhani kuwa ataweza hata kushika bendera. Hii ni ishara ya kuguswa kwa kuhusu kiwango cha chini cha huduma anachopaswa kukifanya ili apate radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Muumini hapaswi kuangukia katika mvunjiko wa moyo na mghafala kwa kudhani kuwa yeye ni dhaifu au kwamba hawezi kufanya jambo. Hatakiwi kuwaza hata kidogo kuwa huduma zake katika njia ya Mwenyezi Mungu zimefikia kikomo. Anatakiwa kuishi na msisimko endelevu wa kutenda mema mpaka wakati wa kuvuta pumzi yake ya mwisho.

Kuwahudumia viumbe ni wajibu wa kijamii, ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu amewataka waja Wake kuutekeleza. Maisha ya muumini hubarikiwa na hupata maana na hadhi kwa kuwahudumia viumbe.

Kwa mujibu wa Aya ifuatayo, kila muumini anatakiwa kujua mahitaji ya kuwahudumia wengine madamu ana uwezo wa kufunga na kufungua macho yake.

وَاعْبُدْ رَبَّكَ حَتّٰى يَأْتِيَكَ الْيَقِينُ

"Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini." (Qur'an, 15: 99)

Tukio lifuatalo linaonyesha hatua tunazotakiwa kuzifuata katika suala hili.

Baada ya vita vya Uhud, Mtukufu Mtume (s.a.w) alitoa agizo kuwa mashahidi na majeruhi wa vita wakusanywe. Aliguswa kwa namna maalum na hali ya Sa'd bin Rabi' (r.a). Mtume (s.a.w) akamtuma swahaba mmoja kwenda katika uwanja wa vita kumtafuta, lakini kadri alivyojaribu, hakuweza kumpata Sa'd (r.a) na kila alipomuita hakupata kuitikiwa. Mwishowe kwa tumaini la mwisho akaita:

"Ewe Sa'd! Mtume ameniagiza na kunitaka nikutafute kama upo miongoni mwa mashahidi au majeruhi."

Sa'd alikuwa akivuta pumzi zake za mwisho lakini aliposikia jina la Mtume (s.a.w), alikusanya nguvu zake zote na kusema:

"Sasa hivi nipo miongoni mwa mashahidi." Swahaba huyo akamkimbilia Sa'd, ambaye alikuwa na majeraha mengi, na kumsikia akisema kwa tabu:

"Wallah! Usipomlinda Mtume (s.a.w) dhidi ya maadui zake na ukaruhusu aumizwe hali ya kuwa una nguvu za kufungua macho

"Muumini anatakiwa kufanya juhudi katika kufanya mambo mema kwa ikhlasi bila kujali udogo wake; kwa sababu watendaji wengi wa mambo mema huyapuuza yale madogo. Kwa maana haijulikani ni jambo gani linalovuta baraka na radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu."

Musa Topbash (q.s)

yako, hutokuwa na udhuru wowote mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu."[39] Haya ndiyo yaliyokuwa maneno ya mwisho ya Sa'd (r.a).

Khalid bin Walid (r.a) alipokuwa katika dakika za mwisho za uhai wake, alisema:

"Masikitiko yaliyoje kwa shujaa aliyepambana maisha yake yote katika njia ya Mwenyezi Mungu kufa kitandani kama mtu dhaifu. Niinueni ili nife angalau nikiwa nimeegemea upanga wangu." Maneno haya yanaonyesha uelewa wake wa kina wa jukumu na wajibu wake kwa Uislamu.

Hisia na mawazo haya tunaweza kuyapanua kwenda kwenye nyanja zote za utoaji huduma katika njia ya Mwenyezi Mungu. Kila muumini anayejitolea kwa dhati kuwahudumia viumbe wa Mwenyezi Mungu analazimika kuchukua fungu lake katika hisia na mawazo haya na kuyafanya kuwa kipimo kikuu cha maisha yake. Anatakiwa kujua ukubwa wa wajibu wake na matokeo yake iwapo ataacha kuutumikia Uislamu hali ya kuwa ana nguvu na uwezo wa kutoa khidma.

Mitume na marafiki wa Mwenyezi Mungu walifikia daraja hii kwa kuwahudumia viumbe wa Mwenyezi Mungu hata walipokuwa katika vita vyao vya mauti. Wenye busara pekee ndiyo wanaoweza kuutumia mfano huu kuelewa umuhimu unaopatikana katika kuwahudumia watu.

"Kuna watu wengi wenye uwezo wa kufanya mambo mema lakini kwa sababu ya ufinyu wa muda na nafasi wanashindwa kutoa huduma zao kwa watu. Wale wanaotoa huduma wanapaswa kuukubali utoaji wa huduma kama baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu; waongeze staha yao na waende mbali zaidi kwa kuwashukuru wale wanaohudumiwa kwa wao ndio sababu yao kupata baraka hii."

Musa Topbash (q.s)

39. Tazama: Ibn Abd al-Barr, Isti'ab, II, uk. 590.

"Hakika Waumini ni wale walio muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake tena wasitie shaka kabisa, na waka-pigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao. Hao ndio wak-weli."

(Qur'an, 49: 15)

2. Kuupamba moyo kwa sifa na tabia za kiroho:

Nyoyo za wale wanaowahudumia watu zinapaswa kujazwa hali ya kiroho na nuru. Ustawi wa roho zetu hupatikana tu kwa virutubisho vya kiroho. Matokeo ya ukomavu huu ni kuwa, maarifa, wepesi wa kung'amua na hisia zetu vitaongezeka. Kama Bahauddin Naqshiband, Aziz Mahmud Hudayi, Ghazali, Mawlana Jalal al-Din Rumi na marafiki wengine wa Mwenyezi Mungu wasingeongeza maarifa ya kiroho kwenye elimu yao ya nje, wasingeweza kufikia daraja hii waliyonayo katika anga za nyoyo zetu kama nyota ya Thurayya.

Kwa kuwa marafiki hawa wa Mwenyezi Mungu waliyatazama mambo yote ya kidunia kutoka katika madirisha ya nyoyo zao kwa macho ya upendo, waliweza kuwa muongozo kwa jamii yao wenyewe na kwa wale wote waliokuwa wakitafuta muongozo. Hata Masultan waliogundua siri za elimu na sayansi, mantiki na akili walipata heshima ya ishara za upendo wa Mwenyezi Mungu. Kwa kweli, ishara hizi ziliwasaidia kupata upendo wa Mwenyezi Mungu.

Japokuwa viwiliwili vya marafiki hawa wa Mwenyezi Mungu vimo chini ya ardhi kwa mamia ya miaka, kazi zao za kiroho na utukufu zimeendelea kuwa hai, na wataendelea kuwa hai kwa kazi hizi, na huduma walizozitoa kwa wanadamu.

Lengo mojawapo muhimu sana la huduma ni kuwaongoza watu kwenye njia ya kweli ya Uislamu, na mafanikio ya lengo hili yanategemea hali ya kiroho inayopatikana katika muongozo

huo wa kiroho. Kadri tunavyoutekeleza Uislamu katika maisha yetu, ndivyo tunavyozidi kuwaathiri wale wanaotuzunguka. Moyo ni dirisha linalofunguka kuelekea kwenye siri za Kimungu. Kwa wale wanaotumia dirisha hili kwa busara, watashuhudia hali ya umilele. Kuingia katika kiuzi cha kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu humfanya mja awe msafiri wa umilele.

Tunapoyachunguza maisha ya Mtume wetu mpendwa (s.a.w), tunagundua kuwa wahy (ufunuo) ulianza kuteremshwa ndani ya moyo wake. Hili limeelezwa katika Aya kama ifuatavyo:

"Na bila ya shaka hii ni Uteremsho wa Mola Mlezi wa walimwengu wote. Ameteremsha Roho muaminifu, juu ya moyo wako, ili uwe katika Waonyaji, kwa lugha ya Kiarabu iliyo wazi." (Qur'an, 26: 192-195)

Qur'an hii kuteremshwa katika moyo wa Mtume (s.a.w) ilichangia kwenye tabia na mwenendo wake kuwa mfano hai wa Qur'an. Maswahaba waliistaajabia nuru hii katika mwenendo na shakhsia yake na wakapata mwenendo na shakhsia yao ya Kiislamu kutoka katika moyo wa Mtume (s.a.w). Watu hao waliobarikiwa, ambao kabla ya kuingia katika Uislamu walikuwa wakiishi maisha ya kinyama, walipata ukamilifu katika mwenendo baada ya kupata nuru iliyotoka katika moyo wa Mtume (s.a.w). Kwa hiyo wakawa "vilele vya ubora" katika historia. Waumini wenye lengo la kutoa khidma katika njia ielekeayo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu wanapaswa kuiga maisha ya Maswahaba, wapate hisa zao kutoka katika siri

"Wallah! Usipomlinda Mtume (s.a.w) dhidi ya maadui zake na ukaruhusu aumizwe hali ya kuwa una nguvu za kufungua macho yako, hutokuwa na udhuru wowote mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu."

Sa'd b. Rabi' (r.a)

hii adhimu na wajitahidi kuzijaza nyoyo zao kwa faydh ya Qur'an au nguvu ya kiroho.

Kuwahudumia wengine bila kuwa na moyo wenye nuru ni kama kumwaga ndoo ya maji jangwani. Mbegu inayopandwa katika ardhi kavu lazima itakuwa chakula cha panya. Ndiyo maana watoaji wa huduma wanapaswa kuwa makini kuhusu chakula chao cha kiroho. Wanapaswa kutoa kipaumbele kwenye hali ya kiroho katika ibada zao; na ithaar, nia njema na mvuto katika adabu na miamala yao. Wanatakiwa kufikia ukomavu wa kiroho. Kufikia hali hiyo ya kiroho kutamfanya mja afikie upendo wa Kimungu. Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema:

"...Mwenyezi Mungu humpenda mja anayemuogopa Mwenyezi Mungu, aliyetajiri wa moyo, anayejificha (na macho ya watu) na anayejishughulisha na kuitakasa nafsi yake." (Muslim, Kitab al-Zuhd,11)

"Na bila ya shaka hii ni Uteremsho wa Mola Mlezi wa walimwengu wote. Ameteremsha Roho muaminifu, juu ya moyo wako, ili uwe katika Waonyaji, kwa ulimi wa Kiarabu ulio wazi."

(Qur'an 26: 192-195)

Nyoyo za wale wanaowahudumia wengine zinatakiwa kuwa kama ardhi yenye rutuba. Kila kiumbe hai hutembea juu yake na kuacha uchafu wake. Lakini ardhi huusafisha uchafu wote huu na kisha hutoa aina mbalimbali za mimea kuwalisha viumbe wanaozagaa juu yake. Moyo wa mtoaji wa huduma unatakiwa kuwa kama ardhi; uzuri na wema wote katika moyo wake unapaswa kuonekana katika matendo na huduma zake anazozitoa. Ili kufikia hali hii, misingi minne ifuatayo inatakiwa kudumishwa:

a. Moyo kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu daima:

Qur'an Tukufu inasema kuwa:

“Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto. Mola wetu Mlezi! Hakika unayemtia Motoni umemhizi; na waliodhulumu hawana wasaidizi.” (Qur’an, 3: 191-192)

“Wale walioamini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!” (Qur’an, 13: 28)

Kumkumbuka na kumdhukuru Mwenyezi Mungu hakuna maana ya kusoma tu neno “Allah”, bali ni kuwa katika hali ya “kumtambua Mwenyezi Mungu.” Ni katika njia hii pekee ndipo nyoyo zinapoweza kupata utulivu, kwa sababu ndiyo njia pekee ya kufika kwenye hali ya kuwa karibu na Mwenyezi Mungu.

Pindi Maiyyat al-Ilahiyyah (au utambuzi wa kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu muda wote) inapochukua nafasi yake ndani ya nyoyo za wale wanaowahudumia viumbe wa Mwenyezi Mungu, shida na tabu zote hulainika mbele yao na kupata nguvu ya kuendelea kutoa huduma. Huduma zinazofanywa kwa juhudi na bidii huwa zenye athari na kumfurahisha anayeitekeleza huduma husika. Moyo unatakiwa kutakaswa dhidi ya mapenzi ya kupenda kitu chochote isipokuwa Mwenyezi Mungu na unatakiwa kujazwa upendo wa Kimungu. Ibn Arabi anasimulia Hadithul Qudsi ifuatayo katika kitabu chake cha Mishkat al-Anwar:

“Masikitiko yaliyoje kwa shujaa aliyepambana maisha yake yote katika njia ya Mwenyezi Mungu kufa kitandani kama mtu dhaifu. Niinueni ili nife angalau nikiwa nimeegemea upanga wangu.”

Khalid b. Walid (r.a)

"Ewe mwanadamu! Nilikuumba kwa ajili Yangu na nikaviumba vitu kwa ajili yako. Usiiharibu nafsi yako kwa vitu nilivyoviumba kwa ajili yako."[40]

b. Kuujaza moyo mapenzi ya kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake:

Upendo katika kutoa huduma ni mwanzo wa maendeleo na ustawi wa kiroho. Kwa kweli huu ni mwanzo wa kila kitu. Moyo huanza maendeleo yake ya kiroho na kuonyesha uzuri wake baada ya kuufikia upendo katika kutoa huduma.

Mapenzi ya kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake yanatakiwa kuwa makubwa zaidi kuliko mapenzi ya chochote katika maisha yetu. Imeelezwa katika Aya zifuatazo:

"...walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana..." (Qur'an, 2: 165)

"Sema: Ikiwa baba zenu, na wanenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mliyoyachuma, na biashara mnazoogopa kuharibika, na majumba mnayo yapenda, ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Jihadi katika Njia yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wapotovu." (Qur'an, 9: 24)

Moyo ukijazwa upendo wa kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, basi uzuri wote utaakisi katika nafsi zetu. Mwenyezi Mungu na Mtume Wake hawawezi kujulikana kutoka katika

"...Mwenyezi Mungu humpenda mja anayemuogopa Mwenyezi Mungu, aliye tajiri wa moyo, anayejificha (na macho ya watu) na anayejishughulisha na kuitakasa nafsi yake."

(Muslim, Kitab al-Zuhd,11)

40. Mishkat al-Anwar – (Nurlar Hazinesi), uk. 126 – 27.



vitabu bali wanaweza kujulikana kwa upendo katika nyoyo. Mpendaji humstaajabia na kumuiga mpenzi wake kulingana na kiwango cha upendo wake; kwa sababu upendo ni kama mkondo wa umeme unaoziunganisha nyoyo mbili. Yule anayependwa kamwe hatengani na moyo wa mpenziwe, na akili ya mpenzi daima huendelea kushughulishwa na yule anayempenda. Hutoa kila alichonacho, hata ikiwezekana kutoa nafsi yake kwa ajili ya mpendwa wake. Hivyo, ili tumpende Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) na kuwa wenye kustahili upendo wake, daima tunatakiwa kuendelea kumtakia rehema (salawat) ili nyoyo zetu zifungamane naye.

Kadri moyo unavyopata nuru kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) ndivyo unavyopata ukamilifu. Katika Aya Mwenyezi Mungu Mtukufu anamsifu Mtume Wake na kusema:

إِنَّ اللهَ وَمَلٰئِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا
الَّذِينَ اٰمَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيماً

"Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Nabii. Enyi mlioamini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu." (Qur'an, 33: 56)

Aya nyingine inasema:

"Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana." (Qur'an, 33: 21)

Kilele cha mfano hai wa Aya hizi tunauona katika maisha ya Maswahaba. Wale waliofika kwe-

Nyoyo za wale wanaowahudumia wengine zinatakiwa kuwa kama ardhi yenye rutuba. Kila kiumbe hai hutembea juu yake na kuacha uchafu wake. Lakini ardhi huusafisha uchafu wote huu na kisha hutoa aina mbalimbali za mimea kuwalisha viumbe wanaozagaa juu yake.

nye chemchem ya kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wataishi kama watu watukufu katika jamii ya Kiislamu mpaka siku ya Kiyama na watakumbukwa kwa dua na rehema. Ifuatayo ni mifano miwili katika mifano kadhaa ya wale wanaompenda Mtume wa Mwenyezi Mungu:

Mtume (s.a.w) alikuwa na utaratibu wa kutuma walimu kwenda kwenye makabila yaliyo jirani na mji wa Madinah kwa kazi ya kufikisha ujumbe wa Uislamu. Lakini, baadhi ya walimu walifanyiwa hiyana na makabila hayo. Tukio mojawapo ni "Tukio la Raji'" ambalo lilitokea katika eneo la Raji'.

Baadhi ya watu wa makabila ya Adal na Qara walikwenda Madinah na kumuomba Mtume (s.a.w) awatumie walimu watakaoweza kuwafundisha watu wa makabila yao kuhusu Uislamu. Ombi lao lilikubaliwa na Maswahaba wapatao kumi wakatumwa pamoja na watu hao. Kundi hilo lilipofika katika eneo la Raji' walikutana na watu mia mbili wenye silaha waliokuwa wamewawekea mtego. Khubaib na Zaid bin Adathna (r.a) walitekwa, huku wengine wakiuawa kishahidi. Kisha wakauzwa kwa washirikina wa Makkah.

Baadae maswahaba hawa wawili waliuawa. Wakati wa kuuawa, Zayd (r.a) aliulizwa:

"Je usingependa kuachiwa huru na Muhammad (s.a.w) akapata adhabu hii badala yako? Je usingependa kuona ukiwa nyumbani umepumzika kwa raha na badala yako akauawa yeye?"

Zayd (r.a) alitazama kwa kumsikitikia Abu Sufyan na kujibu:

"...walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana..." (Qur'an, 2: 165)

"Wallah! Siwezi kuona kuwa na raha mwiba uchome unyayo wa Muhammad (s.a.w) kwa gharama ya mimi kukaa nyumbani na familia yangu."

Abu Sufyan alishangazwa sana na jawabu hili akawaambia wenzake: "Tazameni, upendo wa Maswahaba kwa Muhammad (s.a.w) hayana kifani na hayajawahi kutokea. Kamwe sijawahi kumuona mtu anayempenda mwenzake kama ilivyo kwa wafuasi wa Muhammad."

Kisha wakaenda kwa Khubaib (r.a) na kumwambia kuwa wangemuacha huru kama angeachana na dini yake. Wote Khubaib na Zayd (r.a) wakasema: "Hata kama mngetupatia dunia yote, hatuwezi kuiacha dini yetu."

Khubaib alikuwa na ombi moja kabla ya kuuawa. Alitaka kutuma salamu zake kwa Mtume (s.a.w). Lakini atamtuma nani? Hapakuwepo na Muislamu mahali hapo. Akainyanyua mikono yake na kuanza kuomba:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Hakuna mtu hapa wa kupeleka salamu zangu kwa Mtume Wako (s.a.w). Tafadhali nipelekee salamu zangu kwake."

Wakati huo Mtume (s.a.w) alikuwa amekaa pamoja na maswahaba wake mjini Madinah akaitikia salamu na kusema: "wa alayhi al-Salaam au amani na salamu ziwe juu yake." Maswahaba waliokuwa hapo wakashangaa na kuuliza:

"Ewe Mtume wa Allah! Ni salamu ya nani hiyo uliyoitikia?" Mtume (s.a.w) akasema:

"Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto. Mola wetu Mlezi! Hakika unaye mtia Motoni umemhizi; na walio dhulumu hawana wasaidizi."

(Qur'an, 3: 191-192)

"Ni salamu ya ndugu yenu Khubaib"

Hatimaye makafiri waliwatesa sana maswahaba hao wawili na kuwaua. Wakati wa kufa kwake, Khubib alikuwa akisema maneno yafuatayo:

"Madamu ninakufa katika Uislamu, sijali kwamba ninakufa vipi..."[41]

Vilevile kwa sababu ya mapenzi yao kwa Mtume (s.a.w), maswahaba vijana walikuwa wakishindana kupeleka barua za Mtume (s.a.w) kwa viongozi wa nchi za kigeni. Walijitolea kufanya kazi hiyo bila kutoa udhuru wowote. Walipita katika milima mirefu, wakapita katika majangwa na kila aina ya tabu na kupeleka barua za Mtume wa Allah kwa wafalme mbalimbali wa Arabia. Hata wakiwa mbele ya kifo, walizisoma barua za Mtume (s.a.w) na kuonyesha upendo wao usio na kikomo wa mapenzi yao kwa Mtume (s.a.w).

Hiki ni kiwango cha mapenzi na ujasiri wa Maswahaba. Huku picha za maisha yao zikitustaajabisha, wale wanaompenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake kamwe hawakuingiwa na hofu. Kuzipamba nyoyo zao kwa upendo wa kumpenda Mtume yatakuwa matunda yenye baraka ya huduma yao tukufu.

"Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!"

(Qur'an, 13: 28)

c. Kuujaza moyo mapenzi ya kuwapenda Waislamu:

Palipo na undugu, pana huruma na upendo. Muumini asipowatakia wenzake kila anachoita-

41. Tazama: Bukhari, Maghazi, 10; Waqidi, Maghazi, uk. 280 – 81.

kia nafsi yake, imani yake haiwi kamili. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Hakika Waumini ni ndugu, basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na mcheni Mwenyezi Mungu ili mrehemiwe." (Qur'an, 49: 10)

Mtume wa Mwenyezi Mungu anasema katika mojawapo ya maneno yake:

"Hakika hamtoingia peponi mpaka muamini na hamtoamini mpaka mpendane. Je nikujulisheni kitu ambacho, mkikifanya, mtapendana: peaneni salamu miongoni mwenu (yaani jengeni mazoea ya kutoleana salamu) kwa kusema as-salaamu alaykum." (Muslim, Kitab al-Iman, 93)

Vile vile katika hadith nyingine imeelezwa kuwa:

"Mtume alisema, "Mwenyezi Mungu atawapa kivuli watu saba, katika siku ambayo hapatokuwepo na kivuli isipokuwa kivuli Chake. (Watu hao saba ni) mtawala mwadilifu, kijana aliyekulia katika ibada ya Mwenyezi Mungu (yaani kumuabudu Mwenyezi Mungu kwa Ikhlasi tokea utotoni), mtu ambaye moyo wake umeshikamana na msikiti (yaani huswali swala za wajibu msikitini katika jamaa", watu wawili waliopendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu na hukutana na kuachana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, mtu anayekataa wito wa mwanamke mshawishi kwa ajili ya kufanya jimai ya haramu na kusema: Ninamuogopa Allah, mtu anayetoa sadaka kwa siri sana kiasi kwamba mkono wa kushoto haujui kilichotolewa na mkono wa kulia(yaani hakuna anayejua kuwa

Upendo katika kutoa huduma ni mwanzo wa maendeleo na ustawi wa kiroho. Kwa kweli huu ni mwanzo wa kila kitu. Moyo huanza maendeleo yake ya kiroho na kuonyesha uzuri wake baada ya kuufikia upendo katika kutoa huduma.

ametoa sadaka kiasi gani), na mtu anayemkumbuka Mwenyezi Mungua katika faragha na kisha machozi yakamiminika machoni mwake." (Bukhari, Kitab al-Adhan, 36)

Katika Hadithul-Qudsi, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Upendo wangu umeandikwa kwa wale wanaopenda kwa ajili Yangu; kwa wale wanaopeana zawadi kwa ajili Yangu; kwa ajili ya wale wanaoaminiana na kuwa marafiki kwa ajili Yangu; kwa wale wanaowatembelea ndugu na kutembeleana wao kwa wao kwa ajili Yangu." (Ahmad bin Hanbal, Musnad,V, 229)

Vilevile Mtume wa Allah anasimulia kisa kifuatacho kuhusu undugu na upendo:

"Mtu mmoja alimtembea ndugu yake katika mji mwingine na Mwenyezi Mungu akamtuma malaika kwenda kumsubiri njiana na alipokutana naye akamuuliza: Unakwenda wapi? Akasema: Ninakusudia kwenda kwa ndugu yangu anayeishi katika mji huu. Akasema: Unamfanyia wema wowote (unaokusudia akulipe?) Akasema: Hapana, ninamtembelea kwa sababu tu nampenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hapo akamwambia: Mimi ni mjumbe kutoka kwa Mwenyezi Mungu: (nimekuja kukwambia) kwamba Mwenyezi Mungu anakupenda kwa kuwa unampenda (kwa ajili Yake)" (Muslim, Kitab al-Birr, 46; Ahmad bin Hanbal, Musnad, II, 292)

"Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana."

(Qur'an, 33: 21)

Watu wanaotoa huduma wakipenda, itaongeza nguvu zao na watatengeneza uwanja

wenye baraka kwa ajili ya huduma zao kwa sababu itawapatia umadhubuti. Panapokuwa na upendo hakuna magumu yanayoweza kushindikana. Mwenyezi Mungu anawasifu waumini wanaosimama bega kwa bega na kufanya kazi pamoja:

"Kwa hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanao pigana katika Njia yake kwa safu kama jengo lilio kamatana." (Qur'an, 61: 4)

Historia imeshuhudia ushindi mwingi wa wanajeshi waliosimama pamoja kwa upendo na imani. Mojawapo ya shuhuda za hivi karibuni ni Vita vya Dardanelles. Jeshi letu ambalo kimaada lilikuwa dhaifu lakini kimaanawi likawa imara lilipata ushindi wa kihistoria. Hata maadui walilazimika kukiri kuwa jeshi la Kiuthmaniyya lilipata msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Jenerali wa Kiingereza bwana Hamilton alisema:

"Tulishindwa kwa nguvu ya kiroho ya jeshi la Kituruki siyo nguvu za kimaada. Tuliona viumbe kadhaa wakishuka kutoka mawinguni."

Huu ulikuwa ushuhuda wa Aya iliyotangulia hapo juu; kwa sababu kwa wanajeshi hao kufa kishahidi ilikuwa ni furaha kubwa mno, na kuishi kama veterani wa vita ilikuwa ni heshima. Kila mmoja wao alikuwa kama umma wote. Walikabiliana na adui katika Vita vya Dardanelles kwa moyo wa umma wote wa Kiislamu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu amekataza sifa na tabia mbaya kama vile kudhihaki, kusengenya, kujadili mambo yasiyo na msingi na kutuhumiana kwa sababu mambo hayo hubomoa hisia za up-

"Madamu ninakufa katika Uislamu, sijali kwamba ninakufa vipi..."

Khubayb (r.a)

endo na undugu miongoni mwa waumini. Wale wenye tabia hizi wanaonywa na Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

"Ole wake kila safihi, msengenyaji! Aliye kusanya mali na kuyahisabu." (Qur'an, 104: 1-2)

Kwa hiyo basi wale wanaowaumiza watu kiroho na kimwili kwa mikono na ndimi zao watapata adhabu isikitishayo ndani ya moto wa Jahannam. Uislamu unawahamasisha waumini kujilinda dhidi ya mwisho huo mbaya kwa kuwa wenye kusamehe, wenye huruma na kwa kuombeana mema na heri. Mtukufu Mtume wa Allah (s.a.w) anasema:

"Jiepusheni na dhana, kwani dhana ni uongo mkubwa na mbaya mno katika mazungumzo, msitafitiane, msichunguzane, msioneane husuda, msijizoeze uovu, msishikamane na chuki na kuoneana uadui nyinyi kwa nyinyi. Na kuweni ndugu na waja wa Mwenyezi Mungu." (Muslim, Kitab al-Birr, 30)

"Hakika Waumini ni ndugu, basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na mcheni Mwenyezi Mungu ili mrehemiwe."

(Qur'an, 49: 10)

Mtukufu Mtume (s.a.w) aliasisi undugu wa mfano baina ya Maswahaba, undugu ambao utaiangaza njia ya waumini mpaka siku ya mwisho. Kwa hakika undugu huu ulioanzishwa baina ya wahamiaji wa Makkah (Muhajirun) na wenyeji wa Madinah (Ansar) ni tukio la aina yake katika historia. Wenyeji wa Madina walijitolea mali zao zote na kushirikiana kila walicho nacho pamoja na ndugu zao wahamiaji kwa usawa. Kwa upande mwingine wahamiaji wa Makkah hawakuonyesha kupendelea mali zao wakawaambia:

"Ndugu yangu, sitaki mali yako. Nionyeshe tu njia ya kwenda sokoni; hiyo inanitosha." Undugu

wao wa mfano umesifiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu na umepata heshima ya kutajwa ndani ya Qur'an Tukufu:

"Na walio na maskani zao na Imani yao kabla yao, wanawapenda waliohamia kwao, wala hawaoni choyo katika vifua vyao kwa walivyopewa (Wahajiri), bali wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji. Na mwenye kuepushwa uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufanikiwa." (Qur'an Tukufu, 59: 9)

Tukio lililosimuliwa na Hudhayfa linaonyesha Ithaar ya Maswahaba:

Tulikuwa katika Vita vya Yarmuk. Vita vilikuwa vimemalizika. Nilikuwa nikitembea katika uwanja wa vita katikati ya mashahidi na majeruhi nikiwa na kiriba cha maji. Nilikuwa nikimtafuta mtoto wa ami yangu. Nilimkuta amelala katika dimbwi la damu kwenye mchanga wenye joto kali. Alikuwa yu karibu kukata roho. Nilimuuliza kama alihitaji maji. Alishindwa kuongea akaashiria kuwa alikuwa akihitaji.

Nilikuwa nikijiandaa kumpatia, ndipo tulipomsikia Ikrimah akiugulia:

"Maji! Maji! Tafadhali, nipatie tone la maji!"

Mtoto wa ami yangu, ambaye alikuwa akitwa Harith, alimsikia na kuashiria kuwa nipeleke maji kwa Ikrimah. Nilimkimbilia Ikrimah. Kabla hata hajashika kiriba sauti nyingine ya kuugulia ikasikika kutoka kwa mtu mwingine. Ikrimah akakataa kunywa maji akanitaka nimpelekee yule aliyeku-

"Hakika hamtoingia peponi mpaka muamini na hamtoamini mpaka mpendane. Je nikujulisheni kitu ambacho, mkikifanya, mtapendana: peaneni salamu miongoni mwenu (yaani jengene mazoea ya kutoleana salamu) kwa kusema as-salaamu alaykum."

(Muslim, Kitab al-Iman, 93)

Katika Hadithul-Qudsi, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Upendo wangu umeandikwa kwa wale wanaopenda kwa ajili Yangu; kwa wale wanaopeana zawadi kwa ajili Yangu; kwa ajili ya wale wanaoaminiana na kuwa marafiki kwa ajili Yangu; kwa wale wanaowatembelea ndugu na kutembeleana wao kwa wao kwa ajili Yangu."

(Ahmad bin Hanbal, Musnad, V, 229)

wa akiugulia. Nilipompelekea mtu huyo, alikuwa 'Iyash, alikuwa akiomba dua akisema:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Kamwe hatujaacha kujitolea maisha yetu kwa ajili ya imani yetu. Tupe heshima ya daraja ya vifo vya kishahidi, na utusamehe madhambi yetu!"

'Iyash aliyaona maji lakini hakuweza kuyanywa. Alichoweza ni kutamka shahada na kisha akakata roho. Bila kuchelewa nikarudi na maji mpaka kwa Ikrimah, lakini naye alikuwa amekufa. Kisha nikakimbia mpaka kwa Harith, mtoto wa ami yangu. Kwa bahati mbaya, naye pia alikuwa amelala juu ya mchanga wenye kuunguza akiwa amefariki dunia.[42]

Hudhayfa (r.a) anaelezea hisia zake kama ifuatavyo:

"Hili ndilo tukio lenye kugusa hisia ambalo nimewahi kulishuhudia katika maisha yangu. Japokuwa hawakuwa na uhusiano wa damu, ithaar , wema na huruma yao iliacha athari katika akili yangu. Imani yao isiyotetereka juu ya Uislamu ndiyo iliyowafanya wawe hivyo. Uislamu ndiyo uliotengeneza kiwango hicho cha undugu miongoni mwa watu."

Upendo ni madai tu. Upendo maana yake ni kushirikiana na ndugu zako katika huzuni zao, kuwasaidia katika mahitaji yao, kuonyesha kujitolea na kuweza kushirikiana nao kile ulicho nacho. Un-

42. Tazama: Hakim, Mustadrak,III, 270.

dugu wa kweli huonekana wakati wa shida. Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema katika hadith yake:

"Mfano wa waumini katika kupendana, kuhurumiana ni kama mfano wa mwili mmoja; kiungo kinapouma, mwili wote huuma, kwa sababu ya kukosa usingizi na homa." (Muslim, Kitab al- Birr, 66)

Wakati mwingine Mtume (s.a.w) alikuwa akiwauliza maswahaba wake:

"Enyi marafiki zangu! Je leo mmekipapasa kichwa cha yatima? Je mlimtembelea mgonjwa? Je leo mmehudhuria mazishi?" Kwa maswali haya alikuwa kiashiria na kuonyesha umuhimu wa ithaar na kuwaelekeza Maswahaba kuishi maisha ya kijamii badala ya maisha binafsi.

Katika Hadithul-Qudsi nyingine, alikuwa akieleza kuwa huduma za kijamii ni sababu ya mtu kuwa karibu na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

"Kwa hakika, Mwenyezi Mungu Mtukufu atasema siku ya Kiyama: Ewe mwanadamu, nilikuwa mgonjwa lakini hukunitembelea.

Atasema: "Mola wangu; ningewezaje kukutembelea ilhali Wewe ni Mola Mlezi wa walimwengu?"

Hapo (Mwenyezi Mungu) atasema:

"Je hukujua kuwa mja Wangu fulani alikuwa mgonjwa lakini hukumtembelea na hukujua kuwa kama ungemtembelea ungenikuta kwake?"

"Ewe mwanadamu, nilikuomba chakula lakini hukunilisha."

"Kwa hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanao pigana katika Njia yake kwa safu kama jengo liliokamatana."

(Qur'an, 61: 4)

Atasema: Mola wangu, ningewezaje kukulisha ilhali Wewe ni Mola wa walimwengu?

Atasema (Mwenyezi Mungu): Mja wangu fulani alikuomba chakula lakini hukumlisha, na hujui kuwa kama ungemlisha ungemkuta pembezoni Mwangu? (Mwenyezi Mungu atasema tena):

Ewe mwanadamu,

Nilikuomba maji lakini hukunipa. Atasema: Mola wangu, vipi ningekupa maji ilhali Wewe ni Mola wa walimwengu? Hapo atasema:

Mja Wangu fulani alikuomba maji lakini hukumpa, na kama ungempa ungemkuta karibu Nami." (Muslim, Kitab al-Birr, 43)

Aya ifuatayo kuhusu undugu na kuwatangulizа wengine nayo pia ni ya muhimu sana:

"Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa. Hakika sisi tunakulisheni kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani. Hakika sisi tunaiogopa kwa Mola wetu Mlezi hiyo siku yenye shida na tabu. Basi Mwenyezi Mungu atawalinda na shari ya siku hiyo, na atawakutanisha na raha na furaha." (Qur'an, 76: 8-11)

Katika kuhitimisha, watu wanaotoa huduma wanatakiwa kujitakasa dhidi ya hisia mbaya kama vile kinyongo, wivu na kutojali na wachukue fungu lao kutoka katika misingi ya ukomavu na mitukufu ya kuwahudumia na kuwapenda wengine.

Mwenyezi Mungu Mtukufu amekataza sifa na tabia mbaya kama vile kudhihaki, kusengenya, kujadili mambo yasio na msingi na kutuhumiana kwa sababu mambo hayo hubomoa hisia za upendo na undugu miongoni mwa waumini.

d. Moyo Kujazwa upendo kwa viumbe kwa ajili ya Muumba

Moyo unapojazwa nuru ya kiroho, itokayo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, moja kwa moja tamaa ya kuwasaidia wengine huibuka ndani ya moyo huo. Wale wanaomuweka Mwenyezi Mungu na Mtume Wake katikati ya kitovu cha urafiki huwa marafiki wa viumbe wote. Nyoyo zao hupanuka na kuwa nyoyo zinazojali viumbe wote.

Huduma inaweza tu kutolewa kwa moyo mpana kama huo na aina hii ya moyo inaweza kutoa matunda yenye ufanisi. Mbegu inayopandwa kwa upendo hudumu milele. Hiyo ndiyo sababu kwamba tunahitaji kuyapangilia maisha yetu kwenye misingi iliyowekwa na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (s.a.w).

"Jiepusheni na dhana, kwani dhana ni uongo mkubwa na mbaya mno katika mazungumzo, msitafitiane, msichunguzane, msioneane husda, msijizoeze uovu, msishikamane na chuki na kuoneana uadui nyinyi kwa nyinyi. Na kuweni ndugu na waja wa Mwenyezi Mungu."

(Muslim, Kitab al-Birr, 30)

3. Kudumisha Ikhlasi na istiqamah au msimamo na unyoofu

Ikhlasi na msimamo ni sifa mbili za lazima kwa mtoaji wa huduma. Kuwa mtu wa kweli wa huduma ni baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tunapaswa kushukuru kwa baraka hii na kujaribu kuwa na Ikhlasi na kufuata njia iliyonyooka katika huduma zetu. Vinginevyo tusisahau kwamba tunaweza kuipata baraka hii.

Wale waliokabidhiwa majukumu muhimu sana ya kuwahudumia wengine wanatakiwa kuwa makini sana katika suala hili. Yule anayepanda mlima mrefu lazima awe makini kuhusu mahali pa kukanyaga na tawi gani la kukamata, kwa sababu

akikosea kukanyaga atakabiliwa na hatari kubwa kwenye kilele cha mlima.

Maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w) yasemayo: "... Wenye ikhlasi wameokoka dhidi ya hatari kubwa" (Bayhaqi, Shu'ab al-Iman, V, 345) ni dhihirisho zuri la ukweli huu. Wale wenye kuwahudumia wengine kwa Ikhlasi wapo chini ya ulinzi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu dhidi ya hila na mitego ya shetani. Hili limeelezwa katika Aya zifuatazo:

"Akasema (Iblisi): Naapa kwa utukufu wako, bila ya shaka nitawapoteza wote, isipo kuwa wale waja wako miongoni mwao waliokhitariwa." (Qur'an, 38: 82-83)

Ikhlasi (usafi wa moyo) ndiyo sharti la muhimu zaidi kwa ajili ya uhalali wa kuwatumikia wengine. Palipo na Ikhlasi, ubinafsi na tamaa hutoweka. Kwa namna hii kudai mafanikio kwa ajili yake mwenyewe hupata kuzuiliwa na vikwazo kwenye njia ya kutoa huduma hupungua mpaka kwenye kiwango cha chini kabisa.

Upendo si madai tu. Upendo maana yake ni kushirikiana na ndugu zako katika huzuni zao, kuwasaidia katika mahitaji yao, kuonyesha kujitolea na kuweza kushirikiana nao kile ulicho nacho. Undugu wa kweli huonekana wakati wa shida.

Miongoni mwa shuhuda za Ikhlasi inaweza kuonekana katika kazi za heri, hususan katika taasisi za wakfu. Baadhi ya wakfu hudumu kwa karne nyingi kwa sababu ya Ikhlasi ya mtu aliyezianzisha. Japokuwa wakati mwingine wakfu hizo husimamisha shughuli zake, wakati huo huo baadhi ya watu wa heri huja na kuzifufua tena.

Kamwe hatutakiwi kutia shaka kwamba daima Ikhlasi hushinda; kwa sababu kazi zenye Ikhlasi hulindwa na kamwe hazipotei bure. Kuna majeshi mengi yenye idadi ndogo ya watu wenye Ikhlasi na

subira yaliyashinda majeshi makubwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Hili linathibitisha kwamba Ikhlasi ni misingi wa ushindi. Ushindi wa baada ya Vita vya Badri ni mfano bora wa ukweli huu. Kwa upande mwingine, katika Vita vya Hunayn, kwa sababu ya jeshi la Kiislamu kutegemea idadi yake kubwa na kujigamba kwa idadi hiyo, walikosa Ikhlasi na wakakutana na kushindwa mwanzo wa mapambano. Lakini, baadae Mtukufu Mtume (s.a.w) aliwaonya Maswahaba wake na wakagundua makosa yao na hatimaye wakabarikiwa kupata ushindi.

Ikhlasi na msimamo ni sifa mbili za lazima kwa mtoaji wa huduma. Kuwa mtu wa kweli wa huduma ni baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tunapaswa kushukuru kwa baraka hii na kujaribu kuwa na ikhlasi na kufuata njia iliyonyooka katika huduma zetu. Vinginevyo tusisahau kwamba tunaweza kuipata baraka hii.

Mojawapo ya ishara muhimu za Ikhlasi ni mhusika kutarajia malipo ya huduma yake kutoka kwa Mwenyezi Mungu pekee. Mifano bora ya hili ilionyeshwa na Mitume na watu wa Mwenyezi Mungu. Maelezo yafuatayo yaliyotolewa ndani ya Qur'an Tukufu na kutamkwa na takriban mitume wote yanaelezea ukweli huu katika namna ya wazi kabisa:

"Na sikutakini juu yake ujira, kwani ujira wangu hauko ila kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote."[43]

Mfano mwingine muhimu kutoka ndani ya Qur'an Tukufu ni kisa kinachohusu **"As-hab Qaryah – Watu wa mji."**

Wajumbe watatu walitumwa katika mji wa Antiokia kuwalingania watu wa mji huo kwenye njia iliyonyooka, lakini watu hao siyo tu kwamba

43. Tazama: Qur'an Tukufu, 26: 109, 127, 145, 164, 180; 10: 72; 11: 29.

walikataa wito wao bali pia waliwatishia kuwaua. Pindi Habib al-Najjar kutoka Antiokia aliposikia mwenendo na vitisho vya watu wake, akaenda haraka na kusema:

"Na akaja mtu mbio kutokea upande wa mbali wa mjini, akasema: Enyi watu wangu! Wafuateni hawa waliotumwa. Wafuateni ambao hawakutakini ujira, hali ya kuwa wenyewe wameongoka." (Qur'an, 36: 20-21)

Mtu anayetoa huduma ikiwa hatosubiri manufaa ya kidunia kwa huduma zake anazozitoa bali akatarajia malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu pekee, atapata siyo tu radhi za Mwenyezi Mungu bali pia radhi za watu. Ukweli huu umeelezwa katika hadith ifuatayo ya Mtukufu Mtume (s.a.w):

Siku moja mtu mmoja alikuja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na kusema:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Niambie kitu ambacho nikikifanya, nitapata upendo wa Mwenyezi Mungu na upendo wa watu." Mtume wa Mwenyezi Mungu akajibu:

"Ikane dunia na usiipende hii dunia ili Mwenyezi Mungu akupende. Usitake vile vilivyo kwa watu ili watu wakupende pia." (Ibn Majah, Zuhd,1)

"Ikane dunia na usiipende hii dunia ili Mwenyezi Mungu akupende. Usitake vile vilivyo kwa watu ili watu wakupende pia."

(Ibn Majah, Zuhd,1)

Kwa muhtasari, mawazo na fikra ya kufanya kila kitu kwa ajili ya kutaka radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu yanatakiwa kubadilika kuwa katika hali ya utambuzi wa moyo wa watu wanaotoa huduma.

Wale wanaowahudumia wengine wanatakiwa kufuata njia ya Mitume, siddiqiin au wakweli, mashahidi, na watu wema, kwa maneno mengine njia iliyonyooka. Wale wanaofuata njia iliyonyooka katika imani, katika mazungumzo, matendo, na katika kila hatua ya maisha wamesifiwa katika Aya ifuatayo:

"Hakika waliosema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa, hao huwateremkia Malaika wakawaambia: Msiogope, wala msihuzunike; nanyi furahini kwa Pepo mliyokuwa mkiahidiwa." (Qur'an, 41: 30)

Watu wa huduma wanapaswa kuonyesha mwenendo imara; kwa sababu watu huwastaajabia na kuwafuata watu wa mfano ambao wana mwenendo imara na utu. Kuna mifano mingi ya aina hii ya watu katika historia ya Uislamu.

Wakati wa Ukhalifa wa Bani Abbas, mipaka ya dola ya Kiislamu ilipanuliwa na mali ya umma ikamiminika katika mji mkuu Baghdad. Matokeo ya hali hiyo, idadi ya wale waliohadaiwa na mali na kuangukia katika starehe, raha na anasa ikaongezeka sana. Sherehe ya harusi ya Waziri mkuu Hassan bin Sahl, ambaye alikuwa amemuoa binti wa Khalifa Ma'mun, iliendelea kwa muda wa siku kumi na tisa ambapo matanuzi, anasa na ubadhirifu ulikuwa katika kiwango cha juu kabisa. Hazina ya Dola ilifanyiwa israfu. Mali ya Dola ilizitia utumwani nafsi za viongozi wengi wa ngazi za juu wa Serikali. Mwenendo huo mbaya haukutoa mfano wowote mzuri wa kufuatwa na watu, na

Katika kipindi chote cha historia watu wema waliendelea kuufanya moyo wa jamii uwe hai na kuinyanyua juu heshima na hadhi ya Uislamu kwa mwenendo na shakhsia yao ya hali ya juu. Malipo ya maadili yao ya hali ya juu Mola wetu Mtukufu akawapenda na kuwafanya wapendwe na waumini wote mpaka siku ya mwisho.

haukuacha kumbukumbu yoyote ya heri au athari baada ya kufa kwao.

Kwa upande mwingine, wakati huo huo mjini Baghdad palikuwepo na wengine wanaowalingania watu kuzitakasa nafsi zao, kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Marafiki hawa wa Mwenyezi Mungu, kama vile Abdullah bin Mubarak, Sufyan al-Thawri, Fudayl bin Iyad, Junayd al-Baghdadi, Ma'ruf al-Karkhi, na Bishr al-Khafi, walizitoa wakfu nafsi zao kwa Mwenyezi Mungu na wakawa wanaishi maisha ya uchaji. Mali na anasa za kidunia hazikuweza kuzinunua nafsi zao; nyadhifa za serikali au hadaa ya dunia haikuweza kuwageuza kutoka kwenye malengo na majukumu yao matukufu. Walikuwa kama bandari na hifadhi salama kwa wale waliokaribia kuzama katika bahari ya mambo ya kidunia na umaada. Masultan, mawaziri, na viongozi wa dola walikuwa wakitawala mili ya watu ilhali marafiki wa Mwenyezi Mungu walivishwa taji katika nyoyo za watu. Walikuwa wakiwahudumia watu bila kutarajia manufaa ya kidunia kutoka kwao. Hali yao ya kiroho ilikuwa ikiwaathiri hata wale wasiokuwa Waislamu.

Watu wa huduma wanatakiwa kuyatafakari na kuyataamali majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ya al Rahman na al Rahim (Mwingi wa Rehma na Mwenye kurehemu) na mwenendo wao kuhusu viumbe wauegemeze kwenye msingi wa huruma wa upole, kwa sababu, huduma ni suala la huruma.

Khalifa wa ukoo wa Abbas Harun al-Rashid alikuwa akiishi katika ufahari na anasa mjini Raqqa. Siku moja Abdullah bin Mubarak alikuja mjini Raqqa. Watu wote wa mji wakaenda nje ya mji kwenda kumkaribisha. Khalifa alibaki peke yake mjini. Kijakazi mmoja wa Khalifa alishangazwa na sababu ya hali hii na kusema:

"Jambo gani hili? Jambo gani limetokea?" akaambiwa:

"Msomi mmoja kutoka Khorasan amekuja katika mji huu. Jina lake ni Abdullah bin Mubarak. Watu wamekwenda kumkaribisha."

Kisha kijakazi huyo akasema:

"Huu ndiyo usultani wa kweli siyo wa Harun al-Rashid; kwa sababu, bila polisi hawezi hata kuwakusanya wafanyakazi wake."

Kwa hakika katika kipindi chote cha historia watu wema waliendelea kuufanya moyo wa jamii uwe hai na kuinyanyua juu heshima na hadhi ya Uislamu kwa mwenendo na shakhsia yao ya hali ya juu. Malipo ya maadili yao ya hali ya juu Mola wetu Mtukufu akawapenda na kuwafanya wapendwe na waumini wote mpaka siku ya mwisho. Qur'an Tukufu inasema kwamba:

"Hakika walioamini na wakatenda mema Arrahmani Mwingi wa Rehema atawajaalia mapenzi." (Qur'an, 19: 96)

Ndiyo maana watu wa huduma wanatakiwa kufuata nyayo za Mtume (s.a.w), ambaye alikuwa al-amin (mwaminifu) na al-Sadiq (mkweli), na kuwa wakweli na waaminifu. Hili linaweza kufikiwa kama mja atafuata mwenendo ulionyooka katika kumtumikia Mwenyezi Mungu Mtukufu. Wanatakiwa kuwa waangalifu sana katika kila hatua zao kama vile wanatembea kwenye daraja la sirat katika maisha yao binafsi na vilevile katika kutoa huduma zao kwa watu.

Watu wa huduma wanatakiwa pia kuwa wakarimu; kwa sababu maadili na tabia za hali ya juu ni zenye kutegemeana na hukamilishana. Mtu mwenye huruma ni mkarimu; mtu mkarimu ni mwenye staha na mtu mwenye staha huwa mtu wa kweli wa huduma.

4. Muumini mwenye upendo, huruma na msamehevu

Muumini wa kweli ni mtu wa moyo. Huruma na uungwana ni sifa zake kuu na tabia yake ya msingi na ya lazima. Katika moyo wa muumini, huruma ni kama moto usiozimika. Barabara iendayo kwenye imani kamili hupitia kwenye hatua za huruma na kuwahudumia watu. Huruma ni asili itokayo kwa Mwenyezi Mungu ambayo ni uthibitisho wa imani yetu hapa duniani.

Watu wa huduma wanatakiwa kuyatafakari na kuyataamali majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ya al Rahman na al Rahim (Mwingi wa Rehema na Mwenye kurehemu) na mwenendo wao kuhusu viumbe wauegemeze kwenye msingi wa huruma na upole, kwa sababu, huduma ni suala la huruma. Uzuri wote hupata kupatikana kutokana na huduma zinazotolewa zikiambatana na huruma, upole na staha. Alama ya dhahiri na ya wazi ya huruma ni kutoa sadaka. Ndiyo maana watu wa huduma wanatakiwa pia kuwa wakarimu; kwa sababu maadili na tabia za hali ya juu ni zenye kutegemeana na hukamilishana. Mtu mwenye huruma ni mkarimu; mtu mkarimu ni mwenye staha na mtu mwenye staha huwa mtu wa kweli wa huduma. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) anasema:

"Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Mkarimu na Mwema; anapenda ukarimu na tabia njema..."
(Suyut, al-Jami' al-Saghir, 60)

"Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Karimu na Mwema; anapenda ukarimu na tabia njema..."

(Suyut, al-Jami' al-Saghir, 60)

Kwa upande mwingine tabia na sifa mbaya nazo pia zina uhusiano. Yule asiyekuwa na hu-

ruma na upendo huwa bahili; mtu bahili huwa na kiburi, na mtu mwenye kiburi hujiepusha na suala la kuwahudumia watu.

Kwa hiyo basi, hatuwezi kutarajia matokeo yoyote mema kutoka katika huduma iliyotolewa katika namna ya ukaidi, ukali na yenye kuvunja heshima ya watu. Suala hili hupata umuhimu mkubwa katika masuala ya malezi na ufundishaji wa ujumbe wa Uislamu. Aya ifauatyo inauambia umma wote wa Kiislamu:

"Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungelikuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia..." (Qur'an, 3: 159)

Siku moja Mtume wa Allah (s.a.w) alimwambia A'isha (r.a):

"Ewe Aisha, hakika Mwenyezi Mungu ni mwema anapenda wema na huutunuku wema kwa malipo asiyoyatunuku kwenye ukali na halitunuku jambo lolote kama anavyoutunuku (wema)." (Muslim, Kitab al-Birr, 77)

Vilevile katika hadith nyingine, Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema:

"...Mwenyezi Mungu Mtukufu humpenda kila mwenye kuwafundisha wema watu wenye huzuni kwa sababu ya makosa yao, mwenye kuwahurumia watu na kuwalingania kumtii Mwenyezi Mungu Mtukufu. Anawachukia watu wakali, wanaopoteza muda wao katika mambo ya upuuzi, wanaolala usiku wote bila kujua kama roho zao zitarudi

"Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungelikuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangelikukimbia..."

(Qur'an, 3: 159)

Watu wanaohitaji msaada na huduma yetu ni kama ndege waliojeruhiwa. Kinachoweza kuwafaa ni huduma zinazotolewa zikiwa zimeambatana na huruma na upendo. Vilevile tunahitaji mafunzo maalumu ili kupata sifa hizi. Msingi wa mafunzo haya unaweza kupatika kwa njia na mbinu zilizofundishwa na kuelekezwa na Usufi. Kwa maneno mengine, inaweza kupatikana kwa mafundisho maalumu ya kiroho.

au la, na wachache wa kumkumbuka Mwenyezi Mungu." (Daylami, Musnad, I, 158)

Vipengele vya nje vya dini hujulikana kwa akili na vipengele vyake vya ndani, kwa upande mwingine, hujulikana kwa moyo. Katika kufundisha na kuendesha mambo ya mwanadamu, huruma na upendo hutoa matokeo bora, kwa sababu watu wengi wasioweza kudhibitiwa na mabavu wanaweza kujisalimisha kwenye huruma na upendo.

Upendo wa mwalimu humuongezea uhusiano na mvuto, kwa sababu kutokana na kuamiliana na watu kwa upendo mafundisho yake hupata kueleweka na kusomwa kwa moyo siyo kwa akili. Kwa njia hii, mafundisho huchukua sura sahihi na kuziathiri nyoyo za wapokeaji kwa kiwango kikubwa mno, jambo ambalo ndiyo sababu kwamba wanafunzi, kwa namna maalumu, wanatakiwa kuamliwa kwa huruma na upendo, kwa sababu wanadamu hujisalimisha na kuinyenyekea huruma na upendo. Hivyo washindi wa kweli ni wale wenye kuzishinda na kuzivuta nyoyo.

Kwa kuwa watawala wasiokuwa na huruma na upendo hawawezi kuzidhibiti na kuzitawala nyoyo za wale walio chini ya utawala wao, hutumia nguvu kuhakikisha watu wanawatii. Hujaribu kutawanya na kueneza sumu, na hivyo mafanikio yao yanakomea kwenye himaya ya kimwili tu. Mwishowe huangukia katika kimbuga cha kuchukiwa bila hiyari yao. Kuwapa nyadhifa watu hawa ni kuwadhulumu watu kabisa.

Kiuhalisia, uonevu ni matokeo ya ukosefu wa upendo na huruma. Wale wanaokosa sifa hizi mbili za

hali ya juu daima hukimbilia kwenye kufanya dhulma na uonevu. Huruma ni tunda la upendo. Kama ilivyo amani, utulivu na baraka haviwezi kuwepo ndani ya familia isiyoasisiwa kwenye msingi wa upendo, hatuwezi kutarajia matokeo mema na yenye heri kutoka kwenye huduma iliyokosa upendo.

Watu wanaohitaji msaada na huduma yetu ni kama ndege waliojeruhiwa. Kinachoweza kuwafaa ni huduma zinazotolewa zikiwa zimeambatana na huruma na upendo. Vilevile tunahitaji mafunzo maalumu ili kupata sifa hizi. Msingi wa mafunzo haya unaweza kupatika na kwa njia na mbinu zilizofundishwa na kuelekezwa na Usufi. Kwa maneno mengine, inaweza kupatikana kwa mafundisho maalumu ya kiroho.

Sifa katika moyo wa mwanadamu zinazowakilisha “ubinafsi” na “ ubabe” vinapaswa kubadilishwa kwa upendo na huruma. Maua mazuri yanaweza tu kuchipua kwa upendo. Wale waliofikia ukamilifu katika huruma na upendo daima huwatafuta viumbe wenye shida ili wapate kuwasaidia; kwa sababu, huyahisi maumivu ya viumbe hao katika nyoyo zao.

Taasisi zote, hususan zile zinazotoa mafunzo ya kiroho, zinatakiwa kuwa shule za huruma, uungwana na huduma kwa watu. Badala ya kutoa vipande vitupu vya elimu ndani ya kuta zao nne, mafunzo yao yanatakiwa yajikite kwenye upendo na hamasa ya kuwahudumia wengine. Kwa sababu mwalimu asiyekuwa na hisia ambaye haingizi upendo ndani ya wanafunzi wake, imam asiyewafanya waumini wake wahisi furaha ya im-

Kushauriana kuhusu mambo yao muhimu ni sifa ya waumini kama inavyoelezwa na aya tukufu: “ambao mambo yao ni kwa kushauriana baina yao”

(Qur’an, 42: 38)

Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa na tabia ya kushauriana na Maswahaba wake kuhusu mambo muhimu ya jamii ya Kiislamu. Pamoja na kwamba alikuwa akipokea wahyi (ufunuo) kutoka kwa Mwenyezi Mungu, alikuwa akipendelea kufanya mambo kwa kushauriana ili awe mfano kwa Waislamu.

ani na asiyezifanya akili za wanafunzi wake zihisi upendo wa kuipenda Qur'an, mwajiri asiyewalinda wafanyakazi wake na kuwaonyesha huruma, wote hao ni masikini wa huruma ambao wameondolewa katika rehema za Mwenyezi Mungu. Wale wasiokuwa na hisia yoyote kwa wagonjwa, walemavu, masikini na wapweke ni wabinafsi ambao hawana fungu lolote katika kuwahudumia watu.

Ikumbukwe kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu yu pamoja na wanyonge na waliovunjika moyo. Wale wanaukimbia uadilifu wa kibinadamu kwa kutumia hila mbalimbali, siku moja watakabiliana na uadilifu wa hukumu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu huku wakiwa wamekata tamaa.

Juhudi za walimu wa Qur'an wenye kiburi ambao wakati mwingine huwa na tabia kama majaji na wakati mwingine kama wanyongaji; ambao hufundisha Qur'an kwa kutumia nguvu ya fimbo badala ya kutumia upendo na huruma zitakuwa za kujichosha bure.

Waumini wote, hususan wale wenye jukumu la kuwahudumia wengine, wanatakiwa kukumbuka onyo lifuatalo la Mtukufu Mtume (s.a.w):

"Niwaambie juu ya watu wa Motoni? Ni wale wakali sana, wabahili, wakatili na wenye kiburi." (Bukhari, Ayman,9)

Kama ambavyo muonekano wa mawaridi na maua humfanya hata mtu mkali kabisa atabasamu, mtoaji wa huduma anapaswa kuwa na tabia za mawaridi na awe na uwezo wa kuzilaini-

sha nyoyo ngumu zaidi, na azifanye nyuso za watu wakali sana zitabasamu.

Jina mojawapo katika majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, al-Afuw au Mwenye kusamehe, linahusu usamehevu Wake. Watu wanaotoa huduma wanapaswa kuwa na tabia hiyo ya kusamehe.

Imeelezwa katika Aya tukufu:

"Shikamana na kusamehe, na amrisha mema, na jitenge na majaahili." (Qur'an, 7: 199)

Kusamehe ni matokeo ya moja kwa moja ya kumpenda Mwenyezi Mungu na kupambwa na maadili na tabia Zake. Kuwa na uwezo wa kuwatazama viumbe kwa jicho la yule aliyeviumba huandaa mazingira ya kusamehe. Usamehevu hutoka moyoni. Wale wanaotaka kutia fora kumpenda Mwenyezi Mungu ni wale wanaotoa miale ya usamehevu kutoka katika nyoyo zao, kwa sababu kwa kuwasamehe wengine sisi wenyewe ndipo tunapoweza kustahili msamaha. Kwa hakika wale wasioweza kusamehe wanakuwa wanajiandalia maangamizi yao wenyewe.

Usamehevu ni kuweza kusamehe makosa ya mtu hali ya kuwa una uwezo wa kumuadhibu. Wema wa kweli ni kuidhibiti hasira na ghadhabu ya nafsi na kutanguliza msamaha. Msamaha wa jumla uliotolewa na Mtukufu Mtume (s.a.w) siku ya ufunguzi wa Makkah ni mfano bora wa tabia hii.

Watu wanaowahudumia wengine hawapaswi kutafuta aibu na makosa ya watu bali wanapaswa kuyasitiri. Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) anasema:

"Wale wanaofanya istikharah (kutaka muongozo wa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya uamuzi sahihi kupitia ndoto) hawatohuzunishwa; wale wanaotaka ushauri hawatojuta na wale wanaotumia vizuri katika matumizi yao hawatofukarika."

(Haythami, Majma' al-Zawaid, II, 280)

"Mwenye kumsitiri Muislamu (kwa aibu zake), Mwenyezi Mungu atayasitiri makosa yake siku ya Kiyama; na mwenye kufichua aibu za Muislamu, Mwenyezi Mungu atazifichua aibu zake na kumfedhehesha hata kama yuko nyumbani kwake." (Ibn Majah, Hudud, 5)

"Mwenye kumuaibisha ndugu yake Muislamu kwa kasoro alizonazo hatokufa mpaka akutwe na kasoro hizo." (Tirmidhi,Qiyamah,53)

5. Kutenda jambo kwa mashauriano:

Kutenda jambo kwa mashauriano ni amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu na ni sunnah kubwa sana ya Mtukufu Mtume (s.a.w). Mwenyezi Mungu Mtukufu anaonyesha umuhimu wa waumini kushauriana kwa kumwambia Mtume (s.a.w) kwa niaba yao:

"Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungelikuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia. Basi wasamehe, na waombee maghfira, na shauriana nao katika mambo. Na ukisha kata shauri basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaomtegemea." (Qur'an, 3: 159)

Kushauriana kuhusu mambo yao muhimu ni sifa ya waumini kama inavyoelezwa na Aya tukufu: **"ambao mambo yao ni kwa kushauriana baina yao"** (Qur'an, 42: 38)

"Mwenyezi Mungu Mtukufu amenifunulia ya kuwa tuwe wanyenyekevu baina yetu na asiwepo mtu wa kujiona na kujifadhilisha juu ya wengine..."

(Muslim, Jannah, 64)

Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa na tabia ya kushauriana na Maswahaba wake kuhusu mambo muhimu ya jamii ya Kiislamu. Pamoja na kwamba alikuwa akipokea Wahyi (ufunuo) kutoka kwa Mwenyezi Mungu, alikuwa akipendelea kufanya mambo kwa kushauriana ili awe mfano kwa Waislamu. Mfano halisi wa jambo hili ni katika vita vya Badr na Handaq. Alishauriana na Maswahaba wake kuhusu wapi na namna jeshi la Kiislamu linavyotakiwa kuendesha mapambano. Vilevile katika Vita vya Uhud alifuata mawazo ya Maswahaba wake na kuungana na jeshi nje ya mji wa Madinah, japokuwa mtazamao wake ulikuwa ni kubaki Madinah na kuendesha vita kwa kujilinda wakiwa mjini Madinah.

Binadamu huathiriwa na hisia zao na huwaza na kuchukua maamuzi yao kulingana na hisia zao. Ndiyo maana kufanya mambo kwa kushauriana husababisha kutoa huduma sahihi na zenye baraka; lakini, ni jambo muhimu sana tunapochagua watu wa kushauriana tuchague waumini wenye uelewa, maarifa, wepesi, na wachamungu. Ni ukweli ulio dhahiri kuwa uamuzi unaofanywa na kikundi huwa sahihi zaidi kuliko uamuzi unaofanywa na mtu mmoja. Mtukufu Mtume (s.a.w) anauelezea ukweli huu kama ifuatavyo:

"Wale wanaofanya istikharah (kutaka muongozo wa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya uamuzi sahihi kupitia ndoto) hawatohuzunishwa; wale wanaotaka ushauri hawatojuta na wale wanaotumia vizuri katika matumizi yao hawatofukarika." (Haythami, Majma' al-Zawaid,II, 280)

Kazi na huduma ngumu kuliko zote ni kuwapa malezi wanadamu, kwa sababu daima nafsi isiyokuwa na malezi humuelekeza mtu kwenye maovu. Mwenyezi Mungu Mtukufu aliweka silika ya kutenda dhambi na uchaji ndani ya maumbile ya mwanadamu.

Mashauriano pia huonyesha kwamba tunaheshimu maoni na mawazo ya watu tunaoshauriana nao, jambo ambalo huwapa nguvu na kuwawezesha kutoa huduma kwa bidii. Kwa upande mmoja, hupunguza umimi na ubinafsi wa watu wanaotoa huduma mpaka kiwango cha chini kabisa na kuwalinda dhidi ya hatari za ufahari na kiburi. Kutokuwa na idhilali ya kusikiliza ushauri na kutofanya mashauriano ni alama ya kiburi, jeuri, na kujiona kuwa wewe ni bora kuliko wengine.

Bila shaka matokeo ya mashauriano yanatakiwa kufanyiwa kazi. Mashauriano ya kinafiki yanayofanywa kwa mazoea tu huleta madhara kuliko kuleta manufaa na heri. Mashauriano yanatakiwa kufanywa na watu wataalamu na wenye sifa, na kila mtu awe na uwezo wa kutoa maoni yake ili ukweli na baraka viweze kupatikana. Iwapo mtu unayemtaka ushauri hana sifa, basi matokeo yatakuwa yenye kujaa makosa na ukosefu wa uhakika. Tusiruhusu makosa yatokee katika namna hiyo hiyo ya kubahatisha kwa kumshaurisha mwanasheria kuhusu mambo ya matibabu.

Mtu unayetaka ushauri wake asiwe tu na sifa katika jambo alililoshaurishwa, bali pia anapaswa kuwa mwenye maadili mema na asiyekuwa na upendeleo na chuki binafsi. Vinginevyo kuna uwezekano wa kukupotosha, jambo litakalokuwa na athari mbaya. Kwa upande mwingine, tunapaswa kujiepusha na ubaguzi na uelewa mbaya, na tumsikilize kwa utuvu yule anayetutaka ushauri.

Ukimimina kwa haraka maji kutoka katika chombo kilichojaa ndani ya chombo chenye ukubwa huo huo, baadhi ya maji yatamwagika. Lakini ukifuata kanuni ya hatua kwa hatua na kuyamimina kidogo kidogo, unaweza kuyaingiza maji hayo kwenye chombo husika bila kupoteza au kumwaga hata tone moja.

Mtoaji wa huduma anatakiwa kutanguliza furaha ya wenzake kuliko furaha yake mwenyewe. Wale wanaong'ang'ania kufanya kila kitu peke yao huchoka, kukosa raha na huzielekeza kwa haraka akili zao kwenye hali hasi. Huanza kuwadharau wale wanaowazunguka na kutiwa utumwani na mapenzi yao ya kupenda madaraka. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) anasema kuhusu aina hii ya watu:

"Mwenyezi Mungu Mtukufu amenifunulia ya kuwa tuwe wanyenyekevu baina yetu na asiwepo mtu wa kujiona na kujifadhilisha juu ya wengine..."
(Muslim, Jannah, 64)

Kwa hali hii, mtu wa huduma wa kweli na mkomavu hujiona kuwa wa mwisho kabisa katika safu ya watoaji huduma kwa kuondokana na umimi.

6. Kuzijua sifa na tabia za mtu anayehudumiwa:

Binadamu, ambaye ni kiumbe bora, anatakiwa kuamiliwa kwa heshima kwa sababu moyo wake ni sehemu ya ishara za Kimungu. Ndiyo maana msingi mkuu wa matokeo ya huduma ni kuwa na hisia mno katika kuwahudumia watu. Kutoa huduma kwa njia ya ukali na yenye kuvunja heshima ya watu huwa ni sababu ya mtoaji huduma kukosa thawabu. Badala yake, inaweza hata kuhesabiwa kuwa ni dhambi. Kuurekebisha moyo uliovunjika hakuwezi kulinganishwa na kurekibisha au kukarabati kiatu. Hata kukarabati kiatu ni

"Na vivyo hivyo tumekufanyeni muwe Umma wa wasitani..."

(Qur'an, 2: 143)

Wale wanaojitambua wapo katika aina tatu: (a)Wale wanaovutiwa sana na uwezo wa Mwenyezi Mungu na ni waangalifu mno wasikiumize chochote. (b)Wale wenye staha sana na wana aibu mno kiasi kwamba hawawezi hata kutamka maneno ya Mwenyezi Mungu. (c) Wale wasiowadharau viumbe wa Mwenyezi Mungu, kwa maneno mengine, wale wenye unyenyekevu wa hali ya juu na huwatazama viumbe kupitia macho ya Muumba wao.

jambo gumu zaidi kuliko kukiharibu. Hivyo, moyo unapovunjika, huwa ni vigumu sana kuurekebisha.

Maneno ya wanahekima yanasema:

Wale wanaojitambua wapo katika aina tatu:

a. Wale wanaovutiwa sana na uwezo wa Mwenyezi Mungu na ni waangalifu mno wasikiumize chochote.

b. Wale wenye staha sana na wana aibu mno kiasi kwamba hawawezi hata kutamka maneno ya Mwenyezi Mungu.

c. Wale wasiowadharau viumbe wa Mwenyezi Mungu, kwa maneno mengine, wale wenye unyenyekevu wa hali ya juu na huwatazama viumbe kupitia macho ya Muumba wao.

Katika kuwahudumia watu, kumjua mtu anayehudumiwa ni muhimu sana sawa na huduma yenyewe, kwa maana huduma muafaka inaweza tu kutolewa kwa kumjua anayepewa huduma husika. Kwa mfano, huwezi kumsaidia mtu anayeona haya sana kuelezea shida zake sawa na kumsaidia mtu ambaye anayesita moja kwa moja kuelezea mahitaji yake mwenyewe..

Muislamu anapaswa kufanya mambo kwa busara. Anatakiwa kujua jinsi ya kufanya jambo, lipi la kusema, nani wa kumwambia mambo fulani fulani, lini, wapi na jinsi ya kuongea kwa ufasaha. Namna nzuri iliyotumiwa na Ja'far al-Tayyar (r.a) katika kuueleza Uislamu mbele ya mfalme wa Abyssinia ni ya mfano. Mtawala huyo mkristo wa Abyssinia alipomtaka Ja'far al-Tayyar kusoma Aya

za Qur'an, alichangua Aya zinazomsifu Nabii Issa na Maryam badala ya kusoma sura na Aya zinazowapa changamoto makafiri. Mfalme, ambaye alivutiwa sana na Aya hizi, alichora msitari ardhini na kusema:

"Tofauti iliyopo baina ya dini yako na dini yangu ni ya kiasi hiki." Muda mfupi baadae alisilimu.

Kuwajua na kuwaelewa watu wanaotakiwa kuhudumiwa ni la muhimu pia katika kuteua watu watakaotoa huduma husika. Kwa mfano, Mtukufu Mtume (s.a.w) hakuwahi kumtuma swahaba ambaye ana sifa ya kuwa kamanda wa jeshi kwenda kuwa balozi. Vile vile hakuwateua Maswahaba wa Suffah, ambao walikuwa wasomi, watu wa mahubiri na nyoyo, kuwa makamanda wa jeshi. Alipokuwa akiwapa maswahaba wake majukumu yanayohusu dola ya Kiislamu alikuwa akizingatia sana sifa zao binafsi na hata sifa za kimaumbile walizonazo.

Kutokana na umuhimu wake, tungependa kusisitizia juu ya baadhi ya misingi katika kutoa mafunzo, elimu na malezi kwa watu.

Kazi na huduma ngumu kuliko zote ni kuwapa malezi wanadamu, kwa sababu daima nafsi isiyokuwa na malezi humuelekeza mtu kwenye maovu. Mwenyezi Mungu Mtukufu aliweka silika ya kutenda dhambi na uchaji ndani ya maumbile ya mwanadamu. Tokea utotoni, ishara ya silika hizi mbili huweza kuonekana katika maisha ya mwanadamu. Furaha haiwezi kupatikana kwa kuuzuia mwelekeo wa kutenda dhambi na kuimarisha uchaji. Namna ya kulifikia hili ni kupitia mafunzo.

"Mambo bora ni yale yanayofanywa kwa uwastani (yale yasiyopiondukia mipaka"

(Bayhaqi, Shu'ab al-Iman, V, 261)

Hata wanyama wakali sana wanaweza kufunzwa kwa urahisi zaidi kuliko binadamu wanavyoweza kufunzwa.

Kutoa elimu na malezi ni kazi ya mitume. Ili kuwa muelimishaji, hisia kali za ndani ya moyo zinatakiwa kuwa imara. Kwa sababu wakati wa kuanzisha mawasiliano na wanafunzi, hisia zao lazima zieleweke, zitathminiwe na kisha hatua zichukuliwe kutokana na matokeo husika. Hii ni sawa na kufanya vipimo vya kuutambua ugonjwa kabla ya kufanya matibabu husika. Ikumbukwe kuwa binadamu huweza kuvutwa iwapo tu matatizo yao yametatuliwa.

Kama ambavyo vipawa vya wanadamu hutofautiana, udhaifu wao pia hutofautiana. Ndiyo maana muelimishaji anatakiwa kuamiliana na wanafunzi wake kwa uangalifu sana kama mwanasaikolojia. Neno au mwenendo fulani wenye manufaa kwa mtu fulani unaweza kuwa na madhara kwa mtu mwingine. Hivyo basi, ni muhimu tuwajue vizuri wale tunaowajibika kuwahudumia.

Kwa upande mwingine, muda na kipimo cha matumizi ya mawasiliano ya mazungumzo lazima yapangiliwe vizuri. Kama tunavyokuwa waangalifu kukikunja kitu kigumu, ili tusikivunje, ndivyo tunavyopaswa kuwa waangalifu na makini juu ya wale wenye silika kubwa za umimi na nguvu ya vipawa, na hivyo tusikurupuke katika kuwaokoa. Kipimo kinatakiwa kiwe cha kiwango sahihi. Ukimimina kwa haraka maji kutoka katika chombo kilichojaa ndani ya chombo chenye ukubwa huo huo, baadhi ya maji yatamwagika. Lakini ukifuata kanuni ya hatua kwa hatua na kuyamimina kidogo kidogo,



“Mwenye kuongoza watu katika swala basi aifupishe kwa sababu miongoni mwao kuna wagonjwa, dhaifu, wazee na wenye haja (wenye kazi za kufanya). Mwenye kuswali peke yake anaweza kuirefusha swala yake kadiri atakavyo.”

(Bukhari, Kitab al-‘Ilm, 28)

unaweza kuyaingiza maji hayo kwenye chombo husika bila kupoteza au kumwaga hata tone moja. Umuhimu wa kanuni hiyo ya fizikia haiwezi kupuuzwa katika kuwafunda wanadamu. Kwa maneno mengine, kuwafunda wanadamu kunategemea subira na kuujua vizuri uwezo wa wanafunzi.

Muelimishaji au mkufunzi anapaswa kuwajua wanafunzi wake kama anavyoujua mgongo wa mkono wake na awape mafunzo kulingana na vipawa vyao. Kwa mfano, mwanafunzi mwenye kipawa cha ushairi anapaswa kuelekezwa kwenye vina vya nyoyo, roho na nafsi za wanadamu; mwanafunzi mwenye kipawa cha uongozi, kwa upande mwingine, anatakiwa kupewa mafunzo kuhusu mwenendo wa mwanadamu, huruma, uadilifu na jinsi ya kuwaongoza watu. Vipawa vingine vinafuata mfano huohuo, kila kimoja kinatakiwa kushughulikiwa kwa namna iliyo tofauti na kipawa kingine.

Huduma za kielimu zinatakiwa kupangiliwa kwa umakini kwa kuzingatia uwiano wa mwili na roho na akili na moyo. Iwapo akili tu ndiyo itakayoshughulikiwa na kuangaliwa, mapenzi ya kupenda manufaa, ofisi na manufaa mengine ya kidunia huongezeka na mafunzo ya kiroho hupuuzwa. Mtu aliyepewa mafunzo kwa njia hii huwa mtumwa wa mali, umashuhuri na tamaa. Lakini, kama roho yake itapata mafunzo sambamba na akili yake, ni hapo tu ndipo silika za asili zinapoweza kuingia katika njia sahihi. Ieleweke kuwa elimu isiyopenya katika moyo haiwezi kubadilika na kuwa nuru na maarifa ya kiroho. Elimu bila nuru ya kiroho yaweza kumpelekea mhusika kwenye

"Huweka taswira kuwa kuna kamba iliyo kati yangu na kila mtu anayenizunguka. Kamba hii inapokaza kupita kiasi, huilegeza kidogo; ninapohisi kuwa imelegea sana, huivuta na kuikaza. Kwa njia hii hupata kudumisha uhusiano pamoja na watu wanaonizunguka kwa kufanya mambo kwa uwastani."

Amr b. al-As (r.a)

kupotea. Wale wasiopambwa na hisia na tunu za kiroho wataachwa chini ya udhibiti na huruma ya nafsi zinazoamrisha maovu.

Tunatakiwa kuwa makini sana kuhusu elimu na mafunzo kwa wanadamu. Wanatakiwa kupewa mafunzo sambamba na uwezo wa kukielewa kitabu cha ulimwengu na kuuelewa mpangilio mzuri na uwiano maridhawa unaopatikana ndani ya ulimwengu.

7. Kudumisha hali ya uwastani na kadri katika kufanya mambo:

Kama ilivyo katika mambo mengine, kudumisha uwastani na tabia ya kiasi katika kutoa huduma ni msingi mkuu. Kama ambavyo mtu wa huduma hawezi kuipuuza familia, wazazi na majukumu yake mengine, hatakiwi kutumia familia yake na majukumu yake mengine kama kisingizio cha kuacha kuwahudumia viumbe wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Ndani ya Qur'an Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaita Waislamu kwamba ni umma wa wastani:

"Na vivyo hivyo tumekufanyeni muwe Umma wa wastani..." (Qur'an, 2: 143)

Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema kuwa:

"Mambo bora ni yale yanayofanywa kwa uwasitani (yale yasiyopindukia mipaka" (Bayhaqi, Shu'ab al-Iman, V, 261) na anaupatia umma wake kipimo kamili pale wanapotaka kufanya mambo yao.

Katika hadith nyingine anasema:

"Mwenye kuongoza watu katika swala basi aifupishe kwa sababu miongoni mwao kuna wagonjwa, dhaifu, wazee na wenye haja (wenye kazi za kufanya). Mwenye kuswali peke yake anaweza kuirefusha swala yake kadri atakavyo." (Bukhari, Kitab al-'Ilm, 28)

Kama inavyoonekana katika maandiko yaliyotolewa hapo juu, kudumisha uwastani na kiasi katika mambo yote ya kidunia na ya kiroho ni msingi wa aina yake uliowekwa na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Msingi huu unapodumishwa na kuangaliwa, amani na utulivu wa mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla bila shaka vitapatikana. Kwa hali hiyo, mtu anayehudumia watu anatakiwa kuwa mtu wa kiasi na kadri. Kwa mfano, mtu anayetoa mawaidha anapaswa kumaliza hotuba yake pindi tu adhana inapoanza kutolewa, kwa sababu watu wenye mambo ya dharura ya kufanya wanatakiwa kuzingatiwa, na waumini waweze kuanza swala yao kwa amani. Kwa hiyo, watu wa huduma wanatakiwa kuwa waelewa na wenye werevu. Wanapopenda, kukasirika, kusifu, kukosoa na kulaumu hawatakiwi kuvuka mipaka. Wanatakiwa kuwa wenye Ikhlasi lakini siyo wasiojali watu; na kuwa wenye heshima na hadhi lakini wasiwe wenye kutakabari, na wenye staha lakini siyo wenye kutwezwa.

Watu wa huduma wanapaswa kuamiliana na wale walio chini ya uongozi wao kwa upendo, uadilifu, na huruma na wasiwabebeshe mizigo au kazi ngumu wasizoweza kuzifanya na kuzitekeleza. Ikumbukwe kuwa kutenda kwa uadilifu aina maana ya kutenda kwa usawa, bali kumpa kila mtu kile anachostahiki. Imeelezwa ndani ya Aya tukufu kuwa matendo yote yasiyokuwa ya uadilifu yanapaswa kuepukwa:

“Enyi mlioamini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ijapo kuwa ni juu ya nafsi zenu,

“Na Yeye ndiye aliye ziumba bustani zenye kutambaa juu ya chanja, na zisio tambaa, na mitende, na mimea yenye matunda mbali mbali, na mizaituni na mikomamanga inayo fanana na isiyo fanana. Kuleni matunda yake inapo zaka, na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake. Wala msitumie kwa fujo. Hakika Yeye hawapendi watumiayo kwa fujo.”

(Qur’an, 6: 141)

au wazazi wawili na jamaa zenu. Akiwa tajiri au masikini Mwenyezi Mungu anawastahikia zaidi. Basi msifuate matamanio, mkaacha kufanya uadilifu. Na mkiupotoa au mkajitenga nao basi Mwenyezi Mungu anajua vyema mnayo yatenda." (Qur'an, 4: 135)

Kufanya mambo kwa uwastani ni muhimu zaidi katika uendeshaji wa ofisi mbalimbali. Hili pia huonyesha kiwango cha maarifa, uelewa na akili ya mtu husika. Gavana wa Misri, Amr bin al-As (r.a) alipoulizwa kuhusu sababu ya mafanikio yake, alisema:

"Huweka taswira kuwa kuna kamba iliyo kati yangu na kila mtu anayenizunguka. Kamba hii inapokaza kupita kiasi, huilegeza kidogo; ninapohisi kuwa imelegea sana, huivuta na kuikaza. Kwa njia hii hupata kudumisha uhusiano pamoja na watu wanaonizunguka kwa kufanya mambo kwa uwastani."

Hasira ni jambo lingine linaloharibu uwastani. Ni udhaifu na ukosefu wa urari na upungufu wa kiakili. Ni jambo linaloonyesha udhaifu na upungufu wa mwanadamu. Kwa hali hiyo, watu wanaotoa huduma wanatakiwa wawe na uwezo wa kudhibiti hasira na ghadhabu zao.

Kuwatesa watu walio chini ya utawala kwa jina la kuweka nidhamu hakuwezi kuchukuliwa kama udhuru. Kwa upande mwingine, ni ukweli ulio wazi kuwa ukosefu wa nidhamu matokeo yake ni vurugu. Na hili husababisha matumizi mabaya ya mali, muda na huduma na matumizi mabaya hupelekea kwenye janga na kuanguka. Kamanda aliyeifungua Al-Andalus (Hispania), Tariq bin Ziyad, alipoingia Hispania alikuwa amevaa nguo kuukuu zenye viraka. Lakini ushujaa na ushindi katika moyo na roho yake vilikuwa viking'aa. Mwishoni hali hii ya kiroho ikawa nyenzo muhimu katika kuanzisha ustaarabu adhimu. Lakini pindi Abdullah al-Saghir,

mtawala wa mwisho wa Dola ya Kiislamu, Almohad, nchini Andalusia aliposhindwa na kuikimbia nchi yake, hata tandiko na hatamu za farasi wake vilikuwa vimetengenezwa kwa dhahabu. Hii ina maana kwamba hali ya uwastani inapopotea baada ya ushindi na manufaa ya kidunia, kushindwa na kuanguka hushika hatamu yake. Abdullah al-Saghir alisimama mlimani na kuitazama Granada akaanza kulia baada ya kuona mji huo ukiwaka moto. Mama yake akamwambia maneno yafuatayo, ambayo yaliacha athari katika historia:

"Lia ewe mwenye kughafilika, lia! Umeshindwa kuitetea nchi hii yenye baraka kama mwanaume; sasa lia kama mwanamke..."

Tokea hapo mlima huo ukaitwa "Kilio cha mwisho cha Waarabu" au "mlima wa kilio cha Waarabu."

Amana zisizolindwa kikamilifu hutumika vibaya; na amana zenye kutumika vibaya hupotea. Baada ya kuanguka kwa Al-Andalus, siyo tu ardhi ya Uhispania bali pia kazi nyingi za ustaarabu wa Kiislamu na kwa bahati mbaya vitabu milioni moja vilichomwa moto.

Kwa hiyo, mtu anayetoa huduma anapaswa kujua namna na wapi anapotakiwa kutumia amana alizokabidhiwa. Jinsi anavyolinda mali zake binafsi zisitumike vibaya ndivyo anavyopaswa kuepuka kutumia vibaya mali, elimu na huduma za umma.

Tusiuchukulie utumiaji mbaya kama utumiaji mbaya wa mali. Tunatakiwa kutumia onyo la Mwe-

"Ni mtu gani mnayemchukulia kama shujaa miongoni mwenu? Tukasema: yule anayeshindana na watu wenye nguvu. Akasema: Hapana, sio huyo, bali ni yule anayeweza kujidhibiti pindi anapokuwa na hasira."

(Muslim, Kitab al-Birr, 106)

nyezi Mungu lisemalo: **"Hakika Yeye hawapendi watumiayo kwa fujo"**[44] katika vipengele vyote vya maisha yetu.

Tujue kuwa tutaulizwa kwa kutumia vibaya muda na uhai wetu wenyewe au muda na uhai wa watu wengine. Kwa hali hiyo, mwalimu anayejua umuhimu wa kazi yake hapaswi kutumia vibaya muda na nishati za wanafunzi wake. Tujue kuwa kutofanya kitu na "kuua muda" ni aina mojawapo ya matumizi mabaya na ya fujo. Kutoheshimu vitu tulivyopewa kama amana nao pia ni utumiaji mbaya na wa fujo. Na matumizi mabaya zaidi kuliko yote ni kusahau kuwa binadamu ndiyo viumbe wanaoheshimiwa zaidi kuliko viumbe wengine wote na hivyo kutowapa malezi na mafunzo wanayostahili.

Kwa hali hiyo tunatakiwa kuwa makini sana kuhusu elimu na mafunzo kwa wanadamu. Wanatakiwa kupewa mafunzo sambamba na uwezo wa kukielewa kitabu cha ulimwengu na kuuelewa mpangilio mzuri na uwiano maridhawa unaopatikana ndani ya ulimwengu. Mazingira hayo ya kielimu yatawapa uwezo wa kuwa wanadamu kamili wanaoweza kuibadilisha imani yao kwenda kwenye hali ya ihsan (yaani kumuabudu Mwenyezi Mungu kana kwamba unamuona). Kwa namna moja tunatakiwa kuwapa mafunzo watu wenye uelewa wa imani kama waliokuwa nao maswahaba. Vinginevyo miongoni mwa mabilioni ya watu hitajio la binadamu wa kweli haliwezi kupatikana.

"Na ushike mwendo wa katikati, na teremsha sauti yako. Hakika katika sauti mbaya zote bila ya shaka iliyo zidi ni sauti ya punda."

(Qur'an, 31: 19)

44. Tazama: Qur'an, 6: 141.

Ni lazima tufanye juhudi ya hali ya juu kulea wanadamu kamili na kuwaokoa watoto wengi kadri tuwezavyo dhidi ya moto wa Jahannam wa-takaotumbukia ndani yake. Nani ajuaye? Huenda watoto tunawanyooshea mkono wetu ili kuwa-okoa wakawa ndiyo akina Sultan Mehmed (ka-manda na mfunguzi), Yavuz, Sulaiman (Mkuu), Sinan (Msanifu na mhandisi), Piri Reis (nahodha maarufu), Ibn Kamal (mwanazuoni wa Kiislamu), Aksemseddin au Aziz Mahmud Hudayi (mawalii wa Kisufi) wa kesho.

Umma huwa umma wenye nguvu na kulinda umuhimu wake kutokana na kuwalea na kuwa-tengeneza watu muhimu kama hao. Japokuwa himaya ya Uthmaniyya ilikuwa himaya ndogo ka-bisa iliyoanzishwa mjini Anatolia, ilistawi na kuwa kama mkuyu mkubwa na kutanda kwenye mabara matatu kutokana na watu iliowatengeneza. Lakini baadae himaya hiyo ilitikisika na kuchukua nafasi yake katika historia baada ya kuangukia mikononi mwa viongozi waliotiwa utumwani na manufaa na maslahi binafsi, ambao walipenda zaidi nyadhifa zao badala ya mustakabali wa watu wao.

Katika kutekeleza wajibu wake, mtu anayewa-hudumia watu kwa dhati ni kama keshia anayega-wa haki kwa watu wanaostahili, kwa sababu kila kitu ni mali na milki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kila kitu tulichojaaliwa ni baraka zitokazo Kwake, na tutaulizwa kwa kila neema na baraka hizi alizotupa. Kama hatutaki matokeo ya maswali hayo yawe mateso kwetu, tunatakiwa kusikiliza

Mtukufu Mtume (s.a.w) hakuwahi kumwambia mtu kosa lake moja kwa moja, badala yake alikuwa akielezea vizuri na kusema: “Ni vipi ninaona mkifanya jambo hili na hili”

maonyo yafuatayo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu:

"Na Yeye ndiye aliyeziumba bustani zenye kutambaa juu ya chanja, na zisiotambaa, na mitende, na mimea yenye matunda mbali mbali, na mizaituni na mikomamanga inayofanana na isiyofanana. Kuleni matunda yake inapozaa, na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake. Wala msitumie kwa fujo. Hakika Yeye hawapendi watumiayo kwa fujo." (Qur'an, 6: 141)

"Enyi wanadamu! Chukueni pambo lenu kwenye kila pahala wakati wa ibada, na kuleni, na kunyweni na wala msifanye ubadhirifu. Kwa hakika Yeye hapendi wanao fanya israfu." (Qur'an, 7: 31)

"Hakika wabadhirifu ni ndugu wa Mashet'ani. Na Shet'ani ni mwenye kumkufuru Mola wake Mlezi." (Qur'an, 17: 27)

Israfu na ubadhirifu ni kufanya matumizi yasiyo sahihi na yaliyozidi kiasi kwa kujihudumia wewe mwenyewe. Hata hivyo kutumia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu hakuhesabiwi kama israfu. Badala yake, kadri tunavyozidi kutumia na kutoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ndivyo tunavyozidi kupata thawabu na malipo mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Imeelezwa ndani ya Aya tukufu:

"Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema: Katika hivyo zipo dhambi kubwa na manufaa kwa watu. Lakini dhambi zake ni kubwa zaidi kuliko manufaa yake. Na wanakuuliza watoe nini? Sema: Kilicho chepesi. Namna hivi Mwe-

"Mbora miongoni mwenu (Waislamu) ni yule mwenye kujifunza Qur'an kisha akaifundisha (kwa wengine)."

(Bukhari, Fadail al-Qur'an, 21)

nyezi Mungu anakubainishieni Aya zake mpate kufikiri" (Qur'an, 2: 219)

Kwa muhtasari, njia iliyo bora katika mambo yote ni kuwa na uwastani na kiasi, na kuepuka kutumia kwa fujo, jambo ambalo hatimaye hutufanya tushindwe kutekeleza majukumu yetu ya kiroho na ya kijamii.

Hasira ni jambo lingine linaloharibu uwastani. Ni udhaifu na ukosefu wa urari na upungufu wa kiakili. Ni jambo linaloonyesha udhaifu na upungufu wa mwanadamu. Kwa hali hiyo, watu wanaotoa huduma wanatakiwa wawe na uwezo wa kudhibiti hasira na ghadhabu zao.

Siku moja Mtukufu Mtume (s.a.w) aliwauliza maswahaba:

"Ni mtu gani mnayemchukulia kama shujaa miongoni mwenu? Tukasema: yule anayeshindana na watu wenye nguvu. Akasema:Hapana, siyo huyo, bali ni yule anayeweza kujidhibiti pindi anapokuwa na hasira." (Muslim, Kitab al-Birr, 106)

Kwa hakika maamuzi yanayokuwa na makosa mengi zaidi yanayopelekea kwenye hali ya kusikitisha na kukatisha tamaa ni yale yanayofanywa wakati wa hasira. Kuhusu ukweli huu, Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema:

"... Usihukumu baina ya watu wa wawili hali ya kuwa una hasiria..." (Muslim, Kitab al-Aqdiyah, 16). Alimshauri mara tatu swahaba mmoja aliyemtaka ushauri "Usikasirike" (Bukhari, Kitab al-Adab, 76)

Heshima, upendo na shauku ya kuipenda Qur'an Tukufu huzihuisha roho, ilhali kuipuuza na kutoiheshimu ni dhambi kubwa inayoyafifiza maisha ya kiroho ya wanadamu.

"Zitakuja zama katika umma wangu ambapo idadi ya Qurra (wasomaji wa Qur'an) itaongezeka, ilhali mafuqahaa (wasomi wenye hikma, busara na watendaao mema) watapungua na maarifa yataondoshwa... baada ya kipindi hicho kitakuja kipindi ambacho kile kinachosomwa na watu kutoka ndani ya Qur'an hakitavuka koromeo zao."

(Hakim, Mustadrak, IV, 504)

Wanadamu wana hali tofauti tofauti. Wakati mwingine huwa na hasira na wakati mwingine huwa na furaha. Ili kutosababisha uonevu, mtu mwenye hasira hatakiwi kufanya maamuzi wakati anapokuwa katika hali hiyo. Kwa mujibu wa wosia wa Mtukufu Mtume (s.a.w), mtu anaposhikwa na hasira iwapo atakuwa amesimama basi akae chini, na kama atakuwa amekaa basi alale. Kama bado atashindwa kuidhibiti hasira yake, basi afanye wudhu. Baada ya kuidhibiti kikamilifu hasira yake, hapo anaweza kufanya maamuzi, kwa sababu mara nyingi wakati wa hasira mizania hukosekana na maamuzi huwa dhaifu, na haki za watu zinaweza kukanyagwa. Watu wanaotoa huduma daima wanatakiwa kuwa makini linapokuja suala la uwastani, hisani na neema.

Hali ya kisaikolojia ya watu ni muhimu sana katika kazi na huduma za kielimu. Kama ambavyo rubani asiyejisikia vizuri kisaikolojia huweza kupewa leseni ya kurusha ndege, vivyo hivyo mwalimu mwenye hasira au ghadhabu hatakiwi kupewa ruhusa ya kuingia darasani. Wakati huo huo, mwalimu mwenye hasira anatakiwa kutafuta sababu ya hasira yake na kujaribu kuidhibiti hasira hiyo katika kipindi ambacho mafunzo yanatakiwa kutolewa kwa utulivu, sambamba na maonyo na ushauri, lakini anatakiwa kutokuwa na hasira na ghadhabu zinazoweza kuwaumiza wanafunzi.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anatutaka tutanabahi na kuzingatia hali ya ulaini katika namna yetu ya kuzungumza:

"Na ushike mwendo wa katikati, na teremsha sauti yako. Hakika katika sauti mbaya zote bila ya shaka iliyo zidi ni sauti ya punda." (Qur'an, 31: 19)

Inapohitajika kumkataza mtu kufanya kosa, haitakiwi kuumiza hisia za mkosaji na hapaswi kuambiwa moja kwa moja; jambo husika linatakiwa kuelezwa kwa ujumla bila kutaja jina la mkosaji au mzungumzaji anatakiwa kuliekeza kosa husika kwake mwenyewe. Mtukufu Mtume (s.a.w) hakuwahi kumwambia mtu kosa lake moja kwa moja, badala yake alikuwa akielezea vizuri na kusema:

"Ni vipi ninaona mkifanya jambo hili na hili...." [45]

Watu wenye kukumbukwa daima katika historia ya Kiislamu ambao walilelewa na kukuzwa kwa maadili ya hali ya juu waliwaongoza wanajamii wa Kiislamu kuanzia watu wa kawaida mpaka masultan. Ushauri na wosia wa Sheikh Edebali kwa Othman Ghazi kwa niaba ya viongozi wengine wa dola ni wa busara, hekima na wenye maana kubwa:

"Ewe mwanangu! Wewe ni kiongozi! Kuanzia sasa na kuendelea
Hasira ni zetu; upole ni juu wako
Kero na maudhi ni vyetu; maridhiano ni juu yako
Kulaumu ni kazi yetu; uvumilivu ni kazi yako
Udhaifu, makosa ni kazi yetu; stahamala ni kazi yako

"Ole wao wale wanaozitafuna tu aya hizi (yaani wanazisoma tu) na hawazitafakari..."

Ibn Hibban, Sahih, II, 386

45. Tazama: Bukhari, Manaqib, 25; Muslim, Kitab al-salat, 119.

Migongano, mifarakano na ugomvi ni kazi yetu; kutenda haki na uadilifu ni kazi yako

Jicho baya, kutabiri mabaya na maoni potofu ni kazi yetu; kusamehe ni kazi yako"

"Ewe mwanangu! Kuanzia sasa na kuendelea

Migawanyiko ni kazi yetu, kutuunganisha ni kazi yako

Uvivu ni kazi yetu; kutuhamasisha na kutuzindua ni kazi yako..."[46]

8. Kutoa kipaumbele katika mafunzo ya Qur'an Tukufu:

Qur'an Tukufu ni amana kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu iliyoteremshwa kwa waja wa Mwenyezi Mungu kama muongozo kwao. Kuanza kuibeba amana hii kwetu sisi na kisha kuipeleka kwa watu wengine ni wajibu wetu wa kwanza kabisa na wa muhimu kuliko mambo yote. Mtukufu Mtume (s.a.w) katika hadith yake moja anasema kwamba:

"Mbora miongoni mwenu (Waislamu) ni yule mwenye kujifunza Qur'an kisha akaifundisha (kwa wengine)." (Bukhari, Fadail al-Qur'an, 21)

Huduma bora na kubwa kabisa anayoweza kufanyiwa mwanadamu ni kumsaidia apate mustakabali wake wa milele. Namna ya kulifanya hili ni kumuongoza mja kwenye utiifu, kumnyenyekea na kumtumikia Mwenyezi Mungu akiwa kwenye

Ili tuweze kujiokoa dhidi ya athari hasi za zama tulizo nazo, yaani ukafiri, ulahidi na tatizo la kuridhia tamaduni zisizokuwa za Kiislamu, tunapaswa kujifunza na kuifundisha Qur'an Tukufu kwenye familia zetu na kwa wale wanaotuzunguka.

46. Angalia sehemu iliyobaki ya ushauri na wosia wa Edibili katika sehemu ya mwisho ya kitabu hiki.

njia iliyonyooka. Hili linaweza kufikiwa tu iwapo atapata maadili na hisia za Qur'an Tukufu.

Qur'an ni chimbuko la hekima itokayo kwa Mwenyezi Mungu kwa waja Wake. Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaambia wanadamu kuwa:

"Enyi watu! Yamekujieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu Mlezi, na poza kuponyesha yaliyomo vifuani, na uongofu, na rehema kwa Waumini." (Qur'an, 10: 57)

Qur'an Tukufu ni muongozo mkuu kwa sababu imebeba ukamilifu, ukweli na siri za kimaanawi na kiroho ambazo mwanadamu anazihitajia mpaka Siku ya Mwisho. Hili limeelezwa ndani ya Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

"Hakika hii Qur'ani inaongoa kwenye yaliyonyooka kabisa, na inawabashiria Waumini ambao wanatenda mema ya kwamba watapata malipo makubwa." (Qur'an Tukufu, 17: 9)

Kwa kuwa Qur'an Tukufu ni kitabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ambacho muongozo wake utaendelea mpaka Siku ya Mwisho, waumini walio chini ya kivuli chake wanapaswa kuishi kulingana na muongozo wake mpaka watakapokufa. Kwa maneno mengine, waumini wanapaswa kujitolea nafsi zao kwa ajili ya muongozo wake na walipokee jukumu la muongozo wa kiroho, amani na uhai wa vizazi vya baadae kupitia muongozo wa Qur'an Tukufu kama jukumu lao kuu na tukufu kuliko majukumu mengine yote. Maelezo yafuatayo kutoka katika zama za mwanzo

Kukipa elimu kizazi kichanga bila kukipa nuru ya Qur'an na hisia za kiroho ni hasara na majuto makubwa kwa mwanadamu, kiumbe anayeheshimika ulimwenguni. Jukumu kuu la wazazi sio kuipa chakula mili ya watoto wao bali kuzilisha roho zao na kuwaandalia mustakbali wa milele.

za Uislamu yanaonyesha na kuthibitisha ukuu na utukufu wa jukumu hili.

Kutokana na ombi maalumu, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alituma walimu wa Qur'an wapatao sabini waliojulikana kama "Qurra" kwenda kwenye makabila ya Ra'l, Zaqwan, Usayyah na Banu Lihyan. Walipofika katika eneo liitwalo "Bi'r Maunah", watu wa makabila hayo waliwafanyia hiyana na kuwaua. Mtukufu Mtume (s.a.w) aliposikia habari hizo, aliwaombea maangamizi wauaji hao kwa kipindi cha mwezi mmoja.

Kitendo cha Mtume wa rehema (s.a.w), ambaye hakuwalaani watu wa Taif waliompiga mawe, akawalaani waliowaua walimu wa Qur'an kinaonyesha jinsi dhambi ya kuzuia mafunzo ya Qur'an Tukufu ilivyokuwa kubwa. Hili vilevile linaonyesha kwamba kwa mujibu wa Mtukufu Mtume (s.a.w) kazi na jukumu lenye heshima kuu ni kuifundisha Qur'an Tukufu kwa watu.

Umuhimu mkubwa uliotolewa na Mtukufu Mtume (s.a.w) kwenye mafunzo ya Qur'an Tukufu ulijionyesha katika nyoyo za Maswahaba kwa jinsi walivyokuwa na mahaba makubwa ya kuipenda Qur'an Tukufu. Ufuatao ni mfano wa mapenzi ya Qur'an Tukufu waliyokuwa nayo Maswahaba:

Wakati wa vita vya Dhat al-Riqa', Ammar bin Yasir na Abbad bin Bishr (r.a) walikuja kwa Mtukufu Mtume (s.a.w) na kumwambia kuwa walitaka kujitolea kulinda usiku mzima. Ombi lao lilipokubaliwa, Ammar (r.a) alichukua zamu ya pili na kwenda kulala. Rafiki yake, Abbad (r.a) akasimama na

"Mwenyezi Mungu atainyanyua daraja ya mja Wake Siku ya Kiyama. Mja atashangaa na kuuliza: "Mola wangu! Kwanini umeinyanyua daraja yangu?" Mwenyezi Mungu Mtukufu atasema: "Kwa sababu ya swala na toba ya mwanao aliyoifanya kwa niaba yako"

(Ahmad bin Hanbal, Musnad,II, 509; Ibn Majah, Kitab al-Adab, 1)

kuanza kuswali. Mara kafiri mmoja akamuona na kumpiga mshale. Abbad (r.a) aliuchomoa mshale mwilini mwake na kuendelea kuswali. Lakini akapigwa mshale wa pili na wa tatu. Akafanya kama mwanzo na kuendelea kuswali. Hatimaye alimaliza swala yake na kumuamsha Ammar:

"Amka, nimepigwa mshale." Ammar alipoamka, yule kafiri akamuona na kukimbia. Ammar alipomuona Abbad akiwa na damu akamuuliza:

"Subhanallah! Kwa nini hukuniamsha baada ya mshale wa kwanza?" Abbad (r.a) akajibu:

"Nilikuwa tu nimeanza kusoma sura ya Qur'an na sikutaka kukatisha swala yangu kabla ya kuikamilisha. Lakini mara mishale ikaanza kuja mmoja baada ya mwingine, na nikalazimika kurukuu na kisha nikakuamsha. Wallah! Kama siyo hofu ya kupoteza eneo hili nilililoamrishwa na Mtume (s.a.w) kulilinda, ningependelea kufa badala ya kukatisha kisomo changu."[47]

Heshima, upendo na shauku ya kuipenda Qur'an Tukufu huzihuisha roho, ilhali kuipuuza na kutoiheshimu ni dhambi kubwa inayoyafifiza maisha ya kiroho ya wanadamu. Mtukufu Mtume (s.a.w) alipoonyeshwa madhambi ya umma wake, aliona kwamba "kuisahau Qur'an iliyohifadhiwa" ndiyo dhambi kubwa kuliko yote.[48]

Ndiyo maana sisi na watoto wetu tunatakiwa kujifunza na kujitahidi kuishi kulingana na muongozo wa Qur'an ili tuweze kuhuisha uwezo na

"Kuna maneno mangapi ambayo ni ya jana, yalipita jana. Hii ni siku mpya; kwa hiyo mambo mapya yanapaswa kusemwa."

Jalal al-Din Rumi

47. Angalia Ahmad bin Hanbal, Musnad, III, 343 -44.
48. Abu Dawud, Kitab al-salat, 16.

baraka zake za kiroho. Vinginevyo Qur'an Tukufu haiwezi kuacha athari katika nyoyo zetu. Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema:

"Zitakuja zama katika umma wangu ambazo idadi ya Qurra (wasomaji wa Qur'an) itaongezeka, ilhali mafuqahaa (wasomi wenye hekima, busara na watendao mema) watapungua na maarifa yataondoshwa... baada ya kipindi hicho kitakuja kipindi ambacho kile kinachosomwa na watu kutoka ndani ya Qur'an hakitavuka koromeo zao." (Hakim, Mustadrak, IV, 504)

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an Takatifu:

"Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kuhitalifiana usiku na mchana ziko Ishara kwa wenye akili, ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto." (Qur'an, 3: 190 -91)

Aya hii zilipoteremshwa, Mtukufu Mtume (s.a.w) akasema:

"Ole wao wale wasiozitafakari aya hizi!" Katika riwaya nyingine:

"Ole wao wale wanaozitafuna tu aya hizi (yaani wanazisoma tu) na hawazitafakari..."[49]

Mafunzo ya Qur'an kwanza yanatakiwa kuanza kwa kuingia katika mazingira yake adhimu, kutaamali na kuitafakari Qur'an. Vinginevyo, kuisoma tu Qur'an bila kutafakari maana zake "haitokwenda

49. Tazama, Ibn Hisham, Sahihi, II, 386.

Tunatakiwa kuifanya Qur'an Tukufu kuwa chimbuko la ustawi na nuru ya roho na nyoyo zetu. Usomaji wa Qur'an Tukufu na kuishi kwa mujibu wa misingi yake tulikubali na kulipokea kama wajibu na jukumu letu.

chini ya koo," kwa maneno mengine haitokuwa na manufaa na faida kwa roho ya mja, kama ilivyoelezwa katika hadith tukufu ya Mtukufu Mtume (s.a.w).

"...Na vitu vinavyopendeza zaidi ambavyo mja Wangu kujikurubisha navyo Kwangu, ni vile nilivyomuamrisha; na mja Wangu huendelea kujikurubishwa kwangu zaidi kwa kutekeleza Nawafil (kusali au kufanya mambo ya ziada mbali na yale ya wajibu) mpaka ninampenda, hivyo Mimi huwa sikio lake analosikia kwalo, na macho yake anayotazamia, na mkono wake anaoshikia, na miguu yake anayotembelea; na akiniomba humpa, na akiomba nimlinde humlinda (yaani humpa ulinzi Wangu) na sisiti kufanya jambo kama ninavyosita kuchukua roho ya muumini, kwa sababu yeye hukichukia kifo, nami nachukia kumhuzunisha." (Bukhari, Kitab al-Riqaq, 38)

Njia muhimu ya wokovu dhidi ya zama za mdororo wa kidini ni juhudi ambazo zimekuwa zikifanywa kwa ajili ya Qur'an Tukufu. Leo hii hizi juhudi ni muhimu zaidi kuliko wakati wowote ule. Katika zama hizi, huduma ya dharura na ya lazima tunayotakiwa kuifanya kwa ajili ya Uislamu ni kuongeza mapenzi ya kupenda mafunzo ya Qur'an Tukufu, jambo litakalouwezesha umma wa Kiislamu kuamka na kurejea katika hali yake.

Ni lazima kuamini ahadi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ya kwamba **"atakamilisha (ufunuo wa) nuru Yake."** (Qur'an, 61: 8) Hata hivyo, kwa kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu atatimiza ahadi yake mikononi mwa wanadamu, tunatakiwa kufanya juhudi kubwa kutekeleze jukumu letu. Vinginevyo Mola wetu bado ataikamilisha Nuru Yake bila ya msaada wetu, lakini wale wanaopuuza wajibu huu watakuwa ni wenye kuulizwa kwa kupuuza na kushindwa kutekeleza wajibu wao. Adhabu ya Mungu iliyowakumba watu watatu ambao walishiriki harakati zote za kijeshi isipokuwa Vita vya Tabuk, ni tukio maarufu katika historia ya Kiislamu. Hivyo basi, ili kuwa huru kutokana na jukumu binafsi, ni muhimu kuwa mtu mwenye kujitolea katika kuutumikia Uislamu. Kuna heshima kubwa kama kushiriki katika kuihudumia dini? Lakini kutegemea tu imani na matumaini ya kwamba Mungu ataleta msaada bila sisi kufanya juhudi ni jambo lililo kinyume na moyo wa Uislamu.

Ili tuweze kujiokoa dhidi ya athari hasi za zama tulizonazo, yaani ukafiri, ulahidi na tatizo la kuridhia tamaduni zisizokuwa za Kiislamu, tunapaswa kujifunza na kuifundisha Qur'an Tukufu kwenye familia zetu na kwa wale wanaotuzunguka. Kamwe tusisahau hitajio letu la Qur'an Tukufu. Kuwa katika uhusiano endelevu na Qur'an Tukufu kutatupelekea kuipata njia ya Qur'an na kupambwa na maadili yake. Kufanya kinyume na haya itakuwa ni hasara na majuto kwetu. Ni kupoteza mustakabali wetu wa milele kwa furaha ya muda tu.

Wale wanaoishi mbali na nuru ya Qur'an Tukufu ni wasafiri katika giza la milele. Hususan watoto wetu wenye umri wa kwenda shule wanahitajia mafunzo ya Qur'an, maarifa ya dini, mafunzo ya kiimani na ya kimaadili. Imani kwamba familia peke yake inaweza kutoa mafunzo mazuri ya dini siyo sahihi. Kama ambavyo elimu kamili ya sayansi inatolewa shuleni, elimu na mafunzo ya kidini nayo pia yanatakiwa kutolewa kwa wataalamu wake; hata hivyo, kuwasahau vijana wanaotuzunguka huku tukiwapa elimu watoto wetu siyo tabia sahihi ya Kiislamu.

Watu wanaotoa huduma wanatakiwa kuwa na elimu na uzoefu katika uwanja wa huduma zao. Uwezo huu usipopatikana, huduma haitokuwa na manufaa, inaweza hata ikawa na madhara.

Kukipa elimu kizazi kichanga bila kukipa nuru ya Qur'an na hisia za kiroho ni hasara na majuto makubwa kwa mwanadamu, kiumbe anayeheshimika ulimwenguni. Jukumu kuu la wazazi siyo kuipa chakula mili ya watoto wao bali kuzilisha roho zao na kuwaandalia mustakabali wa milele.

Katika zama hizi ambazo watu wamesalimu amri mbele ya maada, walimu wa Qur'an wanatakiwa kuwa na uangalifu maalumu kwa wanafun-

zi wao. Nyoyo za wanafunzi zinapaswa kujazwa mapenzi ya kumpenda mwalimu wao. Kabla ya kujifunza alfabeti, wanatakiwa kujifunza ukweli na uhalisia wa alfabeti hizo kutoka kwa mwalimu wao. Nyoyo ndogo za wanafunzi zinatakiwa kujazwa upendo wa kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake; uzuri wa Uislamu unatakiwa kupata nafasi ndani ya nyoyo zao.

Tuanze kuwafundisha maneno ya Mwenyezi Mungu kwa kuwapa hisia ya kuwa maneno hayo wanaambiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa njia hii, nyoyo zao ndogo zitaelewa tofauti iliyopo baina ya alfabeti za Qur'an na alfabeti nyingine na wataieshimu Qur'an Tukufu katika kipindi chote cha uhai wao. Roho zao zitastawishwa sambamba na maana za kitabu hiki na kugeuka kuwa hazina ya siri kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.[50]

Nyoyo za watoto zitakapojazwa upendo wa kumpenda Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mtume Wake na Kitabu chake Kitukufu, ibada zao zitasonga mbele kuelekea kwenye ukamilifu. Kwa sababu imani yao itaimarika, ulimwengu wao wa kiroho utastawi. Kisha wataisoma Qur'an Tukufu kwa ladha ya kipekee na kuwa makini sana kuhusu amri na makatazo yake. Watazipamba nafsi zao kwa maadili na mwenendo wa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w).

"Mwenyezi Mungu Mtukufu humpenda mja Wake anayefanya kazi yake kwa namna nzuri na salama."

(Daylami, Musnad, I, 157)

50. Watangulizi wetu waliwakataza watoto waliohifadhi Qur'an kucheza mchezo wa kuchupa kwa sababu ya heshima waliyokuwa nayo juu ya Qur'an Tukufu. Kwa hali hiyo walitengeneza mazingira mazuri ya kuwalea watoto wao kwa kuhakikisha wanakiheshimu kikamilifu kitabu hiki kitukufu.

Kuwa na mtoto kama huyo ni faida kubwa ya milele kwa wazazi wote. Mtukufu Mtume (s.a.w) anaielezea faida hii kama ifuatavyo:

"Mwenyezi Mungu atainyanyua daraja ya mja Wake Siku ya Kiyama. Mja atashangaa na kuuliza:

"Mola wangu! Kwanini umeinyanyua daraja yangu?"

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Kwa sababu ya swala na toba ya mwanao aliyoifanya kwa niaba yako" (Ahmad bin Hanbal, Musnad,II, 509; Ibn Majah, Kitab al-Adab, 1)

Katika hadith nyingine, imeelezwa kuwa:

"Mwanadamu anapokufa, matendo yake hufikia kikomo, isipokuwa mambo matatu, sadaka yenye kuendelea, au elimu yenye manufaa (kwa watu), au mtoto mwema anayemuombea (marehemu)." (Muslim, Kitab al-Wasiyyah, 14; Tirmidhi, Kitab al-Ahkam, 36)

Kwa muhtasari, kuihudumia Qur'an Tukufu ni baraka ya Mwenyezi Mungu kwa waja Wake, ambayo inahitaji usikivu na umakini mkubwa, na siyo kazi ya ulimi tu bali pia moyo wenye hisia.

Iwapo katika jamii fulani watakuwepo watu wenye sifa bora wanaoweza kuibeba kazi ya kutoa huduma, itakuwa rahisi kuwapeleka watu wa jamii hiyo kwenye vilele.

9. Kujiendeleza kielimu na kimaadili

Mtu wa huduma asisahau kujiendeleza ili kutoa huduma bora kwa watu. Juhudi za maendeleo endelevu zinapaswa kuwa sifa na tabia yake ya kawaida. Watu wa huduma wasiokuwa na sifa ambao hawana elimu na uzoefu wa kutosha na ambao hawajali kabisa maendeleo yao ya ki-

maadili na kiroho hawawezi kutoa huduma kamili na ya dhati kabisa.

Kwa upande mwingine, maendeleo na mabadiliko katika maisha ni kanuni ya Kimungu. Kila kiumbe kisichoendana na yale yanayotakiwa na uhai lazima kitatoweka. Ndiyo maana watu wanaotoa huduma wanapaswa kuichunga kanuni hii ya Kimungu na kulipokea suala la kujiendeleza kama jukumu.

Suala jingine muhimu ni ukweli kwamba aina ya huduma na jinsi utekelezaji wake hubadilika kulingana na mazingira ya wakati. Kitu ambacho jana kilikuwa muhimu kinaweza kikapoteza umuhimu wake leo. Njia ya utekelezaji wake pia inaweza kubadilika. Kuwa na uwezo wa kuyaona mambo haya kunawezekana tu iwapo mtoaji wa huduma atajiendeleza. Tungo zifuatazo za Mawlana Jalal al-Din Rumi zinaonyesha udharura na umuhimu wa jinsi tunavyotamka maneno yetu:

"Kuna maneno mangapi ambayo ni ya jana, yalipita jana

Hii ni siku mpya; kwa hiyo mambo yanapaswa kusema"

Ali (r.a) anasema:

"Usiwalee watoto wako kulingana na mahitaji ya wakati wako bali kulingana na mahitaji ya wakati wao". Anaashiria umuhimu wa kuzingatia hali na mazingira ya zama na wakati husika.

Wale wanaowahudumia watu wanatakiwa kujiendeleza hasa katika nukta zifuatazo:

"Mimi ninge-omba nyumba hii ijae watu kama vile Abu Ubayda bin Jarrah, Muadh bin Jabal na Hudhayfa al-Yamani na kuwapa majukumu ya kufikisha ujumbe wa Uislamu na kuendeleza jamii."

(Bukhari, Tarikh al-Saghir, I, 54)

a. Kujiendeleza kielimu

Watu wanaotoa huduma kwanza kabisa wanatakiwa wawe na silaha ya elimu ambayo itawapatia mustakabali wa milele. Ili wasiangukie katika mitego ya fikra na imani potofu, wanatakiwa kupata elimu imara ya kithiolojia. Wakiwa na lengo la kutekeleza ibada mbalimbali kwa mujibu wa miongozo ya Mwenyezi Mungu, wanatakiwa kupata elimu ya uchaji wa Kiislamu. Ili wawe waja wataka-opata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu, wanatakiwa kuyasoma maisha ya Mtukufu Mtume (s.a.w) na kuyaelewa kwa moyo wenye kutaamali na kutafakari.

Tunatakiwa kuifanya Qur'an Tukufu kuwa chimbuko la ustawi na nuru ya roho na nyoyo zetu.

Usomaji wa Qur'an Tukufu na kuishi kwa mujibu wa misingi yake tulikubali na kulipokea kama wajibu na jukumu letu.

Watu wa huduma hawatakiwi kusahau au kupuuza usomaji wa vitabu vingine ili kuongeza utamaduni wao na kuimarisha shakhsia yao. Mara kwa mara wanatakiwa kusoma vitabu vya ushairi na historia, visa vya Qur'an Tukufu, wosia wa Mitume na walimu wa Kisufi, maagizo ya Ali (r.a) kwa magavana[51] pamoja na ushauri na wosia kutoka kwa wataalamu wa masuala ya kiroho.

Mbali na usomaji wa vitabu wanatakiwa kuhudhuria darsa za kielimu na makongamano mbalimbali. Hii ni njia ya kawaida ya

51. Sehemu ya maagizo hayo ya Ali (r.a) inapatikana katika sura husika mwishoni mwa kitabu hiki.

"Akasema: Bali tupeni nyinyi! Tahamaki kamba zao na fimbo zao zikaonekana mbele yake, kwa uchawi wao, kuwa zinapiga mbio. Basi Musa akaingia hofu nafsi yake. Tukasema: Usihofu! Hakika wewe ndiye utakaye shinda. Na kitupe kilicho katika mkono wako wa kulia; kitavimeza walivyo viunda. Hakika walivyounda ni hila za mchawi tu, na mchawi hafanikiwi popote afikapo."

(Qur'an, 20: 66-69)

kutafuta elimu. Kwa namna maalumu kabisa, hawatakiwi kukosa hata kidogo makongamano na darsa za wanazuoni wema wanaoishi maisha ya unyoofu.

b. Kujiendeleza kiroho

Mtu wa huduma anayewahudumia watu anatakiwa vilevile kuiendeleza hali yake ya kiroho, katika kipindi chote anachoendelea kutoa huduma. Anatakiwa kujisalimisha kwa Mola wake na kujitahidi kutekeleza majukumu na wajibu wake kwa Ikhlasi na staha ya hali ya juu. Asipojiendeleza kiroho, huduma yake anayoitoa inaweza kuleta athari zisizotakiwa. Wakati fulani anaweza kufanya jambo ambalo alitakiwa kuliepuka, kwa sababu anakuwa amekosa au amepoteza uwezo wake wa uelewa wa mambo kwa haraka (al-firasah). Huduma yake haitozaa matunda yoyote zaidi ya kujichosha. Ndiyo maana kwamba ili tuweze kupata msaada wa Mwenyezi Mungu tunatakiwa kuweka umuhimu kwenye kuzikomaza roho zetu kwa uchaji.

Kazi yetu katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kufanya juhudi kwa kadiri ya uwezo wetu na kuyaacha yaliyobaki mikononi mwa Mwenyezi Mungu Mtukufu (tawakkul). Na tunapaswa kuamini kuwa matokeo yatapatikana kulingana na mapenzi yake Mwenyezi Mungu.

Kutoa huduma inayokubalika kutawezekana kwa kuwa na uwezo wa uelewa wa mambo kwa haraka (intuition) na kwa kupata msaada wa Mwenyezi Mungu na hili huweza kupatikana kwa kuwa mja wa dhati wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hili limeelezwa katika Hadithul-Qudsi kama ifuatavyo:

"...Na vitu vinavyopendeza zaidi ambavyo mja Wangu kujikurubisha navyo Kwangu, ni vile nilivyomuamrisha; na mja Wangu huendelea kujikurubishwa kwangu zaidi kwa kutekeleza Nawafil (kusali au kufanya mambo ya ziada mbali na yale

ya wajibu) mpaka ninampenda, hivyo Mimi huwa sikio lake analosikia kwalo, na macho yake anayotazamia, na mkono wake anaoshikia, na miguu yake anayotembelea; na akiniomba humpa, na akiomba nimlinde humlinda (yaani humpa ulinzi Wangu) na sisiti kufanya jambo kama ninavyosita kuchukua roho ya muumini, kwa sababu yeye hukichukia kifo, nami nachukia kumhuzunisha." (Bukhari, Kitab al-Riqaq, 38)

Kuwa na moyo imara na ulio hai na kufanya maendeleo kunategemea juu ya kuukomboa moyo na kuuacha huru dhidi ya mapungufu mbalimbali, kwa maana moyo ni sehemu ya ishara za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hili linaweza kufikiwa kwa kuchunga kanuni na misingi ifuatayo:

1. Kuwa makini kuhusu riziki ya halali.

2. Kuchunga haki za waja na viumbe.

3. Kuwa katika hali ya kuendelea kufanya maombi, dua na kufanya istighfaar.

4. Kusoma Qur'an Tukufu na kushikamana na sheria zake.

5. Kufanya ibada kwa unyenyekevu.

6. Kuutumia usiku kwa shughuli za kidini. (Kadiri tunapoziangaza nyakati zetu za usiku kwa swala ndivyo zitakavyokuwa katika nyakati zetu za asubuhi. Nyakati za alfajiri ni nyakati zenye thamani zaidi kuliko nyakati zote za siku. Kuzipoteza nayakti hizo zenye thamani ni hasara kubwa.)

7. Kuendelea kumkumbuka na kutafakari kuhusu Mwenyezi Mungu Mtukufu.

"Iwapo dirisha au nyumba imejaa mwanga, usikikipe hadhi chochote isipokuwa jua. Hapo jua husema, "Ewe uliye makosani (katika imani yako), nikizama itadhihirika (utauona ukweli)."

Jalal al-Din Rumi

8. Kuyatafakari mauti.

9. Kuwa pamoja na watu wema na waaminifu na kujitenga na watenda dhambi na waovu.

10. Kuhudhuria darsa na vikao vya wasomi na watu wenye busara, ambao hufanya wanayoyajua.

11. Kuwa mtu wa kutoa sadaka.

Kwa muhtasari, walimu ambao hutoa mafunzo kwa vizazi vya baadae, wanatakiwa kwanza kuzibadilisha nyoyo zao kuwa makazi ya Kisufi. Iwapo nyoyo zao hazitobadilika kuwa makazi ya kisufi, hazitokuwa na tofauti na kuta za jengo ambazo huanguka na kutoweka baada ya muda mfupi. Wale wanaozifungua nyoyo zao kwa ajili ya wanadamu huendelea kuwa hai na kuishi mpaka Siku ya Hukumu, kama vile mafunzo ya kiroho ya Yunus Emre na Mawlana katika shule zao yanavyoendelea kuwanufaisha watu bila kukwama.

“Mwanangu! Ni lini utakuwa huru dhidi ya minyororo ya elimu ya uwezekano na kufikia daraja ya himaya ya Kimungu? Ni lini matendo yako yatakuchukua kwenda kwenye mamlaka ya Mwenyezi Mungu Mtukufu?”

Abd al-Qadir al-Jailani

c. Maendeleo ya utalaamu

Watu wanaotoa huduma wanatakiwa kuwa na elimu na uzoefu katika uwanja wa huduma zao. Uwezo huu usipopatikana, huduma haitokuwa na manufaa, inaweza hata ikawa na madhara. Huduma zinazotekelezwa na kutolewa katika namna bora kamwe haziwezi kusahaulika. Katika Qur’an Takatifu, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

“...hakika Sisi hatupotezi ujira wa anaye tenda mema.” (Qur’an, 18: 30)

Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) anasema:



"Mwenyezi Mungu Mtukufu humpenda mja Wake anayefanya kazi yake kwa namna nzuri na salama." (Daylami, Musnad, I, 157)

Kwa hiyo basi watu wa huduma wanapaswa kujifunza mbinu bora za kufanyia huduma zao. Suala lingine linaloweza kunyumbuliwa kutoka katika hadith iliyotajwa ni kutoa huduma katika hali ya ihsan, yaani kuwahudumia viumbe kana kwamba tunamuona Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa maana kutoa huduma ukiwa na picha hiyo akilini mwako hupelekea kupendwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kwa muhtasari, kujiendeleza kielimu na kimaadili ni kusonga mbele na kuzikamilisha sifa zetu za nje na ndani, kwa sababu vizazi bora vinaweza tu kulelewa na walimu bora wanaowalea wanafunzi wao kielimu na kimaadili. Walimu wasiokuwa bora hutengeneza wanafunzi wasiokuwa bora na dhaifu. Kwa kuwa malengo adhimu na ya hali ya juu huweza kufikiwa na watu wenye ukamilifu, watu hawa wenye ukamilifu wanatakiwa kulelewa mikononi mwa walimu wenye ustadi na tabia nyoofu.

Waumini wa kweli hujua kwamba nguvu zote ni za Mwenyezi Mungu Mtukufu na hawajinasibishi hata kidogo na mafanikio yao. Huenda mbali zaidi kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuwapa fursa hiyo.

Iwapo katika jamii fulani watakuwepo watu wenye sifa bora wanaoweza kuibeba kazi ya kutoa huduma, itakuwa rahisi kuwapeleka watu wa jamii hiyo kwenye vilele. Iwapo jamii haina watu kama hao wenye sifa bora, basi jamii hiyo itakuwa na mgogoro mkubwa wa nguvu kazi. Kama ilivyo kwa mwili usiokuwa na kichwa, jamii hiyo nayo haiwezi kuendelea kuwa hai. Ndiyo maana suala muhimu zaidi kuliko yote ni kutengeneza watu

bora wenye tabia na sifa za juu kama asemavyo mshairi maarufu marehemu Mehmed Akif:

"Inahitajika mtu wa kweli ili kuubadilisha umma kuwa umma wa kweli..."

Siku moja Umar (r.a) alikuwa amekaa na marafiki zake. Akawauliza iwapo wanatamani wapewe nini kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Baadhi wakasema:

"Natamani kama chumba hiki kingejaa pesa ili niweze kuzitoa sadaka."

Wengine wakasema:

"Ninatamani nyumba hii ijae dhahabu ili niweze kuzitumia katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu."

Hata hivyo, Umar aliposema:

"Kitu gani kingine" wakasema:

"Kitu gani kingine cha kuomba?" Umar akasema:

"Mimi ningeomba nyumba hii ijae watu kama vile Abu Ubayda bin Jarrah, Muadh bin Jabal na Hudhayfa al-Yamani na kuwapa majukumu ya kufikisha ujumbe wa Uislamu na kuendeleza jamii." (Bukhari, Tarikh al-Saghir, I, 54)

Ukitambua udhaifu wako, basi amali ndogo kabisa huwa kama mlima. Mapungufu yako hupata kukamilika, sumu zote hugeuka kuwa mafuta na asali. Milima huwa mabustani ya matunda; ulimwengu wote huwa shamba la mizabibu kwa ajili yako

10. Kuyahusisha makosa na nafsi yako na kuyahusisha mafanikio na Mwenyezi Mungu Mtukufu

Ni muhimu mno kutochanganya hisia za ubinafsi na huduma inayotekelezwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Watu wanaojishughulisha na kutoa huduma wanatakiwa kuwa waangalifu lin-



apokuja suala la kutambua mafanikio yanayoletwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu na wasijipe sifa kamili wao wenyewe, bali wamshukuru Mwenyezi Mungu kwa msaada na mapenzi Yake. Mwenyezi Mungu Mtukufu anaeleza kuhusu ushindi walioupata waumini katika Vita vya Badr:

"Hamkuwauwa nyinyi lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyewauwa. Na wewe hukutupa, walakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyetupa..." (Qur'an, 8: 17)

Mfano mwingine wa suala hili ni huu ufuatao:

Fir'aun alijiona dhaifu baada ya kushuhudia miujiza ya Nabii Musa (a.s). Ili kujiokoa na hali hii, aliwakusanya wachawi mabingwa zaidi katika zama zake na kuandaa shindano baina ya wachawi hao na Nabii Musa (a.s). Hata hivyo, bado alikuwa na wasiwasi kuhusu matokeo, hivyo akawauliza wachawi:

"Niambieni, mtamshinda Musa?"

Kiongozi wa wachawi akamjibu:

"Tupo katika kiwango cha juu kabisa cha uchawi. Hakuna aliye bora zaidi yetu katika uchawi. Labda ije nguvu ya kuvunja uchawi kutoka mawinguni, vinginevyo tunakuhakikishia kuwa tutashinda shindano hili. Hakika sisi tuna nguvu mno."

Ikakubaliwa kuwa shindano lifanyike siku ya sikukuu. Kila mtu alihudhuria na hadhara ilikuwa na shauku kubwa ya kuona kitakachotokea. Wachawi wakatupa kamba zao ardhini na kila

"Enyi mlio amini! Takeni msaada kwa subira na Sala. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanao subiri."

(Qur'an, 2: 153)

kamba ikageuka kuwa nyoka. Tukio hili limeelezwa ndani ya Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

"Akasema: Bali tupeni nyinyi! Tahamaki kamba zao na fimbo zao zikaonekana mbele yake, kwa uchawi wao, kuwa zinapiga mbio. Basi Musa akaingia hofu nafsi yake. Tukasema: Usihofu! Hakika wewe ndiye utakaye shinda. Na kitupe kilicho katika mkono wako wa kulia; kitavimeza walivyoviunda. Hakika walivyounda ni hila za mchawi tu, na mchawi hafanikiwi popote afikapo." (Qur'an, 20: 66-69)

Kisha Nabii Musa (a.s) akatupa chini fimbo yake na tahamaki ikageuka kuwa joka kubwa na kuzimeza kamba zote za wachawi. Huo haukuwa uchawi wa kibinadamu; ulikuwa muujiza kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Walichokifanya wachawi kilikuwa ni hila na ujanja tu.

Kiongozi wa wachawi akamwambia mwenzake mmoja, baada ya kuona yaliyofanywa na Nabii Musa (a.s):

"Mtazame Musa pale fimbo yake inapofanya kazi yake; ninashangazwa na hali yake itakavyokuwa..."

Rafiki yake huyo akafanya alivyoambiwa na akawa anamtazama Nabii Musa (a.s) kwa makini. Alichoona ni kwamba pindi fimbo ya Musa ilipokuwa ikiendelea kufanya kazi yake, Musa alikuwa amesawajika na rangi ya uso wake ikabadilika. Akamtaarifu mchawi mkuu kuhusu alichokiona:

"Tukio hili lilipokuwa likitokea, Musa alisawajika, lakini fimbo yake iliendelea kufanya kazi yake."

"Bwana wa watu ni yule anayewahudumia."

(Daylami, Musnad, 324)

Mchawi mkuu aliposikia hivyo akasema:

"Hizi siyo hila za Musa, bali ni kazi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa sababu mchawi hawezi kuzihofia hila zake mwenyewe, kama ambavyo msanii hawezi kuihofia sanaa yake. Hivyo basi hii ni kazi kutoka kwa Mwenyezi Mungu..." na hivyo akaikubali imani ya Nabii Musa (a.s).

Wachawi wengine nao pia walimfuata na kuingia katika imani mpya, yaani dini ya Nabii Musa (a.s). Tukio hili pia linaonyesha kwamba tusipochanganya hisia zetu binafsi katika huduma zetu na kutarajia tu radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu, tutapata baraka za Mwenyezi Mungu na kupata matokeo yenye mafanikio, hata kama uwezo wetu au vipawa vyetu siyo imara sana kutekeleza huduma husika. Nabii Musa (a.s) alihisi hofu kwa sababu wakati huo aliwaza kuwa hakuwa na uwezo wa kutosha wa kushindana, lakini akajilinda kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kufanya kwa mujibu wa maagizo ya Mwenyezi Mungu na matokeo yake akapokea muujiza wa Mwenyezi Mungu. Kwa maneno mengine alipata msaada wa Mwenyezi Mungu na kuwadhibiti wachawi.

Katika kipindi chote cha historia, raia walidumisha mwenendo mzuri pale viongozi walipokuwa na tabia njema, kwa sababu ya uhusiano uliokuwepo baina ya raia na viongozi.

Hivyo basi, kazi yetu katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kufanya juhudi kwa kadri ya uwezo wetu na kuyaacha yaliyobaki mikononi mwa Mwenyezi Mungu Mtukufu (tawakkul). Na tunapaswa kuamini kuwa matokeo yatapatikana kulingana na mapenzi yake Mwenyezi Mungu. Watangulizi wetu waliuweka ukweli huu katika ka-

nuni ya "Mafanikio yanatoka kwa Mwenyezi Mungu pekee..."

Kwa maneno mengine, sisi ndiyo tunaopanda mbegu ardhini, lakini Mwenyezi Mungu ndiye anayeamua kuifanya mbegu hiyo kuwa mti mkubwa au kuoza na kutoweka. Vilevile, Nabii Musa (a.s) ndiye aliyetupa fimbo, lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye aliyeigeuza kuwa joka kubwa, lililowameza nyoka wengine.

Kwa hiyo tunapaswa kumtazama Mtumaji wa baraka siyo baraka zenyewe. Rumi anasema:

"Japokuwa chuma kimekuwa chekundu, lakini siyo chekundu (kwa asili):(wekundu huo) ni mwali ulioazimwa kutoka katika kitu kinachotoa moto."

"Iwapo dirisha au nyumba imejaa mwanga, usikikipe hadhi chochote isipokuwa jua." [52]

"Hapo jua husema, "Ewe uko makosani (katika imani yako), nikizama itadhihirika (utauona ukweli)." [53]

Abd al-Qadir al-Jailani anatoa usia na ushauri ufuatao kuhusu suala hilo hilo:

"Mwanangu! Ni lini utakuwa huru dhidi ya minyororo ya elimu ya uwezekano na kufikia daraja ya himaya ya Kimungu? Ni lini matendo yako yatakuchukua kwenda kwenye mamlaka ya Mwenyezi Mungu Mtukufu?

"Je! Wakati haujafika bado kwa walio amini zikanyenyekea nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na haki iliyo teremka? Wala wasiwe kama walio pewa Kitabu kabla yao, muda wao ukawa mrefu, kwa hivyo nyoyo zao zikawa ngumu, na wengi wao wakawa wapotovu."

(Qur'an, 57: 16)

52. Juzuu I utenzi 3261-62.
53. Juzuu 1 utenzi 3264.

Usimkimbie Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa sababu tu ya mabalaa anayokutahini. Mwenyezi Mungu anakutahini kwa mabalaa mbalimbali na sababu ni hii hapa: ili aone kama utazitazama sababu na kuondoka mlangoni Mwake au utashikamana na mlango Wake; ili aone kama utategemea sababu za dhahiri au za batini; ili aone kama utayageukia yanayoonekana au yasiyoonekana; ili aone kama utaiangalia elimu, uwezo na vipawa kutoka kwako au kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu...”

Hii ina maana kwamba waumini wa kweli hujua kwamba nguvu zote ni za Mwenyezi Mungu Mtukufu na hawajinasibishi hata kidogo na mafanikio yao. Huenda mbali zaidi kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuwapa fursa hiyo.

Sultan Suleiman, ambaye aliweza kuiunganisha dunia kwa usultani wa kidunia na usultani wa kiroho; msimamo aliouonyesha baada ya kupata ushindi ni kipimo kwa watu wote wa huduma.

Barbarossa Hayreddin Pasha aliyashinda majeshi ya Andrea Doria katika Vita vya Preveza. Andrea Doria alikimbia na akayaokoa maisha yake kwa tabu sana. Barbarossa alirudi Istanbul akiwa na maelfu ya mateka. Eneo la bahari lilikuwa limejaa manchani zilizowabeba mateka. Sultan Suleiman alikuwa akitazama mandhari hii ya ushindi kutokea kwenye kasri lake. Pasha mmoja akamwambia huku akiwa na hamasa kubwa:

“Ewe sultan wangu! Ninashangaa ni mara ngapi ulimwengu umeshuhudia mandhari hiyo ya

“Wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizo”

(Qur’an, 2: 195)

ushindi? Kwa hakika sasa unapaswa kufurahi na kuona ni fahari."

Sultan Suleiman akajibu:

"Ewe Pasha! Je tuone fahari au kumshukuru Mola wetu na Kumsifu kwa kutujalia ushindi huu?"

Watu wa huduma wakifuata miongozo hii, hujiweka huru dhidi ya nafsi huku staha na unyenyekevu wao ukiongezeka. Watakuwa wameokolewa dhidi ya majivuno na kiburi, ambayo ndiyo maradhi hatari zaidi ya nafsi.

Aya ifuatayo inasema kwamba: **"...Usijigambe! Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wanaojigamba."** (Qur'an, 28: 76) Ndiyo maana kwamba mja anatakiwa kujilinda kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu dhidi ya hatari ya maradhi ya nafsi na kiburi. Japokuwa Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa na sifa na ubora wa hali ya juu, lakini alipokuwa akijizungumza, alikuwa akiongeza kwa kusema "hakuna fahari" na kudumisha unyenyekevu wake. Alichokuwa akitaka tu kuzungumzia na kuelezea baraka alizopewa na Mwenyezi Mungu huku akiepuka fahari au kiburi na majivuno. Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) anasema:

"Mimi ni kiongozi wa mitume, lakini sizungumzi haya kwa ufahari. Mimi ni mwisho wa manabii, lakini sizungumzi haya kwa ufahari. Mimi ndiye nitakayekuwa wa kwanza kufanya uombezi na wa kwanza kukubaliwa uombezi wangu, lakini sizungumzi haya kwa ufahari."

"Siku ya Kiyama, pindi ardhi itakapofunguliwa mimi nitakuwa wa kwanza kufufuliwa, lakini si-

Imani, ambayo humuunganisha muumini na Mwenyezi Mungu, ambaye ndiye pekee Mwenye Nguvu, ni aina ya msisimko. Muumini hapaswi kuhofia kitu chochote na wala hapaswi kupoteza matumaini.

zungumzi haya kwa ufahari. Siku hiyo nitapewa bendera ya himidi, lakini sijisifu kwa hili. Siku ya Kiyama, mimi ndiye bwana wa wanadamu, lakini sizungumzi haya kwa ufahari. Siku ya Kiyama nitakuwa wa kwanza kuingia peponi, lakini sizungumzi haya kwa ufahari." (Darimi, Muqaddimah, 8)

Kwa hakika "umimi" na "ukaidi" ni kama saratani kwenye njia ya utoaji wa huduma na tiba yake ni ngumu sana. Ni aghlabu kuona maneno yasemayo "bure" kwenye makazi ya kiroho ya Kisufi. Neno hili hukusudia kuwaelezea watu kuwa wao si chochote. Nukta ya muhimu ni kuutambua udhaifu wetu na kuelewa kuwa sisi ni waja tu. Mja anapofikia hatua hii, hata amali ndogo hutosha kumuokoa. Ukweli huu unaelezwa katika shairi lifuatalo:

Ukitambua udhaifu wako, basi amali ndogo kabisa huwa kama mlima

Mapungufu yako hupata kukamilika, sumu zote hugeuka kuwa mafuta na asali,

Milima huwa mabustani ya matunda; ulimwengu wote huwa shamba la mizabibu kwa ajili yako.[54]

"Wala msilegee, wala msihuzunike, kwani nyinyi ndio wa juu mkiwa ni Waumini."

(Qur'an, 3: 139)

Wale wanajishughulisha na huduma ya kuwahudumia viumbe wanapaswa kuomba msaada wa Mwenyezi Mungu wakijua kwamba wao ni dhaifu. Jambo hili limeelezwa ndani ya Aya ifuatayo:

54. Nukuu hii imechukuliwa kutoka utenzi wa tahmis wa M.Asad Arbili (shairi lililotungwa kwa kuongeza vina vitatu vya utenzi kwa kuambatanisha na msitari wa kwanza wa utenzi wa gazel) kuhusu gazel ya Niyazi Baba.

"Enyi mlioamini! Takeni msaada kwa subira na Sala. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaosubiri." (Qur'an, 2: 153)

Waumini wanapaswa kufuata ushauri huu wa Mwenyezi Mungu na kuomba msaada Wake kwa kuswali rakaa mbili za swalat al-hajah hususan wakati wa alfajiri ili wapate kufanikiwa.

Watu wa huduma hawapaswi kumlaumu yeyote kwa dosari zinazojitokeza wakati wa kutoa huduma na wanatakiwa kuyageukia mapungufu yao. Wanatakiwa kuwa na uwezo wa kuwa na subira na kuwavumilia wengine huku wakijiuliza wao wenyewe, kwa sababu hali ya kiroho ya wale wanaotoa huduma huwaathiri wale wanaohudumiwa. Kosa litakaloonekana kwa wale wanaohudumiwa ni dhihirisho la tatizo la wale wanatoa huduma.

Imam Rabbani (q.s) anatoa usia na ushauri ufuatao katika barua moja aliyomuandikia mwanafunzi wake:

"...Umeandika kwamba una malalamiko kuhusu wanafunzi wako na kwamba hisia zako zimeumizwa. Wakati ambapo ulitakiwa kuumizwa na kuyalalamikia matendo yako mwenyewe; *kwa sababu unaamiliana nao katika namna ambayo malalamiko hayaepukiki; wakati ambapo mwalimu anashauriwa kuamiliana na wanafunzi wake kwa namna nzuri. Kuwaelezea tu visa na methali na kuwa na urafiki nao siyo jambo linalokaribishwa... (Kwa maneno mengine, badala ya kuzungumza tu anatakiwa kuwa mfano kwa matendo yake.)" (Maktubat, 209th letter)*

"Ewe Mwenyezi Mungu! Ninajilinda kwako kutokana na wasiwasi na huzuni, kutokana nakukosa uwezo na uvivu, kutokana na tabu na woga, dhidi ya uzito wa madeni na kuzidiwa na watu."

(Bukhari, Daawat, (maombi),38)

11. Kujaribu kuwa mfano mwema

Watu wa huduma wanatakiwa kubeba kwa kulitekeleza kwa vitendo jukumu lao badala ya kuwaambia tu wengine walifanye. Wale wanaokaa katika kona, kutoa amri na kudhani kuwa wanawahudumia watu ni wale wasioweza kuelewa msingi, asili na kiini cha kuwahudumia wengine.

Wale wanaowaongeza wengine katika huduma wanatakiwa kushikamana na huduma yao zaidi kuliko wale wanaowaongoza. Tabia hiyo huongeza hamasa ya wenzao na kuifanya kazi yao kwa bidii zaidi. Mifano ya jambo hili inapatikana katika maisha ya Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w). Mojawapo katika mifano hiyo ni pale ambapo yeye mwenyewe alibeba matofali wakati wa ujenzi wa msikiti wa Quba na Msikiti wa Madinah. Alifanya kazi moja kwa moja katika kuchimba handaki lililotumika katika Vita vya Khandaq na wakati mwingine aliwahudumia maswahaba wake kwa mikono yake mwenyewe.

Maneno yake yasemayo: *"Bwana wa watu ni yule anayewahudumia."* (Daylami,Musnad, 324) yanathibitisha kwamba wale wanaowahudumia watu (yaani viongozi) hawapaswi kusubiri kuhudumiwa na watu wengine, bali wanatakiwa kuwa wa kwanza kuwahudumia wengine.

Kama viongozi wa umma wao wenyewe watawahudumia watu, jambo hili litawaathiri kiroho watu wengine wanaohudumiwa na kutengeneza moyo wa umoja. Kwa namna hii kazi nyingi ngumu zitatekelezwa kwa urahisi. Historia imejaa mifano ya moyo huu.

"Enyi mlio amini! Subirini, na shindaneni kusubiri, na kuweni macho, na mcheni Mwenyezi Mungu, ili mpate kufanikiwa."

(Qur'an, 3: 200)

Kwa mfano, Sultan Suleiman alikuwa miongoni mwa wale ambao binafsi waliishi na moyo huu. Ushiriki wake katika Vita vya Szigetvar, ilhali yupo katika dakika za mwisho za uhai wake na akiwa hana nguvu za kutosha, inatosha kuonyesha mfano wa moyo huu. Alipokuwa akielekea katika Vita vya Szigetvar, waziri wake mkuu Sokullu alikuja na kumwambia:

"Ewe sultan wangu! Umeshaupa umma huu ushindi mwingi sana. Umechoka. Umeutoa wakfu uhai wako kwa ajili ya ulimwengu wa Kiislamu. Itakuwa vigumu sana kwako kushiriki katika vita hivi ukiwa katika umri huu. Hivyo basi, ninadhani unapaswa kubaki mjini Istanbul na kuendesha mambo ya umma. Mimi, mawaziri wengine tutakwenda na kuliongoza jeshi."

Sultan akajibu:

"Nisikilize vizuri, ewe Sokullu! Waambie kizazi kijacho kuhusu utashi wangu. Kiongozi daima anatakiwa kuwa pamoja na wanajeshi wake katika vita. Wanajeshi wanapomuona kiongozi wao akiwa pamoja nao, hamasa yao huongezeka. Adui, kwa upande mwingine, huliona jeshi letu likiwa imara zaidi na kuingiwa na hofu. Nguzo ya kweli ya ushindi katika vita ni nguvu ya kiroho. Tumepata uzoefu mkubwa sana tangu tukiwa watoto. Uzoefu wetu unaweza kuhitajika katika harakati za kijeshi. Mara nyingi sana dakika na hata sekunde zinaweza kubadili matokeo ya vita. Ndiyo maana nitashiriki katika vita hivi. Nitawezaje kukutana na watangulizi wangu huko Akhera iwapo nitakaa na kufa nikiwa kitandani?"

"Enyi mlio amini! Takeni msaada kwa subira na Sala. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanao subiri."

(Qur'an, 2: 153)

خَيْرُ النَّاسِ أَنْفَعُهُمْ لِلنَّاسِ

Sokullu akasema: “Uamuzi ni wa sultani wetu” kisha akakaa kimya.

Alikuwa akienda kumaliza harakati hii kwa namna gani? Wakati wa vita ili aonekane kuwa amenyooka, alifungwa mikanda. Vita vikaanza na ilikuwa kipindi cha mvua. Walipofika sehemu moja, gari iliyobeba mzinga ilikwama ndani ya tope na mnyama aliyekuwa akilivuta akashindwa kulitoa nje ya tope. Jeshi lilikuwa limetangulia mbele na mahali hapo hapakuwepo na askari wa kutosha. Sultan akatoa amri “maafisa wote wa ngazi za juu wakiwemo majenerali waingie kwenye tope na kuubeba mzinga.” Mzinga huo ukatolewa ndani ya tope kwa msaada wa baadhi ya askari. Sultan akamgeukia mwandishi wa historia wa kifalme (vak’anuvist) na kumwambia:

“Yaandike haya ili vizazi vijavyo visome na kujifunza. Wasaidizi na mawaziri wa Sultan Suleiman waliingia kwenye tope na kulitoa gari la mzinga. Na kwa hiyo balaa likashughulikiwa kwa njia hii.” Sultan alitoa mfano mzuri sana kwa vizazi vijavyo.

Katika kipindi chote cha historia, raia walidumisha mwenendo mzuri pale viongozi walipokuwa na tabia njema, kwa sababu ya uhusiano uliokuwepo baina ya raia na viongozi. Kwa mfano, pindi Umar bin Abd al-Aziz aliposhika Ukhalifa, alikuta mvurugiko mkubwa sana wa kimaadili kwa raia. Katika kipindi cha miaka miwili na nusu ya utawala wake, vitu vingi vilibadilika mafanikio mengi ya kiroho na kimaada yakapatikana. Kwa maneno

“Matatizo na tabu katika njia ya kuufikisha ukweli wa Uislamu yanatakiwa kuhesabiwa kuwa ni baraka. Mitume walikabiliana na matatizo mengi na kukumbana na mashaka ya hali ya juu.”

Imam Rabbani

mengine, mtindo wa maisha ya kiongozi huyu yalijionyesha katika maisha ya raia wake.

Japokuwa kila anayejihusisha na utoaji wa huduma kwa watu anatakiwa kujipamba na sifa hii ya kimaadili, lakini sifa hii ni yenye kuhitajika zaidi kwa viongozi wa umma.

12. Kutopoteza msisimko na kuwa mwenye msimamo na ung'ang'anizi

Nguvu inayowasukuma watu wa huduma kwenda mbio kuwahudumia wengine na kutoa huduma zao kwa furaha ni upendo na msisimko wanaohisi kwa kuwahudumia watu. Wale wasiokuwa na aina hii ya msisimko katika nyoyo zao hawawezi kupata furaha na raha ya kuwahudumia wengine.

Ni ukweli unaojulikana kwamba kupanda kwa hali za uelewa wa mambo na hata kupanda kwa mataifa mengi hutokea wakati wa kilele cha nyakati za msisimko. Kwa mfano, katika kipindi cha Sultan Suleiman, wakati wa kilele cha Dola ya Uthmaniyya, kilikuwa ni kipindi ambacho umma wote ulishikamana kwa imani na msisimko. Imani na msisimko wao vilionekana wazi katika maisha ya kila mwanajamii kuanzia watu wa kawaida mpaka kwa Sultan mwenyewe.

Kwa mfano, baada ya ushindi wa vita vya Preveza, askari mmoja alikuja Istanbul kutoa habari njema za ushindi. Alipoingia katika lango la Ikulu ya Topkapi, alizivuta kwa nguvu hatamu za farasi wake. Akainuka juu na kuzunguka kwa

"Kwenda Horasan na kufikisha ujumbe wa Uislamu kuna faida zaidi kwako kuliko kuishi jirani na Makkah."

Sufyan al-Sawri (r.a.)

muda. Sultan Suleiman alipoona hali hii akamwambia yule askari:

"Farasi pori wako ana nini!" Jibu la askari yule ilikuwa ni ishara ya msisimko aliokuwa nao:

"Ewe Sultan wangu! Meditarania nayo pia ilikuwa kama farasi pori, lakini tuliweza kuituliza."

Katika zama hizo kila mtu katika jamii ya Kiuthamniyya alikuwa na hisia kama hizo; lakini punde tu walipoanza kupoteza hamasa yao, wakaanza kuporomoka. Maendeleo na ukuaji wa huduma katika njia ya Mwenyezi Mungu hutegemea kiwango cha msisimko na hisia za ndani za kidini. Kwa mujibu wa maelezo ya Ibn Abbas (r.a), Aya ifuatayo iliteremka pindi uzembe na uvivu vilipoanza kuonekana katika nyoyo za Waislamu:

"e! Wakati haujafika bado kwa walioamini zikanyenyekea nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na haki iliyoteremka? Wala wasiwe kama waliopewa Kitabu kabla yao, muda wao ukawa mrefu, kwa hivyo nyoyo zao zikawa ngumu, na wengi wao wakawa wapotovu." (Qur'an, 57: 16)[55]

Watu wanaweza kufanya makosa; wakati mwingine hukosea kwa makusudi au bila makusudi. Kama ambavyo wewe humuomba msamaha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili yako mwenyewe, wasamehe na uwatendee wema.

Wakati fulani hisia za kinaa zinaweza kutokea kwa watu wa huduma, hali ambayo ni dalili ya mwanzo wa hali ya hatari kwao. Hisia ya "hii inatosha" ni wasiwasi wa nafsi unaomwita mtu kwenye matamanio ya kidunia. Maelezo yafuatayo kutoka kwa Imran (r.a) yanaonyesha umuhimu wa

55. Ibn Kathir, Tafsir, IV, 332.

kuendelea kuwa na msisimko wa kutoa huduma mpaka mwisho wa uhai:

Katika zama za utawala wa Bani Umayyah, jeshi la Kiislamu chini ya uongozi wa Abdurrahman bin Walid lilikusanyika kwa ajili ya kampeni ya kuifungua Istanbul. Khalid bin Zayd Abu Ayyub al-Ansari (r.a) alikuwa miongoni mwa wanajeshi hao. Wakati wa vita, Ansar mmoja alionekana akiwa anamuendesha farasi wake nyuma ya safu za maadui, na hakurejea. Waumini walipoona alichofanya wakakumbuka Aya isemayo **"wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizo"**[56] na kusema:

"La ilaha illallah! Tazama alichofanya! Alijitupa mwenyewe katika hatari."

Abu Ayyub al-Ansari alipoyasikia maneno yao akasema:

"Ndugu waumini! Tafadhalini msiichukulie vibaya Aya hii. Iliteremka kutuhusu sisi, yaani Ansari. Mwenyezi Mungu alipokuwa amemjaalia ushindi Mtume Wake Mtukufu (s.a.w), tukasema: "Sasa tunaweza kushughulika na maendeleo ya mali zetu." Hapo Mwenyezi Mungu Mtukufu akateremsha Aya hiyo:

"Na toeni katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizo..." (Qur'an, 2: 195) Hatari inayohusu "kujitupa kwa mikono yetu katika maangamizo" ili-

Kamwe usipotoshe haki. Ukifanya hivyo utakuwa dhalimu. Na Mwenyezi Mungu atakuwa mdai kwa niaba ya yule aliyedhulumiwa.

56. Qur'an, 2: 195.

yotajwa katika Aya hii ni kushughulika tu, kusahau na kukaa mbali dhidi ya kuutumikia Uislamu."

Abu Ayyub al-Ansari, ambaye alilisikiliza kwa Ikhlasi onyo hili kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kamwe hakujitenga na kuuhudumia Uislamu na hatimaye aliuawa kishahidi katika vita vilivyotajwa hapo juu na kuzikwa jirani na kuta za mji wa Istanbul.[57]

Abu Ayyub al-Ansari ambaye alishiriki katika vita hivi akiwa katika umri wa miaka themanini na ambaye aliwahi kupata heshima ya kuwa mwenyeji wa Mtukufu Mtume (s.a.w) kwa kipindi cha miezi sita pindi Mtume alipowasili Madina kwa mara ya kwanza, ni mfano tosha wa jinsi mtu wa huduma anavyotakiwa kufanya jitihada na kuwa na hisia ya hamasa ya imani yake.

Imani, ambayo humuunganisha muumini na Mwenyezi Mungu, ambaye ndiye pekee Mwenye Nguvu, ni aina ya msisimko. Muumini hapaswi kuhofia kitu chochote na wala hapaswi kupoteza matumaini. Qur'an Tukufu inasema:

"Wala msilegee, wala msihuzunike, kwani nyinyi ndio wa juu mkiwa ni Waumini." (Qur'an, 3: 139)

Watu wa huduma wanatakiwa kuwa watatuzi wa matatizo na siyo watengenezaji wa matatizo. Wasiongee tu na kutafuta makosa ya kukosoa bali wawe na moyo chanya na wawe na uwezo wa kuyakabili matukio kwa ajili ya kujenga.

Unapojiandaa kufanya jambo au kutekeleza kazi yoyote unayopewa, pendelea njia ya wastani na shirikishi kuhusu kutenda haki na ile inayolinda haki za kila mtu.

57. Tazama Abu Dawud, Jihad 23; Tirmidhi, Tafsir, 2.

Kuonyesha ulegevu na kutofanya chochote mbele ya tatizo ni alama ya udhaifu, na udhaifu hauna faida kwa muumini. Watu wa huduma daima wanapaswa waiweke nyoyoni na katika ndimi zao dua ifuatayo ya Mtume wa Mwenyezi Mungu:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Ninajilinda kwako kutokana na wasiwasi na huzuni, kutokana na kukosa uwezo na uvivu, kutokana na taabu na woga, dhidi ya uzito wa madeni na kuzidiwa na watu." (Bukhari, Daawat,(maombi),38)

Mambo ya msingi kuliko yote katika kuleta mafanikio katika utoaji wa huduma ni subira na azma. Aya zifuatazo za Qur'an Tukufu zinasema:

"Enyi mlioamini! Subirini, na shindaneni kusubiri, na kuweni macho, na mcheni Mwenyezi Mungu, ili mpate kufanikiwa." (Qur'an, 3: 200)

"Enyi mlioamini! Takeni msaada kwa subira na Sala. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaosubiri." (Qur'an, 2: 153)

Elmalili Hamdi Yazir aliandika maelezo yafuatayo katika kutafsiri Aya hii:

"Al-Sabur au Mwenye subira ni mojawapo ya majina matukufu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hii ina maana kwamba yule mwenye kufanya subira huidhihirisha sifa hii ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hasahasa watu wenye subira wanapokutana pamoja katika jamaa, hupata msaada

Shikamana tu na wale wenye staha na wachamungu. Kuwa makini na miili ya watu na usidanganywe na sifa zao, kwa maana kusifiwa mno kunaweza kukujaza jeuri.

wa Mwenyezi Mungu ambapo Mwenyezi Mungu huwa Rafiki na Mlinzi wao."[58]

Ni kawaida sana kukutana na matatizo na taabu kadhaa wakati wa kuwahudumia watu. Matatizo haya ukiyakabili kwa azma na subira, msaada wa Mwenyezi Mungu utakujia na mwishoni utapata mafanikio kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Imam Rabbani anasema:

"Matatizo na taabu katika njia ya kuufikisha ukweli wa Uislamu yanatakiwa kuhesabiwa kuwa ni baraka. Mitume walikabiliana na matatizo mengi na kukumbana na mashaka ya hali ya juu. Hata Mtume Muhammad (s.a.w) ambaye ni Mtume bora zaidi kuliko mitume wote anasema:

"Hakuna Mtume aliyeudhiwa kama nilivyoudhiwa mimi."[59] (Mektubat, 193th letter)

Japokuwa kazi zote unazofanya katika kuwatendea wema na kuwastawisha raia zinakupatia radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu, bado unatakiwa kutenga muda maalumu kwa ajili kuboresha uhusiano wako na Mwenyezi Mungu.

Maelezo yafuatayo ya Muhammad Iqbal yanatoa mwanga kwenye njia ya kila mtoa huduma:

"Insha mmoja alikuwa akimlalamikia insha mwenzake:

"Kuanzia leo nitaishi Makka na kwenye Ka'abah. Huko ninaweza kulala, kutembea tembea na kula; kwa sababu hapa wawindaji wanatutega na kutuwinda. Kuanzia leo nahitaji kuwa salama. Napenda roho yangu ipate utulivu kidogo..."

58. Tazama Yazir, Elmalili M. Hamdi, Hak Dini Kur'an Dili, juzuu I, uk. 546.
59. Tirmidhi, Sifat al-Qiyamah, 34.

Insha mwezake aliposikia hivyo akamwambia:

"Ewe rafiki yangu maridadi! Ukitaka kuishi, ishi katika hatari. Jipatie makali kwa jiwe la kusaga, na kuishi ukiwa na ukali zaidi ya upanga. Hatari humjaribu mwenye nguvu. Hutufanya tujue kile kinachoweza kufanywa na mwili na roho yetu."

Sufyan al-Thawri (q.s) anauelezea ukweli huu akisema:

"kwenda Horasan na kufikisha ujumbe wa Uislamu kuna faida zaidi kwako kuliko kuishi jirani na Makkah."

Mtu wa huduma hapaswi kujikunyata mbele ya shida na maudhi. Badala yake anatakiwa kuwa na nguvu dhidi ya tabu zinazopatikana katika njia ya kuwahudumia watu. Asikisahau kioevu hicho cha wokovu wa milele, ambacho mara zote hujificha ndani ya shida na mateso. Haiwezekani kuzifikia baraka bila kupitia mateso, kwa maana juhudi inayotumika katika njia yenye lengo huyafanya maisha yawe na thamani na baraka.

Kuwahudumia wengine hakutakiwi kuwa mapenzi ya kigeugeu. Badala yake, inatakiwa kuhesabiwa kama jukumu la maisha yote. Riziki ya watu wa huduma inapaswa kuwa subira na msaada wao uwe ni Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Imeelezwa katika maneno ya wazee kuwa:

Watu wenye sifa tatu zifuatazo wako mbali na Mwenyezi Mungu:

"Wahurumie waumini. Kamwe usijitenge na jamii".

Sheikh Edibali

1. Wale wanaokwepa kuwahudumia wengine na kufikiria starehe yao wenyewe.

2. Wale wanaoyakimbia maeneo yenye huzuni wakijifanya kuwa walikuwa na hisia sana za kukaa kule.

3. Wale wanaotumia muda wao kusuhubiana na wao na watenda dhambi.

Na furaha ya matendo mema hujionyesha katika mambo matatu yafuatayo:

1. Katika imani iliyochanganywa na upendo

2. Swala iliyotekelezwa kwa uchaji na unyenyekevu

3. Huduma iliyopambwa kwa wema

Kwa muhtasari, huduma hupokelewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu iwapo itatekelezwa kwa adabu za dhati na umakini. Kama ambavyo kwa kawaida ni vigumu kutegemea matokeo kutokana na huduma zilizofanywa hivyo hivyo, kadhalika zinaweza hata kuishia kuwa na matokeo yenye madhara.

Kuwa na uwezo wa kuwahudumia viumbe wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa huruma na upendo ni kitu ambacho kinahitajia subira na uvumilivu mkubwa. Mtu kamili wa huduma ni yule anayejipamba kwa sifa mbalimbali kama vile huruma, upendo, uungwana na ukarimu na ambaye amejitenga na chuki na ubinafsi.

Ukichunguza kwa makini, utaona kuwa ndani ya Qur'an kuna sifa zote hizo zilizotajwa hapo juu. Aidha, visa vilivyomo ndani ya Qur'an vina-

"Waheshimu baba na mama yako! Juwa kwamba baraka ziko pamoja na wazee."

Sheikh Edibali

toa nyongeza ya ziada kwenye misingi na kanuni hizi. Aya za kisheria ndani ya Qur'an Tukufu, zinaonyesha matumizi ya lazima ya matendo yetu ya kimaadili.

Maadili, ambayo kimsingi ni ukomavu wa kidini, ni kuhama kutoka kwenye hali ya kuwa kama mnyama kwenda kwenye hali ya binadamu, kutoka kwenye sifa za uchanga kwenda kwenye tabia kamili. Msingi wa maadili hupatikana katika kuzigeuza nyuso zetu na kuzielekeza kwa Mola wetu, Mwenye wema halisi. Na njia ielekeayo kwa Mola hupitia kwenye eneo la kuwahudumia viumbe Wake.

Haijalishi kuwa mtu wa huduma anaishi katika jamii gani, huendeleza msisimko, imani na shakhsia yake; na huulinda moyo wake dhidi ya mapenzi ya kupenda mali, ofisi na manufaa ya kidunia; na hatimaye hukimbilia kwenda kuwahudumia wanyonge na wale waliotengwa.

Mola wetu! Tubariki kwa kutupa sifa zote hizi nzuri. Tupe msisimko wa kuwahudumia watu. Tupe baraka ya kuyaelewa majuku yetu kwa ajili ya wale tunaoweza kuwasaidia na tufanye angalau tuhisi huzuni ya unyonge kwa wale tusioweza kwenda kuwasidia!

Amin!

"Ushindi mkubwa zaidi ni kuijua nafsi yako. Adui wa kweli ni nafsi ya mtu, ilhali rafiki ni yule anayejijua."

Sheikh Edibali

SEHEMU YA MAAGIZO YA ALI (R.A) KWENDA KWA HARITH BIN ASHTAR, GAVANA WA MISRI

Upambe moyo wako kwa huruma, upendo na muamala mzuri kwa watu walio chini ya amri na uongozi wako. Usiamiliane nao kama simba mkali anayetafuna hazina.

Watu wanaweza kufanya makosa; wakati mwingine hukosea kwa makusudi au bila makusudi. Kama ambavyo wewe humuomba msamaha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili yako mwenyewe, wasamehe na uwatendee wema.

Usijutie msamaha wako unaowapa au kufurahia adhabu unayowapa. Kama kuna nafasi ya kuepuka tabu, basi usiikimbilie. Usiseme “Nina mamlaka, ninatoa amri na wao wanatii”, kwa sababu hili litauharibu moyo wako na kuidhoofisha imani yako. Inakupa kiburi, na kiburi humpeleka mtu kwenye maangamizo.

Kama cheo ulichonacho kinakupa jeuri na kiburi, ikumbuke Nguvu ya Kweli ya Mwenyezi Mungu na hilo litakurejesha kwenye hali yako. Usiingie katika kushindana na Nguvu za Mwenyezi Mungu; kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu huwadhalilisha madhalimu na kuishusha chini kila jeuri.

Kamwe usipotoshe haki. Ukifanya hivyo utakuwa dhalimu. Na Mwenyezi Mungu atakuwa mdai kwa niaba ya yule aliyedhulumiwa. Mwenyezi Mungu anapokuwa mdai kwa niaba ya mtu, hoja za dhalimu hubatilika na kudhoofika mbele ya nguvu za Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu

Watu wanaweza kufanya makosa; wakati mwingine hukosea kwa makusudi au bila makusudi. Kama ambavyo wewe humuomba msamaha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili yako mwenyewe, wasamehe na uwatendee wema.

huendelea kumchukia dhalimu mpaka afanye toba. Hakuna dhambi nyingine inayozuia baraka na kusababisha ghadhabu ya Mwenyezi Mungu kuliko dhulma.

Unapojiandaa kufanya jambo au kutekeleza kazi yoyote unayopewa, pendelea njia ya wastani na shirikishi kuhusu kutenda haki na ile inayolinda haki za kila mtu.

Jiepushe na wale wanaotafuta aibu za watu, kwa maana ni jukumu la gavana, kabla ya yeyote yule, kuzisitiri aibu za watu.

Usiwaonee inda watu. Kata kamba zitakazokupelekea kulipa kisasi. Mambo ambayo hayajawa wazi kwako jifanye kama hujayaelewa, na usiyaamini kwa haraka maneno ya mpiga filimbi, kwa sababu vyovyote vile yatakavyoonekana kuwa mazuri, kwa asili yake, ni maneno ya udanganyifu.

Usimuingize bakhili, mtu mwoga au mwenye tamaa katika baraza lako; wa kwanza (bakhili) atajaribu kukuhofisha dhidi ya umasikini na njaa katika juhudi zake za kukufanya usiwasaidie watu, wa pili atajaribu kuivunja azma yako, na tamaa za mtu wa tatu za kutaka utukufu na hizi ni sifa ambazo Mwenyezi Mungu Mtukufu anazichukia.

Shikamana tu na wale wenye staha na wachamungu. Kuwa makini na mili ya watu na usidanganywe na sifa zao, kwa maana kusifiwa mnokunaweza kukujaza jeuri.

Usiamiliane na mwema na mbaya kwa namna ya usawa, kwa maana inaweza kuwazuia watu wasifanye wema.

Daima uwe na maoni mazuri kuhusu watu ili uweze kuijiokoa dhidi ya mchoko usiokuwa wa lazima.

Kamwe usipotoshe haki. Ukifanya hivyo utakuwa dhalimu. Na Mwenyezi Mungu atakuwa mdai kwa niaba ya yule aliyedhulumiwa.

Mpe kazi ya kuutumikia umma yule mtu ambaye atakayekuwa na Ikhlasi sana kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (s.a.w), mwema sana na mwenye akili sana kuliko wengine. Awe na uwezo wa kuidhibiti hasira yake pale anapokasirika, awe mpole, ayasikilize malalamiko ya kila mtu kwa upole na utaratibu, awe na huruma kwa wanyonge, ajitenge na wale wanaojisalimisha na kuzinyenyekea tamaa zao na asiwe miongoni mwa wale wanaosimama juu kwa hasira bali wanaokaa chini na kujuta.

Usiyapuuze matendo madogo kwa sababu ya kushughulika na mambo makubwa zaidi.

Hakuna chanzo mujarabu cha maliwazo kwa gavana kilicho bora kuliko kuimarisha haki na uadilifu katika jamii na kuwa gavana anayependwa na watu. Watu hawawezi kuonyesha mapenzi yao mpaka watakapohisi kuwa wako salama.

Elewa vizuri kujitolea kunakofanywa na watu wa huduma. Usiikumbuke huduma ya mtu kwa kuiambatanisha na huduma ya mtu mwingine na usiionyeshe staha ndogo ya mtu kuliko ujasiri na ushujaa unaostahili. Hadhi ya juu ya kijamii aliyonayo mtu isikufanye uyaone matendo yake madogo kuwa makubwa na hadhi ya mtu wa chini isikuzuie kuuona ukubwa wa matendo yake.

Unapojiandaa kufanya jambo au kutekeleza kazi yoyote unayopewa, pendelea njia ya wastani na shirikishi kuhusu kutenda haki na ile inayolinda haki za kila mtu.

Usimpe cheo mtu mwenye mielekeo na misukumo ya kibaguzi au umimi; kwa sababu misukumo hii husababisha dhulma na uasi.

Fuatilia utendaji wa wale unaowapa majukumu. Waagize wangalizi waaminifu na watiifu wakafuatilie kazi zao; kwa sababu kujua jinsi wanavyofanya kazi zao kutawafanya waongeze juhudi na kuwapa imani raia.

Wafikirie watu walio mbali nawe na usiwatenge. Fanya utafiti ujue kama kuna yeyote miongoni mwao asiyeweza kukuletea matatizo yake kwa sababu ya watu waliokuzunguka. Wateue makarani wanaomuogopa Mwenyezi Mungu, wenye staha na waaminifu wayashughulikie matatizo ya watu wa aina hii. Hivyo makarani hawa wanaweza kuwa watu wa kati baina yako na wale watu wasioweza kukufikia na fanya juhudi ya kujua hali zao hasa zilivyo. Kwa ufupi, fanya kazi kwa bidii ili uwe na uwezo wa kumwambia Mwenyezi Mungu Mtukufu siku ya kiyama kwamba: “Nilijitahidi.”

Tenga muda na sehemu maalumu kwa ajili ya kusikiliza matatizo ya wale wenye shida. Kaa nao na waonyeshe staha yako ambayo itakupatia radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Wasamehe kwa mienendo na mazungumzo yao yasiyokuwa sawa sawa. Usiwakaripie au kuwaonyesha mabavu yako. Usipoziumiza hisia zao, basi Mwenyezi Mungu atakufungulia rehema Zake na kukulipa kwa utiifu wako. Unapotoa kitu, toa ukiwa na uso wa tabasamu na roho yenye furaha. Kama huwezi kutoa, basi waombe msamaha na watake radhi kwa udhuru unaoonekana.

Japokuwa kazi zote unazofanya katika kuwatendea wema na kuwastawisha raia zinakupatia radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu, bado unatakiwa kutenga muda maalumu kwa ajili kuboresha uhusiano wako na Mwenyezi Mungu.

Zigawe haki za utumwa wako kwa Mwenyezi Mungu katika wakati wako wa mchana na usiku na uzitekeleze haki hizi kwa ukamilifu bila kujali mazingira uliyonayo. Ukiongoza swala, usiirefushe sana kiasi cha kuwachosha waumini na

Shikamana tu na wale wenye staha na wachamungu. Kuwa makini na mili ya watu na usidanganywe na sifa zao, kwa maana kusifiwa mno kunaweza kukujaza jeuri.

usiifupishe mno, kwa sababu kunaweza kuwa na watu katika jama'ah ambao ni wagonjwa au wenye majukumu yanayotakiwa kufanywa kwa dharura. Mtukufu Mtume (s.a.w) alipokuwa akiniagiza kwenda Yemen, nilimuuliza:

"Niiongoze vipi swala yao?" naye akanijibu:

"Kulingana na hali ya walio dhaifu zaidi katika waumini..."

Wahurumie waumini. Usiishi kwa kujitenga na kujikata na jamii. Kama magavana wataishi kwa kujitenga na umma, itawazuia kuijua kwa usahihi hali ya umma. Kukaa nyuma ya mapazia huwazuia kuona kile kinachohitajika katika jamii. Kwa hiyo, huanza kuyaona matatizo makubwa kuwa ni madogo na yale madogo kuyaona kuwa ni makubwa. Mambo mazuri huwa mabaya na mabaya huwa mazuri. Haki na batili huchanganywa.

Japokuwa kazi zote unazofanya katika kuwatendea wema na kuwastawisha raia zinakupatia radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu, bado unatakiwa kutenga muda maalumu kwa ajili kuboresha uhusiano wako na Mwenyezi Mungu.

Mshawishi kila mtu, akiwa wa karibu au mbali, kuikubali haki. Raia wakifikiri kuwa wewe ni dhalimu, basi watake radhi na ujaribu kubadili mawazo yao mabaya waliyonayo kukuhusu. Kwa namna hii utaweza kujidhibiti wewe mwenyewe na pia kuwatendea wema.

Katika kutekeleza ahadi yako, ikilazimika kabisa, unatakiwa kuwa tayari hata kuyatoa maisha yako. Kamwe usivunje ahadi zako; kwa sababu hakuna yeyote mwenye ujasiri wa kumpinga Mwenyezi Mungu Mtukufu, isipokuwa wapumbavu ambao wameshahukumiwa kuwa fukara. Hivyo, usiyafanye maagano kuwa wazi kutafsiriwa.

Kuwa makini na sifa zilizozidi kiasi! Usiuamini upande unaovutia wa nafsi yako. Usisubiri kusifiwa mbele yako; kwa sababu hii ndiyo silaha kali

zaidi anayoitumia Shetani kuyaharibu matendo mema ya watu wema.

Usiwasute raia kwa kuwakumbushia kile ulichowafanyia. Usiyatie chumvi matendo yako, na wala usizikimbie ahadi zako. Kwa sababu masuto na masimbulizi huziondosha baraka na utiaji chumvi huugeuza ukweli. Kuvunja ahadi husababisha kuchukiwa na Muumba na viumbe pia.

Usianze kufanya kazi kabla ya wakati wake. Wakati wake ukifika, usikurupuke. Using'ang'anie kufanya vitu usivyojua uhakika wake na utakapojua, usisubiri kuanza.

Usijifanye kuwa hujui cha kufanya, pindi unapojua mwenendo mbaya wa maofisa wako. Vinginevyo, utaadhibiwa kwa niaba ya mtu mwingine. Ukweli kuhusu matendo hayo utadhihiri mbele ya macho yako na haki za wanyonge zitachukuliwa kutoka kwako.

Dhibiti hasira yako, mkono wako, ulimi wako, na matamanio yako. Kaa mbali na mabalaa kuilinda nafsi yako ili hasira yako itoweke na uidhibiti nguvu ya matamanio yako; lakini unatakiwa kujua pia kwamba hutoweza kuidhibiti nafsi yako mpaka uhisi hofu na wasiwasi kwa kukumbuka kuwa utarejea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Dua zetu tunazielekeza kwa Mwenyezi Mungu na rehema na baraka ziwe juu ya Mtume Wake!

"Wahurumie waumini. Kamwe usijitenge na jamii".

Sheikh Edibali

USHAURI KUTOKA KWA EDEBALI

Sehemu ya ushauri wa Sheikh Edebali kwenda kwa Othman Ghazi

"Mwanangu!

Wewe ni kiongozi! Kuanzia sasa hasira itatoka kwetu, huruma itatoka kwako... hisia ya kukosewa itatoka kwetu, tulizo la nafsi litatoka kwako... Kulaumu ni kazi yetu, kuvumilia ni kazi yako... Udhaifu na aibu zitatoka kwetu, subira ni kazi yako... Migogoro, mapigano na mabishano yatatoka kwetu, kutenda haki ni kazi yako... Jicho baya, kutabiri mabaya na tafsiri zisizokuwa za haki zitatoka kwetu, msamaha utatoka kwako..."

"Mwanangu!

Kuanzia sasa kugawanyika ni kazi yetu, kutuunganisha ni kazi yako... Uvivu ni kazi yetu, kuonya, kuhamasisha na kuweka mipango ni kazi yako..."

"Mwanangu!

Mzigo wako ni mzito, kazi yako ni ngumu na nguvu zako zinapeperuka angani. Mwenyezi Mungu Mtukufu akusaidie na aubariki utawala na himaya yako. Aifanye kuwa njema kwa ajili ya njia ya Haki na iangaze nuru yake na kuifanya iweze kuonekana kutoka mbali. Akupatie nguvu za kuubeba mzigo wako na hekima na moyo ili uweze kuisafisha njia yako."

"Mwanangu!

Wewe ni mzungumzaji imara, mwenye busara na mzuri; lakini kama hujui namna na mahali pa

"Waheshimu baba na mama yako! Juwa kwamba baraka ziko pamoja na wazee."

Sheikh Edibali

kuvitumia, utasombwa na upepo wa kwanza wa asubuhi. Hasira yako na nafsi yako vitaungana na kuishinda busara yako. Ndiyo maana daima unatakiwa kuwa mvumilivu, imara na mwenye azma."

"Subira ni muhimu sana. Kiongozi anapaswa kuwa na subira. Ua halichanui kabla ya wakati. Tunda bichi haliwezi kuliwa, hata kama likiliwa, litakukwama kooni mwako. Upanga bila elimu ni kama tunda bichi..."

"Yafanye maarifa na elimu ya umma iishi ndani mwao. Usiyageuzie mgongo. Daima sikia uwepo wake. Elimu na Maarifa haya ndicho kitu kinachouongoza umma na kuufanya uendelea kuwa hai..."

"Mwanangu!

Kuna watu wanaozaliwa alfajiri na kufariki usiku."

"Ulimwengu siyo mkubwa kama macho yako yanavyouona. Siri zote ambazo hazijafunguliwa na kujulikana zitafichuliwa tu kupitia fadhila na uadilifu wako."

"Waheshimu baba na mama yako! Juwa kwamba baraka ziko pamoja na wazee."

"Ukipoteza imani yako, utageuka kutoka kwenye kijani kibichi na kuwa jangwa au ardhi kame."

"Zungumza wazi wazi! Usiudhike kwa urahisi! Ukiona kitu (ambacho ni kizuri na chenye kufaa kufichwa) usikiseme; ukisikia, usikifichue! Usiende (mara watu wanapokuchoka) mahali ambapo unapendwa; kwa sababu hili litaumiza upendo na heshima yao kwako..."

"Ushindi mkubwa zaidi ni kuijua nafsi yako. Adui wa kweli ni nafsi ya mtu, ilhali rafiki ni yule anayejijua."

Sheikh Edibali



“Kuna watu wanaozaliwa alfajiri na kufariki usiku. Ulimwengu sio mkubwa kama macho yako yanavyouona. Siri zote ambazo hazijafunguliwa na kujulikana zitafichuliwa tu kupitia fadhila na uadilifu wako.”

Sheikh Edibali

“Wahuzunikie watu watatu: mtu mwenye busara aliye baina ya wajinga, tajiri aliyefukarika na mheshimiwa anayepoteza heshima ya watu.”

“Usiwasahau wale walio katika sehemu za juu kwamba hawako salama kama wale walio katika sehemu za chini.”

“Usiogope kusisitiza juu ya jambo lako la haki. Unapaswa kujua kuwa farasi mzuri huitwa mwekundu, na kijana mzuri huitwa mwendawazimu (shujaa, jasiri, na thabiti.”

“Ushindi mkubwa zaidi ni kuijua nafsi yako. Adui wa kweli ni nafsi ya mtu, ilhali rafiki ni yule anayejijua. Mtu anapokaa chini, itakuwa vigumu sana kumuinua. Mtu anapokaa sana, huanza kupata ganzi. Anapopata ganzi, huanza kuongea. Kisha maongezi yake hubadilika kuwa umbeya. Umbeya unapoanza, hawezi tena kupona. Rafiki huwa adui, na adui huwa mbaya...”

“Siku moja nguvu za mtu huchoka lakini elimu yake huishi. Nuru ya elimu hupita hata katika macho yaliyofungwa.”

“Mnyama anapokufa, huacha shogi; mtu anapokufa huacha kazi zake. Tusiwalilie wale wanaokufa, bali tuwalilie wale ambao hawakuacha kitu nyuma yao. Tunapaswa kuendelea kuanzia pale walipoishia.”

“Hatuna haki ya kusimama; kwa sababu hatuna muda wa kutosha...”

“Upendo unapaswa kuwa msingi wa kazi zetu. Upendo una maana ya kukaa kimya; huwezi kuonyesha upendo wako kwa kupiga makelele au kukaripia...”

"Ewe Othman! Wale wasioyatambua mambo yao yaliyopita hawawezi kujua mambo ya mustakabali wao. Ijue vizuri historia yako ili uweze kutembea kwa ukakamavu kuuelekea mustakabali. Usisahau ulitoka wapi ili usije kusahau unakokwenda."

Wasia huu wa aina yake kutoka kwa Sheikh Edibali kwenda kwa Othman Ghazi ndiyo nguvu ya msukumo iliyokuwa chanzo cha ushindi mwingi sana wa kimaada na kimaanawi kwa jamii yote ya Uthmaniyyah, kuanzia kwa Sultan mpaka kwa wasomi, na kuanzia kwa wanajeshi mpaka kwa viongozi wa kiroho. Kwa hiyo waasisi hasa wa Dola ya Uthmaniyya walikuwa masultani wa nyoyo kama vile Edebali na wale waliopata mafunzo kwa kutumia mbinu na njia zake. Uzuri ulioje wa maelezo ya jambo hili katika kisa kifuatacho kutoka katika kitabu kiitwacho Gülistan:

Sheikh Sadi anasema:

"Siku moja rafiki yangu alinipa udongo wenye harufu nzuri (yaani kipande safi cha udongo wa ardhi) katika bafu kwa ajili ya kujisafishia. Nikauuliza udongo huo:

"Wewe ni kitu gani? Je wewe ni miski au ambari? Nimevutiwa sana na harufu yako mwanana."

Udongo ukanijibu:

"Mimi ni udongo kutoka katika shamba la mawaridi. Wakati wa alfajiri majani yake hupatwa na umande na kisha huudondosha umande huo juu yangu. Nililowa kwa umande huu. Kwa kweli mimi ni kipande tu cha udongo, lakini harufu yangu nzuri inatokana na mawaridi haya..."

"Siku moja nguvu za mtu huchoka lakini elimu yake huishi. Nuru ya elimu hupita hata katika macho yaliyofungwa."

Sheikh Edibali

Katika zama za Dola ya Uthmaniyyah, hususan baraka za wanazuoni katika karne tatu za mwanzo, zilieneza harufu isiyokwisha ulimwenguni kama udongo uliolowa kwa maji ya waridi. Waridi ni alama ya Mtukufu Mtume (s.a.w), na maadili na mwenendo wake ni wafalme wa mawaridi haya.

Tunamuomba Mola wetu atubariki kwa cheche za halia yenye ukamilifu ya Mtume Wake (s.a.w). Tunamuomba atujalie kuwa tone la umande kwenye Uaridi hilo la kipekee.

Amin!

"Subira ni muhimu sana. Kiongozi anapaswa kuwa na subira. Ua halichanui kabla ya wakati. Tunda bichi haliwezi kuliwa, hata kama likiliwa, litakukwama kooni mwako. Upanga bila elimu ni kama tunda bichi..."

Sheikh Edibali

VITABU REJEA

Abdullah Yusuf Ali, The Holy Qur'an: text, translation and commentary, Elmhurst, N.Y. : Published by Tahrike Tarsile Qur'an, 2001.

Ahmed bin Hanbel, el-Müsned, I-VI, İstanbul, 1992.

Ali b. Husain Vaiz-i Kashifi, Rashahat 'Ayn al-Hayat (ed. Ali Asğar Muîniyân), I-II, Tahran, 1977.

Ali Özek, Hayrettin Karaman, Ali Turgut, Mustafa Çağrıcı, İ. Kâfî Dönmez, Sadreddin Gümüş, Kur'ân-ı Kerîm ve Türkçe Açıklamalı Meâli, Suudî Arabistan, 1992.

Asqalani, Ibn Hajar Shihab al-din Ahmad b. Ali, el-İsâbe fî Temyîzi's-Sahâbe, ed. M. Fuad Abdülbâkî; Egypt, 1959.

Asqalani, Ibn Hajar Shihab aldin Ahmad b. Ali, Hady al-Sari Muqaddimat al-Fath al-Bari Sharh al-Sahih al-Bukhari, I-XXVI II, (n.d.). Dar al-Fikr,

Atalar, Münir, Surre-i Humâyûn ve Surre Alayları, Ankara, 1991.

Bayhaki, Abu Bakr Ahmad b. al-Husain, Shuab al-Iman, I-IX, Beyrut, 1990; es-Sunan al-Kubra, (n.d.) Dar al-Fikr.

Berki, Ali Himmet, Açıklamalı Mecelle: Mecelle-i Ahkâm-ı Adliye, İstanbul, 1982.

Bukharî, Ebû Abdillâh Muhammed bin İsmâil, el-Câmiu's-Sahîh, I-VIII, Istanbul, 1992; al-Tarikh al-Saghir, I-II, Kâhire, 1977.

Bursevî, İsmâil Hakkı, Rûhu'l-Beyân, I-X, İstanbul, 1969.

Busti, Ibn Hibban Abu Hatim, Sahih Ibn Hibbân, I-XVIII, Beirut, 1993.

Can, Şefik, Mesnevî Tercümesi,
I-VI, Istanbul, 1997.
Canan, İbrahim, Hadis Ansiklopedisi,
I-XVIII, İstanbul, (n.d.).
Çantay, Hasan Basri, Kur'ân-ı
Hakîm ve Meâl-i Kerîm, I-III, Istanbul, 1996.
Dânâ, Sâdık, Külliyât, Erkam
Yayınları.
Danişmend, İsmail Hâmi, Eski
Türk Seciye ve Ahlâkı, İstanbul,
1982.
Dârimî, Ebû Muhammed
Abdullâh bin Abdirrahman, Sünenü'd-Dârimî, I-II, Istanbul,
1992.
Daylami, Abu Shuja' Shiruyah b.
Shahridar, el-Firdevs bi-Me'sûri'l-
Hitâb, Beyrut, 1986.
Ebû Dâvud, Süleyman bin Eş'as
es-Sicistânî, Sünenü Ebî Dâvud,
I-V, İstanbul, 1992.
Ebû Nuaym, Hilyetü'l-Evliyâ, I-X,
Beyrut, 1967.
Ebu'l-Hasan en-Nedevî, İslâm
Önderleri Târihi, I-VIII, İstanbul,
1992.
Erbilî, Muhammed Es'ad, Mektûbât,
(ed. H. Kâmil Yılmaz, İrfan
Gündüz), İstanbul, 1983; Dîvân-ı
Es'ad, İstanbul, 1991.
Esed, Muhammed, Kur'ân Mesajı
(trans. Câhid Koytak, Ahmet
Ertürk), I-III, İstanbul, 1999.
Gölpınarlı, Abdülbâkî, Mesnevî ve
Şerhi, I-VI, İstanbul, 1973-1974.
Güzel, Abdurrahman and Tatçı,
Mustafa, Yunus Emre, Ankara,
1991.
Hayrât Neşriyât İlmî Araştırma
Merkezi Meâl Hey'eti, Kur'ân-ı
Kerîm ve Muhtasar Meâli, Istanbul, 2001.
Haythami, Hafız Nuraddin Ali
b. Abi Bakr, Majma' al-Zawaid
wa Manba' al-Fawâid, I-X, Beyrut, 1988.
Hunke, Sigrid, Avrupa'nın Üzerine
Doğan İslâm Güneşi, İstanbul,
1991.
Ibn Abdilberr, Abu Umar Yusuf

b. Abdullah b. Muhammad, al-Isti'ab fi Ma'rifat al-Ashab, I-IV, Cairo, (n.d.)
Ibn Hisham, al-Sirat al-Nabawi-yya,
Beyrut, 1992.
Ibn Kathir, Imad al-din Abu al-Fida, al-Sirat al-Nabawiyya, I-IV, Cairo, 1964.
Ibn Kathir, Imad al-din Abu al-Fida, el-Bidâye ve'n-Nihâye, I-XV, Cairo, 1993;
Ibn Kathir, Imad al-Din Abu al-Fida, Tafsir al-Qur'an al-Azim, I-V, Beirut, 1988;
Ibn Qudamah, al-Mughni, I-IX, Cairo, (n.d.)
Ibn Sa'd, at-Tabaqat al-Kubra, I-IX,
Beirut, (n.d.)
Ibn-i Arabî, Mişkâtü'l-Envâr - Nurlar Hazînesi, (Trans. Prof. Dr. Mehmed Demirci), Istanbul, 2001.
İmâm Mâlik, Muvattâ, I-II, İstanbul, 1992.
İmâm Rabbânî, Mektûbât, I-II, Sirâc Kitabevi, Tıpkı basım, İstanbul, (n.d.).
Jilani, Abdulqadir, al-Fathu'r-Rabbânî (trans. Yaman Arıkan), İstanbul, 1987.
Kazıcı, Ziya, İslâmî ve Sosyal Açıdan Vakıflar, Istanbul, 1985.
Kazvinî, İbn-i Mâce Ebû Abdillâh Muhammed bin Yezid, Sünenü İbn-i Mâce, İstanbul, 1992.
Kuşeyrî, Müslim Ebû'l-Hüseyin bin Haccâc, el-Câmiu's-Sahîh (thk. M. Fuad Abdülbâkî), I-III, İstanbul, 1992.
Mısıroğlu, Kadir, Külliyât, Sebil Yayınevi.
Nawawi, Abu Zakariyya Yahya b. Sharaf, Riyad al-Salihin, Beirut,
Nawawi, Abu Zakariyya Yahya b. Sharaf, Riyâzü's-Sâlihîn (trans. and ed. Yaşar Kandemir, İsmâil Lütfi Çakan, Râşit Küçük), I-VIII, İstanbul, 1997.
Naysaburi, Hakim Abu Abdillah Muhammad b. Abdillah, Mustadrak ala al-Sahihayn, I-V,

Beyrut, 1990.
Nesâî, Ebû Abdirrahmân Ahmed
bin Şuayb, Sünenü'n-Nesâî, I-VIII,
İstanbul, 1992.
Pickthall, Marmaduke William,
The meaning of the glorious Koran;
an explanatory translation,
New York: Dorset Press, [1988?]
Ramazanoğlu, Mahmud Sâmi,
Külliyât, Erkam Yayınları.
Rumi, Mawlana Jalal al-Din, The
Mathnawí of Jalálu'ddín Rúmí, edited
from the oldest manuscripts
available, with critical notes, translation
& commentary, ed. Reynold
A. Nicholson, Konya Metropolitan
Municipality, 2004
Shakir, M.H. (trans.), The
Qur'an = [al-Qur'ān al-'akīm],
Elmhurst, N.Y.: Tahrike Tarsile
Qur'an, 1997.
Şirâzî, Şeyh Sâdî, Bostan, Istan-bul,
1995.
Suyuti, Abu al-Fadl Jalal al-din
Abdurrahman b. Abu Bakr, al-
Jami' al-Saghir, Egypt, 1888.
Tabari, Abu Ja'far Muhammad b.
Jarir, Jami' al-Bayan 'an Ta'wil Ay
al-Qur'an, Beirut, 1995.
Tirmizî, Ebû İsâ, Muhammed
bin İsâ, Sünenü't-Tirmizî, I-V, Istanbul,
1992.
Topbaş, Osman Nuri, Külliyât,
Erkam Yayınları.
Wahidi, Asbab al-Nuzul al-Qur'an,
Beirut, 1990.
Waqidi, Maghazi, Egypt, 1948.
Yazır, Elmalılı M. Hamdi, Hak
Dîni Kur'ân Dili, I-X, İstanbul,
1971.

YALIYOMO

DIBAJI 5

Sura ya kwanza
USTAARABU WA WAKFU

USTAARABU WETU WA WAKFU 13

Sura ya Pili
SADAKA NA NJIA ZAKE

ZAKA NA INFAQ 47
A. *Zaka* 47
Hekima za Zaka kwa mtu mmoja na jamii 51
Mwisho wenye kutisha wa wale wanaopuuza kutoa Zaka 58
Zaka ya mazao ya kilimo: ‘Ushr (Moja ya kumi) 76
B. *Infaq* *80*
a. Asili yake 80
b. Adabu za Infaq 94
Zaka kutokana na wa kisheria 104
Shuruti za wajibu wa Zaka 104
Aina na viwango vya mali zinazotolewa Zaka 107

Watu wanaostahili kupokea Zaka 110

Orodha ya wale wasiopewa Zaka 111

'Ushr (moja ya kumi): Zaka ya mazao ya kilimo 112

Mahojiano kuhusu Wakfu, Zaka na infaq.....115

Mali ni amana 115

Sura ya Tatu

HATUA KUU KUELEKEA KWENYE KILELE CHA KIROHO

KUTOA HUDUMA KWA AJILI YA MWENYEZI MUNGU.....135

Uislamu unahuisha ubinaadamu.....148

Njia na Mbinu ya Muongozo wa Kiroho na Huruma Katika Kuwahudumia Watu 165

Ulaini na upole katika kuwahudumia watu 179

Adabu na kanuni za maadili katika kutoa huduma 192

1. Kutambua umuhimu wa kutoa huduma 194

2. Kuupamba moyo kwa sifa na tabia za kiroho 200

a. Moyo kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu daima: 202

b. Kuujaza moyo mapenzi ya kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake.....204

c. Kuujaza moyo mapenzi ya kuwapenda Waislamu 208

d. Moyo Kujazwa upendo kwa viumbe kwa ajili ya Muumba 217

3. Kudumisha Ikhlasi na istiqamah au msimamo na unyoofu....217

4. Muumini mwenye upendo, huruma na msamehevu.....224

5. Kutenda jambo kwa mashauriano..... 230

6. Kuzijua sifa na tabia za mtu anayehudumiwa..... 233

7. Kudumisha hali ya uwastani na kadri katika kufanya mambo 238

8. Kutoa kipaumbele katika mafunzo ya Qur'an Tukufu..... 248

9. Kujiendeleza kielimu na kimaadili..... 256

a. Kujiendeleza kielimu 258

b. Kujiendeleza kiroho 259

c. Maendeleo ya utalaamu 261

10. Kuyahusisha makosa na nafsi yako na kuyahusisha mafanikio na Mwenyezi Mungu Mtukufu 263

11. Kujaribu kuwa mfano mwema 272

12. Kutopoteza msisimko na kuwa mwenye msimamo na ung'ang'anizi..... 275

SEHEMU YA MAAGIZO YA ALI (R.A) KWENDA KWA HARITH BIN ASHTAR, GAVANA WA MISRI..... 284

USHAURI KUTOKA KWA EDEBALI..... 290

VITABU REJEA..... 295

FOR FREE IN PDF FORMAT

ISLAMIC WORKS

YOU CAN DOWNLOAD IN PDF FORMAT

1550 BOOKS IN **59 LANGUAGES** FOR FREE

Islamic books in different languages are waiting
for you in PDF format at the web site
www.islamicpublishing.org

ERKAM PUBLICATIONS | islamicpublishing.org